

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO**



**HOTUBA YA WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO,
MHESHIMIWA ENG. ISACK ALOYCE KAMWELWE (MB),
AKIWASILISHA BUNGENI MPANGO NA MAKADIRIO YA MAPATO NA
MATUMIZI YA FEDHA KWA MWAKA WA FEDHA 2020/21**

HOTUBA YA WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO, MHESHIMIWA ENG. ISACK ALOYCE KAMWELWE (MB), AKIWASILISHA BUNGENI MPANGO NA MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA FEDHA KWA MWAKA WA FEDHA 2020/21

A. UTANGULIZI

1. Mheshimiwa Spika, kufuatia taarifa iliyowasilishwa humu Bungeni na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Miundombinu, ninaomba kutoa hoja kwamba Bunge lako sasa lipokee na kujadili Taarifa ya Utekelezaji wa Mpango na Bajeti ya Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano kwa mwaka wa fedha 2019/20. Aidha, kwa mara nyingine ninaomba Bunge lako Tukufu lijadili na kupitisha Mpango na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano kwa mwaka wa fedha 2020/21.

2. Mheshimiwa Spika, sisi sote kwa ujumla wetu, hatuna budi kumshukuru Mwenyezi Mungu, kwa kutujalia uhai na afya njema na hivyo kutuwezesha kukutana leo kwa ajili ya kushiriki katika Mkutano huu wa 19 na wa mwisho wa Bunge la 11, ili kujadili utekelezaji wa majukumu ya Sekta za Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano kwa mwaka wa fedha 2019/20 pamoja na kujadili Mipango na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Sekta hizo kwa mwaka wa fedha 2020/21. Aidha, ninamuomba Mwenyezi Mungu aendelee kutupatia ulinzi wake dhidi ya janga linaloisumbua dunia kwa sasa la mlipuko wa ugonjwa wa homa kali ya mapafu inayosababishwa na virusi vya Corona (COVID -19).

3. Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2019/20, Bunge lako Tukufu lilipatwa na simanzi kubwa kufuatia vifo vya wapendwa wetu ambao ni Mhe. Rashid Ajali Ahkbar aliyekuwa Mbunge wa jimbo la Newala Vijijini, Richard Mganga Ndassa aliyekuwa Mbunge wa Jimbo la Sumve na Mhe. Mchungaji Dkt. Getrude Pangalile Rwakatare, Mbunge wa Viti Maalum. Ninachukua fursa hii kutoa pole kwako wewe binafsi, Mheshimiwa Naibu Spika, Familia za Marehemu hao, Bunge lako Tukufu, Wananchi wa Jimbo la Newala Vijijini na Watanzania kwa ujumla kwa kuondokewa na wanasiasa hao wakongwe na mahiri. Mwenyezi Mungu aziweke roho za marehemu hao mahali pema peponi. Amina.

4. Mheshimiwa Spika, nitumie fursa hii kuwapa pole ndugu wa marehemu na wafanyakazi wa Shirika la Reli Tanzania (TRC) kwa

msiba mkubwa wa wafanyakazi watano (5) waliopoteza maisha na mmoja kujeruhiwa katika ajali iliyotokea eneo la Mwakinyumbi na Gendagenda ambapo treni iligongana na kiberenge, wananchi 104 waliopoteza maisha kutokana na moto uliosababishwa na lori la mafuta mjini Morogoro, ajali ya lori kugongana na basi la abiria eneo la Mkuranga - Pwani ambapo abiria 20 walipoteza maisha na 15 kujeruhiwa. Aidha, ninawapa pole wote waliofikwa na majanga ya kupoteza ndugu zao kufuatia mvua zilizonyesha kupita kiwango katika maeneo mbalimbali nchini. Mwenyezi Mungu awape nafuu ya haraka majeruhi wote na aziweke roho za marehemu hao mahali pema peponi. Amina.

5. Mheshimiwa Spika, kwa heshima na taadhima ninaomba uniruhusu kutumia fursa hii kumpongeza Mhe. Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kusimamia utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2015 kwa umakini mkubwa na hivyo kuendelea kuiongoza nchi yetu kwa amani na utulivu. Aidha, ninampongeza Mhe. Rais kwa kuchaguliwa kuwa Mwenyekiti wa Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC) pamoja na kuiongoza vyema Jumuiya hiyo hususan katika kipindi hiki cha mlipuko wa ugonjwa wa homa kali ya mapafu inayosababishwa na virusi vya Corona (COVID -19). Vilevile, ninawapongeza Mhe. Samia Suluhu Hassan, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Mhe. Kassim Majaliwa Majaliwa (Mb), Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa uongozi wao thabiti.

6. Mheshimiwa Spika, ninaomba nikupongeze wewe binafsi, Naibu Spika, Wenyeviti wa Bunge, Katibu wa Bunge, Watendaji wa Ofisi ya Bunge pamoja na Bunge lako Tukufu kwa ushirikiano ninaoendelea kuupata wakati wote ninapotekeleza majukumu yangu ikiwa ni pamoja na kuwasilisha taarifa mbalimbali kuhusu sekta ninazosisimamia. Ninapenda kuwahakikishia kuwa, Wizara yangu itaendelea kutoa ushirikiano unaohitajika ili kufikia malengo ya Kisekta na Kitaifa kwa ujumla. Vilevile, kwa namna ya pekee ninaomba kuishukuru familia yangu na wapiga kura wa Jimbo langu la Uchaguzi la Katavi kwa kuendelea kunipa ushirikiano katika kutekeleza majukumu yangu kwa Watanzania.

7. Mheshimiwa Spika, nitumie pia fursa hii kuwapongeza Mhe. Mussa Azzan Zungu (Mb), Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Rais

(Muungano na Mazingira) na Mhe. George Boniface Taguluvala Simbachawene (Mb), Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi kwa kuteuliwa kuwa Mawaziri. Aidha, ninapenda kutoa pongezi kwa Mhe. Miraji Jumanne Mtaturu, Mbunge wa Jimbo la Singida Mashariki na Mhe. John Danielson Pallangyo, Mbunge wa Jimbo la Arumeru Mashariki kwa kuchaguliwa kuwa Wabunge katika chaguzi ndogo zilizofanyika nchini katika mwaka wa fedha 2019/20. Ushindi wao wa kishindo ni kielelezo tosha cha kuonyesha namna Chama cha Mapinduzi kinavyoendelea kuaminika na kupendwa na Watanzania. Vilevile, ninampongeza Dkt. Zainab Abdi Seraphin Chaula kwa kuteuliwa kuwa Katibu Mkuu wa Sekta ya Mawasiliano.

8. Mheshimiwa Spika, mwisho lakini siyo kwa umuhimu, ninapenda kuchukua fursa hii kuishukuru Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Miundombinu inayoongozwa na Mhe. Seleman Moshi Kakoso (Mb), Mbunge wa Mpanda Vijijini na Makamu Mwenyekiti wa Kamati Mhe. Hawa Mchafu Chakoma (Mb). Nakiri kuwa Wizara imenufaika sana na umahiri, umakini na ushirikiano wa Kamati hiyo katika kuchambua, kushauri na kufuatilia maendeleo ya Sekta za Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano. Ninapenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kwamba maoni, ushauri na mapendekezo yaliyotolewa na Kamati yamezingatiwa katika Bajeti hii.

9. Mheshimiwa Spika, kabla ya kuwasilisha Hotuba hii, ninapenda kuwashukuru Mhe. Kassim Majaliwa Majaliwa (Mb), Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Mhe. Dkt. Philip Isdor Mpango (Mb), Waziri wa Fedha na Mipango kwa hotuba zao zilizotangulia. Hotuba hizo zimeeleza kwa ujumla maendeleo ya sekta za Kijamii na Kiuchumi kwa mwaka 2019/20 na mwelekeo kwa mwaka 2020/21. Ninawashukuru na kuwapongeza pia Mawaziri wote waliowasilisha hotuba zao.

10. Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo ya utangulizi, ninaomba sasa kuwasilisha hotuba yangu ambayo imejikita katika Utekelezaji wa Mipango na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano kwa mwaka wa fedha 2019/20 pamoja na Mpango na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara yangu kwa mwaka wa fedha 2020/21. Aidha, kabla ya kuelezea utekelezaji wa majukumu ya Wizara kwa kipindi cha mwaka wa fedha 2019/20, ninapenda nitoe kwa muhtasari taarifa ya utekelezaji wa Ilani

ya Uchaguzi ya CCM ya Mwaka 2015` kwa kipindi cha miaka minne ya Serikali ya Awamu ya Tano.

B. UTEKELEZAJI WA MALENGO YALIYOAINISHWA KATIKA ILANI YA UCHAGUZI YA CCM YA MWAKA 2015 KWA KIPINDI CHA MWAKA 2016/17 – 2019/20

B-1 SEKTA YA UJENZI

11. Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha kuanzia mwaka 2015 hadi 2020, Serikali kupitia Wizara yangu imepata mafanikio makubwa katika kuboresha miundombinu ya barabara na madaraja kwa kuzingatia vipaumbele ambavyo ni; Kujenga barabara zetu zinazounganisha nchi yetu na nchi jirani, kujenga barabara zinazounganisha mikoa kwa kiwango cha lami na kujenga barabara zinazokwenda kwenye maeneo yenye fursa za kiuchumi. Katika kipindi hicho, barabara zenye urefu wa jumla ya kilometa **2,624.27** zimejengwa na kukamilika kwa kiwango cha lami. Aidha, jumla ya kilometa **82.6** za barabara za kupunguza msongamano wa magari katika miji zimejengwa kwa kiwango cha lami na barabara kuu zenye urefu wa kilometa **1,298.44** zinaendelea kujengwa kwa kiwango cha lami. Vilevile, ukarabati wa barabara kuu zenye urefu wa kilometa **300.9** umekamilika.

12. Mheshimiwa Spika, katika kipindi hicho, jumla ya **madaraja makubwa 13** yalikuwa katika hatua mbali mbali za utekelezaji. Kati ya hayo, madaraja makubwa **nane (8)** yamekamilika, ambayo ni Daraja la Magufuli, Magara, Mlalakuwa, Momba, Lukuledi II, Mara, Sibiti na Daraja la Nyerere (Kigamboni). Aidha, **madaraja makubwa matano (5)** yapo katika hatua mbalimbali za ujenzi, ambayo ni Daraja Jipya la Selander, Msingi, Wami, Kitengule na Ruhuhu. **Madaraja makubwa nane (8)** ya Kigongo – Busisi, Sukuma, Simiyu, Mkenda, Mtera, Godegode, Malagarasi Chini na Ugalla yako kwenye hatua mbalimbali za maandalizi ya kazi za ujenzi.

13. Mheshimiwa Spika, Wizara yangu imekamilisha upembuzi yakinifu na usanifu wa kina wa **kilometa 4,856** kwa ajili ya kuanza ujenzi kwa kiwango cha lami wa barabara kuu na za mikoa pamoja na madaraja mapya **12**. Aidha, upembuzi yakinifu wa **kilometa 452.3** kwa ajili ya ukarabati wa barabara kuu na za mikoa kwa kiwango cha lami ulikamilika. Vilevile kazi za upembuzi yakinifu na usanifu wa kina wa

jumla ya **kilometa 3,653.13** upo katika hatua mbalimbali za utekelezaji.

14. Mheshimiwa Spika, Wizara yangu iliendelea kujenga na kuboresha miundombinu ya viwanja vya ndege nchini. Viwanja vya ndege vilivyokamilika ni: Ujenzi wa Jengo la Tatu la Abiria (Terminal III) katika Kiwanja cha Ndege cha Kimataifa cha Julius Nyerere (JNIA) pamoja na ukarabati na uboreshaji wa Kiwanja cha Ndege cha Mwanza. Ujenzi wa Kiwanja cha Ndege cha Kimataifa cha Msalato upo katika hatua ya maandalizi ya kuanza utekelezaji. Aidha, Viwanja vya Ndege vya Songea, Kigoma, Shinyanga, Sumbawanga, Tabora, Iringa na Musoma vipo katika hatua mbalimbali za utekelezaji. Vilevile, kati ya viwanja kumi na moja (11) vilivyofanyiwa upembuzi yakinifu na usanifu wa kina, viwanja **vinne (4)** vya Songea, Musoma, Moshi na Iringa vipo katika hatua mbalimbali za utekelezaji. Serikali inaendelea kutafuta fedha za ujenzi wa Viwanja **saba (7)** vilivyobaki. Viwanja hivyo ni: Lindi, Kilwa Masoko, Singida, Tanga, Simiyu, Lake Manyara na Njombe.

15. Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha kuanzia mwaka 2015 hadi 2020, Wizara yangu imekamilisha kununua jumla ya vivuko **vitatu (3)** ambavyo ni MV Tanga (Pangani – Bweni) mkoani Tanga, MV Kazi (Magogoni – Kigamboni) mkoani Dar es Salaam na MV Mwanza (Kigongo – Busisi) mkoani Mwanza, upanuzi wa Awamu ya kwanza wa Jengo la Abiria upande wa Kigamboni katika kivuko cha Magogoni – Kigamboni, Dar es Salaam. Kwa sasa ununuzi wa Kivuko cha Rugezi – Kisorya pamoja na Awamu ya Pili ya Upanuzi wa Jengo la Abiria upande wa Kigamboni unaendelea.

16. Mheshimiwa Spika, Wizara yangu imekamilisha ujenzi wa jumla ya majengo ya ofisi za Serikali **33** zikiwemo zilizojengwa katika mji wa Serikali Mtumba - Dodoma pamoja na nyumba **323** za Watumishi wa Umma katika mikoa mbalimbali. Aidha, ukarabati wa Karakana sita za kutengeneza samani katika mikoa ya Arusha, Dar es Salaam, Dodoma, Tabora, Mwanza na Mbeya uko katika hatua mbalimbali za utekelezaji.

B-2 SEKTA YA UCHUKUZI

17. Mheshimiwa Spika, kwa upande wa Sekta ya Uchukuzi malengo ya Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2015-2020 yanahusu ujenzi na uboreshaji wa bandari na usafiri katika maziwa;

miundombinu na huduma za reli; huduma za viwanja vya ndege na usafiri wa anga; na huduma za hali ya hewa.

18. Mheshimiwa Spika, katika bandari ya Dar es Salaam, Serikali imekamilisha ujenzi wa Jengo la ghorofa 35 kwa ajili ya kuwaweka pamoja wadau wanaotoa huduma za kibandari. Aidha, kazi ya uboreshaji wa gati namba 1 – 4 na gati la kushusha magari (RoRo) imekamilika. Kazi nyingine zilizokamilika ni ujenzi wa Bandari Kavu ya Kwala (Ruvu), ujenzi wa Bandari ya Nyamisati, awamu ya kwanza ya ukarabati wa gati la kuhudumia mizigo ya Mwambao, ukarabati wa Mnara wa Kuongozea Meli, uwekaji wa mfumo wa ulinzi wa kisasa, mashine za kukagua mizigo (scanners) na Ununuzi wa Mitambo ya kuhudumia mizigo bandarini.

19. Mheshimiwa Spika, kwa upande wa bandari ya Tanga, kazi zilizofanyika ni Ukarabati wa Maghala na Gati namba 1 na 2; kuongeza kina na lango la kuingilia bandarini, ujenzi wa Gati la Pangani na ununuzi wa mitambo ya kuhudumia mizigo. Aidha, kwa upande wa Bandari ya Mtwara, kazi za ujenzi wa uzio na sakafu ngumu katika eneo la mita za mraba 600 zimekamilika na ujenzi wa gati kubwa lenye urefu wa mita 300 umekamilika kwa asilimia 61.

20. Mheshimiwa Spika, kwa upande wa huduma katika maziwa, Ilani ya CCM imetekelezwa kwa kukamilisha ujenzi wa Magati ya Lushamba, Ntama, Magarini, Mwigobero, na Nyamirembe katika Ziwa Victoria; Gati la Kagunga katika Ziwa Tanganyika; na bandari za Kiwira na Itungi katika Ziwa Nyasa pamoja na kununuzi vifaa vya kuhudumia mizigo. Aidha, katika kuboresha huduma za usafiri katika maziwa, Serikali imekamilisha ujenzi wa Tishari 2 zenye uwezo wa kubeba tani za shehena 1,000 kila moja na meli moja yenye uwezo wa kubeba abiria 350 na tani 200 za mizigo ya katika Ziwa Nyasa; Ujenzi wa Chelezo na ukarabati wa meli za MV. Victoria, MV. Butiama, MV. Clarias na ML. Wimbi katika Ziwa Victoria; na ukarabati wa MT. Sangara katika Ziwa Tanganyika. Vile vile, Ujenzi wa Meli mpya ya MV. Mwanza (Hapa Kazi tu) yenye Uwezo wa kubeba abiria 1,200 na tani 400 za mizigo umekamilika kwa asilimia 60.

21. Mheshimiwa Spika, kwa upande wa huduma na miundombinu ya reli ya Kati, kazi zilizokamilika ni pamoja na ujenzi wa Reli ya *Standard Gauge* kutoka Dar es Salaam hadi Morogoro (km 300)

kwa asilimia 76.63 na Morogoro hadi Makutupora (km 422) kwa asilimia 28; ununuzi wa vichwa 11 vipya vya Treni; ukarabati wa mabehewa 367; Upembuzi yakinifu na usanifu wa awali wa ujenzi wa SGR kutoka Mtwara hadi Mbambabay (km 1,000), Tanga – Arusha - Musoma (km 1,023), Kaliua - Mpanda – Karema, Tabora hadi Kigoma (km 411), Uvinza hadi Musongati (km 156), Isaka hadi Kigali (km 356) na reli ya Jijini Dar es Salaam. Aidha, ukarabati wa reli ya Tanga hadi Moshi (Km 359) umekamilika na huduma zimeanza kutolewa Disemba 2019 na ukarabati wa reli ya Dar es Salaam hadi Isaka (Km 970) umekamilika kwa asilimia 86. Kwa upande wa TAZARA iliyokamilika ni ununuzi wa vichwa vipya vinne (4) vya Treni ya njia kuu, vichwa vinne (4) vya sogeza, mabehewa mapya 18 ya abiria, ukarabati wa mabehewa 400 ya mizigo, uboreshaji wa Kituo cha Reli cha Fuga na nyumba Nyumba nane (8) za watumishi kwa ajili ya kuhudumia Mradi mkubwa wa Umeme wa Mto Rufiji.

22. Mheshimiwa Spika, kwa upande wa usafiri wa Anga, kazi zilizofanyika ni pamoja na ufufuaji wa Kampuni ya Ndege Tanzania kwa kununua Ndege 11 ambapo Ndege nane (8) zimewasili na zinaendelea kutoa huduma; ufungaji wa Rada nne (4) za kuongozea Ndege, ukarabati wa Mnara wa kuongozea Ndege katika Kiwanja cha Pemba, ujenzi wa Jengo la Tatu la Abiria katika Kiwanja cha Ndege cha Julius Nyerere (JNIA), ukarabati wa Jengo la abiria KIA, Ununuzi wa Magari mapya matatu (3) ya Zimamoto, na ufungaji wa Mifumo ya kuongozea Ndege (AGL) katika Viwanja vya Ndege vya Dodoma, Tabora na Mwanza. Aidha, huduma za hali ya hewa zimeboreshwa kwa ununuzi wa Rada tatu (3) kwa ajili ya kufungwa Mikoja ya Mtwara, Mbeya na Kigoma.

23. Mheshimiwa Spika, Wizara imeendelea kushirikiana na Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto pamoja vyombo mbalimbali vikiwemo vya Ulinzi na Usalama katika kudhibiti maambukizi ya virusi vya Corona (COVID - 19) kwa wageni wote wanaoingia nchini.

B-3 SEKTA YA MAWASILIANO

24. Mheshimiwa Spika, Serikali imeweza kufikisha huduma za mawasiliano katika kata **703** zenye vijiji **2,501**. Vile vile, Serikali imejenga vituo vya kijamii vya kutoa huduma za TEHAMA, vikiwemo vituo 10 Zanzibar na vituo 8 Tanzania Bara. Aidha, laini za simu za

viganjani zimeongezeka kutoka laini milioni 39 mwaka 2015 hadi laini milioni 43 Machi, 2020 na idadi ya watumiaji wa intaneti iliongezeka kutoka milioni 9 mwaka 2015 hadi kufikia milioni 25 Machi, 2020.

25. Mheshimiwa Spika, kwa upande wa ujenzi wa Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano, Awamu ya III ulikamilika Juni, 2016 ukijumuisha ujenzi wa kituo cha Taifa cha *Data* cha Dar es Salaam, uunganishwaji wa Zanzibar kwenye Mkongo wa Taifa; pamoja na upanuzi wa Mkongo uliojengwa Awamu ya kwanza na ya pili. Aidha, kupitia utekelezaji wa mradi kwa kushirikiana na watoa huduma binafsi, miundombinu ya Mkongo imefikishwa kwenye Ofisi za Halmashauri za Wilaya 150, Hospitali za Wilaya 150, Vituo vya Polisi 121, Vituo vya Posta 65, Mahakama 25 na kutoa huduma ya intaneti bure kwenye Shule za Sekondari 455, kuanzisha mradi wa shule mtandao (e-Schools) ambao unatekeleza mpango wa Taifa wa kuunganisha shule pamoja na kuunganisha mifumo ya mikutano mtandao (Video Conference Systems) ambapo vituo 43 vimeunganishwa katika mikoa ya Tanzania Bara na Zanzibar.

C. MAPITIO YA UTEKELEZAJI WA MPANGO NA BAJETI YA WIZARA NA TAASISI ZAKE KWA MWAKA WA FEDHA 2019/20

C.1 UTEKELEZAJI WA MPANGO NA BAJETI YA WIZARA KISEKTA

26. Mheshimiwa Spika, katika sehemu hii, nitaeleza kuhusu utekelezaji wa Mpango na Bajeti ya Wizara kwa mwaka wa fedha 2019/20 kwa kila sekta kwa mtiririko, nikianzia na Sekta ya Ujenzi, Sekta ya Uchukuzi na hatimaye Sekta ya Mawasiliano.

C.1.1 SEKTA YA UJENZI

Bajeti ya Matumizi ya Kawaida

27. Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2019/20, Wizara (Ujenzi) ilitengewa kiasi cha Shilingi **36,264,751,504.04** kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida. Kati ya fedha hizo, Shilingi **33,788,265,000.00** ni kwa ajili ya Mishahara ya Watumishi wa Wizara na Taasisi zake na Shilingi **2,476,486,544.04** ni kwa ajili ya Matumizi Mengineyo ya Wizara na Taasisi zake. Aidha, Bajeti ya Matumizi ya kawaida imeongezewa wigo kutoka **Shilingi 36,142,664,000.00** hadi **Shilingi 36,264,751,504.04** sawa na

ongezeko la **Shilingi 122,087,544.04**. Ongezeko hili ni kwa ajili ya malipo ya madeni ya Wazabuni mbalimbali ambayo yamehakikiwa na Wizara ya Fedha na Mipango.

Hadi Machi, 2020 jumla ya **Shilingi 24,128,094,762.08** zilikuwa zimetolewa na HAZINA kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida, sawa na asilimia **66.53** ya kiasi kilichoidhinishwa na Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Kati ya fedha hizo, **Shilingi 22,111,449,258.04** ni kwa ajili ya Mishahara ya Watumishi wa Wizara na Taasisi na **Shilingi 2,016,645,504.04** ni kwa ajili ya Matumizi Mengineyo ya Wizara na Taasisi.

Bajeti ya Miradi ya Maendeleo

28. Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2019/20, Sekta ya Ujenzi ilitengewa **Shilingi 1,294,051,604,268.00** kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo. Kati ya fedha hizo, **Shilingi 990,000,000,000.00** ni fedha za ndani na **Shilingi 304,051,604,268.00** zilikuwa ni fedha za nje. Fedha za ndani zilijumuisha fedha za Mfuko Mkuu wa Serikali (Consolidated Funds) **Shilingi 402,611,000,000.00** na fedha za Mfuko wa Barabara **Shilingi 587,389,000,000.00**. Aidha, Bajeti ya fedha za ndani za miradi ya maendeleo imeongezewa wigo kutoka **Shilingi 990,000,000,000.00** hadi **Shilingi 1,713,862,494,259.91** sawa na ongezeko la **Shilingi 723,862,494,259.91**. Ongezeko hili ni kwa ajili ya malipo ya madeni na madai ya Makandarasi na Wahandisi Washauri yaliyohakikiwa na Wizara ya Fedha na Mipango. Hivyo, jumla ya fedha za maendeleo zilizoidhinishwa ni **Shilingi 2,017,914,098,527.91**.

Hadi Machi, 2020 fedha zilizopokelewa ni **Shilingi 1,663,224,452,809.45**. Kati ya fedha hizo, **Shilingi 1,387,232,923,133.44** ni fedha za ndani na **Shilingi 275,991,529,676.01** ni fedha za nje. Fedha za ndani zilizopokelewa zinajumuisha **Shilingi 936,146,859,501.27** kutoka Mfuko Mkuu wa Serikali na **Shilingi 451,086,063,632.17** ni fedha za Mfuko wa Barabara. Kwa ujumla, hadi kufikia Machi, 2020 fedha za maendeleo zilizotolewa ni sawa na asilimia **82.42** ya fedha zilizoidhinishwa na Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo kwa mwaka wa fedha 2019/20.

UTEKELEZAJI WA MIRADI YA MAENDELEO

Miradi ya Barabara na Madaraja

29. Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2019/20, Wizara kupitia Wakala wa Barabara Tanzania (TANROADS) ilipanga kujenga barabara zenye urefu wa **kilometa 432.30** kwa kiwango cha lami, ujenzi wa madaraja **13** pamoja na ukarabati wa **kilometa 56** kwa kiwango cha lami katika barabara kuu.

Hadi kufikia Machi, 2020, jumla ya **kilometa 405.7** za barabara kuu zimekamilika kujengwa kwa kiwango cha lami na jumla ya **kilometa 16.2** za barabara kuu zimekarabatiwa kwa kiwango cha lami. Aidha, ujenzi wa madaraja mawili (**2**) umekamilika na ujenzi wa madaraja **11** ulikuwa katika hatua mbalimbali za utekelezaji.

30. Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2019/20 Wizara kupitia TANROADS ilipanga kujenga kwa kiwango cha lami barabara za mikoa zenye urefu wa **kilometa 72.01** ambapo **kilometa 40.81** zilipangwa kujengwa kwa kutumia fedha za Mfuko Mkuu wa Serikali na **kilometa 31.20** zilipangwa kujengwa kwa kutumia fedha za Mfuko wa Barabara. Aidha, **kilometa 893.04** zilipangwa kukarabatiwa kwa kiwango cha changarawe ambapo kati ya hizo ilipangwa **kilometa 486.03** na madaraja **12** kukarabatiwa kwa kutumia fedha za Mfuko Mkuu wa Serikali na ilipangwa **kilometa 407.01** pamoja na madaraja **15** kujengwa/kukarabatiwa kwa kutumia fedha za Mfuko wa Barabara.

Hadi Machi, 2020 jumla ya kilometa **24.23** za barabara za mikoa zilijengwa kwa kiwango cha lami na jumla ya kilometa **255.21** zilifanyiwa ukarabati kwa kiwango cha changarawe na ujenzi wa madaraja ulikuwa katika hatua mbalimbali za utekelezaji.

31. Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2019/20 Wizara ilipanga kufanya matengenezo ya barabara kuu na barabara za mikoa ambayo yanahusisha matengenezo ya kawaida (routine and recurrent maintenance) kwa kilometa **32,944.31**, matengenezo ya muda maalum na sehemu korofi ya kilometa **5,031.14** na matengenezo ya madaraja **3,376**. Mpango huu pia unajumuisha shughuli za udhibiti wa uzito wa magari na ulinzi wa hifadhi za barabara, kazi za dharura pamoja na mradi wa matengenezo ya barabara kwa mikataba ya muda mrefu.

Hadi Machi, 2020 utekelezaji wa matengenezo katika barabara kuu na za mikoa ulifikia kilometa **17,134.14**, matengenezo ya muda maalum na sehemu korofi kilometa **2,820.08** na matengenezo ya madaraja **1,695**.

32. Mheshimiwa Spika, Wizara kupitia TANROADS iliendelea na kazi ya kudhibiti uzito wa magari kwa kutumia mizani **55** ya kudumu na **17** inayohamishika katika barabara kuu za lami. Hadi kufikia Machi, 2020, magari **3,297,187** yalikuwa yamepimwa ambapo kati ya hayo, magari **948,247** sawa na asilimia **29** yalikuwa yamezidisha uzito. Jumla ya **Shilingi 3,147,619,811** zilikusanywa kutokana na tozo ya uzidishaji uzito unaoruhusiwa kupita barabarani. Aidha, Wizara inaendelea na utoaji wa vibali vya mizigo maalum nchini. Hadi Machi, 2020 jumla ya **Shilingi 13,661,292,803.00** zilikusanywa kutokana na tozo ya upitishaji wa mizigo maalum.

33. Mheshimiwa Spika, utekelezaji wa miradi ya barabara hadi Machi, 2020 ilikuwa ni kama ifuatavyo:

34. Mheshimiwa Spika, mradi wa ujenzi wa **Barabara za Kuelekea kwenye mradi wa Kufua Umeme katika Maporomoko ya Mto Rufiji;** hadi Machi, 2020 maandalizi ya ujenzi kwa kiwango cha lami wa sehemu ya barabara ya Bigwa – Kisaki (km 50) yalikuwa yanaendelea.

35. Mheshimiwa Spika, katika mradi wa ujenzi wa barabara ya **Dar es Salaam – Chalinze – Morogoro – Dodoma (km 467.9)**, mkataba kwa ajili ya mradi wa ujenzi wa barabara ya **Ubena Zomozi – Ngerengere** kwa kiwango cha lami, kazi ya usanifu wa kina na utayarishaji wa nyaraka za zabuni zimekamilika. Mkataba wa ujenzi wa kilometa 0.7 za barabara ya **Kwa Mathias – Msangani (km 8.3)** umesainiwa na Mkandarasi yupo kwenye maandalizi ya awali (mobilization) ya ujenzi. Kwa upande wa upembuzi yakinifu na usanifu wa kina wa barabara ya **Morogoro – Dodoma (km 256)**, taratibu za manunuzi kwa ajili ya kumpata Mhandisi Mshauri wa kufanya kazi hizo zinaendelea.

36. Mheshimiwa Spika, ujenzi wa barabara ya **Wazo Hill – Bagamoyo – Msata** sehemu ya **Tegeta – Bagamoyo (km 46.9)**, **Mbegani – Bagamoyo (km 7.2)** na **Makofia – Mlandizi (km 36.7)**,

kazi za upembuzi yakinifu na usanifu wa kina zimekamilika na Serikali inaendelea kutafuta fedha za ujenzi.

Kazi za ujenzi kwa kiwango cha lami wa barabara za **TAMCO – Vikawe – Mapinga (km 24)** na **Kisarawe – Maneromango (km 54)** zinaendelea. Mkataba wa ujenzi wa sehemu ya **Tanga – Pangani (km 50)** umesainiwa na Mkandarasi anaendelea na maandalizi ya awali (mobilization) ya kuanza kazi za ujenzi. Aidha, Benki ya Maendeleo ya Afrika (AfDB) imekubali kutoa fedha za mkopo nafuu kwa ajili ya ujenzi wa daraja la Pangani na barabara za lami zenye urefu wa kilometa 124.5 kutoka Pangani hadi Mkange. Majadiliano kuhusu mkopo huo yamekamilika na mkataba wa mkopo umesainiwa tarehe 13 Machi, 2020.

37. Mheshimiwa Spika, katika mradi wa ujenzi kwa kiwango cha lami wa barabara ya **Usagara – Geita – Buzirayombo – Kyamyorwa**, usanifu wa kina na utayarishaji wa nyaraka za zabuni kwa ajili ya ujenzi kwa kiwango cha lami umekamilika kwa sehemu ya **Geita – Bulyanhulu Junction (km 58.3)**, **Bulyanhulu Junction – Kahama (km 61.7)** na **Nyamirembe Port – Katoke (km 50)**. Taratibu za kutangaza zabuni za ujenzi zinasubiri upatikanaji wa fedha.

38. Mheshimiwa Spika, hadi Machi 2020, katika barabara ya **Kigoma – Kidahwe – Uvinza – Kaliua – Tabora**, ujenzi kwa kiwango cha lami wa barabara ya **Urambo – Kaliua (km 28)** ulikuwa umefikia asilimia 80 na Mhandisi Mshauri kwa ajili ya ujenzi wa barabara ya **Uvinza – Malagarasi (km 51.1)** anaendelea na kazi ya kufanya mapitio ya usanifu na makabrasha ya zabuni za kazi za ujenzi. Aidha, mkataba wa ujenzi kwa kiwango cha lami wa barabara ya **Chagu – Kazilambwa (km 36)** umesainiwa na Mkandarasi yuko katika maandalizi ya kuanza kazi.

39. Mheshimiwa Spika, katika mradi wa barabara ya **Marangu – Tarakea – Rongai – Kamwanga na Bomang’ombe – Sanya Juu**, hadi Machi, 2020 ujenzi kwa kiwango cha lami kwa sehemu ya **Sanya Juu – Elerai (km 32.2)** umekamilika. Aidha, ujenzi kwa kiwango cha lami mita 800 za barabara ya **Kiboroloni – Kiharara – Tsuduni – Kidia (km 10.8)** umekamilika na ujenzi wa kilometa 1.4 kati ya kilometa 3.5 zilizobaki katika barabara ya **Kwa Sadala – Masama – Machame Junction (km 16)** umekamilika. Aidha, ujenzi kwa kiwango cha lami

wa kilometa 3 zilizobaki kati ya kilometa 14 za barabara ya **Kijenge – Usa River (Nelson Mandela AIST)** kwa kiwango cha lami unaendelea na maandalizi kwa ajili ya ujenzi wa sehemu ya **Mianzini – Ngaramtoni (km 18)** yanaendelea.

40. Mheshimiwa Spika, mradi wa upanuzi wa barabara ya **Arusha – Moshi – Himo – Holili (sehemu ya Tengeru – Moshi – Himo (km 105.0) pamoja na mizani ya Himo)**, mazungumzo kati ya Serikali na JICA kwa ajili ya kupata fedha za upanuzi wa barabara hii yanaendelea.

41. Mheshimiwa Spika, mradi wa barabara ya **Dodoma – Manyoni** unahusisha ujenzi wa Kituo cha Ukaguzi wa Pamoja (One Stop Inspection Station - OSIS) cha Muhalala (Manyoni) pamoja na ujenzi wa mizani inayopima uzito wa magari yakiwa kwenye mwendo (WIM) eneo la Nala Mkoani Dodoma. Hadi Machi, 2020 kazi za ujenzi wa Kituo cha Ukaguzi wa Pamoja (OSIS) cha Muhalala unaofadhiliwa na Jumuiya ya Ulaya (EU) bado zimesimama. Serikali inaendelea na majadiliano na Mkandarasi ili kufikia maridhiano kwa ajili ya kuendelea na kazi za ujenzi. Aidha, ununuzi wa mizani ya kupima magari yakiwa kwenye mwendo (Weigh in Motion – WIM) umefanyika na imejengwa kwenye eneo la Nala (Dodoma).

42. Mheshimiwa Spika, hadi Machi, 2020, utekelezaji wa mradi wa barabara ya **Dumila – Kilosa - Mikumi** sehemu ya **Rudewa – Kilosa (km 24)** ulikuwa umefikia asilimia 20.

43. Mheshimiwa Spika, hadi Machi, 2020 ujenzi kwa kiwango cha lami wa barabara ya **Sumbawanga – Matai – Kasanga Port (km 112)**, ulikuwa umefikia asilimia 95 ambapo kilometa 106 zimejengwa kwa kiwango cha lami na kazi za ujenzi zinaendelea. Aidha, taratibu za manunuzi kwa ajili ya kumpata Mkandarasi wa ujenzi kwa kiwango cha lami sehemu ya **Matai – Kasesya (km 50)** zinasubiri upatikanaji wa fedha.

44. Mheshimiwa Spika, utekelezaji wa mradi wa **ujenzi wa madaraja makubwa** uliendelea katika mwaka wa fedha 2019/20. Hadi Machi, 2020 ujenzi wa madaraja ya Mara na Magara umekamilika. Madaraja ambayo ujenzi wake unaendelea ni pamoja na ujenzi wa nguzo za daraja la Ruhuhu (asilimia 85), Mitomoni (asilimia 75), Kitengule (asilimia 50), Msingi (asilimia 40), Selander (asilimia 34) na

Wami (asilimia 53). Aidha, Mkandarasi anajiandaa kuanza kazi za nyongeza za kuweka lami kwenye barabara unganishi kwa daraja la Sibiti; Mkandarasi wa ujenzi wa daraja la Kigongo - Busisi amepatikana na yupo kwenye maandalizi (mobilization) ya kuanza ujenzi; taratibu za manunuzi kwa ajili ya kumpata Mkandarasi wa kufanya ukarabati wa daraja la Kirumi na kuanza ujenzi wa daraja la Sukuma zinaendelea na usanifu wa kina wa madaraja ya Mzinga, Mkenda na Ugalla umekamilika.

45. Mheshimiwa Spika, kazi nyingine zinazoendelea ni upembuzi yakinifu kwa ajili ya ujenzi wa madaraja ya Mtera na Godegode pamoja na taratibu za manunuzi kwa ajili ya kuwapata Wahandisi Washauri watakaofanya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina wa madaraja ya Malagarasi Chini na Mkundi. Aidha, taratibu za manunuzi kwa ajili ya kumpata mzabuni (supplier) wa madaraja ya chuma (*Mabey Compact Bridges*) zilikuwa katika hatua ya mwisho.

46. Mheshimiwa Spika, kazi ya usanifu wa awali (Preliminary Design) ili kuwezesha utaratibu wa Kusanifu na Kujenga (Design & Build) kwa daraja la Simiyu imekamilika. Hata hivyo, mpango wa ujenzi wa daraja la Simiyu pamoja na barabara ya Nyanguge – Simiyu/Mara Border uliingizwa kwenye programu ya Benki ya Dunia ya kuimarisha barabara zinazounganisha bandari zilizoko ukanda wa Ziwa Victoria (Lake Victoria Transport Programme - LVTP). Hadi Machi, 2020 Serikali ilikuwa imekamilisha majibu ya hoja zilizotolewa na Benki ya Dunia na inasubiri idhini (No Objection) ya Benki ya kuendelea na programu hiyo.

47. Mheshimiwa Spika, hadi Machi, 2020 katika mradi wa barabara ya **New Bagamoyo (Morocco Junction - Mwenge – Tegeta: km 18.3)**, kazi za upanuzi wa sehemu ya **Morocco – Mwenge (km 4.3)** zilikuwa zimefikia asilimia 44 na uboreshaji wa mifereji ya maji ya mvua sehemu ya Mwenge – Tegeta (km 14.0) ulikuwa unaendelea.

48. Mheshimiwa Spika, katika mradi wa ujenzi wa barabara ya **Kyaka – Bugene – Kasulo**, hadi Machi, 2020 taratibu za mapitio ya usanifu wa kina kwa sehemu ya **Bugene – Kasulo (km 124.0)**, Upembuzi yakinifu na usanifu wa kina wa sehemu ya **Kumunazi – Kasulo (km 9)** na **Kyaka – Mutukula (km 30)** kwa upande wa Tanzania na sehemu ya Mutukula – Masaka (km 89.1) kwa upande wa Uganda chini ya ufadhili wa Benki ya Maendeleo ya Afrika (AfDB)

zilikwa zinaendelea. Mhandisi Mshauri alikuwa anakamilisha taarifa ya mwisho. Aidha, Serikali inaendelea kutafuta fedha kwa ajili ya ujenzi kwa kiwango cha lami wa barabara ya **Omugakorongo – Kigarama – Murongo (km 105)** baada ya kukamilika kwa upembuzi yakinifu na usanifu wa kina.

49. Mheshimiwa Spika, hadi Machi, 2020 katika barabara ya **Isaka – Lusahunga – Rusumo**, kazi ya ukarabati wa sehemu ya **Ushirombo – Lusahunga (km 110)** imekamilika na kazi ya matengenezo ya dharura katika sehemu korofi kwenye sehemu ya **Lusahunga – Rusumo (km 92)** ilikuwa inaendelea. Aidha, Benki ya Dunia imeonyesha nia ya kugharamia ukarabati wa barabara ya **Lusahunga – Rusumo (km 92)** kwa kiwango cha lami chini ya programu ya *Development Corridor Transport Programme (DCTP)*. Nyaraka za zabuni kwa ajili ya ujenzi zilikuwa zimewasilishwa Benki ya Dunia kwa ajili ya kupata kibali cha kutangaza zabuni.

Kwa upande wa Kituo cha Ukaguzi wa Pamoja (OSIS) cha Nyakanazi, kazi za ujenzi bado zimesimama. Kwa sasa Serikali inajadiliana na Mkandarasi ili kufikia maridhiano kwa ajili ya kuendelea na kazi za ujenzi.

Kwa upande wa barabara ya **Nyakahura – Kumubuga – Murusagamba/Rulenge – Murugarama** na barabara ya **Rulenge – Kabanga Nickel** zenye jumla ya kilometa 141, upembuzi yakinifu na usanifu wa kina ulikuwa unaendelea chini ya ufadhili wa Benki ya Maendeleo ya Afrika (AfDB).

50. Mheshimiwa Spika, hadi kufikia Machi, 2020 katika mradi wa barabara ya **Manyoni – Itigi – Tabora**, ujenzi wa sehemu za **Manyoni – Itigi – Chaya (km 89.35)** na **Tabora – Nyahua (km 85)** umekamilika. Aidha, sehemu ya **Chaya – Nyahua (km 85.4)** kazi ya ujenzi kwa kiwango cha lami ilikuwa imefikia asilimia 65.

51. Mheshimiwa Spika, zabuni kwa ajili ya kumpata Mhandisi Mshauri wa kufanya kazi za usanifu wa kina kwa ajili ya ukarabati kwa kiwango cha lami wa barabara ya **Mwanza/Shinyanga Border – Mwanza** zilitangazwa upya Machi, 2020 baada ya Kampuni iliyopatikana awali kuwa na gharama kubwa.

52. Mheshimiwa Spika, katika mradi wa barabara za kupunguza msongamano wa magari katika jiji la Dar es Salaam; miradi inayoendelea ni ujenzi kwa kiwango cha lami barabara ya **Kibamba – Kisopwa – Kwembe – Makondeko (km 14.66)** ambapo hadi Machi, 2020 kazi za ujenzi wa barabara hii sehemu ya **Kibamba – Mloganzila (km 4.0)** zilikuwa zimekamilika. Aidha, ujenzi wa sehemu ya **Mloganzila – Kisopwa (km 1)** unasubiri upatikanaji wa fedha. Mradi mwingine unaoendelea ni ujenzi wa barabara ya **Banana – Kitunda – Kivule – Msongola (km 14.7)** ambapo hadi Machi, 2020 kazi za ujenzi wa sehemu ya **Kitunda– Kivule (km 3.2)** zilikuwa zimefikia asilimia 40.

Mkataba wa ujenzi wa barabara ya **Wazo Hill – Madale (km 6)** umeshasainiwa na Mkandarasi anaendelea na maandalizi ya kuanza kazi za ujenzi. Kwa barabara ya **Ardhi – Makongo – Goba (km 9)**, kazi za ujenzi wa sehemu ya **Goba – Makongo (km 4)** zimekamilika. Ujenzi wa sehemu ya **Ardhi – Makongo (km 5)** unasubiri ulipaji wa fidia. Vilevile, kazi ya usanifu wa kina na utayarishaji wa nyaraka za zabuni zimekamilika kwa ajili ya ujenzi kwa kiwango cha lami wa barabara za **Mjimwema – Kimbiji (km 27.0)** na **Kongowe – Mjimwema – Kivukoni (km 25.1)** ambapo Serikali inaendelea kutafuta fedha kwa ajili ya kuanza ujenzi. Taratibu za kutangaza zabuni kwa ajili ya ujenzi wa barabara ya **Mwai Kibaki (km 9.1); Kawe round about – Garden Rd Junction (km 2.9)** zinasubiri upatikanaji wa fedha.

53. Mheshimiwa Spika, katika barabara ya **Kidatu - Ifakara – Lupiro – Mahenge/Malinyi – Londo – Lumecha/Songea**, kazi ya ujenzi kwa kiwango cha lami wa barabara ya **Kidatu – Ifakara (km 66.0)** inaendelea na imefikia asilimia 12. Aidha, Serikali inaendelea kutafuta fedha za ujenzi wa barabara za **Ifakara – Kihansi – Mlimba – Taweta/Madeke (km 220.22)**, sehemu ya **Ifakara – Kihansi (km 126.74)** na **Ifakara – Lupiro – Malinyi – Londo – Lumecha (km 396)**.

54. Mheshimiwa Spika, hadi Machi, 2020 katika mradi wa barabara ya **Tabora – Ipole – Koga – Mpanda**, kazi za ujenzi kwa kiwango cha lami kwa sehemu ya **Tabora – Sikonge (Usesula - km 30)** zimekamilika. Kwa sehemu ya **Sikonge (Usesula) – Ipole – Koga – Mpanda (km 359)**, ujenzi wa barabara hii kwa kiwango cha lami kwa sehemu ya **Usesula – Komanga (km 108)** na **barabara ya kuingia mji wa Sikonge, (km 7.5)** umefikia asilimia 40, **Komanga – Kasinde (km 108)** na **barabara ya kuingia mji wa Inyonga (km 4.8)** umefikia

asilimia 56 na **Kasinde – Mpanda (km 108)** na **barabara ya kuingia mji wa Urwira (km 3.7)** umefikia asilimia 44.5.

55. Mheshimiwa Spika, mradi wa ujenzi wa barabara ya **Makutano – Natta – Mugumu – Loliondo na Loliondo – Mto wa Mbu** umeendelea kutekelezwa ambapo hadi Machi, 2020 ujenzi kwa kiwango cha lami wa sehemu ya **Makutano – Sanzate (km 50)** ulikuwa umefikia asilimia 82.5. Kwa upande wa sehemu ya **Sanzate - Natta (km 40)**, taratibu za kumpata Mkandarasi wa ujenzi zilikuwa zinaendelea na ujenzi wa sehemu ya **Natta – Mugumu (km 45)** unasubiri upatikanaji wa fedha. Aidha, ujenzi wa barabara ya **Loliondo – Mto wa Mbu** (sehemu ya Waso – Sale: km 49) ulikuwa umefikia asilimia 46 na kazi za upembuzi yakinifu na usanifu wa awali wa ujenzi kwa kiwango cha lami wa barabara ya **Karatu – Mbulu - Hydrom – Sibiti River – Lalago – Maswa (km 389)** zilikuwa katika hatua za mwisho. Serikali inaendelea kutafuta fedha za ujenzi wa sehemu ya **Mbulu – Hydrom (km 50)**.

56. Mheshimiwa Spika, katika barabara ya **Ibanda – Itungi/Kiwira**, hadi Machi, 2020 kazi ya ujenzi wa barabara ya **Kikusya – Ipinda – Matema Beach (km 39)**, sehemu ya **Tenende – Matema (km 34.6)** na kilometa 10 za sehemu ya **Bujesi – Mbambo (km 15)** kwa kiwango cha lami zilikuwa zimekamilika. Kazi za ujenzi wa kilometa 5 zilizobaki kwenye mradi wa **Bujesi – Mbambo (km 15)** na **Tukuyu – Mbambo (km 17.0)** zimeanza na zilikuwa zimefikia asilimia 7.

57. Mheshimiwa Spika, ujenzi wa barabara ya **Nzega – Tabora (km 115)** kwa kiwango cha lami umekamilika. Aidha, hadi Machi, 2020, taratibu za manunuzi kwa ajili ya kumpata Mhandisi Mshauri wa kufanya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina kwa ajili ya ukarabati wa barabara ya **Shelui – Nzega (km 110)** kwa kiwango cha lami zilikuwa zinaendelea.

58. Mheshimiwa Spika, hadi Machi, 2020 barabara ya **Sumbawanga – Mpanda – Kanyani – Nyakanazi**, sehemu ya **Mpanda – Ifukutwa – Vikonge (km 37.65)** ujenzi umefikia asilimia 87, ambapo kilometa 28.64 zimekamilika kwa kiwango cha lami. Aidha, ujenzi wa sehemu za **Kibaoni – Sitalike (km 71.0)**, **Kizi – Lyambalyamfipa – Sitalike (km 86.31)**, **Namanyere – New Katongoro Port (km 64.8)** na **Vikonge – Magunga – Uvinza (km 159.0)** unasubiri upatikanaji wa fedha.

59. Mheshimiwa Spika, hadi Machi, 2020 miradi ya ukarabati wa barabara ya **Nyanguge – Musoma,** sehemu ya **Nyanguge – Simiyu/Mara Border (km 100.4)** na ujenzi wa **daraja la Simiyu** ilikuwa haijaanza. Hata hivyo, miradi hii imejumuishwa kwenye programu ya Benki ya Dunia ya kuimarisha barabara zinazounganisha bandari zilizoko ukanda wa Ziwa Victoria (Lake Victoria Transport Programme - LVTP). Serikali ilikuwa inasubiri idhini (No Objection) ya Benki ya Dunia kuendelea na miradi hii.

Katika barabara ya **Nansio – Kisorya – Bunda – Nyamuswa;** sehemu ya **Bulamba –Kisorya (km 51),** kazi za ujenzi zimekamilika kwa asilimia 84. Aidha, Mkandarasi wa ujenzi wa sehemu ya **Nyamuswa – Bunda – Bulamba (km 55.0)** anaendelea na maandalizi ya kuanza ujenzi (mobilization).

Vilevile, hadi Machi, 2020 kazi za upanuzi wa **barabara ya kwenda Kiwanja cha Ndege cha Mwanza (km 12)** na ukarabati wa barabara ya **Makutano – Sirari (km 83)** zimekamilika. Aidha, kwa barabara ya **Musoma – Makojo – Busekela (km 92),** kazi za ujenzi wa sehemu ya **Suguti – Kusenyi (km 5)** zilikuwa zinaendelea.

60. Mheshimiwa Spika, mradi wa barabara ya **Magole – Turiani – Mziha,** unaendelea ambapo hadi Machi, 2020 ujenzi wa sehemu ya **Magole – Turiani (km 45.2)** kwa kiwango cha lami umekamilika. Aidha, Serikali inaendelea kutafuta fedha kwa ajili ya ujenzi wa sehemu ya **Turiani – Mziha – Handeni (km 104).**

61. Mheshimiwa Spika, hadi Machi, 2020, mradi wa ujenzi wa **barabara za juu (flyovers/interchange) na maboresho ya makutano ya barabara katika jiji la Dar es Salaam** ulikuwa unaendelea. Katika kipindi hicho, ujenzi wa barabara za juu (**Interchange**) **katika makutano ya Ubungo** umefikia asilimia 70. Aidha, usanifu wa kina kwa ajili ya kuboresha makutano ya barabara katika maeneo ya *Fire*, Magomeni, Mwenge, Tabata/Mandela, Morocco, Buguruni pamoja na makutano ya barabara za Kinondoni/Ali Hassan Mwinyi na Selander (Ali Hassan Mwinyi/UN Road Junction) ulikamilika. Hivi sasa tathmini ya fidia kwa watakapoathirika na utekelezaji wa mradi inaendelea. Vilevile, maandalizi ya ujenzi wa *Mabey Flyovers* katika Jiji la Dar es Salaam, Dodoma na Mwanza yanaendelea.

62. Mheshimiwa Spika, katika barabara ya **Mwigumbi – Maswa**

- **Bariadi – Lamadi**, ujenzi kwa kiwango cha lami wa sehemu ya **Maswa – Bariadi (km 49.7)** ulifikia asilimia 77.6. Aidha, ujenzi kwa kiwango cha lami wa barabara za **Kolandoto – Mwanhuzi (km 10)**, **Lalago – Ng’oboko – Mwanhuzi (km 74)** na **Isabdula (Magu) – Bukwimba – Ngudu – Ng’hungumalwa (km 10)** unasubiri upatikanaji wa fedha.

63. Mheshimiwa Spika, hadi Machi, 2020 kazi za upembuzi yakinifu na usanifu wa kina wa barabara ya **Tabora - Ipole – Rungwa (km 172)**, zilikuwa zimekamilika. Serikali inaendelea kutafuta fedha kwa ajili ya ujenzi kwa kiwango cha lami.

64. Mheshimiwa Spika, hadi Machi, 2020 ujenzi wa barabara ya **Kidahwe – Kibondo – Nyakanazi**, uliendelea ambapo kazi za ujenzi kwa kiwango cha lami kwa sehemu ya **Kidahwe – Kasulu (km 63)** zilikuwa zimefikia asilimia 98.5 na kwa sehemu ya **Nyakanazi – Kibondo (km 50)** zimefikia asilimia 78. Aidha, mikataba minne ya ujenzi kwa kiwango cha lami wa barabara ya **Kakonko (Kabingo) – Kibondo – Kasulu – Manyovu (km 260)** imesainiwa na makandarasi wapo kwenye maandalizi ya kuanza ujenzi. Mkandarasi wa ujenzi wa sehemu ya **Nduta Junction – Kibondo (km 25.6)** amepatikana na anaendelea na maandalizi ya kuanza kazi za ujenzi.

65. Mheshimiwa Spika, kwa upande wa mradi wa barabara ya **Chuo Kikuu cha Dodoma (km 12)**, hadi Machi, 2020, kazi za ujenzi kwa kiwango cha lami kwa barabara hii zimekamilika. Aidha, ujenzi wa **barabara za Ikulu Chamwino** ulikuwa unaendelea. Kwa upande wa **barabara ya pete ya Dodoma (km 112.3)** hatua za manunuzi za kuwapata Makandarasi na Wahandisi Washauri kwa ajili ya kuanza ujenzi zilikuwa zinaendelea.

66. Mheshimiwa Spika, hadi Machi, 2020 katika mradi wa ujenzi wa **daraja la Nyerere (Kigamboni) na barabara unganishi**, ujenzi wa daraja umekamilika na ujenzi wa barabara unganishi za daraja unaendelea. Vilevile, upembuzi yakinifu na usanifu wa kina wa barabara za **Tungi – Kibada (km 3.8)** na **Kibada – Mwasonga – Tundwisongani – Kimbiji (km 41)** umekamilika.

67. Mheshimiwa Spika, mradi wa ujenzi wa **njia za magari mazito na maegesho ya dharura katika Ushoroba wa Kati** umepangwa kujumuishwa kwenye kazi za upembuzi yakinifu na usanifu wa kina wa ukarabati wa barabara za ushoroba wa kati.

Barabara hizo ni **Morogoro – Dodoma (km 260)**, **Singida – Shelui (km 108)** na **Shelui – Nzega (km 110)** ambazo ziko katika hatua za manunuzi za kuwapata Wahandisi Washauri.

68. Mheshimiwa Spika, mradi wa barabara ya **Kimara – Kibaha (km 25.7)** unahusisha upanuzi wa sehemu ya **Kimara – Kiluvya (km 19.2)** kuwa njia nane ikijumuisha **upanuzi wa madaraja ya Kibamba, Kiluvya na Mpiji**. Hadi Machi, 2020 kazi za upanuzi zimefikia asilimia 74.

69. Mheshimiwa Spika, kazi ya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina barabara ya mzunguko ya **Pugu – Kifuru - Mbezi Mwisho – Mpiji Magoe – Bunju (km 34)**, kwa ajili ya kuijenga kuwa njia sita itaanza kulingana na upatikanaji wa fedha.

70. Mheshimiwa Spika, hadi Machi, 2020 ujenzi kwa kiwango cha lami wa barabara ya **Tunduma – Sumbawanga**, sehemu ya **Mpemba – Isongole (km 51.2)** ulikuwa umefikia asilimia 59.36. Aidha, maandalizi ya ujenzi kwa kiwango cha lami kwa barabara ya **Ruanda – Iyula – Nyimbili (km 21)** yanaendelea.

71. Mheshimiwa Spika, ujenzi wa barabara ya **Kagoma – Lusahunga** umekamilika. Kazi za ujenzi wa kilometa 5.2 za barabara ya **Muhutwe – Kamachumu – Muleba (km 54.0)** zimefikia asilimia 25 na kwa kilometa 8 za barabara ya **Muleba – Kanyambogo – Rubya (km 18.5)**, kazi zimefikia asilimia 45. Aidha, Serikali inaendelea na maandalizi ya kuanza kazi ya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina wa barabara ya **Mutukula – Bukoba – Muhutwe – Kagoma (km 136)** kwa ajili ya kuifanyia ukarabati.

72. Mheshimiwa Spika, ujenzi na ukarabati wa barabara ya **Arusha – Minjingu – Babati – Singida** umekamilika. Hadi Machi, 2020 taratibu za manunuzi kwa ajili ya kumpata Mhandisi Mshauri wa kufanya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina wa barabara ya **Singida – Shelui (km 108)** kwa ajili ya kuifanyia ukarabati barabara hii zilikuwa zinaendelea.

73. Mheshimiwa Spika, katika mradi wa ujenzi wa barabara ya **Dar es Salaam – Mbagala (Kilwa Road) na daraja la Gerezani**; hadi Machi, 2020 ujenzi wa **daraja la Gerezani** umefikia asilimia 80. Aidha, kazi za upembuzi yakinifu, usanifu wa kina na utayarishaji wa

nyaraka za zabuni kwa sehemu ya **Mbagala Rangi Tatu – Kongowe** pamoja na **daraja la Mzinga** zimekamilika.

74. Mheshimiwa Spika, hadi Machi, 2020, katika barabara ya **Msimba – Ruaha/Ikokoto – Mafinga – Igawa**, kazi za ujenzi wa barabara ya **Igawa – Mbarali – Ubaruku (km 16)** sehemu ya **Mbarali – Ubaruku (km 8.9)** zimekamilika kwa kiwango cha lami. Aidha, hadi Machi, 2020 kazi za ujenzi kwa kiwango cha lami wa barabara ya **Njombe – Moronga (km 53.9)** zilikuwa zimefikia asilimia 64 na **Moronga – Makete (km 53.5)** zilikuwa zimefikia asilimia 47. Kazi za ujenzi wa barabara ya **Njombe – Lupembe – Madeke (km 125)** zinasubiri upatikanaji wa fedha. Kwa upande wa barabara ya **Iringa – Ruaha National Park (km 104.0)** na **Makambako – Songea (km 295.0)**, taarifa ya mapitio ya tathimini za athari za mazingira pamoja na mali zitakazoathirika wakati wa ujenzi na ukarabati wa barabara hizi zimewasilishwa Benki ya Dunia kwa ajili ya kuomba kibali cha kuendelea na taratibu za manunuzi kwa ajili ya ujenzi na ukarabati kwa kiwango cha lami. Aidha, Wahandisi Washauri wanaendelea na kazi za upembuzi yakinifu na usanifu wa kina kwa ajili ya ujenzi na ukarabati kwa kiwango cha lami wa barabara ya **Igawa – Songwe – Tunduma (km 218)** ikijumuisha **barabara ya mchepuo ya Mbeya (Uyole – Songwe Bypass) (km 48.9)** na barabara ya **Mafinga – Mgololo (km 78.0)**.

75. Mheshimiwa Spika, mradi wa ukarabati wa barabara ya **Korogwe – Mkumbara – Same (km 172)** umekamilika. Hadi Machi, 2020 Mhandisi Mshauri katika mradi wa barabara ya **Soni – Bumbuli – Dindira – Korogwe (km 74)** alikuwa anaendelea na kazi ya usanifu wa kina. Aidha, Serikali inaendelea kutafuta fedha ili kuanza kazi za ukarabati wa barabara za **Same – Himo (km 76)**, **Mombo – Lushoto (km 32)** na ujenzi kwa kiwango cha lami wa barabara ya **Lushoto – Magamba – Mlola (km 34.5)**.

76. Mheshimiwa Spika, katika barabara ya **Mbeya – Makongolosi**, hadi Machi, 2020 kazi za ujenzi kwa kiwango cha lami sehemu ya **Chunya – Makongolosi (km 43)** zimefikia asilimia 61. Aidha, Serikali inaendelea kutafuta fedha kwa ajili ya ujenzi kwa kiwango cha lami wa sehemu ya **Mkiwa – Itigi – Noranga (km 56.9)** na **Mbalizi – Makongolosi (km 50)**.

77. Mheshimiwa Spika, hadi Machi, 2020 katika mradi wa

barabara ya **Chalinze – Segera – Tanga**, Mkandarasi yuko katika hatua ya maandalizi ya kuanza kazi za ujenzi wa kilometa 7 za sehemu ya **Amani – Muheza (km 36)**.

78. Mheshimiwa Spika, mradi wa barabara ya **Itoni – Ludewa – Manda** hadi Machi, 2020, kazi ya ujenzi kwa kiwango cha zege kwa sehemu ya **Lusitu – Mawengi (km 50)** imefikia asilimia 42.4.

79. Mheshimiwa Spika, hadi Machi, 2020 ujenzi wa **daraja jipya la Selander** ulikuwa umefikia asilimia 34.

80. Mheshimiwa Spika, katika barabara ya **Handeni – Kibirashi – Kijungu – Kibaya – Njoro – Olboloti – Mrijochini – Dalai – Bicha – Chambalo – Chemba – Kwa Mtoro – Singida (km 460)**, kutokana na umuhimu wa barabara hii kwa ujenzi wa Bomba la Mafuta kutoka Tanga hadi Hoima (Uganda), Serikali inaendelea kutafuta fedha za ujenzi wa barabara hii.

81. Mheshimiwa Spika, katika barabara ya **Dodoma – Mtera – Iringa** hadi Machi, 2020 Mkandarasi alikuwa ameanza kazi za ujenzi katika barabara ya **Mchepuo wa Iringa (Iringa Bypass: km 7.3)**.

82. Mheshimiwa Spika, katika barabara ya **Dodoma – Babati**, hadi Machi, 2020 kazi ya Upembuzi yakinifu na usanifu wa kina wa barabara ya **Mchepuo wa Babati (Babati Bypass: km 12)** zilikuwa zinaendelea.

83. Mheshimiwa Spika, mradi wa ujenzi wa barabara ya **Masasi – Songea – Mbamba Bay na Masasi – Newala – Mtwara** unaendelea. Hadi Machi, 2020 ujenzi kwa kiwango cha lami wa sehemu ya **Mbinga – Mbamba Bay (km 66)** umefikia asilimia 52 na ujenzi wa barabara ya **Mtwara – Newala – Masasi (km 210)**, sehemu ya **Mtwara – Mnivata (km 50)** kwa kiwango cha lami umefikia asilimia 76. Kazi za upembuzi yakinifu na usanifu wa kina wa barabara ya **Masasi – Nachingwea (km 45.0)** na barabara ya **Nanganga – Ruangwa – Nachingwea (km 107)** zimekamilika na Serikali inaendelea kutafuta fedha kwa ajili ya ujenzi wa barabara hizi. Kwa upande wa ujenzi wa barabara ya **Likuyufusi – Mkenda (km 122.5)**, mapitio ya usanifu wa kina na nyaraka za zabuni yamefanyika kwa asilimia 40. Kwa barabara ya **Nachingwea – Liwale (km 130)** hadi Machi, 2020 Mhandisi Mshauri anaendelea na kazi ya usanifu wa kina.

Ujenzi wa kilometa 5 za barabara ya **Kitahi – Lituhi (km 90)** kuelekea machimbo ya makaa ya mawe unaendelea na umefikia asilimia 65. Aidha, kwa upande wa barabara ya **Mtwara – Mingoyo – Masasi (km 200)** hadi Machi, 2020 ukarabati wa barabara hii ulikuwa haujaanza. Aidha, Benki ya Dunia imeonyesha nia ya kugharamia ukarabati wa barabara ya hii chini ya programu ya *Development Corridor Transport Program* (DCTP) ambapo maandalizi ya utekelezaji wa programu hii yanaendelea.

84. Mheshimiwa Spika, katika mradi wa ujenzi wa barabara ya mchepuo kutoka barabara ya Bagamoyo kuingia kwenye **Chuo cha Uongozi cha Bagamoyo** pamoja na barabara za ndani ya Chuo hicho, Serikali inaendelea kutafuta fedha kwa ajili ya ujenzi wa barabara hizo.

85. Mheshimiwa Spika, hadi Machi, 2020, ujenzi wa **Miundombinu ya Mabasi Yaendayo Haraka Awamu ya Pili hadi ya Tano**, ulikuwa unaendelea ambapo ujenzi wa barabara za Mabasi Yaendayo Haraka Awamu ya Pili *Lot 1* (barabara) unaendelea na umekamilika kwa asilimia 3.3 na *Lot 2* (majengo) unaendelea na umefikia asilimia 22. Kwa upande wa mradi wa Mabasi Yaendayo Haraka Awamu ya Tatu, usanifu wa kina na uandaaji wa nyaraka za zabuni umekamilika na kuwasilishwa Benki ya Dunia kwa ajili ya kupata kibali cha kutangaza zabuni za ujenzi. Aidha, Serikali inaendelea kutafuta fedha za kuanza ujenzi wa Mradi wa BRT Awamu ya Nne na Tano ikiwa ni pamoja na kuendelea kufanya mazungumzo na Washirika wa Maendeleo.

86. Mheshimiwa Spika, hadi Machi, 2020 **ujenzi wa jengo la Makao Makuu ya Wakala wa Barabara Tanzania (TANROADS)** ulifikia asilimia 25. Aidha, utekelezaji wa miradi ya majengo ya Ofisi za Dar es Salaam, Katavi, Geita, Simiyu, Njombe na Lindi utanza kulingana na upatikanaji wa fedha.

87. Mheshimiwa Spika, Wizara inaendelea kutekeleza miradi mbalimbali ya barabara kwa kutumia fedha za Mfuko wa Barabara. Kazi zilizopangwa kutekelezwa katika Barabara Kuu kwa kutumia fedha za Mfuko wa Barabara ni kufanya Upembuzi Yakiniifu na Usanifu wa Kina wa **kilometa 5,602.73** za barabara ambapo hadi Machi, 2020 utekelezaji wa miradi hiyo ni kama ifuatavyo:

- i) **Barabara ya Kyaka – Bugene – Kasulo/Benaco (km 183.1) – Sehemu ya Bugene – Kasulo/Benaco (km 124)**
Kazi za upembuzi yakinifu na usanifu wa kina zimekamilika. Aidha, kazi ya kufanya mapitio ya usanifu kwa sehemu ya Kumunazi – Kasulo (km 9), Kasulo – Bugene (km 124) na Kyaka – Mutukula (km 30) kwa kutumia fedha za Benki ya Maendeleo ya Afrika kupitia Jumuiya ya Afrika Mashariki zipo katika hatua ya mwisho.
- ii) **Kufanya Mapitio na Kuandaa Miongozo (Standards and Specifications)**
Hadidu za Rejea kwa ajili ya kuanza taratibu za manunuzi za kumpata Mhandisi Mshauri wa kufanya mapitio ya miongozo mbalimbali ya kufanya usanifu wa barabara zilizoandaliwa miaka ya 1999 na 2000 zilikuwa zimekamilika. Serikali imeendelea kutafuta fedha za kugharamia mradi huu.
- iii) **Barabara ya Musoma – Makojo – Busekela (km 92)**
Upembuzi yakinifu na usanifu wa kina wa barabara hii umekamilika na Serikali inatafuta fedha za ujenzi kwa kiwango cha lami.
- iv) **Barabara ya Karatu – Mbulu – Haydom – Mto Sibiti – Lalago – Maswa (km 389)**
Kazi za upembuzi yakinifu na usanifu wa awali wa barabara hii zilikuwa zimefikia hatua ya mwisho kukamilika. Hatua inayofuata ni kuanza usanifu wa kina kabla ya kuanza ujenzi.
- v) **Barabara ya Isyonje – Kikondo – Makete (km 96.2)**
Kazi ya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina imekamilika. Hatua inayofuata ni Serikali kutenga fedha za ujenzi kwa kiwango cha lami.
- vi) **Kuimarisha Uwezo wa Maabara (Central Material Laboratory – CML) katika Kupima Vifaa vya Ujenzi na Kuanzisha Teknolojia ya Kisasa ya ‘Asphalt Mix Design’**
Tafiti sita (6) kuhusu vifaa ujenzi na matabaka ya lami (pavement) zilikuwa zinaendelea. Aidha, kazi ya uboreshaji wa maabara ili iweze kukidhi viwango vya kimataifa pamoja na mafunzo kwa wahandisi na Mafundi Sanifu kuhusu utumiaji wa Mwongozo wa Uchanganyaji Lami zilikuwa zinaendelea.
- vii) **Barabara ya Nyamirembe Port – Katoke (km 50)**
Kazi za upembuzi yakinifu na usanifu wa kina zilikuwa zimekamilika. Hatua inayofuata ni Serikali kutenga fedha kwa ajili ya kuanza ujenzi kwa kiwango cha lami.

- viii) **Mifumo ya Kompyuta (Software) kwa Ajili ya Usanifu wa Barabara na Kuandaa Mipango ya Usafiri (Highway/Transport Planning)**
Taratibu za manunuzi kwa ajili ya kumpata Mshauri Elekezi wa kutoa mafunzo juu ya mifumo ya kompyuta ya usanifu wa barabara na mipango ya usafiri zilikuwa zinaendelea.
- ix) **Daraja la Kigongo - Busisi katika Barabara ya Usagara – Geita**
Kazi za upembuzi yakinifu na usanifu wa kina zilikuwa zimekamilika na Mkandarasi alikuwa anaendelea na maandalizi ya kuanza ujenzi.
- x) **Mpanda – Ugalla – Kaliua – Ulyankulu – Kahama (km 457)**
Taratibu za kumpata Mhandisi Mshauri wa kufanya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina zilikuwa zinaendelea.
- xi) **Barabara ya Ipole – Rungwa (km 172)**
Kazi za upembuzi yakinifu na usanifu wa kina zilikuwa zimekamilika. Hatua inayofuata ni Serikali kutenga fedha za ujenzi kwa kiwango cha lami.
- xii) **Barabara ya Mtwara Pachani – Lusewa - Lingusenguse – Nalasi (km 211)**
Kazi za upembuzi yakinifu na usanifu wa kina zilikuwa zimekamilika. Serikali inaendelea kutafuta fedha za ujenzi kwa kiwango cha lami.
- xiii) **Barabara ya Arusha – Kibaya – Kongwa (km 430)**
Kazi za upembuzi yakinifu na usanifu wa kina zinaendelea.
- xiv) **Barabara ya Nanganga – Ruangwa – Nachingwea (km 91):**
Kazi za upembuzi yakinifu na Usanifu wa Kina imekamilika. Hatua inayofuata ni ya Serikali kutenga fedha za ujenzi kwa kiwango cha lami.
- xv) **Kuboresha Eneo la Mlima Kitonga (km 10)**
Taratibu za manunuzi kwa ajili ya kumpata Mhandisi Mshauri wa kufanya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina zinaendelea.
- xvi) **Barabara ya Dar es Salaam Road (Nanenane) – Miyuji (Arusha Road) – Mkonze (km 23)**
Kazi za upembuzi yakinifu na usanifu wa kina zinaendelea.
- xvii) **Barabara ya Emmaus – Mlimwa – Wajenzi (km 5)**
Kazi za upembuzi yakinifu na usanifu wa kina na kazi za ujenzi

kwa kiwango cha lami wa barabara hii imekamilika.

- xviii) Dodoma Outer Ring Road / Dodoma Bypass (Mtumba - Veyula - Nala - Matumbulu - Mtumba: km 104)*
Kazi za upembuzi yakinifu na usanifu wa kina zimekamilika. Hatua inayofuata ni ya Serikali kutenga fedha za ujenzi kwa kiwango cha lami.
- xix) Barabara ya Ngaresh - Enguik (Monduli Juu) (km 104)*
Kazi za upembuzi yakinifu na usanifu wa kina zimekamilika. Hatua inayofuata ni ya Serikali kutenga fedha za ujenzi kwa kiwango cha lami.
- xx) Uchunguzi wa Kina wa Chanzo cha Mafuriko Eneo la Kibaigwa katika Barabara ya Morogoro - Dodoma*
Taratibu za manunuzi kwa ajili ya kumpata Mhandisi Mshauri wa kufanya kazi ya uchunguzi wa kina wa chanzo cha mafuriko eneo la Kibaigwa zinaendelea.
- xxi) Uchunguzi wa Kina Kuhusu Chanzo cha Mafuriko na Kupata Ufumbuzi wa Kudumu Kwenye Daraja la Mkundi*
Taratibu za manunuzi kwa ajili ya kumpata Mhandisi Mshauri wa kufanya kazi hii zinaendelea.
- xxii) Barabara ya Babati (Dareda) - Dongobeshi (km 60)*
Taratibu za manunuzi kwa ajili ya kumpata Mhandisi Mshauri wa kufanya kazi ya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina zinaendelea.
- xxiii) Barabara ya Soni - Bumbuli - Dindira - Korogwe (km 70)*
Taratibu za manunuzi kwa ajili ya kumpata Mhandisi Mshauri wa kufanya kazi ya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina zipo katika hatua za mwisho.
- xxiv) Barabara ya Kibaoni - Majimoto - Inyonga (km 152)*
Kazi ya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina inaendelea.
- xxv) Barabara ya Kiranjeranje - Namichiga - Ruangwa (km 120)*
Kazi ya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina imekamilika. Hatua inayofuata ni ya Serikali kutenga fedha za ujenzi kwa kiwango cha lami.
- xxvi) Barabara ya Masaninga - Matandu - Nangurukuru - Kilwa Masoko (km 55)*
Kazi za upembuzi yakinifu na usanifu wa kina zilikuwa zinaendelea.

- xxvii) Barabara ya Sabasaba – Sepuka – Ndago – Kizaga (km 77)*
Kazi za upembuzi yakinifu na usanifu wa kina zinaendelea.
- xxviii) Barabara ya Singida Urban – Ilongero – Haydom (km 93)*
Taratibu za manunuzi kwa ajili ya kumpata Mhandisi Mshauri wa kufanya kazi ya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina zinaendelea.
- xxix) Daraja la Mpiji Chini na Barabara za Maingilio (km 1.7)*
Kazi ya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina zipo katika hatua ya mwisho.
- xxx) Barabara za Mkiu – Liganga – Madaba (Km 112); Liganga – Nkomang’ombe (km 70) na Nkomang’ombe – Coal Power Plant (km 4.14)*
Kazi za upembuzi yakinifu na usanifu wa kina zilikuwa zipo katika hatua ya mwisho.
- xxxi) Barabara ya Mkuyuni – Nyakato (km 10)*
Taratibu za manunuzi kwa ajili ya kumpata Mhandisi Mshauri wa kufanya kazi ya upembuzi yakinifu na usanifu wa Kina zilikuwa zinaendelea.
- xxxii) Barabara ya Tarime – Mugumu (km 86)*
Kazi za upembuzi yakinifu na usanifu wa kina zilikuwa zimekamilika. Hatua inayofuata ni ya Serikali kutenga fedha za ujenzi kwa kiwango cha lami.
- xxxiii) Barabara ya Morogoro (Tumbaku Roundabout) – Mangae/Melela – Mikumi – Iyovi (km 156.45) na Daraja la Doma*
Taratibu za manunuzi kwa ajili ya kumpata Mhandisi Mshauri wa kufanya kazi ya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina zilikuwa zinaendelea.
- xxxiv) Barabara ya Mbulu – Magugu (Mbuyu wa Mjerumani) (km 63)*
Mkataba kwa ajili ya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina umesainiwa Machi, 2020. Maandalizi ya kuanza kazi yanaendelea.
- xxxv) Barabara ya Morogoro (Msamvu Roundabout) – Morogoro Centre – Bigwa Junction (km 10)*
Taratibu za manunuzi kwa ajili ya kumpata Mhandisi Mshauri wa kufanya kazi ya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina zilikuwa zinaendelea.
- xxxvi) Barabara ya Buhongwa – Igoma (km 12)*
Taratibu za manunuzi kwa ajili ya kumpata Mhandisi Mshauri wa

kufanya kazi ya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina zilikuwa zinaendelea.

- xxxvii) **Barabara ya Omurushaka – Murongo (km 125)***
Taratibu za manunuzi kwa ajili ya kumpata Mhandisi Mshauri wa kufanya kazi ya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina zilikuwa zinaendelea.
- xxxviii) **Barabara ya Simanjiro (Orkesumet) – Kia – Mererani (Part Of Kongwa Ranch – Kiteto – Simanjiro – Kia (km 60)***
Taratibu za manunuzi kwa ajili kumpata Mhandisi Mshauri wa kufanya kazi ya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina zilikuwa zinaendelea.
- xxxix) **Barabara ya Babati – Orkesumet – Kibaya (km 255):***
Taratibu za manunuzi kwa ajili ya kumpata Mhandisi Mshauri wa kufanya kazi ya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina zilikuwa zinaendelea.
- xl) **Barabara ya Singida Bypass (km 46):***
Taratibu za manunuzi kwa ajili ya kumpata Mhandisi Mshauri wa kufanya kazi ya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina zilikuwa zinaendelea.
- xli) **Barabara ya Songea Bypass (km 11)***
Mkataba kwa ajili ya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina umesainiwa. Maandalizi ya kuanza kazi yanaendelea.
- xlII) **Barabara ya Nyakato – VETA – Buswelu (km 3)***
Taratibu za manunuzi kwa ajili ya kumpata Mhandisi Mshauri wa kufanya kazi ya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina zilikuwa zinaendelea.
- xlIII) **Daraja la Godegode (Meta 70) na Barabara za Maingilio (km 6) Kati ya Barabara ya Mpwapa – Makutano na Pawaga – Lumuma***
Kazi ya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina imeanza.
- xlIV) **Barabara ya Mlandizi – Chalinze (km 44)***
Taratibu za manunuzi kwa ajili ya kumpata Mhandisi Mshauri wa kufanya kazi ya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina zilikuwa zinaendelea.
- xlV) **Barabara ya Salawe – Old Shinyanga (km 64.70)***
Kazi ya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina imeanza.

- x/vi) Barabara ya Mbezi Mwisho Interchange na Kuunganisha Barabara za Kuingia na Kutoka Katika Mradi wa Kituo Kikuu cha Mabasi ya Nje na Mikoani*
Kazi za upembuzi yakinifu na usanifu wa kina zilikuwa zinaendelea.
- x/vii) Barabara ya Mwapwa - Gulwe - Rudi - Chipogoro; Sehemu ya Kibakwe - Chipogoro (km 75.84)*
Kazi za upembuzi yakinifu na usanifu wa kina zilikuwa zinaendelea.
- x/viii) Barabara ya Kihansi – Mlimba – Madeke (km 220.22)*
Kazi za upembuzi yakinifu na usanifu wa kina wa barabara hii zimejumuishwa kwenye mkopo nafuu wa AfDB ambao pia utatumika kujenga daraja la Pangani na barabara ya Pangani – Mkange - Tungamaa (km 124).
- xlix) Barabara ya Ntendo – Muze – Kilyamatundu (km 200.00)*
Taratibu za manunuzi kwa ajili ya kumpata Mhandisi Mshauri wa kufanya mapitio ya upembuzi yakinifu na usanifu wa Kina zilikuwa zinaendelea.
- l) Barabara ya Mbamba Bay – Lituhi (km 121.00)*
Kazi za upembuzi yakinifu na usanifu wa kina zimekamiliwa. Hatua inayofuata ni ya Serikali kutenga fedha za ujenzi kwa kiwango cha lami.
- li) Barabara ya Nangurukuru - Liwale (km 210.00)*
Taratibu za manunuzi kwa ajili ya kumpata Mhandisi Mshauri wa kufanya mapitio ya upembuzi yakinifu na usanifu wa Kina zilikuwa zinaendelea.
- lii) Barabara ya Ushirombo – Nyikonga – Geita (Katoro) (km 59.00)*
Mkataba wa upembuzi yakinifu na usanifu wa kina umesainiwa mwezi Machi, 2020.
- liii) Barabara ya Makete – Ndulamo – Nkenja - Kitulo (km 42)*
Taratibu za manunuzi kwa ajili ya kumpata Mhandisi Mshauri wa kufanya mapitio ya upembuzi yakinifu na usanifu wa Kina zilikuwa zinaendelea.

Utekelezaji wa Miradi ya Ujenzi na Ukarabati wa Vivuko na Maegesho ya Vivuko

88. Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2019/20,

kuhusu **ujenzi na ukarabati wa maegesho ya vivuko**, Wizara kupitia Wakala wa Ufundi na Umeme Tanzania (TEMESA) ilipanga kuendelea na upanuzi wa eneo la maegesho ya Kigamboni katika kivuko cha Magogoni - Kigamboni mkoani Dar es Salaam, maegesho ya Bukondo na Zumacheli katika kivuko cha Chato - Nkome mkoani Geita, ujenzi wa maegesho ya Nyamisati - Mafia katika mkoa wa Pwani, ujenzi wa miundombinu (jengo la abiria, ofisi na uzio) katika kivuko cha Lindi – Kitunda Mkoani Lindi na ukarabati wa maegesho ya Bugolora – Ukara (Mwanza), Rugezi – Kisorya (Mwanza), Kilambo – Namoto (Mtwara) na Utete – Mkongo (Pwani).

Hadi Machi, 2020 ujenzi wa miundombinu (jengo la abiria, ofisi na uzio) katika kivuko cha Lindi – Kitunda umekamilika. Aidha, awamu ya pili ya upanuzi wa jengo la abiria na maegesho ya kivuko cha Kigamboni – Magogoni ilikuwa imeanza. Ujenzi wa maegesho ya Bukondo umeanza na maegesho ya Zumacheli katika kivuko cha Chato – Nkome na Nyamisati – Mafia upo hatua ya kumpata mkandarasi.

89. Mheshimiwa Spika, kwa upande wa **ununuzi wa vivuko**, kazi zilizopangwa ni kumalizia ununuzi wa kivuko cha Nyamisati – Mafia, Bugolora – Ukara pamoja na ununuzi wa boti nne (4) kwa ajili ya kisiwa cha Ukerewe (Ilugwa, Nafuba na Gana) na Magogoni – Kigamboni. Kazi nyingine ni ununuzi wa boti moja (1) ya uokozi kwa ajili ya Lindi – Kitunda na ununuzi wa vifaa vya karakana za TEMESA kwa ajili ya kuboresha huduma ya matengenezo ya magari, pikipiki na mitambo ya Serikali.

Hadi Machi, 2020 ujenzi wa kivuko kipyaa cha Nyamisati – Mafia (Pwani) umefikia asilimia 40 na Bugolora – Ukara (Mwanza) umefikia asilimia 70. Ununuzi wa boti mpya za uokozi kwa ajili ya kisiwa cha Ukerewe (Ilugwa, Nafuba na Gana), Magogoni - Kigamboni pamoja na boti moja ya uokozi kwa kivuko cha Lindi – Kitunda unaendelea. Aidha, vitendea kazi vya karakana vimenunuliwa kwa ajili ya karakana 15 katika mikoa ya Dar es Salaam (Vingunguti), Pwani, Morogoro, Lindi, Mtwara, Iringa, Njombe, Katavi, Kigoma, Mwanza, Dodoma, Singida na wilaya za Kahama na Ifakara pamoja na karakana ya MT Depot (Dar es Salaam).

90. Mheshimiwa Spika, miradi ya **Ukarabati wa Vivuko**, iliyopangwa kutekelezwa katika mwaka wa fedha 2019/20 ni pamoja na kufanya ukarabati wa vivuko MV Tegemeo, MV Musoma, MV Mara, MV KIU, MV Sengerema, MV Ujenzi, MV Kigamboni, MV Kome II na MV

Misungwi.

Hadi Machi, 2020 ukarabati mkubwa wa MV Kigamboni umekamilika, ukarabati wa MV Sengerema umefikia asilimia 60 na ukarabati wa MV Misungwi umefikia asilimia 35. Aidha, ukarabati wa MV Tegemeo, MV Musoma na MV Mara upo katika hatua za uchambuzi wa zabuni.

Utekelezaji wa Miradi ya Ujenzi na Ukarabati wa Nyumba na Majengo ya Serikali

91. Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2019/20, Wizara kupitia Wakala wa Majengo Tanzania (TBA) ilipanga kuendelea na ujenzi wa nyumba za Majaji katika mikoa ya Dar es Salaam (1), Kilimanjaro (1), Mtwara (1) na Shinyanga (1); ujenzi wa nyumba 50 za Viongozi, Ikulu ya Dodoma; Ujenzi wa jengo la ofisi ya Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano; ujenzi wa nyumba za makazi eneo la Magomeni (Magomeni Quarters) pamoja na Ikulu ya Chamwino.

Vilevile, Wizara ilipanga kufanya ukarabati wa nyumba za Viongozi pamoja na kufanya manunuzi ya samani za nyumba za Viongozi na kwenye Ikulu Ndogo za Serikali; ukarabati wa nyumba zilizokuwa zinamilikiwa na Mamlaka ya Ustawishaji wa Makao Makuu Dodoma (CDA); ukarabati wa nyumba zilizokuwa zinamilikiwa na TAMISEMI/NHC. Aidha, Wizara ilipanga kuendelea na ukarabati wa karakana za TBA katika mikoa ya Arusha, Mwanza, Dodoma, Mbeya, Tabora na Dar es Salaam. Kazi nyingine ni ukarabati wa karakana tano (5) za TEMESA zilizopo Mwanza, Arusha, Mtwara, Mbeya na M.T Depot Dar es Salaam; ujenzi wa karakana mpya ya kisasa ya magari Jijini Dodoma pamoja na kuanza ujenzi wa Karakana za TEMESA katika mikoa mipya ya Songwe, Simiyu, Geita, Njombe na Katavi pamoja na kuendelea na kuwajengea uwezo Wabunifu Majengo na Wakadiriaji Majenzi na Huduma za Ushauri.

92. Mheshimiwa Spika, hadi Machi, 2020, ujenzi wa nyumba moja ya Jaji Jijini Dar es Salaam umekamilika, kazi za ujenzi wa nyumba 5 za Majaji zipo katika hatua mbalimbali na ujenzi wa nyumba za Makazi ya Magomeni “Quarters” umefikia asilimia 70. Ujenzi wa nyumba 50 za viongozi Dodoma haukufanyika kutokana na uhaba wa fedha na usanifu wa jengo la ofisi ya Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano katika Mji mpya wa Serikali eneo la Mtumba Jijini Dodoma upo kwenye hatua ya mapitio ya michoro na gharama.

Aidha, awamu ya kwanza ya ukarabati wa karakana ya TBA Dodoma imekamilika kwa asilimia 90 na ukarabati wa karakana tano za TBA katika mikoa ya Mwanza, Arusha, Mbeya, Dar es Salaam na Tabora upo katika hatua za awali za utekelezaji.

Kwa upande wa karakana za TEMESA, ukarabati wa karakana zilizopo Mwanza na Mbeya unaendelea. Aidha, ujenzi wa karakana ya Simiyu na karakana mpya ya jijini Dodoma upo kwenye hatua za kusaini mikataba na ujenzi wa karakana za TEMESA katika mikoa mipya ya Geita, Njombe na Katavi upo katika hatua za manunuzi.

Usalama Barabarani na Mazingira

93. Mheshimiwa Spika, Wizara inaendelea kuratibu shughuli za usalama barabarani na kudhibiti uzito wa magari yanayotumia barabara. Kazi zilizopangwa kwa mwaka wa fedha 2019/20 ni ujenzi wa Vituo vya Pamoja vya Ukaguzi; uanzishwaji wa mfumo wa usimamizi wa usalama wa vivuko; ukaguzi wa usalama wa barabara; mapitio ya Sera ya Usalama Barabarani; kuendelea na ujenzi wa mizani ya kisasa ya kupima magari yakiwa kwenye mwendo mdogo (Slow Weigh in Motion Weighbridge) Mkoani Dar es Salaam pamoja na ujenzi wa miundombinu na uwekaji wa Mfumo wa Upatikanaji na Utoaji Taarifa za Ajali Barabarani katika vituo vya Polisi nchini. Kazi nyingine ni kujenga uwezo na uelewa wa masuala ya usalama barabarani kwa umma.

94. Mheshimiwa Spika, hadi Machi, 2020 Wizara imeendelea na ukamilishaji wa malipo ya fidia ya ujenzi wa Vituo vya Pamoja vya Ukaguzi (*One Stop Inspection Station – OSIS*) katika maeneo ya Idofi – (Njombe), Iboya (Mbozi-Songwe) na Himo (Kilimanjaro). Ujenzi wa mizani ya kisasa ya kupima magari yakiwa kwenye mwendo mdogo (slow weigh in motion weighbridge) mkoani Dar es Salaam upo katika hatua za manunuzi. Vile vile ujenzi wa miundombinu na uwekaji wa mfumo wa upatikanaji na utoaji taarifa za ajali barabarani katika vituo vya Polisi nchini upo katika hatua za manunuzi. Aidha, Wizara imeanza kufuatilia na kutathmini utendaji kazi wa vituo vya mizani kwa kutumia mfumo wa Ufuatiliaji wa Utendaji Kazi wa Mizani kwa masaa 24 kila siku kwa juma (24/7) katika mizani 13 zilizofungwa mfumo huo. Wizara inaendelea kufunga mfumo huo kwenye mizani nyingine zilizobaki kote nchini.

Kwa upande wa mazingira, Wizara imeendelea kusimamia utekelezaji wa Sheria ya Mazingira Na. 20 ya mwaka 2004 katika Sekta ya Ujenzi. Aidha, mfumo wa TEHAMA wa ukusanyaji wa taarifa za mazingira upo kwenye hatua za manunuzi. Vile vile Wizara imeendelea kushiriki katika maandalizi ya Taarifa ya Tatu ya Hali ya Mazingira (State of Environment Report III) yanayoratibiwa na Ofisi ya Makamu wa Rais.

MIRADI YA UJENZI WA MIUNDOMBINU YA VIWANJA VYA NDEGE

95. Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2019/20, Wizara kupitia TANROADS imeendelea kutekeleza miradi ya ujenzi na ukarabati wa miundombinu ya viwanja vya ndege kama ifuatavyo:

96. Mheshimiwa Spika, mradi wa ujenzi wa **Kiwanja cha Ndege cha Kigoma**, kazi zilizopangwa kwa mwaka wa fedha 2019/20 ni ujenzi wa jengo jipya la abiria, upanuzi na ukarabati wa maegesho ya ndege, ujenzi wa jengo la kuongozea ndege pamoja na miundombinu yake (mitambo ya kuongozea ndege), ujenzi wa kituo kidogo cha umeme, ujenzi wa kituo cha uangalizi wa hali ya hewa pamoja na ujenzi wa barabara ya kuingilia uwanjani na maegesho ya magari.

Hadi Machi, 2020 mradi huu ulikuwa kwenye hatua za mwisho za manunuzi kwa ajili ya kumpata Mkandarasi atakayeutekeleza.

97. Mheshimiwa Spika, katika mradi uliokamilika wa ujenzi wa **Kiwanja cha Ndege cha Mpanda**, lengo la mwaka 2019/20 lilikuwa ni ujenzi wa uzio. Hadi Machi, 2020 Serikali ilikuwa inaendelea kutafuta fedha kwa ajili ya kazi hii.

98. Mheshimiwa Spika, kwa upande wa mradi wa **Kiwanja cha Ndege cha Songwe**, mikataba ya ukarabati wa barabara ya kuruka na kutua ndege pamoja na usimikaji wa taa za kuongozea ndege imesainiwa. Aidha, Serikali kupitia TANROADS inaendelea na taratibu za manunuzi ya kumpata Mkandarasi wa kuendeleza ujenzi wa jengo la abiria baada ya Mkandarasi aliyekuwepo kusimamishwa.

99. Mheshimiwa Spika, katika mradi wa **Kiwanja cha Ndege cha Tabora**, lengo la mradi lilikuwa ni kutekeleza awamu ya tatu ya kuboresha kiwanja. Hadi Machi, 2020 mikataba ya Mkandarasi na Mshauri Elekezi kwa ajili ya kazi za ujenzi wa barabara ya kuruka na kutua jengo jipya la abiria, barabara ya kuingilia na kutoka kiwanjani, maegesho ya magari, barabara ya kiungio na jengo la uchunguzi wa

hali ya hewa ilikuwa imesainiwa. Wizara inasubiri idhini ya Mfadhili (No Objection) ili ianze hatua za utekelezaji wa kazi hizo.

100. Mheshimiwa Spika, katika mradi wa **Kiwanja cha Ndege cha Shinyanga,** lengo la mradi lilikuwa ni ujenzi wa barabara ya kutua na kuruka ndege na viungio vyake, maegesho ya ndege, jengo la abiria, jengo la kuongozea ndege, jengo la uchunguzi wa hali ya hewa, barabara ya kuingia na kutoka kiwanjani na maegesho ya magari pamoja na usimikaji wa taa na mitambo ya kuongozea ndege. Hadi Machi, 2020 mikataba ya Mkandarasi na Mshauri Elekezi kwa ajili ya kazi hizo ilikuwa imesainiwa. Wizara inasubiri idhini ya Mfadhili (No Objection) ili ianze hatua za utekelezaji wa kazi hizo.

101. Mheshimiwa Spika, katika mradi wa **Kiwanja cha Ndege cha Sumbawanga,** lengo la mradi lilikuwa ni ujenzi wa barabara ya kutua na kuruka ndege na viungio vyake, maegesho ya ndege, jengo la abiria, jengo la kuongozea ndege, jengo la uchunguzi wa hali ya hewa, barabara ya kuingia na kutoka kiwanjani na maegesho ya magari pamoja na usimikaji wa taa na mitambo ya kuongozea ndege na uzio wa usalama wa kiwanja cha ndege. Hadi Machi, 2020 mikataba ya Mkandarasi na Mshauri Elekezi kwa ajili ya kazi hizo ilikuwa imesainiwa. Wizara inasubiri idhini ya Mfadhili (No Objection) ili ianze hatua za utekelezaji wa kazi hizo.

102. Mheshimiwa Spika, kwa upande wa **Kiwanja cha Ndege cha Mwanza,** kazi zilizopangwa ni kusimika taa za kuongozea ndege, ujenzi wa jengo jipya la abiria, maegesho ya magari, uzio wa usalama pamoja na mfumo wa maji safi, maji taka na maji ya mvua.

Hadi Machi, 2020, kazi za ukarabati na upanuzi ambazo zilihusisha ujenzi wa maegesho ya ndege, ujenzi wa jengo la mizigo (Cargo Terminal) pamoja na maegesho ya ndege za mizigo, jengo la kuongozea ndege, kituo cha umeme, maegesho ya magari, kusimika taa za kuongozea ndege na mfumo wa maji safi, maji taka na maji ya mvua zimekamilika. Aidha, kazi ya mapitio ya usanifu wa jengo jipya la abiria inaendelea.

103. Mheshimiwa Spika, katika mradi wa **Kiwanja cha Ndege cha Arusha,** kazi zilizopangwa ni kurefusha barabara ya kuruka na kutua ndege kwa meta 200 na ujenzi wa maeneo ya kugeuzia ndege (Turning Pad). Kazi nyingine ni ujenzi wa uzio wa usalama, kujenga

barabara mpya ya kuingilia na kutoka kiwanjani pamoja na kukarabati maegesho ya magari. Hadi Machi, 2020, mradi huu upo katika hatua ya manunuzi ya Mkandarasi.

104. Mheshimiwa Spika, kwa upande wa mradi wa **Kiwanja cha Ndege cha Mtwara,** kazi zilizopangwa ni kufanya ukarabati wa barabara ya kuruka na kutua ndege, viungio vyake pamoja na maegesho ya ndege pamoja na kusimika taa na mitambo ya kuongozea ndege. Kazi nyingine ni na ujenzi wa barabara ya kuingilia na kutokakiwanjani na maegesho ya magari. Hadi Machi, 2020 kazi hizo zilikuwa zimekamilika kwa asilimia 33.

105. Mheshimiwa Spika, katika mradi wa **Kiwanja cha Ndege cha Kimataifa cha Kilimanjaro,** kazi zilizopangwa ni kufanya usanifu wa kina na kuanza ukarabati na upanuzi wa barabara ya kuruka na kutua ndege, ujenzi wa barabara mpya ya kiungio na usimikaji wa taa za kuongozea ndege. Hadi Machi, 2020, taratibu za manunuzi ya Mhandisi Mshauri kwa ajili ya usanifu wa kina wa ukarabati wa barabara ya kutua na kuruka ndege zilikuwa zinaendelea.

106. Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2019/20 katika mradi wa **Uendelezaji wa Viwanja vya Ndege vya Mikoa** kazi zilizopangwa zilikuwa ni pamoja na kuendelea na ujenzi wa kiwanja kipya cha mikoa ya Geita na Simiyu na upanuzi na ukarabati viwanja vya ndege vya Iringa, Songea, Lindi, Lake Manyara, Tanga na Musoma. Kazi nyingine ni kumalizia ulipaji wa fidia kwa wananchi walioathirika na mradi wa kiwanja cha ndege cha Dodoma pamoja na kuanza ukarabati wa kiwanja cha ndege cha Moshi na viwanja vingine vya mikoa.

Hadi Machi, 2020, ujenzi wa barabara ya kuruka na kutua ndege, barabara ya kiungio na maegesho ya ndege kwenye kiwanja cha ndege cha Geita umefikia asilimia 78. Wizara inaendelea na manunuzi ya Mkandarasi kwa ajili ya ukarabati wa kiwanja cha Musoma. Upanuzi wa kiwanja cha ndege cha Songea umefikia asilimia 34; Awamu ya kwanza ya ukarabati wa kiwanja cha ndege cha Iringa ipo kwenye hatua ya manunuzi; manunuzi wa makandarasi kwa ajili ya viwanja vya Iringa (Awamu ya II), Lake Manyara na Tanga yanasubiri idhini (no objection) kutoka Benki ya Dunia na ulipaji wa fidia wa kiwanja cha ndege cha

Dodoma umekamilika. Ukarabati wa kiwanja cha ndege cha Moshi unasubiri upatikanaji wa fedha.

107. Mheshimiwa Spika, kwa upande wa ujenzi wa **Kiwanja cha Ndege cha Msalato**, kazi zilizopangwa kwa mwaka wa fedha 2019/20 ni kulipa fidia kwa mali zitakazoathirika na utekelezaji wa mradi huu pamoja na kufanya mapitio ya upembuzi na usanifu wa kina.

Hadi Machi, 2020, uhakiki kwa ajili ya ulipaji wa fidia ulikuwa unaendelea. Aidha, taratibu za awali za manunuzi ya kumpata Mkandarasi na Mhandisi Mshauri zilikuwa zinaendelea.

108. Mheshimiwa Spika, katika **Kiwanja cha Ndege cha Bukoba**, kazi zilizopangwa zilikuwa ni usanifu wa kina kwa ajili ya kurefusha barabara ya kuruka na kutua ndege pamoja na ufungaji wa taa za kuongozea ndege. Hadi Machi, 2020 Serikali inaendelea kutafuta fedha kwa ajili ya utekelezaji wa mradi huu.

109. Mheshimiwa Spika, katika mradi wa ujenzi wa **Jengo la Tatu la Abiria (Terminal III)** katika **Kiwanja cha Ndege cha Kimataifa cha Julius Nyerere (JNIA)**, lengo lilikuwa ni kukamilisha ujenzi wa Jengo la Tatu la Abiria (Terminal Building III), kulipa fidia kwa wakazi wa Kipunguni na Kigilagila waliohamishwa kupisha utekelezaji wa mradi huu pamoja na kufanya Usanifu wa kina kwa ajili ya ukarabati na upanuzi wa jengo la pili la abiria (Terminal II). Hadi Machi, 2020 ujenzi wa Jengo la Tatu la Abiria umekamilika. Ulipaji fidia kwa wakazi wa Kipunguni na Kigilagila na Usanifu wa kina kwa ajili ya ukarabati na upanuzi wa jengo la pili la abiria (Terminal II) unasubiri upatikanaji wa fedha.

UTENDAJI WA TAASISI ZILIZO CHINI YA SEKTA YA UJENZI

Bodi ya Mfuko wa Barabara

110. Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2019/20, Mfuko wa Barabara ulipanga kukusanya jumla ya **Shilingi 839,127,000,000** kwa ajili ya matengenezo ya barabara nchini. Kati ya fedha hizo, **Shilingi 587,389,000,000** ni kwa ajili ya matengenezo ya barabara za kitaifa (Barabara Kuu na Barabara za Mikoa) ambazo husimamiwa na Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano kupitia Wakala wa Barabara Tanzania (TANROADS) na **Shilingi 251,738,000,000** zilitengwa kwa ajili ya kugharamia barabara za Wilaya ambazo

husimamiwa na Ofisi ya Rais – TAMISEMI.

Kati ya fedha hizo, Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano (Ujenzi) ilitengewa **Shilingi 58,233,735,546**, TANROADS ilitengewa **Shilingi 524,103,619,914**, TARURA ilitengewa Shilingi **224,615,837,106**, Ofisi ya Rais – TAMISEMI ilitengewa **Shilingi 24,957,315,234** na **Shilingi 7,216,492,200** zilitengwa kwa ajili ya kugharamia uendeshaji wa Bodi ya Mfuko wa Barabara.

111. Mheshimiwa Spika, hadi Machi, 2020 Bodi imekusanya na kugawanya jumla ya **Shilingi 661,114,850,437.44** sawa na **asilimia 79** ya bajeti ya mwaka. Kati ya hizo, Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano (Ujenzi) ilipokea **Shilingi 45,878,807,037.32**, TANROADS **Shilingi 412,909,263,335.92**; Ofisi ya Rais – TAMISEMI **Shilingi 19,662,335,504.29**, TARURA **Shilingi 176,961,019,538.14** na Bodi ya Mfuko wa Barabara **Shilingi 5,703,425,021.77**.

112. Mheshimiwa Spika, katika kuimarisha usimamizi wa mizani nchini, Bodi ya Mfuko wa Barabara kwa kushirikiana na TANROADS na Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano imekamilisha uwekaji mfumo wa kielektroniki na kamera za CCTV kwenye vituo 13 vya mizani ya kupima uzito wa magari. Mfumo huo umewezesha taasisi husika kufuatilia moja kwa moja na kwa wakati (real time) jinsi upimaji wa magari unavyoendelea kwenye vituo vya mizani nchini. Mfumo huu utakapounganishwa na Mfumo wa Bodi ya Mfuko wa Barabara (RFB Management Information System), Bodi itakuwa na uwezo wa kujua magari yaliyozidisha uzito na faini iliyotozwa muda uleule.

113. Mheshimiwa Spika, Bodi kupitia Mtaalam Mshauri inaendelea na utafiti kuhusu uwezekano wa kuwa na mgawanyo mpya wa fedha za Mfuko (Allocation Formula) zinazotengwa kwa ajili ya Barabara za Kitaifa (Barabara Kuu na za Mikoa) zinazosimamiwa na TANROADS na barabara za Wilaya zinazosimamiwa na TARURA. Aidha, Bodi inaendelea na taratibu za kufanya tathmini ya mtandao wa barabara (Road inventory and condition survey) ili kubaini thamani, urefu na hali ya barabara nchini kwa ufadhili wa Benki ya Dunia. Matokeo ya tathmini hii yatasaidia kuboresha mipango na usimamizi wa matengenezo ya barabara kikamilifu na kwa wakati.

Wakala wa Majengo Tanzania

114. Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2019/20, Wakala wa Majengo Tanzania ulipanga kumalizia ujenzi wa nyumba 5 za majaji Tanzania Bara katika mikoa ya Dar es Salaam, Kilimanjaro, Kagera, Mtwara, Shinyanga na Tabora; kuendelea na ujenzi wa nyumba za Makazi, Magomeni Kota; ujenzi wa nyumba 50 za Viongozi Dodoma, nyumba 5 za watumishi mikoa mipya pamoja na ujenzi wa nyumba ya Makazi kwenye Ikulu ya Chamwino, Dodoma.

Wakala vilevile ulipanga kufanya ukarabati wa nyumba za iliyokuwa Mamlaka ya Ustawishaji Makao Makuu Dodoma (CDA); ukarabati/ Matengenezo nyumba za viongozi Jijini Dodoma; ukarabati wa Karakana za Wakala kwa mikoa ya Dar es Salaam, Tabora, Arusha, Mwanza, Mbeya na Dodoma pamoja na ununuzi wa samani kwa nyumba 55 za viongozi mkoani Dodoma na Mikoa mipya. Aidha, Wakala ulipanga kuendelea kutoa huduma ya ushauri katika ujenzi na marekebisho ya majengo ya Serikali pamoja na kuendesha programu za kuwajengea uwezo Wataalam wa Ujenzi na Ushauri.

115. Mheshimiwa Spika, hadi kufikia Machi, 2020, miradi iliyotekelezwa na Wakala wa Majengo ni pamoja na kukamilisha ujenzi wa kambi ya Mkandarasi katika Mradi wa Bwawa la Kufua Umeme la Mwalimu Nyerere, ukarabati wa nyumba **34** na ujenzi wa nyumba **3**.

116. Mheshimiwa Spika, Wakala vilevile umefanikiwa kukarabati nyumba **139** Dar es Salaam na Mikoani, Hati Miliki **19** zimepatikana tayari kwa Mikoa ya Tabora (1), Geita (10), Kilimanjaro (1), Mwanza (2), Katavi (1), Manyara (2), Shinyanga (1) na Iringa (1). Aidha, michoro pamoja na gharama za mradi wa ujenzi wa nyumba **5** kati ya nyumba 100 za watumishi wa umma Dodoma vimeandaliwa.

117. Mheshimiwa Spika, Wakala pia umetekeleza jumla ya miradi **47** ya Ubunifu na Ujenzi. Miradi hiyo ni pamoja na ujenzi wa Jengo la Ofisi ya Mkurugenzi wa Manispaa ya Kigamboni pamoja na Ofisi ya Mkuu wa wilaya ya Kigamboni umekamilika, Jengo la utawala la Ofisi ya Wilaya ya Mlele (asilimia 30), Jengo la Ofisi ya Halmashauri ya Wilaya ya Butiama (asilimia 47), Jengo la Ofisi ya Mkurugenzi wa Halmashauri ya Mji wa Ifakara (asilimia 40), Jengo la Ofisi ya Mkuu wa wilaya Mkalama (asilimia 51), Jengo la Ofisi ya Mkuu wa wilaya ya

Ubungo (asilimia 98), Jengo la Ofisi ya Mkuu wa Wilaya ya Busega (asilimia 95), majengo ya hospitali ya rufaa Geita na Chato (asilimia 89), mradi wa jengo la Ofisi ya TANROADS – Dodoma (asilimia 25) na jengo la Mkurugenzi wa Halmashauri ya Ubungo (asilimia 50).

118. Mheshimiwa Spika, vilevile Wakala umetekeleza jumla ya miradi 38 ya ujenzi. Baadhi ya miradi hiyo ni ujenzi wa jengo la Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, ujenzi wa Jengo la Hospitali ya Halmashauri ya Mji wa Tunduma awamu ya pili, ujenzi wa Jengo la Mionzi na Upasuaji, jengo la Maabara pamoja na banda la kuunguzia taka katika Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Simiyu ukarabati wa Ofisi ya Mkuu wa Mkoa Tabora na hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Tabora ambayo imekamilika. Miradi mingine ni ukarabati wa jengo la Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu awamu ya kwanza (asilimia 95), ukarabati wa nyumba tisa za viongozi wa Serikali Wilaya ya Mwanga (asilimia 75), ujenzi wa jengo la Ofisi ya Halmashauri ya Wilaya Madaba - Songea awamu ya pili (asilimia 63), ujenzi wa Jengo la Ofisi ya Mkuu wa Mkoa Songwe awamu wa pili (asilimia 80), ukarabati wa Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Iringa (asilimia 43) na ujenzi wa jengo la maktaba Chuo Kikuu cha Sayansi na Teknolojia Mbeya (asilimia 95).

119. Mheshimiwa Spika, Wakala pia umetekeleza jumla ya miradi 81 ya ushauri. Miradi hiyo ni pamoja na ujenzi wa majengo ya Ofisi za Wizara na Taasisi mbalimbali za Serikali awamu ya kwanza kwenye Mji wa Serikali (Government City) Dodoma, ujenzi wa jengo la hospitali ya Wilaya ya Kilolo, ukarabati wa jengo la Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Tabora ambayo imekamilika. Miradi mingine ni ujenzi wa majengo ya Ofisi za Wizara na Taasisi mbalimbali za Serikali awamu ya pili ambao uko kwenye hatua za mwisho ya ubunifu, ujenzi wa Ofisi za maji Kimani na Mkoji (asilimia 65), ujenzi wa jengo la utawala la Halmashauri ya Mji wa Bunda (asilimia 87), ujenzi wa makazi ya Mkuu wa Wilaya ya Butiama (asilimia 95), ujenzi wa Mahakama ya Mwanzo Laela Sumbawanga (asilimia 85), ujenzi wa Mahakama ya Mwanzo Mtowisa pamoja na Msanzi (asilimia 100), ukarabati upanuzi na ujenzi wa miundombinu ya Mahakama Kuu katika mikoa mitano (asilimia 70) na ujenzi wa Jengo la Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Simiyu (asilimia 25).

120. Mheshimiwa Spika, vilevile Wakala umetekeleza jumla ya miradi miwili ya usimamizi. Miradi hiyo ni ujenzi wa majengo ya rada katika mikoa minne ya Dar es Salaam, Kilimanjaro, Mwanza na Songwe

ambapo ujenzi umekamilika katika mikoa mitatu isipokuwa mkoa wa Songwe (asilimia 95). Mradi mwingine ni ujenzi wa Vihenge (Silos) vya kuhifadha nafaka pamoja na maghala kwa ajili ya hifadhi ya chakula (National Food Reserve Agency) katika mikoa nane ya Dodoma, Katavi, Manyara, Njombe, Rukwa, Ruvuma, Shinyanga na Songwe (asilimia 50).

121. Mheshimiwa Spika, hadi kufikia Machi, 2020, miradi iliyotekelezwa na Wakala wa Majengo ni pamoja na kukamilisha ujenzi wa kambi ya Mkandarasi katika Mradi wa Bwawa la Kufua Umeme la Mwalimu Nyerere, ukarabati wa nyumba 34 na ujenzi wa nyumba 3 pamoja na ujenzi wa nyumba za makazi zenye uwezo wa kubeba kaya 656 zilizopo Magomeni Kota Dar es Salaam ambao umefika asilimia sabini (70). Aidha, ukarabati wa Karakana za TBA katika mikoa sita (6) ya Dar es Salaam, Arusha, Mwanza, Tabora, Mbeya na Dodoma unaendelea.

122. Mheshimiwa Spika, Wakala vilevile umefanikiwa kukarabati nyumba 139 Dar es Salaam na Mikoani, Hati Miliki 19 zimepatikana tayari kwa Mikoa ifuatayo:- Tabora 1, Geita 10, Kilimanjaro 1, Mwanza 2, Katavi 1, Manyara 2, Shinyanga 1, Iringa 1. Aidha, michoro pamoja na gharama za mradi wa ujenzi wa nyumba 5 kati ya nyumba 100 za watumishi wa umma Dodoma vimeandaliwa.

123. Mheshimiwa Spika, hadi kufikia Machi, 2020 Wakala umetekeleza jumla ya Miradi 47 ya Ubunifu na Ujenzi. Miradi hiyo ni pamoja na ujenzi wa Jengo la Ofisi ya Mkurugenzi wa Manispaa ya Kigamboni pamoja na Ofisi ya Mkuu wa wilaya ya Kigamboni umekamilika, Jengo la utawala la Ofisi ya Wilaya ya Mlele (asilimia 30), Jengo la Ofisi ya Halmashauri ya Wilaya ya Butiama (asilimia 47), Jengo la Ofisi ya Mkurugenzi wa Halmashauri ya Mji wa Ifakara (asilimia 40), Jengo la Ofisi ya Mkuu wa wilaya Mkalama (asilimia 51), Jengo la Ofisi ya Mkuu wa wilaya ya Ubungo (asilimia 98), Jengo la Ofisi ya Mkuu wa Wilaya ya Busega (asilimia 95), majengo ya hospitali ya rufaa Geita na Chato (asilimia 89), mradi wa jengo la Ofisi ya TANROADS – Dodoma (asilimia 25) na jengo la Mkurugenzi wa Halmashauri ya Ubungo (asilimia 50).

124. Mheshimiwa Spika, Wakala vilevile umetekeleza jumla ya miradi 38 ya ujenzi. Baadhi ya miradi hiyo ni Ujenzi wa jengo la Ofisi ya

Rais, Menejimenti ya Utumishi na Utawala Bora, ujenzi wa Jengo la Hospitali ya Halmashauri ya Mji wa Tunduma awamu ya pili, ujenzi wa Jengo la Mionzi na Upasuaji, jengo la Maabara pamoja na banda la kuunguzia taka katika Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Simiyu ukarabati wa Ofisi ya Mkuu wa Mkoa Tabora na hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Tabora ambayo imekamilika. Miradi mingine ni ukarabati wa jengo la Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu awamu ya kwanza (asilimia 95), ukarabati wa nyumba tisa za viongozi wa Serikali Wilaya ya Mwanga (asilimia 75), ujenzi wa jengo la Ofisi ya Halmashauri ya Wilaya Madaba - Songea awamu ya pili (asilimia 63), ujenzi wa Jengo la Ofisi ya Mkuu wa Mkoa Songwe awamu wa pili (asilimia 80), ukarabati wa Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Iringa (asilimia 43) na ujenzi wa jengo la maktaba Chuo Kikuu cha Sayansi na Teknolojia Mbeya (asilimia 95).

125. Mheshimiwa Spika, Wakala pia umetekeleza jumla ya miradi 81 ya ushauri. Miradi hiyo ni pamoja na ujenzi wa majengo ya Ofisi za Wizara na Taasisi mbalimbali za Serikali awamu ya kwanza kwenye Mji wa Serikali (Government City) Dodoma, ujenzi wa jengo la hospitali ya Wilaya ya Kilolo, ukarabati wa jengo la Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Tabora ambayo imekamilika. Miradi mingine ni ujenzi wa majengo ya Ofisi za Wizara na Taasisi mbalimbali za Serikali awamu ya pili ambao uko kwenye hatua za mwisho ya ubunifu, ujenzi wa Ofisi za maji Kimani na Mkoji (asilimia 65), ujenzi wa jengo la utawala la Halmashauri ya Mji wa Bunda (asilimia 87), ujenzi wa makazi ya Mkuu wa Wilaya ya Butiama (asilimia 95), ujenzi wa Mahakama ya Mwanzo Laela Sumbawanga (asilimia 85), ujenzi wa Mahakama ya Mwanzo Mtowisa pamoja na Msanzi (asilimia 100), ukarabati upanuzi na ujenzi wa miundombinu ya Mahakama Kuu katika mikoa mitano (asilimia 70) na ujenzi wa Jengo la Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Simiyu (asilimia 25).

126. Mheshimiwa Spika, vilevile Wakala umetekeleza jumla ya miradi miwili ya usimamizi. Miradi hiyo ni ujenzi wa majengo ya rada katika mikoa minne ya Dar es Salaam, Kilimanjaro, Mwanza na Songwe ambapo ujenzi umekamilika katika mikoa mitatu isipokuwa mkoa wa Songwe (asilimia 95). Mradi mwingine ni ujenzi wa Vihenge (Silos) vya kuhifadhia nafaka pamoja na maghala kwa ajili ya hifadhi ya chakula (National Food Reserve Agency) katika mikoa nane ya Dodoma, Katavi, Manyara, Njombe, Rukwa, Ruvuma, Shinyanga na Songwe (asilimia 50).

Wakala wa Ufundi na Umeme

127. Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2019/20, Wizara kupitia Wakala wa Ufundi na Umeme Tanzania (TEMESA) ilipanga kuendelea na kazi zifuatazo: Upanuzi wa maegesho upande wa Kigamboni kwa ajili ya kivuko cha Magogoni – Kigamboni; ujenzi wa maegesho ya Bukondo na Zumacheli kwa ajili ya kivuko cha Chato – Nkome; ujenzi wa maegesho ya Nyamisati na Mafia kwa ajili ya kivuko cha Nyamisati – Mafia, ujenzi wa maegesho ya Kayenze na Bezi kwa ajili ya kivuko cha Kayenze – Bezi, ujenzi wa maegesho ya Mlimba na Malinyi kwa ajili ya kivuko cha Mlimba – Malinyi na maegesho ya Itungi Port. Kazi nyingine ni ujenzi na ukarabati wa maegesho ya Kigongo na Busisi kwa ajili ya kivuko cha Kigongo – Busisi, maegesho ya Kilambo na Namoto kwa ajili ya kivuko cha Kilambo – Namoto pamoja na maegesho ya Utete na Mkongo kwa ajili ya kivuko cha Utete – Mkongo.

Wakala vilevile ulipanga kuendelea na ujenzi wa vivuko vipya vitakavyotoa huduma ya usafiri kati ya Nyamisati - Mafia, Bugorola – Ukara, Kayenze – Bezi na Chato – Nkome. Aidha, Wakala ulipanga kufanya manunuzi ya boti tano (5) zitakazotoa huduma ya usafiri kati ya Lindi – Kitunda, Ukerewe (Ilungwa, Nafuba na Gana) na Magogoni – Kigamboni pamoja na manunuzi ya vitendea kazi kwa ajili ya karakana za TEMESA.

128. Mheshimiwa Spika, vilevile Wakala ulipanga kukamilisha ukarabati wa MV Sengerema, MV Kigamboni na MV Misungwi. Aidha, Wakala ulipanga kukarabati MV Tegemeo, MV Mara, MV Ujenzi, MV Ruhuhu na MV KIU. Wakala pia ulipanga kujenga karakana tano (5) mpya katika mikoa ya Songwe, Simiyu, Geita, Njombe na Katavi; kujenga karakana mpya ya kisasa makao makuu ya Serikali (Dodoma) pamoja na kukarabati karakana tano (5) ambazo ni karakana ya Dar es Salaam (MT. Depot), Mtwara, Mbeya, Mwanza na Arusha. Aidha, Wakala ulipanga kuendelea na jukumu lake la msingi la kufanya matengenezo ya magari ambapo magari **46,604** yalipangwa kufanyiwa matengenezo. Kazi nyingine zilizopangwa kutekelezwa ni usimikaji na matengenezo ya mifumo ya umeme, elektroniki, viyoyozzi na majokofu.

129. Mheshimiwa Spika, hadi Machi, 2020 ujenzi wa maegesho ya Kayenze na Bezi pamoja na awamu ya kwanza ya upanuzi wa jengo la abiria katika maegesho ya Magogoni – Kigamboni upande wa Kigamboni mkoani Dar es Salaam umekamilika na awamu ya pili ya upanuzi wa

jengo la abiria na eneo la maegesho ya Kigamboni imeanza. Aidha, ujenzi wa maegesho ya Mlimba na Malinyi pamoja na maegesho ya Itungi *Port* unaendelea, ujenzi wa maegesho ya Bukondo umeanza na ujenzi wa maegesho ya Zumacheli katika kivuko cha Chato – Nkome na maegesho ya Nyamisati – Mafia upo katika hatua ya kumpata mkandarasi.

130. Mheshimiwa Spika, kwa upande wa miradi ya ujenzi wa vivuko, kazi za ujenzi wa kivuko kipya cha Kayenze – Bezi imekamilika. Aidha ujenzi wa kivuko cha Nyamisati – Mafia (Pwani) umefikia asilimia 40, Bugolora – Ukara (Mwanza) umefikia asilimia 70 na Chato - Nkome umefikia asilimia 70. Aidha, ununuzi wa boti mpya 4 za uokozi kwa ajili ya kisiwa cha Ukerewe (Ilugwa, Nafuba na Gana) na Magogoni - Kigamboni pamoja na boti moja ya uokozi kwa kivuko cha Lindi – Kitunda unaendelea.

131. Mheshimiwa Spika, kwa upande wa ukarabati wa vivuko, ukarabati mkubwa wa vivuko MV Sengerema na MV Kigamboni upo katika hatua za mwisho za kukamilika. Aidha, ukarabati wa MV Misungwi unaendelea. Vilevile Wakala upo katika hatua za uchambuzi wa zabuni kwa ajili ya ukarabati wa vivuko MV Tegemeo, MV Musoma, MV Mara pamoja na boti MV KIU.

132. Mheshimiwa Spika, TEMESA imeendelea kutekeleza majukumu ya matengenezo ya magari ambapo hadi Machi, 2020 jumla ya magari **15,960** yalifanyiwa matengenezo. Aidha, miradi **392** ya umeme, miradi **474** ya viyoyozi na miradi **562** ya kieletroniki imetekelezwa. Vilevile, Wakala ulitekeleza miradi ya ushauri wa kihandisi ambapo miradi **16** ni ya umeme, **17** ya majokofu na viyoyozi na **5** ya elektroniki (ICT). Aidha, Wakala umeendelea kusimamia na kuendesha vivuko vya Serikali **30** katika vituo **20** mbalimbali nchini pamoja na kutoa huduma za ukodishaji wa magari na mitambo katika mikoa **19** na kituo kimoja cha *Government Transport Agency* (GTA).

Bodi ya Usajili wa Wahandisi

133. Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2019/20 Bodi ya Usajili wa Wahandisi (ERB) iliweka malengo ya kusajili wahandisi **2,846**, mafundi sanifu **400**, Kampuni za Ushauri wa Kihandisi **23**, kusimamia mafunzo ya kujiendeleza kitaaluma kwa wahandisi wataalam na wahandisi washauri (CPD), kusimamia utekelezaji wa

Mpango wa Mafunzo kwa Vitendo kwa Wahandisi Wahitimu (SEAP) **3,000** pamoja na kukagua shughuli za kihandisi nchini ili shughuli zote za kihandisi zifanywe na wahandisi waliosajiliwa wenye kufuata maadili ya utendaji kazi za kihandisi.

Hadi Machi, 2020, Bodi imesajili wahandisi **2,073** na Kampuni za ushauri wa kihandisi **11**. Idadi hii imefikisha jumla ya wahandisi waliosajiliwa katika ngazi mbalimbali kuwa **27,739** na makampuni ya ushauri wa kihandisi kuwa **359**. Kati ya Wahandisi hao, **25,401** ni Wahandisi wazalendo na **2,338** ni wa kigeni. Kampuni za ushauri wa kihandisi za kizalendo ni **246** na za kigeni ni **113**. Aidha, katika kipindi hicho, Bodi ilifuta usajili kwa wahandisi wataalamu **417**, Wahandisi Washauri **46** na kampuni za ushauri wa Kihandisi **104** kwa kukiuka Sheria ya Usajili wa Wahandisi. Aidha, katika kipindi hiki, jumla ya miradi **81** ilikaguliwa. Wahandisi wa kigeni **97** walibainika kufanya kazi bila usajili ambapo kati yao **65** walikuwa na sifa na hivyo walisajiliwa, na **32** hawakuwa na sifa na hivyo kurejeshwa kwenye nchi zao. Vilevile, Bodi iliandaa warsha 4 katika kanda **4** kwa Wahandisi Wataalam wanaosimamia mafunzo kwa vitendo kwa wahandisi wahitimu.

134. Mheshimiwa Spika, vilevile, Bodi iliendesha Kiapo cha Utii kwa Taaluma (Professional Oath) ambapo jumla ya wahandisi **3,745** waliapishwa. Aidha, Bodi iliendelea kusimamia utekelezaji wa Mpango wa Mafunzo kwa Vitendo kwa wahandisi wahitimu **2,796**. Jumla ya wahandisi wahitimu **7,582** wamepitia Mpango huu tangu uanzishwe mwaka 2003. Vilevile, Bodi kwa kushirikiana na Bodi nyingine za Sekta ya Ujenzi (CRB na AQRB) ziliandaa na kuadhimisha Siku ya Wahandisi 2019 (Annual Engineers' Day 2019 ambayo ilihudhuriwa na wahandisi zaidi ya **3,830**. Mada iliyojadiliwa katika siku ya wahandisi ilikuwa ni **“wajibu wa Wadau wa Sekta ya Ujenzi katika kufikia uchumi endelevu kwa ustawi wa Jamii”**.

Bodi ya Usajili wa Wabunifu Majengo na Wakadiriaji Majenzi

135. Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2019/20, Bodi ya Usajili wa Wabunifu Majengo na Wakadiriaji Majenzi ilipanga kusajili Wataalam **117** katika fani za Ubunifu Majengo, Ukadiriaji Majenzi na fani zinazoshabihiana nazo. Aidha, Bodi ilipanga kusajili kampuni **15** za Ubunifu Majengo na Ukadiriaji Majenzi. Vile vile Bodi ilipanga kuwajengea uwezo wahitimu **60** katika fani za ubunifu majengo, ukadiriaji majenzi na fani zinazoshabihiana nazo kupitia mpango maalumu wa mafunzo kwa vitendo. Bodi pia ilipanga kufanya ukaguzi

wa miradi ya ujenzi **2,000** katika mikoa yote ya Tanzania bara na miradi ya majengo **950**. Aidha, katika kutangaza huduma zake na za wataalamu inaowaratibu.

Hadi Machi, 2020 Bodi imesajili Wataalam **75** ikiwa ni asilimia **64** ya malengo. Aidha, kampuni **16** za Ubunifu Majengo na Ukadiriaji Majenzi zilisajiliwa ikiwa ni asilimia 107 ya malengo. Vilevile wahitimu **108** katika fani za Ubunifu Majengo, Ukadiriaji Majenzi na fani zinazoshabihiana nazo walipatiwa mafunzo kupitia mpango maalumu wa mafunzo kwa vitendo ikiwa ni asilimia 180 ya malengo.

Vilevile, miradi ya ujenzi **1,254** ilikaguliwa ikiwa ni asilimia 63 ya malengo ambapo wataalam na waendelezaji wake walichukuliwa hatua kwa mujibu wa sheria ikiwemo kutozwa faini, kusimamishiwa ujenzi na kufunguliwa mashtaka mahakamani. Kazi nyingine zilizotekelezwa na Bodi ni usajili wa miradi ya majengo **555** ikiwa ni asilimia **58** ya malengo.

Bodi ya Usajili wa Makandarasi

136. Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2019/20, Bodi ilipanga kusajili jumla ya Makandarasi wapya **900** na kukagua jumla ya miradi ya ujenzi **3,100**. Aidha, Bodi ilipanga kuendesha kozi nane (8) za mafunzo katika mikoa ya Dar es Salaam, Mwanza, Mtwara, Arusha, Bukoba, Njombe, Dodoma na Morogoro.

Hadi Machi, 2020 Bodi imesajili jumla ya Makandarasi wapya **718** hivyo kufanya jumla ya makandarasi waliosajiliwa kufikia **11,060**. Aidha, jumla ya miradi **2,711** ilikaguliwa ambapo jumla ya miradi **719** sawa na asilimia **26.5** ilipatikana na mapungufu mbalimbali yakiwemo kutozingatia afya na usalama kazini, kutosajili miradi na kufanya kazi za thamani inayozidi kiwango kinachoruhusiwa kwa daraja husika. Makandarasi waliokutwa na mapungufu walichukuliwa hatua mbalimbali kwa mujibu wa sheria ikiwemo kutozwa faini, kupewa onyo, kusimamishwa kufanya biashara ya ukandarasi na kufutiwa usajili.

Bodi iliendesha kozi **5** za mafunzo kupitia Mpango Maalum wa Mafunzo Endelevu kwa Makandarasi (Sustainable Structured Training Programme – SSTP) katika mikoa ya Dar es Salaam, Arusha, Kagera, Mtwara na Mwanza. Jumla ya makandarasi **441** walishiriki katika mafunzo hayo. Bodi pia iliendelea kuendesha Mfuko wa Kusaidia Makandarasi (Contractors Assistance Fund - CAF) unaotoa dhamana za zabuni na malipo ya awali kwa makandarasi wa ndani walio katika daraja la chini na la kati ili kuwezesha ushiriki wa makandarasi wa ndani katika zabuni na utekelezaji wa miradi mbalimbali. Mfuko huu

umeendelea kuwa na mtaji wa **Shilingi bilioni 3.75** kwa mwaka 2019/20. Aidha idadi ya wanachama wa Mfuko ilipungua kutoka **1,186** mwaka wa fedha 2018/19 hadi kufikia **1,134** mwaka 2019/2020. Kushuka kwa idadi ya wanachama kumetokana na zoezi la kufuta makandarasi waliokosa sifa ya kuendelea na ukandarasi kwa mujibu wa sheria iliyofanyiwa marekebisho mwishoni mwa mwaka 2019.

Baraza la Taifa la Ujenzi

137. Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2019/20, Baraza la Taifa la Ujenzi (NCC) lilitokeleza majukumu mbalimbali ikiwemo kutoa ushauri wa kiufundi kwa wadau mbalimbali wa Sekta ya Ujenzi na kutoa mafunzo ya Usimamizi wa Mikataba katika miradi ya ujenzi kwa wadau **42** kutoka taasisi mbalimbali za umma na binafsi. Kazi nyingine zilizofanyika ni utatuzi na usuluhishi wa migogoro ambapo hadi Machi, 2020 Baraza limefanya utatuzi wa mashauri **144** na usuluhishi wa mashauri **26** kwa njia ya *Adjudication*. Katika kipindi hiki migogoro mipya iliyosajiliwa ilikuwa **37** kwa *Arbitration* na **8** ya *Adjudication*.

138. Mheshimiwa Spika, Baraza pia limeendelea kufanya tafiti kuhusu ushiriki wa wataalam washauri wa ndani (local consultants) katika kutekeleza miradi ya ujenzi, tathmini ya gharama za ujenzi wa majengo yaliyokamilika ili kupata viwango vya gharama (unit cost) ya ujenzi wa majengo ya aina mbalimbali na tathmini ya mafanikio na changamoto za utekelezaji wa miradi ya ujenzi kwa njia ya “Design and Build”. Aidha, Baraza lilifanya ukaguzi wa kiufundi wa miradi ya ujenzi **42** iliyohusisha miradi ya barabara **38** na **4** ya madaraja inayotekelezwa kwa kutumia fedha za Mfuko wa Barabara inayosimamiwa na TANROADS na TARURA mkoa wa Dar es Salaam.

139. Mheshimiwa Spika, Baraza pia limeendelea na jukumu la kukusanya takwimu na taarifa za Sekta ya Ujenzi kwa mwaka 2019/20 ili kuwezesha wadau wa Sekta ya Ujenzi kufuatilia ukuaji wa sekta. Aidha, Baraza liliendelea kukusanya na kuandaa bei za vifaa vya ujenzi na viwango vya mabadiliko ya bei hizo “indices” kwa ajili ya usimamizi wa mabadiliko ya bei ya miradi (Price Fluctuation Formula). Baraza limeandaa na kuchapisha nakala 1,000 za kitabu chenye taarifa za huduma ya vifaa vya ujenzi kwa mwaka 2019/20 (Directory of Construction Materials 2019/20) na lilikuwa linakamilisha uchapishaji wa Jarida la “Construction Business Journal Vol 13, Issue 1/2” la Februari 2020.

140. Mheshimiwa Spika, Baraza limeendelea kuratibu Mpango wa kukuza uwazi na uwajibikaji “Construction Sector Transparency Initiative (CoST)” kupitia ufadhili wa *CoST International Secretariat* ambapo semina kwa taasisi nunuzi za umma na asasi za kiraia Mkoa wa Dodoma juu ya umuhimu wa uwazi katika utekelezaji wa miradi ya ujenzi zimetolewa.

Kituo cha Usambazaji wa Teknolojia Katika Sekta ya Ujenzi na Usafirishaji (Tanzania Transportation Technology Transfer Centre)

141. Mheshimiwa Spika, Kituo hiki kilianzishwa kwa lengo la kuimarisha/kuboresha sekta ya ujenzi na uchukuzi kwa ujumla kwa kutumia mbinu ya ukusanyaji na usambazaji wa teknolojia katika sekta ya ujenzi na uchukuzi kwa wadau.

Katika mwaka wa fedha 2019/20, Kituo kilifanya kazi zifuatazo:

- i. Kituo kimeshiriki katika mkutano mmoja wa kimataifa na mikutano miwili ya ndani ya nchi inayohusu ubunifu na usambazaji wa teknolojia katika sekta ya Ujenzi na Usafirishaji.
- ii. Kituo kilishiriki katika Mkutano wa Kamati ya Kujenga Uwezo ya SADC (Regional Technology Transfer and Capacity Building Committee) chini ya Shirikisho la Mamlaka za Barabara za nchi za SADC uliofanyika Lusaka Zambia kwenye masuala yanayohusu usambazaji wa teknolojia katika Sekta ya Ujenzi na usafirishaji.
- iii. Kituo kimeandaa na kuchapisha nakala 300 za jarida la kituo lenye mada mbalimbali zinazohusu teknolojia, usalama barabarani na agenda mbalimbali za Serikali ya Awamu ya Tano katika kukuza miundombinu ya usafirishaji. Awamu ya tatu ya jarida hilo ipo katika hatua za maandalizi
- iv. Kituo kilishirikiana na Shirikisho la Barabara Tanzania (Tanzania Road Association – TARA) kuandaa *International training on Road Safety Engineering and Audit* iliyofanyika Dar es Salaam na Arusha.
- v. Kituo kimeendelea kutoa huduma za maktaba kuhusu Sekta ya Ujenzi na Usafirishaji na kutekeleza mradi unaolenga kuboresha mifumo na njia za Kituo za utunzaji wa kumbukumbu na upashanaji wa habari za teknolojia.

C.1.2 SEKTA YA UCHUKUZI

142. Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2019/2020, Sekta ya Uchukuzi iliidhinishiwa kiasi cha **Shilingi 3,629,130,373,895** kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo.

Bajeti ya Matumizi ya Kawaida

143. Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2019/2020, Sekta ya Uchukuzi (Fungu 62) ilitengewa **Shilingi 85,408,131,000** kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida. Kati ya fedha hizo, kiasi cha **Shilingi 58,337,187,000** ni fedha za Mishahara na **Shilingi 27,070,944,000** ni fedha za Matumizi Mengineyo. Hadi kufikia Machi, 2020, kiasi cha fedha za Matumizi ya Kawaida kilichotolewa kwa Sekta ya Uchukuzi na Taasisi zake ni **Shilingi 53,404,102,071.14** sawa na asilimia 62.5 ya bajeti iliyoidhinishwa.

Bajeti ya Maendeleo

144. Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2019/2020, Sekta ya Uchukuzi iliidhinishwa jumla ya **Shilingi 3,543,722,242,895** kwa ajili ya kutekeleza Miradi ya Maendeleo. Kati ya fedha hizo, **Shilingi 3,327,716,600,000** ni fedha za Ndani na **Shilingi 216,005,642,895** ni fedha za Nje (mkopo) kutoka Benki ya Dunia. Hadi Machi, 2020, jumla ya fedha zilizokuwa zimetolewa ni **Shilingi 1,009,049,881,683**. Kati ya fedha zilizotolewa, **Shilingi 863,848,881,683** ni fedha za Ndani na Shilingi **145,201,000,000** ni fedha za Nje. Aidha, Mradi wa Ujenzi wa Reli ya *Standard Gauge* uliendelea kutumia **Shilingi 455,623,760,000** zilizobaki katika bajeti ya Mradi huo mwaka 2018/2019 ambazo ziliwekwa katika Akaunti ya Amana (Deposit). Hivyo, kwa ujumla fedha zilizotumika katika utekelezaji wa Miradi katika kipindi cha Julai, 2019 hadi Machi, 2020 ni **Shilingi 1,464,673,641,683** sawa na asilimia **41.3** ya bajeti ya Maendeleo mwaka 2019/20. Utumiaji wa fedha uliathiriwa na mvua kubwa zaidi ya kiwango iliyonyesha kuanzia mwezi Oktoba, 2019 ambapo kazi za ujenzi wa reli ya SGR na ukarabati wa reli ya kati ya *Metre Gauge* (MGR) zilisimama mara kwa mara.

HUDUMA ZA USAFIRI MIJINI NA VIJIJINI

Udhibiti wa Usafiri kwa Njia ya Barabara

145. Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini (LATRA) iliyoanzishwa kwa Sheria ya Bunge Na. 3 ya Mwaka 2019, imeendelea kuhakikisha kuwa huduma za usafiri wa abiria na mizigo mijini na vijijini inapatikana kulingana na mahitaji ya

wananchi na ukuaji wa uchumi. Katika kipindi cha Julai, 2019 hadi Machi, 2020, jumla ya Leseni 41,826 za usafirishaji Abiria zilitolewa ikilinganishwa na Leseni 43,356 zilizotolewa katika kipindi kama hicho katika mwaka 2018/2019. Hii ikiwa ni upungufu wa asilimia 3.53. Kupungua kwa Leseni za Mabasi kulitokana na kupungua kwa mabasi madogo katika njia kuu; na baadhi ya mabasi kukosa sifa ya kutoa huduma na hivyo kuzuiliwa kuendelea kutoa huduma ya usafirishaji. Aidha, katika kipindi cha Julai, 2019 hadi Machi, 2020, Leseni za Malori 94,902 zilitolewa ikilinganishwa na Leseni 84,299 zilizotolewa katika kipindi kama hicho katika mwaka 2018/2019. Hii ni sawa na ongezeko la asilimia 12.58.

146. Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia LATRA imeendelea kudhibiti Viwango vya Tozo na nauli katika usafiri wa barabara kwa kuzingatia maboresho ya barabara kwa kiwango cha lami, kuanzishwa njia mpya na maombi maalum ya watoa huduma. Katika kipindi cha Julai, 2019 hadi Machi, 2020, Mamlaka ilifanya mapitio ya viwango vya nauli za mabasi na kuhuisha viwango hivyo kwa njia za Mikoa ya Dar es Salaam, Mwanza, Njombe, Manyara, Katavi, Dodoma, Rukwa, Kigoma na Pwani. Taarifa kuhusu viwango hivyo inapatikana kupitia tovuti ya Mamlaka (www.latra.go.tz). Aidha, katika kipindi hicho, Mamlaka ilifanya ufuatiliaji wa taarifa zilizoashiria kuwepo kwa ukiritimba katika utoaji wa huduma kwa njia ya Dar es Salaam – Songea kupitia Lindi ili kujiridhisha na ubora wa huduma inayotolewa, nauli na kiwango cha ushindani. Katika uchunguzi huo, ilibainika kuwa huduma inayotolewa ni ya ubora unaokubalika na nauli zilionekana kuwa chini ya nauli elekezi iliyotolewa na Mamlaka.

147. Mheshimiwa Spika, Wizara kwa kushirikiana na wadau mbalimbali imeendelea kuchukua hatua ili kupunguza ajali zinazoendelea kutokea. Hatua zilizochukuliwa ni pamoja na kuimarisha usalama wa huduma za usafiri wa nchi kavu, kuepuka makosa ya kibinadamu katika vivuko vya Reli na Barabara na kudhibiti waendesha pikipiki (bodaboda). Katika kipindi cha Julai, 2019 hadi Machi, 2020, LATRA ilifanya kaguzi za barabarani kwa Malori, Mabasi, Pikipiki na Bajaji zipatazo 800 katika Mikoa 26. Lengo ni kubaini utekelezaji wa masharti ya Leseni na kufuatilia utendaji wa Mfumo wa Kudhibiti Mwendu kasi (Vehicle Tracking System). Mfumo huo ulibaini matukio 17,895 ya Mabasi kutembea zaidi ya mwendo unaokubalika kwa Mabasi hayo. Mabasi hayo yalichukuliwa hatua mbalimbali ikiwa

ni pamoja na kuwatoza faini na kufungia baadhi ya Mabasi kuendelea kutoa huduma ya usafirishaji wa abiria.

148. Mheshimiwa Spika, Serikali imeendelea kuhakikisha kuwa Mifumo ya Kielektroniki inatumika katika usafiri wa Nchi Kavu. Utumiaji wa Mifumo hii unarahisisha utendaji kazi, kuongeza uwazi na uwajibikaji, kudhibiti mapato ya Serikali, kutoa takwimu sahihi, kupunguza gharama za uendeshaji na kusaidia kuondoa changamoto ya wapiga debe kwenye vituo vya mabasi. Katika kipindi cha Julai, 2019 hadi Machi, 2020, Mamlaka iliendelea kuimarisha matumizi ya Mfumo wa Kufuatilia Mwenendo wa Vyombo vya Uchukuzi (Vehicle Tracking System - VTS). Vyombo hivyo ni Mabasi ya masafa marefu na Treni. Lengo ni kuimarisha shughuli za udhibiti wakati wote na mahali popote vyombo hivyo vilipo. Hadi Machi, 2020, jumla ya Mabasi ya masafa marefu 4,030 na Treni tatu (3) zilikuwa zimeunganishwa kwenye mfumo huo. Kazi ya uunganishaji wa Mabasi mengine zaidi katika mfumo huu inaendelea kwa Mabasi yote yanayotoa huduma kwenye njia ndefu na fupi.

Aidha Machi 2020 LATRA ilizindua mfumo wa Tiketi za kielektroniki kwa mabasi ya Abiria.

Napenda kuwasihi wamiliki wote wa vyombo vya usafiri kupitia ushirika wao waongeze juhudi za kutoa Tiketi za Kielektroniki. Tunakoelekea, Tiketi zisizo za Kielektroniki hazitatambulika kabisa. Utaratibu huu utasaidia katika kurahisisha upatikanaji wa huduma na udhibiti wa mapato yatokanayo na huduma inayotolewa.

Udhibiti wa Usafiri kwa Njia ya Reli

149. Mheshimiwa Spika, usafiri kwa njia ya Reli umeendelea kudhibitiwa na LATRA. Mamlaka hii imeendelea kutoa huduma za udhibiti ili kuboresha usalama wa usafiri wa Treni nchini. Katika kipindi cha Julai, 2019 hadi Machi, 2020, Mamlaka imefanya ukaguzi wa usalama wa Treni, Mabeheva ya Mizigo na Abiria, na madaraja ya Treni; ufuatiliaji wa vyanzo vya ajali za Treni na umwagikaji wa mafuta katika njia zote za Reli zinazoendeshwa na Mamlaka ya Reli ya Tanzania na Zambia (TAZARA) na Shirika la Reli (TRC). Kazi nyingine zilizotekelezwa ni ufungaji wa Mfumo wa *Vehicle Tracking System* kwenye vichwa vitatu (3) vya Treni ya TAZARA kwa ajili ya majaribio.

Baada ya kukamilika kwa majaribio hayo, vichwa vyote vya Treni vitafungwa Mfumo huo ili kuboresha utendaji na kuongeza ufanisi wa usafiri wa Reli.

150. Mheshimiwa Spika, Serikali inaendelea kujiandaa na utoaji wa huduma za usafiri wa Reli ya Kati ya *Standard Gauge* (SGR). Katika maandalizi hayo TRC limekabidhiwa orodha ya Viwango vya Ukaguzi wa mwisho wa Miundombinu ya SGR (SGR Commissioning Checklist) ili kuliandaa Shirika kutambua vipengele muhimu vya kiusalama na viwango vitakavyotumika kwenye ukaguzi wa mwisho wa SGR kabla ya kuanza kutumika. Aidha, ili kuwapa watendaji wa Shirika la Reli uelewa wa vipengele vya kiusalama vya SGR, Disemba, 2019, LATRA iliratibu zoezi la utoaji wa mafunzo ya kitaalam kwa watendaji 50 wa TRC.

Huduma za Usafiri wa Treni Mijini

151. Mheshimiwa Spika, Serikali imeendelea kutekeleza maelekezo ya Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2015 katika eneo la uboreshaji wa utoaji wa huduma za usafiri katika Jiji la Dar es Salaam ili kupunguza msongamano wa Magari barabarani. Katika kipindi cha Julai, 2019 hadi Machi, 2020, jumla ya abiria 1,626,194 walisafirishwa kwa njia ya Reli kati ya Stesheni za Dar es Salaam na Mwakanga kwa kutumia Reli ya TAZARA. Hii ni sawa na upungufu wa asilimia 4.3 ikilinganishwa na abiria 1,700,685 waliosafirishwa katika kipindi kama hicho mwaka 2018/2019. Upungufu uliojitokeza umetokana na maboresho makubwa yaliyofanyika katika usafiri wa Barabara na kufunguliwa kwa barabara ya juu eneo la TAZARA (Mfugale Flyover).

Kwa upande wa TRC, katika kipindi cha Julai, 2019 hadi Machi, 2020, Abiria waliohudumiwa kati ya Stesheni ya Kamata - Ubungo na Pugu ni 2,421,258 ikilinganishwa na abiria 3,077,966 waliosafirishwa katika kipindi kama hicho mwaka 2018/2019. Sababu za kushuka kwa utendaji ni pamoja na kuhamishwa kwa kituo (Station) kutoka Stesheni ya Dar es Salaam kwenda Kamata ili kupisha ujenzi wa Reli ya SGR na kukamilika kwa daraja la juu la Mfugale ambalo limepunguza msongamano katika eneo la makutano la TAZARA.

Shirika la Reli Tanzania (TRC)

152. Mheshimiwa Spika, katika Hotuba ya mwaka 2019/2020, tuliahidi kuendelea na ujenzi wa awamu ya kwanza ya Mradi wa Reli ya kati kwa *Standard Gauge* kutoka Dar es salaam hadi Mwanza (Km 1,219). Napenda kulitaarifu Bunge lako tukufu kuwa hadi kufikia Machi, 2020, ujenzi wa kipande cha reli kutoka Dar es Salaam hadi Morogoro (Km 300) umekamilika kwa asilimia 76.63. Kazi zilizotekelezwa ni pamoja na:

- i. Ujenzi wa Makalvati umekamilika kwa asilimia 97;
- ii. Ujenzi wa Madaraja umekamilika kwa asilimia 76;
- iii. Ujenzi wa Daraja refu katikati ya Jiji la Dar es Salaam lenye urefu wa kilomita 2.54 umekamilika kwa asilimia 85.04;
- iv. Kazi ya ukataji wa miinuko na ujazaji wa mabonde (earthworks) umekamilika kwa asilimia 83.14;
- v. Ujenzi wa Miundominu ya umeme kwa ajili ya kuendeshea Treni umekamilika kwa asilimia 82;
- vi. Utandikaji wa Reli umekamilika kilometa 73; na
- vii. Kazi ya ujenzi wa Stesheni za Dar es Salaam, Pugu, Soga, Ruvu na Ngerengere umekamilika kwa asilimia 48.08.

153. Mheshimiwa Spika, hadi kufikia Machi, 2020, ujenzi wa Reli sehemu ya Morogoro hadi Makutupora (km 422) umekamilika kwa asilimia 28 na ujenzi huo unatarajiwa kukamilika Februari, 2021. Kazi zinazoendelea kwa sasa ni pamoja na utwaaji wa ardhi; ukataji wa miinuko na ujazaji wa mabonde kwa ajili ya kujenga tuta la reli (earthworks). Aidha, majadiliano na mtoa huduma (Manufacturer) kuhusu ujenzi wa mabehewa ya abiria yatakayotumika kutoa huduma ya usafiri wa abiria kwenye reli ya *Standard Gauge* yanaendelea.

154. Mheshimiwa Spika, kwa upande wa ujenzi wa vipande vilivyobaki vya Makutupora – Tabora (km 295), Tabora – Isaka (km 133), na Isaka – Mwanza (km 250), upembuzi yakinifu na usanifu wa awali umekamilika na Serikali imepanga kuanza ujenzi huku ikiendelea na juhudi za kutafuta fedha. Aidha, Serikali inaendelea na majadiliano na Taasisi za fedha na washirika wa maendeleo. Walioonesha nia hadi sasa ni pamoja na Benki ya Maendeleo ya Biashara (Trade Development Bank - TDB) na Benki ya Maendeleo ya Afrika (AfDB).

155. Mheshimiwa Spika, njia ya reli ya Kati inayotumika sasa (Meter Gauge Railway - MGR) ni muhimu kwa kusafirisha mizigo, abiria na bidhaa mbalimbali kuelekea katika maeneo ya kanda za Ziwa, Magharibi na Kaskazini mwa nchi yetu. Pia, njia hii inatumika kusafirisha mizigo inayoelekea nchini Uganda, DR Congo, Rwanda na Burundi. Ili reli hii iendelee kutoa huduma hizo ikiwa ni pamoja na kusaidia katika ujenzi wa reli ya SGR, kazi ya ukarabati wa njia ya reli kwa kuondoa reli zote nyepesi na kuweka reli mpya zenye uzito wa ratili 80 kwa yadi kati ya stesheni ya Dar es Salaam na Isaka imeendelea kutekelezwa. Kazi ya ukarabati wa sehemu ya Dar es Salaam hadi Kilosa (km 283) imekamilika kwa asilimia 83.7 na inatarajiwa kukamilika Juni, 2020. Aidha, sehemu ya Kilosa hadi Isaka (km 687) imekamilika kwa asilimia 85 na itakamilika mwishoni mwa Mei, 2020.

156. Mheshimiwa Spika, kwa upande wa ufufuaji wa njia ya reli ya kutoka Tanga hadi Arusha (km 439), Serikali kupitia TRC inaendelea na ukarabati wa reli hii ili kutoa huduma za usafiri wa abiria na mizigo. Aidha, kazi ya ukarabati wa reli imekamilika kwa kipande cha Tanga hadi Moshi (km 353) na njia inapitika. Ukarabati kwa kipande cha Moshi hadi Arusha (km 86) unaendelea na kazi ya urudishaji njia imefikia asilimia 95 wakati kazi ya kubadilisha reli zenye uzito wa ratili 45 kwenda uzito wa ratili 60 imefikia asilimia 40. Lengo ni kukamilisha kazi hizo ifikapo Juni, 2020.

157. Mheshimiwa Spika, mvua zilizonyesha kuanzia Oktoba, 2019 zilileta athari kubwa katika miundombinu ya uchukuzi nchini. Kwa upande wa miundombinu ya Reli, mvua hizi ziliathiri kwa kiasi kikubwa miundombinu hiyo hususan Reli ya Kati inayotumika sasa (Meter Gauge Railway - MGR). Katika kipindi cha Oktoba, 2019 hadi Januari, 2020, Reli ya Tanga hadi Arusha ilifungwa kutokana na uharibifu wa reli uliosababishwa na mvua katika maeneo ya Mkalamo - Korogwe Korogwe na Muheza. Aidha, katika kipindi cha Januari hadi Februari 2020, huduma za usafiri wa abiria na mizigo kwa watumiaji wa Reli ya Kati kuanzia Dar es Salaam hadi Mwanza na Kigoma pia iliathirika baada ya eneo la Zuzu – Kigwe – Bahi na Kilosa – Gulwe kujaa maji kutokana na mvua. Vile vile, reli ya Kaliua hadi Mpanda ilisombwa na maji eneo la Mto Ugala na kusababisha kusitisha huduma mapema Aprili 2020. Hata hivyo, Serikali imeendelea kuchukua hatua mbalimbali ili kuhakikisha kuwa huduma zinarejea haraka. Hatua hizo ni pamoja na kurudisha miundombinu

iliyoharibiwa, kukarabati madaraja na mifereji ili kuruhusu maji kupita kwa haraka na kuendelea kufanya tafiti ili kupata ufumbuzi wa kudumu wa athari za maji ya mvua.

158. Mheshimiwa Spika, miradi mingine iliyoendelea kutekelezwa katika mwaka 2019/2020 ni pamoja na:

- (i) Kazi ya usanifu wa kina wa kuinua kiwango cha njia ya reli kati ya Tabora - Kigoma na Kaliua – Mpanda. Kazi hii inatarajiwa kukamilika Juni, 2020;
- (ii) Usanifu wa awali kwa ajili ya ujenzi wa reli ya Uvinza - Musongati (Burundi) yenye urefu wa Km 200 kwa *Standard Gauge*. Kazi hii inategemewa kukamilika Juni, 2020;
- (iii) Kuboresha eneo la treni la kupakia/kupakua mizigo katika Bandari ya Dar es Salaam na kukarabati vituo vya kuhudumia mizigo vya Ilala na Isaka. Kazi hii inategemewa kukamilika Juni, 2020;
- (iv) Upembuzi yakinifu na usanifu wa awali wa ujenzi wa njia za reli katika Jiji la Dodoma. Kazi hii inategemewa kukamilika Septemba, 2020;
- (v) Ukarabati wa mabehewa ya mizigo 200 na vichwa vya treni saba (7) vya TRC kwa ajili ya sogeza. Kazi hii inategemewa kukamilika Juni, 2020;
- (vi) Kukamilisha ujenzi wa njia ya reli kwenda bandari kavu ya Kwala, Ruvu;
- (vii) Ununuzi wa vichwa vya treni vitatu (3) ambavyo vinategemewa kufika Oktoba, 2020 na mabehewa ya mizigo 44 yanayotarajiwa kuwasili Juni, 2020; na
- (viii) Kuendelea na maandalizi ya ujenzi wa reli ya Mtwara – Mbambabay na matawi ya Mchuchuma na Liganga kwa Ubia kati ya Sekta Binafsi na Umma (PPP).

159. Mheshimiwa Spika, kwa upande wa utoaji wa huduma za usafiri, katika kipindi cha Julai, 2019 hadi Machi, 2020, TRC ilisafirisha tani 211,392 za mizigo ikilinganishwa na tani 275,843 zilizosafirishwa katika kipindi kama hicho kwa mwaka 2018/2019. Huu ni upungufu wa asilimia 23.4. Kwa upande wa abiria, katika kipindi cha Julai, 2019 hadi Machi, 2020, abiria 327,727 walisafirishwa ikilinganishwa na abiria 421,585 waliosafirishwa katika kipindi kama hicho mwaka 2018/2019. Huu ni upungufu wa asilimia 22.3. Sababu

za upungufu katika utoaji wa huduma ni pamoja na kufungwa kwa njia kwa saa 72 kwa wiki ili kupisha ukarabati wa njia ya reli ya kutoka Dar es Salaam hadi Isaka pamoja na kufungwa kwa njia kutokana na mafuriko katika maeneo mbalimbali ya miundombinu ya reli.

Mamlaka ya Reli ya Tanzania na Zambia (TAZARA)

160. Mheshimiwa Spika, reli ya TAZARA ina umuhimu wa kipekee katika kuchangia maendeleo ya jamii kwa kuinua uchumi wa Tanzania na Zambia kupitia huduma za usafirishaji, upatikanaji wa ajira na kuchochea ukuaji wa miji na biashara. Aidha, reli hii imebeba historia na mahusiano ya kidiplomasia baina ya Tanzania, Zambia na China. Kutokana na umuhimu huo, nchi wanahisa zimeendelea kuchukua hatua mbalimbali za kuhakikisha kuwa TAZARA inaendelea kutoa huduma. Hatua hizo kwa upande wa Tanzania ni pamoja na kuendelea na taratibu za kutunga Sheria mpya ya TAZARA ili kuimarisha utendaji; kulipa mishahara ya wafanyakazi wa TAZARA upande wa Tanzania; kuendelea kukarabati injini na mabehewa; kuendelea kutoa fedha za uendeshaji na uwekezaji wa TAZARA na kuendelea kufanya matengenezo makubwa ya njia ili kupunguza idadi ya sehemu zilizowekwa katazo la mwendo kasi wa treni.

161. Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha Julai, 2019 hadi Machi, 2020, TAZARA imeendelea kutoa huduma za kusafirisha abiria na mizigo kati ya Dar es Salaam na New Kapiri Mposhi, Zambia. Katika kipindi hicho, jumla ya shehena ya tani 125,562 za mizigo zilisafirishwa ikilinganishwa na tani 134,701 zilizosafirishwa katika kipindi kama hicho mwaka 2018/2019 sawa na upungufu wa asilimia 6.7. Upungufu huu umetokana na uchache na umadhubuti (Reliability) wa injini, nchi za Zambia na DR Congo kuanzisha tozo kwenye madini yanayosafirishwa nje ya nchi na uchaguzi wa DR Congo. Kuhusu usafirishaji wa abiria, katika kipindi cha Julai, 2019 hadi Machi, 2020, jumla ya abiria 661,551 wa njia ndefu walisafirishwa ikilinganishwa na abiria 673,904 waliosafirishwa katika kipindi kama hicho mwaka 2018/2019. Utendaji huu ni pungufu kwa asilimia 1.8.

Ili kukabiliana na changamoto ya kushuka kwa utendaji, TAZARA ilikarabati mabehewa ya mizigo 19, mabehewa ya abiria matatu (3), kubadilisha mataruma ya zege 6,731 na mataruma ya mbao 2,647, kusambaza na kushindilia kokoto tani 9,350, na kufanya matengenezo

ya kawaida ya njia na vitendea kazi.

162. Mheshimiwa Spika, itakumbukwa kuwa katika mwaka 2017/2018, Serikali ilitenga fedha kwa ajili ya kununua vipuri 42 vya Injini (Traction Motors) na mitambo ya kusaidia uzalishaji wa kokoto na mataruma ya zege (Dump Truck, Excavator and Drill Rig) katika mgodi wa kokoto ulioko Kongolo - Mbeya. Napenda kutoa taarifa kuwa, hadi Machi, 2020, vipuri 18 vya injini (Traction Motors) na mitambo mitatu (3) (Dump Truck, Excavator na Drill Rig) tayari vimepokelewa. Kazi ya kufunga vifaa na mitambo hii ili kuboresha utendaji inaendelea. Vipuri 24 vya injini vilivyobaki vitawasili nchini mwishoni mwa Mei, 2020.

163. Mheshimiwa Spika, Serikali za Tanzania na Zambia kwa upande mmoja na Serikali ya Jamhuri ya Watu wa China kwa upande mwingine zipo katika hatua za mwisho za kukamilisha taratibu za Makubaliano ya Itifaki ya 16 ya ushirikiano wa kiufundi. Kupitia Itifaki hizi, Serikali ya China imekuwa ikitoa mikopo yenye masharti nafuu kwa TAZARA. Miradi itakayotekelezwa kupitia Itifaki ya 16 ni pamoja na ununuzi wa vipuri vya kuimarisha njia ya reli, vichwa vya treni na mabehewa.

USAFIRI NA UCHUKUZI KWA NJIA YA MAJI

164. Mheshimiwa Spika, Wizara imeendelea kuhakikisha kuwa usafiri na uchukuzi kwa njia ya maji unaendelea kutolewa kwa ufanisi na weledi. Aidha, Serikali itaendelea kuhakikisha kuwa Tanzania inanufaika na uchumi wa bahari (blue economy) na maziwa. Lengo ni kufaidika na fursa zitokanazo na kuboresha huduma bora za kibandari na usafiri kwa njia ya maji. Katika mwaka 2019/2020, huduma za usafiri kwa njia ya maji zimeendelea kutolewa na Kampuni inayomilikiwa kwa pamoja kati ya Tanzania na China (SINOTASHIP), Kampuni ya Huduma za Meli katika Maziwa (MSCL) na Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari Tanzania (TPA) pamoja na sekta binafsi.

Huduma za Uchukuzi Baharini

165. Mheshimiwa Spika, uchukuzi wa masafa marefu baharini umeendelea kutolewa na SINOTASHIP. Kampuni hii imeendelea kuimarisha ushirikiano kati ya Tanzania na China kwa zaidi ya miaka 50 kwa meli zake kubeba mizigo kati ya nchi hizi mbili na sehemu

nyingine ulimwenguni kote. Aidha, SINOTASHIP imeendelea kutoa huduma ya uchukuzi wa mizigo wa masafa marefu baharini kwa kutumia meli yake kubwa (MV Changshun II) yenye uwezo wa kubeba tani 57,000 kwa ufanisi.

166. Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha Julai, 2019 hadi Machi, 2020, Kampuni hii ilisafirisha jumla ya tani 600,000 za shehena ya mizigo ikilinganishwa na jumla ya tani 598,000 zilizosafirishwa katika kipindi kama hicho mwaka 2018/2019.

167. Mheshimiwa Spika, pamoja na utendaji huo, Kampuni ya SINOTASHIP imekuwa na manufaa yafuatayo kwa Serikali yetu:

- i. Kuimarisha uhusiano kati ya Tanzania na China ili kuendelea kuenzi maono yalioanzishwa na hayati Baba wa Taifa Mwalimu Julius K. Nyerere na aliyekuwa Waziri Mkuu wa China Zhou Enlai;
- ii. Kutoa fursa ya mafunzo kwa vitendo kwa vijana wa kitanzania wanaosoma masomo ya masuala ya uchukuzi kwa njia ya maji kutoka Vyuo vya DMI, NIT na Chuo cha Bandari; na
- iii. Kukiunganisha Chuo cha Bahari (DMI) na mashirika ya meli ya China yanayohitaji vijana wa kufundisha na kuajiri kutoka Tanzania.

Huduma za Uchukuzi Katika Maziwa

168. Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2019/2020, Kampuni ya Huduma za Meli kwenye Maziwa (MSCL) iliendelea kutoa huduma za uchukuzi na usafiri kwenye maziwa ya Victoria, Tanganyika na Nyasa. Aidha, Serikali imeendelea kuhamasisha na kuboresha utoaji wa huduma hizo kupitia sekta binafsi. Katika kipindi cha Julai, 2019 hadi Machi, 2020, Kampuni ya Huduma za Meli kwenye Maziwa ilisafirisha abiria 67,922 ikilinganishwa na abiria 79,049 waliosafirishwa katika kipindi kama hicho mwaka 2018/2019. Huu ni upungufu wa asilimia 14.08. Sababu za kushuka kwa abiria waliosafirishwa ni pamoja na MV. Liemba kusimama kutoa huduma na idadi kubwa ya meli zikiwa katika matengenezo; hivyo, Kampuni kutoa huduma ya usafirishaji wa abiria kwa kutumia Meli moja ya MV Clarias. Kuhusu usafirishaji wa mizigo, katika kipindi cha Julai, 2019 hadi Machi, 2020, jumla ya tani za mizigo 27,576 zilisafirishwa ikilinganishwa na tani mizigo 22,773.36

zilizosafirishwa katika kipindi kama hicho mwaka 2018/2019. Hii ni sawa na ongezeko la asilimia 21.1.

169. Mheshimiwa Spika, Serikali imeendelea kuhakikisha kuwa Kampuni inapata watumishi wenye weledi ili kuimarisha utendaji wake. Katika kipindi cha Julai, 2019 hadi Machi, 2020, Kampuni iliajiri watumishi wapya watano (5) na kupata kibali cha kuajiri watumishi wapya 48 wenye fani ya uendeshaji wa Meli, watumishi 12 wa kuhamia kutoka katika Taasisi nyingine za Serikali na kuazima wataalamu wanane (8) waliobobea katika fani ya uendeshaji meli kutoka Jeshi la Wanamaji Tanzania (Navy). Kampuni kwa kushirikiana na mamlaka mbalimbali za Serikali inaendelea kutekeleza maelekezo yaliyo katika vibali vya kuongeza idadi ya wataalam, zoezi ambalo litakamilika Juni, 2020.

170. Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha Julai, 2019 hadi Machi, 2020, MSCL iliendelea kutekeleza kazi zifuatazo:

- i. Ujenzi wa Meli mpya ya MV. Mwanza (Hapa Kazi tu) yenye Uwezo wa kubeba abiria 1,200 na tani 400 za mizigo katika Ziwa Victoria. Ujenzi wa Meli hii umekamilika kwa asilimia 60;
- ii. Ujenzi wa Chelezo ambao umekamilika kwa asilimia 96.5; na
- iii. Ukarabati wa Meli ya MV Victoria ambao umekamilika kwa asilimia 98 na ukarabati wa Meli ya MV Butiama uliokamilika kwa asilimia 98. Meli hizi ziko katika Ziwa Victoria.

Huduma za Bandari

171. Mheshimiwa Spika, Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari (TPA) imeendelea kusimamia jumla ya bandari 89 zilizo katika mwambao wa bahari ya Hindi na kwenye Maziwa Makuu ya Victoria, Tanganyika na Nyasa. Kati ya bandari hizo, bandari 18 ziko katika mwambao wa Bahari ya Hindi; bandari 31 katika Ziwa Victoria; bandari 25 katika Ziwa Tanganyika; na bandari 15 katika Ziwa Nyasa. Aidha, hadi Machi, 2020, jumla ya Bandari zisizo rasmi 694 zilitambuliwa. Kati ya hizo, bandari 240 ziko katika mwambao wa bahari ya Hindi; Bandari 329 katika ziwa Victoria, Bandari 108 katika ziwa Tanganyika na Bandari 17 katika ziwa Nyasa. Hadi sasa, Bandari 120 sawa na asilimia 17 ya Bandari zisizo rasmi zimerasimishwa.

172. Mheshimiwa Spika, ili kuhimili ushindani wa kimasoko, Januari, 2020, Wizara kupitia Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari ilifanya utafiti wa kimasoko wa kufahamu mahitaji ya soko la Zambia na uwezo wa Bandari ya Beira. Kwa kuwa Zambia ni soko kubwa la Bandari ya Dar es Salaam, utafiti huu utasaidia kujua mahitaji ya wateja na wadau wengine. Lengo la utafiti huu ni kuzidi kuboresha huduma za Bandari za Tanzania na kuendelea kuongeza kiwango cha umiliki wa soko hili. Aidha, katika kipindi cha Julai, 2019 hadi Machi, 2020, Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari ilihudumia jumla ya tani za mapato milioni 7.137 za shehena za mizigo ikilinganishwa na tani za mapato milioni 6.934 zilizohudumiwa katika kipindi kama hicho mwaka 2018/2019. Utendaji huu ni sawa na ongezeko la asilimia 14. Kati ya shehena hiyo, Bandari ya Dar es Salaam ilihudumia jumla ya tani milioni 6.454 na bandari nyingine tani laki 683 za shehena. Pia, katika kipindi hicho, Kitengo cha Shehena Mchanganyiko (General Cargo) cha TPA kilihudumia makasha (TEUs) 110,193 ikilinganishwa makasha (TEUs) 77,327 yaliyohudumiwa katika kipindi kama hicho katika mwaka 2018/2019, sawa na ongezeko la asilimia 42.5. Kwa upande wa TICTS, Kitengo kilihudumia makasha (TEUs) 453,837 ikilinganishwa makasha (TEUs) 389,428 yaliyohudumiwa katika kipindi kama hicho katika mwaka 2018/2019, sawa na ongezeko la asilimia 16.5.

173. Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha Julai, 2019 hadi Machi, 2020, shehena ya nchi jirani iliyohudumiwa kupitia Bandari ya Dar es Salaam ilikuwa tani milioni 5.545 ikilinganishwa na tani milioni 4.694 zilizohudumiwa katika kipindi kama hicho katika mwaka 2018/19. Hili ni ongezeko la asilimia 18.1. Nchi zinazohudumiwa na Bandari zetu ni Uganda, Rwanda, Burundi, DR Congo, Zambia na Malawi. Vilevile, TPA inahudumia kwa kiasi kidogo shehena za Zimbabwe, Comoro, Sudani Kusini na Msumbiji.

174. Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha Julai, 2019 hadi Machi, 2020, Shehena ya Magari iliyohudumiwa katika Bandari ya Dar es Salaam iliongezeka hadi magari 129,714 kutoka magari 120,229 yaliyohudumiwa katika kipindi kama hicho mwaka 2018/19, sawa na ongezeko la asilimia 7.8.

175. Mheshimiwa Spika, ongezeko la mizigo na magari katika bandari za humu nchini lilitokana na kampeni zilizoendelea kufanyika

katika nchi zote za jirani na kupunguza vikwazo visivyo vya kiforodha. Aidha, ili kuongeza uwezo wa bandari ya Dar es Salaam na kupunguza msongamano, kazi ya ujenzi wa Bandari Kavu eneo la Kwala, Ruvu inaendelea kutekelezwa kupitia Mkandarasi SUMA JKT na Shirika la Reli Tanzania. Kazi ya ujenzi wa yadi, njia ya reli na ofisi za muda kwenye eneo la ujenzi wa awamu ya kwanza lenye ukubwa wa hekta 5 ilianza Juni, 2019 na inatarajiwa kukamilika mwishoni mwa Mei, 2020. Mradi huu unafuatiliwa kwa pamoja na wadau wote wa Sekta ya Umma na Binafsi ili kuhakikisha kuwa uendeshaji wake unakidhi mahitaji ya wadau wote.

176. Mheshimiwa Spika, miradi ya kuboresha Bandari za Mwambao wa Bahari ya Hindi za Dar es Salaam, Tanga na Mtwara inaendelea kutekelezwa kwa mafanikio. Kazi zinazoendelea kutekelezwa ni pamoja na:

a. Bandari ya Dar es Salaam:

- i. Uboreshaji wa Gati namba 5 – 7 na kuchimba lango la kuingilia Meli na eneo la kugeuzia Meli (entrance channel and turning basin);
- ii. Ujenzi wa Yadi ya shehena ya magari;
- iii. Ujenzi wa Bandari kavu eneo la Kwala-Ruvu (Vigwaza);
- iv. Ununuzi wa mitambo na vifaa vya kuhudumia mizigo; na
- v. Ujenzi wa Maghala ya Kuhifadhia mizigo.

b. Bandari ya Tanga:

- i. Kupanua na kuchimba lango la kuingilia na eneo la kugeuzia Meli (entrance channel and turning basin);
- ii. Kuongeza kina cha Bandari kutoka mita nne (4) hadi mita 15;
- iii. Maandalizi ya ujenzi wa miundombinu ya Gati la mafuta ghafi kutoka Uganda;
- iv. Ukarabati wa Zahanati;
- v. Ujenzi wa nyumba moja ya wafanyakazi; na
- vi. Ujenzi wa uzio katika eneo la Chongoleani.

c. Bandari ya Mtwara:

- i. Ujenzi wa awamu ya kwanza ya Gati la mita 300 la kuhudumia Shehena mchanganyiko (Multi-Purpose Terminal);

- ii. Ujenzi wa kituo cha mafuta;
- iii. Ukarabati wa Gati la Kilwa; na
- iv. Ujenzi wa Kinu cha kuhifadha korosho bandarini.

177. Mheshimiwa Spika, katika bandari za kwenye Maziwa ya Victoria, Tanganyika na Nyasa, kazi zilizoendelea kutekelezwa ni pamoja na:

a. Bandari za Ziwa Victoria:

- i. Ujenzi wa Ghala la mizigo, sehemu ya Abiria na majengo mengine katika Bandari ya Kyamkwikwi na Mwigobero;
- ii. Ujenzi wa Bandari ya Kasenda iliyopo kijiji cha Mganza wilayani Chato;
- iii. Ujenzi wa Nyumba moja ya wafanyakazi katika Bandari ya Mwanza; na
- iv. Kuboresha Gati la Chato.

b. Bandari za Ziwa Tanganyika:

- i. Ujenzi wa Bandari ya Karema;
- ii. Ujenzi wa Barabara - Bandari ya Kagunga;
- iii. Ujenzi wa Gati za Kibirizi, Ujiji na Ofisi ya Mkuu wa Bandari-Kigoma;
- iv. Uboreshaji na upanuzi wa Bandari ya Kasanga;
- v. Ujenzi wa Miundombinu na Gati la Bandari ya Kabwe; na
- vi. Ujenzi wa miundombinu na Gati la Bandari ya Lagosa.

c. Bandari za Ziwa Nyasa:

- i. Ujenzi wa Nyumba ya Meneja wa Bandari;
- ii. Ujenzi wa Gati la Ndumbi; na
- iii. Ujenzi wa Uzio wa Bandari ya Itungi.

Udhibiti wa Huduma za Usafiri wa Majini

178. Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia Shirika la Uwakala wa Meli Tanzania (Tanzania Shipping Agencies Corporation - TASAC) imeendelea kuratibu zoezi la utafutaji, uokozi na uchunguzi wa matukio ya ajali za usafiri wa majini. Katika juhudi za kuimarisha zoezi la utafutaji na uokoaji katika ajali zinazotokea majini, TASAC imeendelea kutoa elimu kuhusu umuhimu na majukumu ya Kituo cha Kuratibu Utafutaji na Uokoaji Majini (Maritime Rescue Coordination Centre – MRCC) kilichopo Dar es Salaam pamoja na kuratibu mafunzo

ya mazoezi ya utafutaji na uokoaji. Aidha, Shirika liliendelea na jukumu la kufanya chunguzi za ajali za vyombo vya usafiri majini ambapo jumla ya ajali na matukio ya ajali nane (8) ya vyombo vidogo (boats) yaliripotiwa na kufanyiwa uchunguzi. Katika ajali hizo, jumla ya watu 15 walipoteza maisha na wengine 43 kuokolewa. Uchunguzi ulibaini kuwa ajali hizo zilisababishwa na weledi mdogo wa waendesha boti hizo, hali mbaya ya hewa, upakiaji wa mizigo kupita uwezo na boti hizo kufanya kazi usiku. Mbali ya ajali hizo za boti, kumekuwepo na tukio moja la meli ya MV. Zuhra (No. 100224/IMO No.9880544) iliyosajiliwa Tanzania Zanzibar kupelea na kugoa (grounding) katika miamba ya Bahari maeneo ya Kimbiji, Dar es Salaam. Katika tukio hilo mabaharia 13 waliokolewa na baadaye meli kutolewa salama kwenye miamba hiyo ambapo hakukuwa na madhara kwa binadamu wala mazingira. Pia, Shirika limeendelea kutumia taarifa za hali ya hewa kutoka Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania (TMA) ambapo jumla ya taarifa 874 za utabiri wa hali ya hewa zilipokelewa na kusambazwa kwa watumiaji.

179. Mheshimiwa Spika, Serikali imeendelea kuhakikisha kuwa huduma za Bandari na Meli zinaendelea kuwa endelevu. Hivyo, katika kipindi cha Julai, 2019 hadi Machi, 2020, Shirika lilipokea, kufanya tathmini na kutoa Leseni kwa watoa huduma za kibandari kama ifuatavyo:

- i. Uwakala wa Meli zilitolewa Leseni 24;
- ii. Mawakala wa Uondoshaji na Uingizaji wa shehena bandarini zilitolewa Leseni 828;
- iii. Wakusanyaji wa mizigo (Cargo Consolidators/ Deconsolidators) zilitolewa Leseni 18;
- iv. Watoa huduma ndogo ndogo bandarini (Miscellaneous Port Services) Leseni 23, hata hivyo bado kuna Leseni hai 48; na
- v. Wapimaji wa makasha (Gross Mass Verifiers) Leseni 37.

180. Mheshimiwa Spika, TASAC imeendelea kuimarisha ukaguzi wa meli ili kudhibiti usalama wa watu, mali na kulinda uchafuzi wa mazingira. Katika kutekeleza jukumu hilo, Shirika limeendelea kudhibiti ujenzi wa meli mpya, ukarabati wa meli zilizopo, ukaguzi na utoaji vyeti vya ubora kwa meli zilizosajiliwa Tanzania Bara. Lengo ni kuhakikisha kuwa vyombo vyote vya usafiri majini vinakidhi viwango vya ubora na usalama vilivyowekwa na Sheria ya Usafiri wa Majini ya mwaka 2003 (Merchant Shipping Act, 2003). Katika kipindi cha Julai,

2019 hadi Machi, 2020, Shirika lilikagua ujenzi wa Meli mpya nne (4) za MV. Ilemela (Mwanza), MV. Mbeya II (Kyela) na Tishari mbili (2) za mizigo za Mamlaka ya Bandari (TPA) zinazojengwa Mombasa, Kenya. Aidha, ukaguzi wa Meli 2 zilizokarabatiwa za MV. Victoria na MV. Butiama ulifanyika. Pia, Shirika limeendelea kufanya ufuatiliaji wa kazi za wajenzi wadogo wa vyombo vidogo ili kukagua ubora wa vifaa na vyombo vinavyotumika pamoja na weledi wa waundaji wa vyombo hivyo.

181. Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha Julai, 2019 hadi Machi, 2020, Serikali kupitia TASAC imeendelea kufanya ukaguzi wa ubora na usalama wa Meli zifanyazo kazi nchini na zinazotoka Nje ya Nchi (flag and port State control inspection). Lengo la ukaguzi huu ni kudhibiti ubora na usalama wa vyombo vinavyotoa huduma katika uchukuzi majini. Katika kipindi hicho, jumla ya kaguzi 255 kwa meli zenye ukubwa wa Tani 50 na zaidi zinazotoa huduma katika Pwani ya Bahari ya Hindi na Maziwa Makuu zilizosajiliwa Tanzania Bara na zile zinazotoka Nje ya Nchi zilikaguliwa. Kati ya Meli zilizokaguliwa, asilimia 62.7 zilikidhi viwango vya ubora. Aidha, vyeti vya Usajili wa Meli tisa (9) za MV. Orion, MV. Nyehunge, MV. Nyehunge I, MV. Bijli, MT. Sangara, MT. Munanka, MV. Orion II, MV. Saint Mathew na MV. Wankyo vilihuishwa.

182. Mheshimiwa Spika, Shirika limeendelea kuimarisha ulinzi na usalama wa Meli zinazoingia kwenye Bandari zetu zilizopo kwenye Ukanda wa Bahari ya Hindi. Katika kipindi cha Julai, 2019 hadi Machi, 2020, Bandari za Tanga, Pangani, Bagamoyo, Mtwara, Lindi, Kilwa na Mafia zilifanyiwa ukaguzi wa miundombinu ya kuongoza Meli zinapoingia bandarini. Aidha, Bandari za Dar es Salaam katika maeneo ya *General Cargo*, *Kurasini Oil Jetty - KoJ* na *Single Point Mooring - SPM, Tanzania International Container Terminal Services-TICTS*; na bandari za Tanga; Mtwara; Kilwa na Zanzibar zilifanyiwa ukaguzi kwa lengo la kuimarisha ulinzi katika bandari hizo.

USAFIRI NA UCHUKUZI KWA NJIA YA ANGA

Udhibiti wa Huduma za Usafiri wa Anga

183. Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2019/2020, Wizara imeendelea kuboresha usafiri wa Anga ili kuhakikisha kuwa Tanzania

inakuwa kitovu (hub) cha usafiri wa Anga kwa nchi za Afrika Mashariki na ya Kati. Matakwa ya kiusalama na kiulinzi ya kitaifa na kimataifa yameendelea kuzingatiwa katika Viwanja vya Ndege nchini. Hii imelifanya anga la Tanzania kuwa salama na hivyo kuvutia wawekezaji katika kutoa huduma za usafiri wa Anga. Aidha, Wizara kupitia Mamlaka ya Usafiri wa Anga (TCAA) iliendelea kusimamia na kudhibiti ubora wa viwanja vya Ndege vya Julius Nyerere, Kilimanjaro, Amani Abedi Karume, Dodoma, Songwe, Iringa, Mtwara, Lindi, Mwanza, Musoma, Shinyanga, Kigoma, Tabora, Bukoba, Tanga, Sumbawanga, Mpanda, Nachingwea, Kilwa Masoko na Songea. Pia, Viwanja vya Ndege vinavyomilikiwa na Mamlaka ya Hifadhi ya Taifa (TANAPA), Wizara ya Maliasili na Utalii, Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro (NCAA) na Sekta Binafsi vimeendelea kudhibitiwa ili kuimarisha utoaji huduma, kukuza utalii nchini na kuendelea kuhakikisha utekelezaji wa Sheria na Kanuni za uendeshaji wa Viwanja vya Ndege zinafuatwa. Katika udhibiti huo, jumla ya viwanja vidogo vidogo 208 vilivyobainika kukiuka Sheria na Kanuni za uendeshaji wa Viwanja vya Ndege vimefungiwa hadi Machi, 2020 hadi vitakaporekebisha kasoro zilizojitokeza.

184. Mheshimiwa Spika, udhibiti wa usalama wa usafiri wa Anga katika Viwanja vya Ndege, Mashirika ya Ndege pamoja na watoa huduma za usafiri wa Anga umesaidia kuhakikisha kuwa viwanja vyetu havitumiki katika vitendo vya kihalifu dhidi ya usalama wa usafiri wa Anga pamoja na kudhibiti upitishaji wa madawa ya kulevya na nyara za Serikali. Aidha, Wizara imeendelea kushirikiana na Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto pamoja vyombo mbalimbali vikiwemo vya Ulinzi na Usalama katika kudhibiti maambukizi ya virusi vya Corona (COVID - 19) kwa wageni wote wanaoingia nchini.

185. Mheshimiwa Spika, pamoja na juhudi hizo, katika kipindi cha Julai, 2019 hadi Machi, 2020, jumla ya Maafisa wa Usalama wa Usafiri wa Anga 423 kutoka Tanzania Bara na Tanzania Zanzibar walitahiniwa na kupewa Leseni za Ukaguzi (Screeners Certificate). Wizara itaendelea kuhakikisha kuwa Maafisa wa Usalama katika Viwanja vya Ndege wanapatiwa mafunzo stahiki na kupewa Leseni baada ya kupitia mchakato kama ulivyoainishwa kwenye Mpango wa Mafunzo wa Kitaifa wa Usalama wa Usafiri wa Anga (National Civil Aviation Security Training Programme).

186. Mheshimiwa Spika, idadi ya Abiria wanaotumia usafiri wa Anga inategemewa kuongezeka kwa asilimia 6.5 na kufikia Abiria 5,845,382 ifikapo Juni, 2020 kutoka Abiria 5,487,679 waliotumia usafiri huo katika mwaka 2018/2019. Aidha, idadi ya Abiria wanaosafiri kwenda na kutoka nje ya nchi inategemewa kupungua kutokana na janga la virusi vya Corona.

187. Mheshimiwa Spika, kukua kwa utendaji wa Kampuni ya Ndege Tanzania (ATCL) kwa kiasi kikubwa kumechangia kuongezeka kwa idadi ya Abiria wanaosafiri Ndani ya Nchi. Katika kipindi cha Julai, 2019 hadi Juni 2020, idadi ya Abiria wanaosafiri ndani ya nchi inakadiriwa kufikia abiria 4,398,500 kutoka abiria 5,309,611 waliosafiri katika kipindi kama hicho katika mwaka 2018/2019. Huu ni upungufu wa abiria kwa asilimia 17.2. Aidha, katika kipindi cha Julai, 2019 hadi Juni, 2020, mizigo iliyosafirishwa nchini inakadiriwa kufikia tani 21,456.6 ikilinganishwa na tani 24,444 zilizosafirishwa katika kipindi kama hicho mwaka 2018/19. Upungufu huu ni sawa na asilimia 12.2. Pia, hadi Juni, 2020, miruko ya safari za Ndege inakadiriwa kushuka hadi miruko 179,283 kutoka miruko 234,048 ya mwaka 2018/19. Huu ni upungufu wa miniko kwa asilimia 23.4. Kushuka kwa utendaji huu katika usafirishaji wa abiria, mizigo na miruko ya Ndege kwa kiasi kikubwa kunatokana na mlipuko wa virusi vya Corona unaoendelea duniani kote.

188. Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha Julai, 2019 hadi Machi, 2020, Serikali imeingia Mikataba mipya ya usafiri wa Anga (Bilateral Air Services Agreements - BASA) kati yake na nchi za Mauritius, Rwanda na Hispania. Aidha, Mikataba ya BASA kati ya Tanzania na nchi za Zambia, Uturuki, Oman, Sri Lanka, Uingereza, Zimbabwe, Ethiopia, Afrika ya Kusini na Jordan ilipitiwa upya. Hivyo, hadi Machi, 2020, Tanzania ilikuwa imeingia Mikataba ya BASA na nchi 74 ikilinganishwa na nchi 70 zilizosaini Mikataba hiyo katika mwaka 2018/2019. Kati ya Mikataba hiyo, Makampuni/Mashirika ya Ndege 22 kutoka nchi 19 yalikuwa yameanza kufanya safari za Ndege 175 kwa juma kati ya Tanzania na nchi hizo hadi kufikia Machi, 2020.

189. Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2019/20, Sekta ya Uchukuzi iliahidi kukamilisha Mradi wa kufunga Mfumo wa kuongoza Ndege kutua salama (Instrument Landing System - ILS) katika Kiwanja

cha Kimataifa cha Abeid Amani Karume - Zanzibar. Napenda kutoa taarifa katika Bunge lako Tukufu kuwa Mradi huo uliogharimu Shilingi bilioni 4.6 chini ya Mkandarasi PEJA East Africa ya Uholanzi umekamilika na uko katika hatua za majaribio. Hata hivyo, majaribio hayo yanayotakiwa kufanywa na Mkandarasi yamesitishwa hadi hapo janga la virusi vya Corona litakapokwisha.

190. Mheshimiwa Spika, pamoja na mafanikio yaliyopatikana kutokana na kukamilika kwa miradi mbalimbali, katika kipindi cha Julai, 2019 hadi Machi, 2020, Serikali kupitia Mamlaka ya Usafiri wa Anga imeendelea na utekelezaji wa miradi ifuatayo:

- i. Kununua na kufunga vifaa vya mawasiliano ya sauti kati ya Marubani na waongozaji Ndege katika Viwanja vya JNIA na KIA;
- ii. Kununua na kufunga vifaa vya mawasiliano katika jengo jipya la kuongozea Ndege kituo cha Mwanza;
- iii. Ukamilishaji wa ujenzi wa uzio katika eneo la ujenzi wa Chuo cha Usafiri wa Anga;
- iv. Kufanya utafiti na hatua za awali za ununuzi na ufungaji wa Mtambo wa kuongozea Ndege kwa njia ya *Satelaiti* upande wa Magharibi mwa Nchi;
- v. Ukamilishaji wa Upembuzi Yakinifu wa ujenzi wa Chuo cha kisasa cha Usafiri wa Anga; na
- vi. Ukamilishaji wa uhakiki wa vifaa vya kuongozea mienendo ya Ndege vituo vya KIA, JNIA, Zanzibar na Mwanza.

Huduma za Viwanja vya Ndege

191. Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia Mamlaka ya Viwanja vya Ndege (TAA) imeendelea kuhudumia Viwanja vya Ndege 58 kwa kuzingatia Sera, Sheria, Kanuni na Miongozo mbalimbali ya Usafiri wa Anga. Aidha, TAA imeendelea kuimarisha Viwanja vya Ndege ili kuboresha huduma, mapato na kuimarisha Ulinzi na Usalama viwanjani. Katika kipindi cha Julai, 2019 hadi Machi, 2020, TAA iliboresha Ulinzi na Usalama viwanjani kwa kununua na kufunga Mashine 15 za ukaguzi wa mizigo; milango sita (6) ya ukaguzi wa Abiria pamoja na vifaa vya mawasiliano kwa Viwanja vya Ndege vya JNIA (3), Iringa (1), Songea (1), Kigoma (1), Mwanza (2), Songwe (1), Arusha (2), Bukoba (1), Tanga (1), Lindi (1) na Shinyanga (1).

192. Mheshimiwa Spika, Wizara imeendelea kuhakikisha kuwa kila Mkoa unakuwa na Kiwanja cha Ndege. Katika kipindi cha Julai, 2019 hadi Machi, 2020, uthamini wa mali za Wananchi wanaotakiwa kupisha ujenzi wa viwanja vipya vya Ndege vya Kisumba (Sumbawanga), Msalato (Dodoma), Mwada (Manyara) na Igegu (Simiyu) umekamilika. Mamlaka inaendelea na taratibu za utwaaji wa maeneo hayo kwa kushirikiana na Mikoa husika.

193. Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2019/2020, TAA imekamilisha maandalizi ya Programu za Ulinzi na Usalama (Safety and Security Programs) kwa Viwanja vya Ndege vya JNIA, Mwanza, Songwe, Mtwara, Lindi, Nachingwea, Arusha, Lake Manyara, Kilwa Masoko, Mafia, Iringa, Dodoma, Songea na Tanga. Aidha, TAA ilitoa mafunzo ya usalama kwa wafanyakazi wa viwanja vyote vya Ndege vinavyoendeshwa na Mamlaka. Pia, Mamlaka imefanya mazoezi ya uokoaji wakati wa ajali kwa Viwanja vya Ndege vya Songwe, Iringa, Lake Manyara na Kahama na Mazoezi ya Usalama (Security Contingency Exercises) kwa Viwanja vya Ndege vya Songwe, Dodoma na Mwanza.

194. Mheshimiwa Spika, kazi ya ununuzi na ufungaji wa Mifumo ya taa za kuongozea Ndege (AGL) katika Viwanja vya Ndege vya Dodoma, Songwe na Bukoba inaendelea. Mfumo wa taa za kuongozea Ndege katika Kiwanja cha Ndege cha Dodoma upo na unaweza kutumika kwa dharura. Hata hivyo, kazi za kufunga Mfumo mpya imeanza na inatarajiwa kukamilika Juni, 2020. Kuhusu Kiwanja cha Ndege cha Songwe, ufungaji wa taa hizo utafanyika kupitia Mradi unaoendelea wa ukarabati wa barabara ya kutua na kuruka Ndege (runway). Aidha, kazi za kufunga Mfumo wa taa za kuongozea Ndege katika Kiwanja cha Ndege cha Bukoba zitatekelezwa baada ya kurefushwa kwa barabara ya kuruka na kutua Ndege pamoja na ujenzi wa mnara wa kuongozea Ndege kukamilika. Kazi inayoendelea sasa ni Mhandisi Mshauri kufanya Usanifu na Upembuzi wa Kina kwa ajili ya kazi za urefushaji wa barabara ya kuruka na kutua Ndege.

195. Mheshimiwa Spika, Serikali imeendelea kuhakikisha kuwa Kiwanja cha Ndege cha Arusha kinaboreshwa ili kuvutia watalii wengi kutumia kiwanja hicho na kuwezesha Ndege zenye uwezo wa kubeba abiria zaidi ya 50 kutumia kiwanja hicho. Katika kipindi cha Julai, 2019 hadi Machi, 2020 kazi zilizotekelezwa ni pamoja na:

- i. Kujenga maegesho ya Ndege (Apron);
- ii. Kuboresha barabara ya Ndege (taxiway) ya kuingia na kutoka katika maegesho ya Ndege;
- iii. Kujenga maegesho ya Magari (Car Park);
- iv. Kufunga Mfumo wa maegesho ya Magari;
- v. Kujenga maegesho mapya ya Ndege (remote Apron);
- vi. Kuanza urefushaji wa barabara ya kutua na kuruka Ndege kwa mita 200 pamoja na maeneo ya kugeuzia (Turning bay); na
- vii. Kuanza ujenzi wa barabara mbadala ya kuingilia Gereza la Mkoa wa Arusha (Kisongo) badala ya kupita katikati ya eneo la Kiwanja cha Ndege.

196. Mheshimiwa Spika, Kampuni ya Kuendeleza Kiwanja cha Ndege cha Kilimanjaro (KADCO) imeendelea kukisimamia na kukiendesha Kiwanja cha Ndege cha Kimataifa cha Kilimanjaro (KIA) kwa faida bila kutegemea ruzuku ya uendesaji kutoka Serikalini. Hata hivyo, Serikali imeendelea kutoa ruzuku kwa ajili ya utekelezaji wa miradi mikubwa ya uboreshaji na uendelezaji wa miundombinu ya Kiwanja cha Ndege. Kwa mfano, Mradi wa uboreshaji njia ya kurukia na kutua Ndege (runway) ulipata fedha kutoka Serikalini. Katika kipindi cha Julai, 2019 hadi Machi, 2020, KADCO imeendelea kutoa huduma kwa Makampuni ya Ndege zenye ratiba maalum ya safari. Makampuni hayo ni pamoja na Air Tanzania, Kenya Airways, Ethiopian Airline, Precision Air, Qatar Airways, KLM, Turkish Airlines na Rwandair. Aidha, kuna Mashirika ya Ndege za kukodi yanayofanya safari zisizokuwa na ratiba maalum yanayotoa huduma KIA. Mfano wa Mashirika hayo ni Coastal Aviation, Regional Air, Northern Air, Zurik Air, na El-Al Israel airlines.

197. Mheshimiwa Spika, kazi nyingine zilizotekelezwa na KADCO katika mwaka 2019/2020 ni pamoja na:

- i. Kuboresha nyumba za Wafanyakazi, Majengo ya Mitambo na ofisi mbali mbali;
- ii. Kutoa elimu kwa Wafanyakazi katika kada mbalimbali za Ulinzi, Ufundi, Zimamoto na Mafunzo mengine ya kitaalam;
- iii. Kuboresha mazingira kwenye eneo la kiwanja na maeneo jirani kwa kupanda miti, kutoa elimu ya mazingira vijijini na kushiriki kikamilifu katika sherehe zinazohusu mazingira

kitaifa na kimataifa.

- iv. Kukamilisha ununuzi wa vifaa mbalimbali vya TEHAMA ili kuongeza ufanisi katika utoaji huduma; na
- v. Kushiriki shughuli za kijamii na vijiji vinavyopakana na kiwanja kwa kutoa misaada. Misaada hiyo ni pamoja na Huduma za zimamoto na uokoaji, ukarabati wa nyumba za Taasisi kama Polisi na Halmashauri ya Hai na Arumeru na vijiji mbalimbali vinavyozunguka Kiwanja cha Ndege.

Huduma za Usafiri wa Anga

198. Mheshimiwa Spika, napenda kutumia fursa hii kuyashukuru Mashirika ya Ndege yanayotoa huduma ya usafiri wa Anga Ndani ya Nchi kwa kuendelea kutoa huduma. Mashirika hayo yamekuwa yanatoa huduma za usafiri wa Anga kwa Ndege za Ratiba maalumu (scheduled flight) na zisizo na ratiba maalumu (General Aviation). Kwa upande wa ratiba maalumu, Kampuni ya Ndege Tanzania (ATCL) na Precision Air zimendelea kutoa huduma za usafiri wa Anga katika vituo vingi huku Kampuni nyingine ndogo hasusan Auric na Coastal Air zikifuatia. Kwa upande wa huduma zinazotolewa kupitia ratiba zisizo maalumu, Kampuni za Auric, Coastal Air, Zanair, Air Excel, Tanzaniar, Sky aviation na Tropical air zimendelea kutoa huduma kwa ufanisi.

199. Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha Julai, 2019 hadi Machi, 2020, Serikali ilipokea Ndege mbili (2) mpya. Ndege ya kwanza ni Boeing 787 – 8 Dreamliner yenye uwezo wa kubeba abiria 262 kwa ajili ya masafa marefu iliyowasili nchini Oktoba, 2019. Ndege nyingine ni aina ya Dash 8 Q 400 yenye uwezo wa kubeba abiria 76 kwa ajili ya masafa mafupi iliyowasili nchini Disemba, 2019. Ongezeko hili la idadi ya Ndege limefanya ATCL kuwa na jumla ya Ndege 8. Ndege hizo zinajumuhisha Ndege nne (4) za masafa mafupi aina ya Dash 8 Q400, Ndege mbili (2) za masafa ya kati aina ya Airbus A220 – 300 na Ndege mbili (2) za masafa marefu aina ya Boeing 787-8 Dreamliner. Aidha, Ndege hizo zimeongeza mtandao wa safari wa ATCL kutoka vituo vitatu (3) vya ndani ya nchi na kituo kimoja (1) cha kikanda vilivyokuwepo kabla ya mwaka 2016 hadi vituo 13 ndani ya nchi na vituo saba (7) vya nje ya nchi. Ndege aina ya Dash 8 Q300 ambayo inayohitaji matengenezo makubwa inatarajiwa kupelekwa nchini Malta mara baada ya mlipuko wa ugonjwa wa COVID -19 kuisha.

200. Mheshimiwa Spika, vituo vya ndani ambavyo ATCL inatoa huduma ni pamoja na Dar es Salaam, Zanzibar, Dodoma, Kilimanjaro, Mwanza, Bukoba, Kigoma, Mbeya, Tabora, Songea, Iringa, Mtwara na Mpanda. Hata hivyo, ukarabati unaoendelea katika kiwanja cha Songea umesababisha kushindwa kuendelea kutoa huduma katika kituo cha Mtwara kutokana na uchache wa abiria. Hivyo, Safari za Mtwara na Songea zitarejea baada ya kukamilika kwa ukarabati wa kiwanja cha Songea kwa Mfumo uleule wa kuunganisha safari za vituo hivyo viwili ili kuwa na Abiria wa kutosha na tija. Kwa safari za kikanda na kimataifa, hadi Machi, 2020, ATCL ilikuwa inatoa huduma katika vituo vya Hahaya (Comoro), Entebbe (Uganda), Bujumbura (Burundi), Mumbai (India), Lusaka (Zambia), Johannesburg (Afrika Kusini) na Harare (Zimbabwe). Aidha, vibali vyote vya kuanza safari za kwenda Guangzhou, China, vimepatikana tangu Februari, 2020. Pamoja na kupata vibali vya kuanza safari za Guangzhou, pia ATCL imesaini Mkataba wa safari maalum (Charter flight) wa kubeba watalii kati ya mji wa Hangzhou, China, na Dar es Salaam. Safari hizi za China zitaanza baada ya mlipuko wa ugonjwa wa COVID – 19 kuisha.

201. Mheshimiwa Spika, mazingira ya utendaji kazi kwa Watumishi wa ATCL yameendelea kuboreshwa. Katika kipindi cha Julai, 2019 hadi Machi, 2020, mafunzo ya lazima na yale yanayofuata ratiba ya mafunzo kwa Watumishi yametolewa kwa Marubani 78, Wahandisi Ndege 127 na Wahudumu wa Ndani ya Ndege 131. Aidha, Mfumo wa mauzo wa Serikali (Government Electronic Payment Gateway - GePG) unaendelea kufanyiwa majaribio kuona kama utaweza kutumika katika mauzo ya Tiketi Ndani na Nje ya Nchi. Lengo ni kuhakikisha kuwa malipo yote ya Tiketi yanathibitiwa na kupunguza gharama za uendeshaji.

202. Mheshimiwa Spika, napenda kulijulisha Bunge lako Tukufu kuwa Agosti, 2019, ATCL ilitunukiwa cheti cha kukidhi matakwa ya usalama katika uendeshaji wa shughuli za usafiri wa Anga kutoka Shirikisho la Mashirika ya Ndege Ulimwenguni (IATA). Kufuzu ukaguzi huo ni muhimu katika uendeshaji wa shughuli za Usafiri wa Anga kwani kunaongeza imani ya Wateja na Wadau muhimu wa usafiri wa Anga kwenye mashirikiano ya kibiashara.

203. Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha Julai, 2019 hadi Machi, 2020, Miradi iliyoendelea kutekelezwa ni pamoja na:

- i. Ununuzi wa Ndege moja aina ya Dash 8 Q400. Ndege hii inatarajiwa kuwasili Juni, 2020. Aidha, Ndege nyingine mbili aina ya A220 – 300 zinazotarajiwa kuwasili Juni, 2021;
- ii. Kufanya matengenezo ya Ndege ndogo aina ya Dash 8 Q300;
- iii. Maandalizi ya safari za Guangzoug (China) na Lubumbashi, Nairobi, Kigali na Uingereza. Utoaji wa huduma utanza baada ya mlipuko wa ugonjwa wa virusi vya corona kuisha;
- iv. Kukarabati Karakana za JNIA na KIMAFa ili kufanya matengenezo madogo na makubwa nchini; na
- v. Kujenga uwezo wa Chuo cha Taifa cha Usafirishaji (NIT) kuanza kutoa Mafunzo ya Wataalam wa Usafiri wa Anga nchini.

HUDUMA ZA HALI YA HEWA

204. Mheshimiwa Spika, huduma za Hali ya Hewa nchini zimeendelea kutolewa na Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania. Huduma hizo zinajumuisha takwimu na taarifa za hali ya hewa iliyopita, iliyopo na ijayo; tahadhari dhidi ya matukio ya hali mbaya ya hewa; klaimatolojia ya hali ya anga na mabadiliko ya hali ya hewa. Huduma hizi zinaongeza mchango katika kuendeleza sekta za kiuchumi na kijamii na kupunguza athari zitokanazo na mabadiliko ya tabia nchi. Aidha, Mamlaka imeendelea kutoa elimu kwa jamii juu ya umuhimu wa kutumia huduma za hali za hewa kupitia maonesho mbalimbali, vipindi vya redio na runinga, tovuti, blogu na semina kwa jamii.

205. Mheshimiwa Spika, Wizara imeendelea kutekeleza program ya kukabiliana na mabadiliko ya nchi, kufuatilia mwenendo wa mabadiliko ya hali ya hewa na kutoa taarifa za mabadiliko hayo kwa wadau wa sekta mbalimbali. Aidha, Mamlaka hutoa taarifa ya Klimatolojia ya tathmini ya hali ya hewa na mabadiliko ya hali ya hewa kila mwaka ikijumuisha tathmini ya mwelekeo wa joto na mvua pamoja na matukio ya hali mbaya ya hewa ili kujenga uelewa kwa umma juu ya athari za mabadiliko ya hali ya hewa.

206. Mheshimiwa Spika, Mamlaka ya Hali ya Hewa imeendelea kutekeleza Mradi wa Rada tatu (3) za hali ya hewa zitakazofungwa Mtwara, Mbeya na Kigoma. Rada inayotarajiwa kufungwa Mtwara imewasili nchini Februari, 2020 na taratibu za kuifunga zinaendelea. Ujenzi wa rada mbili (2) zilizobaki unaendelea kutekelezwa nchini

Uholanzi. Aidha, ujenzi wa miundombinu ya Rada itakayofungwa katika maeneo hayo inayohusisha ujenzi wa barabara, uzio, majengo pamoja na uwekaji wa umeme unaendelea. Kukamilika kwa ununuzi wa Rada hizo kutaongeza ubora wa utabiri wa hali ya hewa kwani tutakuwa na jumla ya Rada tano (5) nchini.

207. Mheshimiwa Spika, Mamlaka imeendelea na utekelezaji wa Mfumo wa kudhibiti ubora wa huduma za hali ya hewa kwa Sekta ya Usafiri wa Anga kulingana na viwango vya kimataifa. Ukaguzi wa kimataifa uliofanyika Disemba, 2019 ulithibitisha Mamlaka kuendelea kukidhi vigezo na hivyo kuendelea kumiliki cheti cha ubora (ISO 9001:2015). Kwa upande wa usafiri kwa njia ya maji, utekelezaji wa Mfumo wa kudhibiti ubora wa huduma za hali ya hewa zinazotolewa katika usafiri wa majini umeanza kutekelezwa katika ofisi tano (5) za hali ya hewa zilizopo katika Bandari za Dar es Salaam, Zanzibar, Pemba, Mwanza na Kigoma.

208. Mheshimiwa Spika, kazi nyingine zinazoendelea kutekelezwa katika kipindi cha Julai, 2019 na Machi, 2020 ni pamoja na:

- i. Matengenezo ya vifaa vipya vya hali ya hewa katika karakana iliyopo JNIA;
- ii. Kufanya uhakiki wa usahihi (calibration) wa vifaa vya hali ya hewa;
- iii. Kuhakiki Rada ya hali ya hewa iliyoko Mwanza ili kuhakikisha kuwa inaendelea kufanya kazi kwa usahihi;
- iv. Kuwajengea uwezo Wafanyakazi kwa lengo la kuboresha huduma. Jumla ya Wafanyakazi 61 walihitimu mafunzo ya muda mfupi, 51 wanaendelea na mafunzo ya muda mrefu katika vyuo mbalimbali na 72 wanaendelea na mafunzo ya muda mfupi; na
- v. Kutengeneza Mifumo mitatu (3) ya TEHAMA ambayo inatumika katika uangazi (Digital Meteorological Observatory), utoaji wa huduma za hali ya hewa kwa usafiri wa Anga (MAIS) na utoaji wa huduma za hali ya hewa kwa usafiri wa kwenye maji (MMIS).

C.1.3 SEKTA YA MAWASILIANO

Ukusanyaji wa Mapato

209. *Mheshimiwa Spika*, katika mwaka wa fedha 2019/20, kwa kipindi cha kuanzia mwezi Julai, 2019 hadi Machi, 2020 Sekta ya Mawasiliano imekusanya jumla ya **Shilingi 290,417,311,401.97** kwa mchanganuo ufuatao: TCRA imekusanya Jumla ya **Shilingi 137,059,249,584.29** kutoka kwenye vyanzo vyake. Pia katika kipindi hicho TCRA ilipeleka katika Mfuko Mkuu wa Serikali asilimia 15 ya Mapato Ghafi ya **Shilingi 18,621,401,160.00** na mapato kutokana na mtambo wa TTMS **Shilingi 9,033,895,792.19**; Shirika la Mawasiliano Tanzania (TTCL) limekusanya jumla ya **Shilingi 85,710,460,445.06**; Shirika la Posta Tanzania (TPC) limekusanya jumla ya **Shilingi 24,319,843,901.52**; Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote (UCSAF) umekusanya kiasi cha **Shilingi 25,388,181,843.00** na Tume ya TEHAMA (ICTC) imekusanya jumla ya **Shilingi 735,184,392.00**. Aidha, **Shilingi 17,204,391,236.10** zilikusanywa kutokana na mauzo ya huduma za Mkongo wa Taifa.

210. *Mheshimiwa Spika*, Taasisi za Sekta ya Mawasiliano katika mwaka wa fedha 2017/18 zilipata faida na hivyo zimeweza kutoa gawio Serikalini la jumla ya **Shilingi 89,315,814,942.00** kwa mchanganuo ufuatao; Mamlaka ya Mawasiliano imetoa **Shilingi 85,855,814,942.00**, Shirika la Mawasiliano limetoa **Shilingi 2,100,000,000.00**, Shirika la Posta limetoa **Shilingi 350,000,000.00**, Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote ulitoa Shilingi **1,000,000,000.00** na Tume ya TEHAMA ilitoa **Shilingi 10,000,000.00**.

Bajeti ya Matumizi ya Kawaida

211. *Mheshimiwa Spika*, katika mwaka wa fedha 2019/20, Sekta ya Mawasiliano ilitengewa kiasi cha **Shilingi 3,973,197,000.00** kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida. Kati ya fedha hizo, **Shilingi 2,047,259,000.00** ni kwa ajili ya Mishahara ya Watumishi na **Shilingi 1,925,938,000.00** ni kwa ajili ya Matumizi Mengineyo. Hadi kufikia mwezi Machi, 2020 **Shilingi 3,021,554,809.24** zilikuwa zimetolewa na Hazina. Kati ya fedha hizo, **Shilingi 1,457,738,432.00** zimetolewa kwa ajili ya Mishahara na **Shilingi 1,563,816,377.24** kwa ajili ya Matumizi Mengineyo.

Ukuaji wa Sekta ya Mawasiliano

212. Mheshimiwa Spika, Sekta ya Mawasiliano imeendelea kuwa moja ya sekta zinazochangia kwa kiasi kikubwa katika ukuaji wa uchumi. Katika kipindi cha Januari hadi Disemba, 2019 Sekta ya Mawasiliano ilichangia ukuaji wa uchumi kwa **asilimia 11** ikilinganishwa na **asilimia 9.1** kwa kipindi kinachoishia **Disemba, 2018**. Aidha, kuna ongezeko kubwa la huduma kwa wananchi zinazotolewa na Serikali na pia sekta binafsi kupitia mawasiliano ya simu za kiganjani kama vile kutuma na kupokea pesa, kununua umeme, kulipia huduma za maji na ving'amuzi. Kimsingi huduma za mawasiliano zimechangia kurahisisha utendaji kazi na kuboresha maisha ya wananchi kijamii na kiuchumi kutokana na kupata huduma mbalimbali kwa uwazi, urahisi, haraka na pasipo na ubaguzi. Vilevile, ukuwaji wa sekta ya mawasiliano umesaidia Serikali kuimarisha ukusanyaji wa kodi mbalimbali na maduhuli kwa kutumia mifumo ya TEHAMA.

213. Mheshimiwa Spika, laini za simu za viganjani zimeongezeka kutoka **43,749,086** Julai, 2019 hadi laini **43,932,080** mwezi Machi, 2020 na idadi ya watumiaji wa intaneti iliongezeka kutoka **23,142,960** Julai, 2019 hadi kufikia **25,794,560** mwezi Machi, 2020. Vituo vya kurusha matangazo ya redio vimeongezeka kutoka vituo **158** mwaka 2019 hadi kufikia vituo 180 mwezi Machi, 2020 na vituo vya kurusha matangazo ya runinga kwa kutumia mitambo iliyosimikwa ardhini vimeongezeka kutoka vituo **37** mwaka 2019 hadi kufikia vituo **43** mwezi Machi, 2020. Pia, watoa huduma za mawasiliano ya simu na posta wameongezeka na kuleta ushindani wenye tija na ufanisi nchini kwa sekta zote.

UTEKELEZAJI WA MIRADI YA MAENDELEO

Ujenzi wa Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano

214. Mheshimiwa Spika, Serikali inaendelea kuboresha Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano ili kuhakikisha huduma za Mkongo zinapatikana kwa uhakika. Katika mwaka wa fedha 2019/20 betri zinazotumika pindi umeme unapokatika kwenye vituo sabini na moja (71) vya mkongo wa Taifa vimebadilishwa kutokana na uchakavu wa betri za awali. Hii inawezesha Mkongo wa Taifa kufanya kazi kwa masaa hadi nane pindi umeme unapokatika.

215. Mheshimiwa Spika, Serikali inaendelea na maandalizi ya kufikisha huduma ya Mkongo wa Taifa katika ofisi ambazo hazina huduma ya mkongo ambapo unganishaji wa Halmashauri za Siha, Ngorongoro, Nyang'hwale, Bukombe, Mbogwe, Kyerwa, Nsimbo, Mlele, Buhigwe, Malinyi, Buchosa, Kalambo, Ushetu, Busokelo, Momba na kituo cha Manyovu uko kwenye hatua za mwisho. Uunganishwaji huu unahusisha baadhi ya vituo vya afya, polisi, posta, mahakama na taasisi nyingine kwenye maeneo hayo ili kuboresha huduma kwa wananchi zitakazotolewa na taasisi hizo.

216. Mheshimiwa Spika, Serikali imekamilisha uaandaji wa Mkakati wa Taifa wa Brodibendi (National Broadband Strategy) wenye lengo la kuhakikisha kuwa mawasiliano ya Brodibendi yanapatikana nchini nzima. Mkakati huu umeanisha namna bora ya kufikisha huduma za inteneti vijijini, kwenye mashule, hospitali na maeneo ya umma. Aidha, Mkakati huu unasisitiza matumizi ya teknolojia ya kuanzia 3G ili wananchi waweze kupata huduma za data.

217. Mheshimiwa Spika, kituo cha Taifa cha Kutunza Data cha Dar es Salaam (Internet Data Centre) kimeendelea kutoa huduma bora kwa taasisi za Serikali na taasisi binafsi. Kituo kimeweza kuongeza wateja kutoka **wateja 79** mwezi julai, 2019 hadi **wateja 107** mwezi Machi, 2020.

UTENDAJI WA TAASISI ZILIZO CHINI YA SEKTA YA MAWASILIANO

Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA)

218. Mheshimiwa Spika, Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA) kwa kushirikiana na watoa huduma za mawasiliano, imeendelea na zoezi la usajili wa laini za simu kwa njia ya biometria ambapo hadi kufikia tarehe 31 Machi, 2020 idadi ya laini zilizosajiliwa zilikuwa **37,678,816** sawa na asilimia **85.8** ya laini zote **43,932,080** zilizounganishwa mitandaoni. Laini zilizozimwa hadi kufikia tarehe 31 Machi, 2020 zilikuwa **5,082,458**. Aidha, laini ambazo bado hazijasajiliwa kwa alama za vidole lakini zilisajiliwa kwa kitambulisho cha Mpiga Kura na kitambulisho cha Mzanzibar Mkaazi ni laini **6,134,477**. Uhakiki unaendelea kwa kushirikiana na NIDA kwa ajili ya taratibu za kuzifungia laini ambazo hazijasajiliwa.

219. Mheshimiwa Spika, Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania

(TCRA) imeendelea na ujenzi wa mifumo na uratibu wa huduma za mawasiliano kwa kutumia mtambo wa Telecommunications Traffic Monitoring System (TTMS) ili kuhakikisha Serikali inapata mapato stahiki kutokana na huduma za mawasiliano. Mfumo huo unawezesha kuhakiki ubora wa huduma za Mawasiliano ya simu; kutoa takwimu za mawasiliano ya simu yanayofanyika ndani na nje ya nchi (Local and International Traffic); kugundua mawasiliano ya ulaghai (fraudulent traffic); Kubaini na kufungia simu zenye namba tambulishi zilizopakiliwa (Duplicate IMEIs) ambapo taarifa hii inapatikana kwenye rajisi ya namba tambulishi ya simu na kutambua mapato na takwimu za miamala ya fedha mtandao. Katika kipindi cha Julai, 2019 hadi Machi, 2020 jumla ya miamala **2,502,352,515** imepita katika mitandao ya simu na jumla ya fedha zilizopita ni **Shilingi 133,493,772,366,263**.

220. Mheshimiwa Spika, Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania inaendelea kusimamia uendeshaji wa mfumo wa usimamizi wa ubora wa huduma (Quality of Service) uliowekwa katika mtambo wa TTMS na kuwezesha kupatikana kwa taarifa za ubora wa mawasiliano ya simu za kimataifa pamoja na zile za ndani (Local off-net traffic) yanayofanyika kutoka katika mtandao mmoja wa mtoa huduma kwenda mtandao mwingine wa mtoa huduma hivyo kuiwezesha Mamlaka kufuatilia kwa ufanisi ubora wa huduma za mawasiliano. Vile vile, TCRA inasimamia uendeshaji wa mfumo uliowekwa katika mtambo wa TTMS na kuwezesha kupatikana kwa taarifa za ubora wa sauti kwa mawasiliano ya simu za ndani (Local off-net traffic) yanayofanyika kutoka katika mtandao mmoja wa mtoa huduma kwenda mtandao mwingine wa mtoa huduma.

221. Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia TCRA inaendelea kusimamia kwa ufanisi uendeshaji wa Mfumo wa Rajisi wa Namba Tambulishi za simu za kiganjani hivyo kuwezesha kudhibiti matumizi ya simu ambazo hazina ubora (bandia). Simu bandia haziwezi tena kuunganishwa na mtandao wowote wa simu hapa nchini. Tangu mfumo huu uanze kufanya kazi mwezi Oktoba, 2013 hadi kufikia mwezi Machi, 2020 jumla ya namba tambulishi (IMEIs) zilizofungiwa ni **1,277,048**. Mfumo huo umepunguza kwa kiasi kikubwa wizi wa simu za mkononi. Mteja anapoibiwa au kupoteza simu yake hutoa taarifa ya kuibiwa au kupotea kwa simu hiyo na kuifungia isiweze kutumika tena kwenye mitandao ya simu za mkononi.

222. Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia Mamlaka ya Mawasiliano imeendelea na zoezi la kuzitambua na kuzifungia namba za simu ambazo zimekuwa zikiingiza mawasiliano ya simu za kimataifa kwa njia za ulaghai. Katika kipindi cha Julai, 2019 hadi Machi, 2020 TCRA imefanikiwa kupunguza mawasiliano ya simu za kimataifa kwa njia ya ulaghai kutoka **asilimia 15** hadi kufikia chini ya **asilimia 5**. Kabla ya udhibiti huu mawasiliano kwa njia ya ulaghai yamepelekea watoa huduma kukosa mapato na hivyo Serikali kupoteza mapato.

223. Mheshimiwa Spika, Sekta ya Mawasiliano imeendelea kukua kwa kasi kutokana na mabadiliko ya Teknolojia. Mabadiliko haya yamekuja na athari mbalimbali za usalama na uhalifu katika mitandao. Athari hizo ni pamoja na uhalifu kimtandao (cyber crime), ugaidi kwenye mifumo wa mitandao (Cyber terrorism) na uharibifu wa mila na desturi (mfano picha za utupu kwenye mitandao). TCRA inaendelea kudhibiti vitendo hivi kwa kujenga uwezo kwa watumishi wake pamoja na kushirikiana kwa karibu na vyombo vya ulinzi na usalama. Aidha, Mamlaka imeweka taratibu mahsusi wa kushughulikia malalamiko kati ya watumiaji na watoa huduma. Vile vile mamlaka ya Mawasiliano inaendelea kutoa elimu juu ya wajibu na haki za watumiaji na watoa huduma za mawasiliano. Mpaka Machi, 2020, Mamlaka ilikuwa imepokea na kushughulikia jumla ya malalamiko 502.

224. Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha Julai, 2019 hadi Machi 2020, TCRA imetoa mafunzo juu ya usalama wa mifumo kwa wasimamizi wa mifumo kutoka taasisi mbalimbali nchini Tanzania. Pia, imefanya tathmini ya hatari na matishio ya kiusalama ya mifumo ya kompyuta na mtandao kwa lengo la kubaini mapungufu yaliyopo dhidi ya mashambulio ya mtandao (cyber-attacks) ambapo tahadhari za usalama (security alert) (137); mashauri (security advisories) (280) na taarifa kwa umma (public notice) tatu (3) za kiusalama zilitolewa ili hatua stahiki ziweze kuchukuliwa kuimarisha usalama wa mtandao na mifumo.

225. Mheshimiwa Spika, nitoe wito kwa wananchi waendeleo kutumia vizuri huduma za mawasiliano kwa kuwa zinachangia ukuaji wa uchumi na maendeleo ya taifa letu na tuepuke matumizi yasiyo sahihi ya huduma hizo kwa kutoitumia katika kufanya uhalifu na wizi kwa njia ya mtandao; vitendo vinavyokiuka maadili, mila na desturi zetu na uvunjifu wa amani. Aidha, nawahimiza wananchi tuendeleo

kulinda miundombinu ya Mawasiliano kwa kuwa ni muhimu katika kukuza uchumi wetu.

Shirika la Posta Tanzania (TPC)

226. Mheshimiwa Spika, Shirika la Posta limeendelea kuboresha huduma zake za usambazaji wa barua, nyaraka, na vipeto kupitia masanduku ya barua na huduma ya Posta Mlangoni kwenye maeneo yenye miundombinu ya Anwani za Makazi na Postikodi. Jitihada za Serikali zinaendelea ili kuwezesha huduma za Posta kuwafikia wananchi wengi zaidi kupitia miundombinu hiyo.

227. Mheshimiwa Spika, Shirika limeendelea kuimarisha biashara zake ikiwemo biashara ya kubadili fedha za Kigeni (Bureau de Change). Kufikia tarehe 31 mwezi Machi, 2020 Shirika limefikisha **maduka 26** kutoka maduka **19 mwaka 2018** katika maeneo mbalimbali ya Kimkakati. Aidha, Shirika linakamilisha ufunguzi wa huduma za 'Freight and Fowarding' (shehena na usafirishaji wa mizigo) ambapo kwa sasa Shirika liko katika hatua za kuhuisha leseni ya biashara hiyo. Vilevile kwa kushirikiana na Mfuko wa Mawasiliano kwa wote (UCSAF), Shirika limekamilisha mradi wa kuanzisha vituo **11** vya mawasiliano 'Tele-centres' katika maeneo ya Chato, Tarime, Maswa, Lushoto, Mahenge, Newala, Mbinga, Ludewa, Ileje, Mpanda, na Sumbawanga.

228. Mheshimiwa Spika, Shirika limeanza kuendesha mafunzo ya matumizi ya huduma ya Posta kiganjani 'Smart Posta' (mfumo au jukwaa la kidigiti unaorahisisha kuzifikia huduma zote za msingi zinazotolewa na Shirika la Posta Tanzania na kuwezesha kufanya malipo kupitia mtandao) kwa majiji mawili ya majaribio (Dar es Salaam na Dodoma).

229. Mheshimiwa Spika, Shirika la Posta limeunganisha **ofisi 161** katika mfumo wa uendeshaji wa kielekitroniki ambao huwezesha huduma zote kutolewa kimtandao. Shirika pia limeunganisha ofisi hizo katika Mfumo wa Malipo wa Kielekitroniki wa Serikali (GePG). Vilevile, Shirika linaendelea kuimarisha vituo vya kutolea intaneti kwa wananchi ambavyo vinasaidia jamii kupata huduma kupitia mtandao kama vile matokeo ya mitihani, nafasi za mafunzo mbalimbali, nafasi za ajira na taarifa mbalimbali.

230. Mheshimiwa Spika, Shirika limeanza ukarabati na kubadilisha muonekano wa majengo yake kulingana na mabadiliko ya Nembo ya kulitambulisha Shirika (**Let's Go!**). Mpaka sasa ofisi za Zanzibar pamoja na majengo saba ya Ofisi kuu za mikoa (Morogoro, Dodoma, Kigoma, Kagera, Dar es Salaam na Arusha) yamefanyiwa ukarabati na kubadilishwa mwonekano wake. Aidha, zoezi hili ni endelevu kwa majengo yote nchi nzima kulingana na upatikanaji wa fedha na mpango wa maendeleo wa Shirika. Maandalizi yanaendelea kwa ajili ya kuanza ukarabati wa majengo ya ofisi kuu za mikoa ya Singida, Mtwara, Mara, Lindi, Songea, Iringa, Shinyanga na Sumbawanga.

231. Mheshimiwa Spika, Shirika linaendelea kuendesha Kituo cha Huduma Pamoja (Jamii Centre) katika Posta Kuu ya Dar es Salaam ambacho kinawezesha upatikanaji wa huduma za kiserikali mahali pamoja. Upanuzi wa kituo hiki na uongezaji wa huduma zinazotolewa unaendelea kufanywa. Aidha, Shirika linaendelea kuboresha majengo na kuweka muonekano mzuri. Katika mwaka 2019/20 Shirika limekamilisha uboreshaji wa majengo yake katika mikoa ya Dodoma, Arusha, Morogoro, Kigoma, Kagera, Dar es Salaam na Mjini Magharibi kwa upande wa Zanzibar, tayari kwa utoaji wa huduma hii. Aidha, katika kuhakikisha ulinzi na usalama wa wateja na mali zao unaimarika kamera za ulinzi (CCTV) zimenunuliwa na kufungwa katika Ofisi za Mjini Magharibi Zanzibar na mikoa ya Dodoma, Kigoma, Kagera, Mwanza, Kilimanjaro na Tanga.

Shirika la Mawasiliano Tanzania (TTCL)

232. Mheshimiwa Spika, Shirika limefanikiwa kuongeza idadi ya wasambazaji wakubwa wa muda wa maongezi kutoka 7 hadi 17 kufikia mwezi machi, 2020 ili kuhakikisha muda wa maongezi unapatikana nchi nzima. Aidha Shirika limeendelea kuboresha upatikanaji wa muda wa maongozi kwa kuwaelimisha na kuwaunganisha wateja wake na huduma ya T-pesa ili waweze kununua muda wa maongezi kupitia T-pesa kila wanapohitaji bila kulazimika kufika ofisi za Shirika au wakala.

233. Mheshimiwa Spika, Shirika limeendelea kupata faida na kuondoka katika Mashirika yaliyokuwa yakijiendesha kwa hasara. Kwa mwaka wa fedha 2018/19 Shirika limepata faida baada ya kodi ambayo

ni zaidi ya Shilingi **bilioni 6** na hivyo linatarajia kutoa gawio kwa Serikali baada ya taratibu za ndani kukamilika. Vilevile, Shirika limeendelea kusimamia Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano nchi nzima kwa Ufanisi ambapo makampuni ya Simu, sekta binafsi, Serikali na Taasisi zake zinanufaika na huduma hizo za Mkongo.

234. Mheshimiwa Spika, Shirika limeendelea kutoa huduma za fedha kwa njia ya mtandao kupitia TTCL Pesa (T-PESA) ambapo tangu ilipoanzishwa mwezi Julai, 2017 hadi mwezi Februari, 2020 ilikuwa na jumla ya watumiaji wa huduma hiyo **796,421** na jumla ya **mawakala 22,364**. Ili kutanua wigo wa biashara, T-Pesa imeunganishwa kwenye mfumo wa malipo wa Serikali wa GePG, benki na watoa huduma za mawasiliano wengine.

Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote (UCSAF)

235. Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote imesaini mikataba na makampuni ya simu ili kupeleka huduma za mawasilino katika **kata 252** zenye **vijiji 555** na wakazi zaidi ya **milioni 3** ambapo huduma za mawasiliano zinatarajiwa kuwa tayari katika maeneo hayo ifikapo Oktoba, 2020. Hatua hii ni mwendelezo wa utekelezaji wa miradi iliyotangulia ambapo Serikali kupitia Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote imeshapeleka huduma za mawasiliano katika **kata 704** zenye **vijiji 2,501** na wakazi zaidi ya **milioni 5** Tanzania Bara na Tanzania Zanzibar.

236. Mheshimiwa Spika Serikali iko kwenye maandalizi ya kupeleka mawasiliano katika **kata 38** kwenye maeneo ya mipakani na yenye uhitaji maalum ambayo yatapatiwa mawasiliano katika tenda awamu ya tano (5) ambayo itatekelezwa na Shirika la Mawasiliano Tanzania (TTCL). Kazi hii inatarajiwa kuanza mwezi Aprili, 2020.

237. Mheshimiwa Spika Serikali kupitia Mfuko wa Mawasiliano imefanya malipo ya fedha za ununuzi wa vifaa vya TEHAMA kwa ajili ya taasisi ya MOI na Hospitali ya Taifa MUHIMBILI ili kuunganisha hospitali katika mtandao na ukaguzi wa Hospitali na vituo vitakavyohusika. Hospitali zitakazounganishwa ni MOI, Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Morogoro na Hospitali ya Mkoa Ruvuma.

Tume ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (ICTC)

238. Mheshimiwa Spika, Tume imefanya majaribio (pilot) ya usajili wa wataalam wa TEHAMA kuanzia tarehe 26 Juni, 2019 kupitia mfumo wa kielektroniki wa kusajili wataalam wa TEHAMA. Hadi kufikia tarehe 30 Novemba, 2019 jumla ya **maombi 1,559** yalisajiliwa katika Mfumo wa Kielektroniki wa IPRS. Jumla ya maeneo 29 ya ubobezi (specialization) ambayo yamegawanywa katika makundi 11 yamebainishwa. Mwongozo wa kisera umeandaliwa na umeainisha madaraja manne ya utaalam wa TEHAMA (professional categories) ambayo ni *ICT Consultant, ICT Professional, ICT Graduate na ICT Technician*. Serikali imeanza hatua za awali za kutunga Sheria mahsusi kwa ajili ya usajili na uendelezaji wa wataalam wa TEHAMA nchini kote.

239. Mheshimiwa Spika, Tume ilifanya kongamano la Tatu la Mwaka la TEHAMA (Tanzania Annual ICT Conference, TAIC) tarehe 23 hadi 25 Oktoba, 2019 jijini Dar es Salaam ambapo zaidi ya watu 400 kutoka ndani na nje ya nchi; kampuni saba kutoka nje ya Tanzania, kumi za hapa nchini pamoja na taasisi za Serikali zilishiriki maonesho na kujenga mashirikiano ya kibiashara na utoaji huduma za TEHAMA. Kupitia mikutano hii, Tume ya TEHAMA imeweza kukuza fursa za uwekezaji na mashirikiano ya kibiashara katika TEHAMA baina ya wajasiriamali wadogo na wakubwa pamoja na kubaini masuala yanayohitaji mikakati ya kisera ili nchi iweze kunufaika kiuchumi na maendeleo ya ukuaji wa TEHAMA duniani.

240. Mheshimiwa Spika, Tume imeanzisha kituo cha kuwaendeleza watengeneza bidhaa za TEHAMA inayoitwa *SoftCenter*. Kituo cha hicho kimeanzishwa kupitia mradi wa kutengeneza bidhaa za TEHAMA kutokana na TEHAMA zinazofikia mwisho wa mtumizi unaotekelezwa na Tume ya TEHAMA; ni mpango wa Serikali wa kuendeleza vijana wa kitanzania wanaojihusisha na utengenezaji wa bidhaa za TEHAMA. Hadi kufikia mwezi Desemba, 2019 bidhaa za vikundi Sita (6) vya kijasiriamali zilikuwa zimesajiliwa na kushiriki program ya kuziendeleza. Tume pia imewezesha ushiriki wa bidhaa za TEHAMA zilizotengenezwa na vijana wa kitanzania kupitia kituo cha *SoftCenter* katika maonesho ya Nanenane Morogoro na SADC Dar es Salaam mwezi Agosti 2019; Kongamano la Tatu la Mwaka la TEHAMA Tanzania (TAIC) mwezi Oktoba, 2020; Wiki ya Viwanda Tanzania iliyofanyika Dar es Salaam mwezi Desemba, 2019 na tamasha la

kuendeleza bidhaa za TEHAMA huko Luxembourg lililoitwa *Catapult: Inclusion Africa* mwezi Machi, 2020 ambalo liliandaliwa na *Luxembourg House of Financial Technology*. Mpango huu umewezesha bidhaa za kampuni zinazoshiriki mpango wa *SoftCenter* kuwafikia walengwa, kupata washirika wa kibiashara na kujulikana katika soko la bidhaa za TEHAMA.

241. Mheshimiwa Spika, Tume imeendelea kutekeleza program ya kuwezesha wahitimu wa program za TEHAMA kutoka vyuo mbalimbali. Programu hii ilianza kutekelezwa Agosti 2019. Vijana sita (6) wamenufaika na program hii, wawili kati yao wamepata ajira katika Kampuni nyingine nchini.

Baraza la Ushauri la Watumiaji wa Huduma za Mawasiliano (TCRA CCC)

242. Mheshimiwa Spika, Baraza la Ushauri la Watumiaji wa Huduma za Mawasiliano (TCRA CCC) ni taasisi yenye jukumu la kulinda na kutetea maslahi ya watumiaji wa huduma za mawasiliano zinazodhibitiwa kisheria na TCRA. Katika mwaka 2019/20 Baraza limeendelea kutoa elimu na kuhamasisha watumiaji wa huduma na bidhaa za mawasiliano juu ya fursa na masuala muhimu kwa watumiaji wakiwemo Wanafunzi wa Sekondari, vyuo na watumiaji wenye mahitaji maalum (viziwi, wasioona na walemavu wa viungo) ambapo idadi ya watumiaji takriban **3470** walifikiwa. Aidha, kupitia Maadhimisho ya wiki ya mtumiaji mwezi Machi, 2020 Baraza limewafikia watumiaji takribani **12,542**.

243. Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2019/2020 Baraza limeanzisha kamati za watumiaji katika Mkoa wa Kusini Pemba na kuendelea kushauriana na Kamati zingine 11 katika mikoa ya Arusha, Tanga, Morogoro, Mbeya, Iringa, Mwanza, Kagera, Mtwara, Lindi, Mjini Magharib na Dodoma. Aidha, Kamati ziliwafikia Watumiaji takribani **48,769** kutoka makundi ya vijana, wajasiriamali, wanawake, viongozi wa dini na Serikai za Mitaa pamoja na Watumiaji wenye mahitaji maalum. Katika Maadhimisho ya nanenane; Kamati katika mikoa ya Arusha, Lindi, Mbeya, Morogoro na Tanga zilihamasisha na kupokea maoni kutoka kwa watumiaji takriban **13,760**.

244. Mheshimiwa Spika, Baraza limeendelea kuwakilisha watumiaji wa huduma za mawasiliano kwa kuwasilisha maoni, taarifa

na kushauriana na Mamlaka ya Mawasiliano. Aidha, Baraza limeshauriana na watoa huduma za mawasiliano kuhusu masuala yanayogusa watumiaji ikiwemo changamoto zitokanazo na huduma za vifurushi vya inteneti na sauti na kushauriana na Shirika la Posta Tanzania.

C.2 TAASISI ZA MAFUNZO

245. Mheshimiwa Spika, Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano inasimamia vyuo vya mafunzo vifuatavyo:

Chuo cha Ujenzi Morogoro (Morogoro Works Training Institute – MWTI)

246. Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2019/20, Chuo cha Ujenzi kilipanga kufundisha jumla ya wanafunzi **1,200** wa fani za Barabara na Ukaguzi wa Madaraja, Majengo, Magari, Mfumo wa Umeme na Elektroniki. Chuo kilipanga kutoa pia mafunzo ya Madereva wa magari ya Umma (Public Professional Drivers), Madereva wa magari ya abiria (PSV), fani za ufundi mbalimbali (Basic Artisans), Madereva wa awali, Madereva wa Magari ya Abiria, utengenezaji wa Mitambo (Plant Mechanics) na uendeshaji wa mitambo (Plant Operation) pamoja na Nguvukazi stahiki (Labour Based Technology). Aidha, Chuo kilipanga kutoa mafunzo kwa makandarasi wanaotekeleza shughuli za ukarabati wa barabara, majengo na umeme hasa kwa wale makandarasi wa kazi maalum (Specialized Contractors) wa Daraja la I – III na waliosajiliwa na Bodi ya Usajili wa Makandarasi katika madaraja ya kuanzia IV - VII.

Hadi Machi, 2020 jumla ya wanafunzi **888** wa fani za ufundi stadi wa kozi za barabara na madaraja, majengo, Nguvukazi stahiki (Labour Based Technology), umeme, udereva wa mitambo, uchoraji majengo pamoja na udereva wa awali na magari ya abiria walipatiwa mafunzo. Aidha, Chuo kiliendelea na ukarabati wa majengo, ununuzi wa samani, ukarabati wa zana za kufundishia na magari, kukitangaza Chuo pamoja na kununua vifaa vya kufundishia.

Chuo cha Matumizi ya Teknolojia Stahiki ya Nguvukazi Mbeya (Appropriate Technology Training Institute - ATTI)

247. Mheshimiwa Spika, Chuo hiki kilianzishwa kwa lengo la kuratibu, kutoa na kuendeleza matumizi stahiki ya teknolojia ya nguvukazi katika ukarabati na matengenezo ya barabara nchini.

248. Mheshimiwa Spika, hadi Machi, 2020 Chuo kimefanikiwa kuandaa na kuendesha mafunzo ya ukarabati na matengenezo ya barabara za changarawe, kozi maalumu ya vikundi vya wanawake na vijana katika kozi ya ujenzi wa barabara kwa kiwango cha lami; kufanya ukarabati wa miundombinu ya Chuo ili kuboresha huduma kwa watendaji wake na washiriki wa kozi; pamoja na kutoa mafunzo kwa njia ya vitendo kupitia barabara za mafunzo ambapo kilomita 1.2 zilikarabatiwa katika Halmashauri ya Rungwe na kilomita 21 zilizo chini ya Wakala wa Barabara (TANROADS) Mbeya zilifanyiwa matengenezo ya kawaida kwa ajili ya mafunzo kwa vitendo. Katika kutekeleza mafunzo ya vitendo wananchi wapatao 428 wamenufaika pamoja na kupata ujuzi wa kukarabati na kutengeneza barabara kwa kutumia Teknolojia Stahiki ya Nguvukazi. Aidha, mita 40 ziliwekwa tabaka la lami (Single Surface Dressing) katika Barabara ya Lugombo, Mbeya.

Chuo vilevile kimeendelea kuhamasisha matumizi ya Teknolojia Stahiki ya Nguvukazi hapa nchini kwa kushiriki kwenye semina ya kimataifa iliyoandaliwa na Tanzania Roads Association (TARA) Mkoani Arusha, maonesho ya Nane nane kikanda yaliyofanyika Mkoa wa Mbeya na mkutano wa mwaka wa mashauriano wa pamoja kati ya Bodi za Usajili wa Wakandarasi (CRB), Wahandisi (ERB) na Wasanifu na Wakadiriaji Majenzi (AQRB). Aidha, Chuo kilifanya ziara ya kuhamasisha matumizi ya teknolojia stahiki ya nguvukazi na kutangaza shughuli za Chuo katika ofisi za Halmashauri za Mikoa ya Iringa, Morogoro, Lindi na Mtwara ambapo jumla ya Halmashauri ishirini na saba (27) zilitembelewa na kuhamasishwa. Chuo vilevile kimeendelea na maandalizi ya marekebisho ya miundombinu ya Chuo ili kukidhi mahitaji ya uanzishwaji wa Taasisi ya Teknolojia ya Ujenzi (ICoT).

Chuo cha Bahari Dar es Salaam (DMI)

249. Mheshimiwa Spika, Chuo cha Bahari Dar es Salaam (DMI) kimeendelea kutoa mafunzo ya Ujuzi na Utaalamu (Certificates of Competency) masuala ya usafiri majini kwa kuzingatia viwango vilivyowekwa na Shirika la Uwakala wa Meli Tanzania (TASAC) na Shirika la Bahari Duniani (IMO). Aidha, Chuo hiki kinaendeshwa kwa kuzingatia Ubora wa Viwango vya Kimataifa yaani ISO 9001:2015. Katika kipindi cha Julai, 2019 hadi Machi, 2020, DMI ilitekeleza kazi zifuatazo:

- (i) Kutoa kozi ndefu 21 ambapo Wanafunzi 1,126 walidahiliwa katika mwaka wa masomo 2019/20. Aidha, jumla ya Wanafunzi

- 1,266 walidahiliwa kwa mafunzo ya kozi fupi za awali katika taaluma ya bahari;
- (ii) Kununua Boti ndogo ya mafunzo ili kuboresha elimu kwa vitendo katika kozi fupi za usalama baharini;
 - (iii) Kukamilisha taratibu za kumpata Mtaalamu Mwelekezi wa kupanga matumizi bora ya Ardhi (Master Plan) katika eneo la Chuo lililopo Mkuranga na Sokoine Drive;
 - (iv) Kukamilisha uboreshaji wa Mitaala 18 na kuandaa Mitaala mipya ya fani mbalimbali katika Sekta ya Bahari ikiwemo fani za utafiti na uchimbaji wa Gesi na Mafuta baharini;
 - (v) Kuanza kutoa mafunzo ya Shahada ya Uzamili katika taaluma ya Uchumi wa Usafirishaji wa Shehena Baharini na Lojistiki; na
 - (vi) Kupeleka Walimu wanane (8) nchini China kwa ajili ya masomo ya juu kwenye fani ya Bahari ambapo Walimu wawili (2) wanasoma Shahada ya uzamivu (PhD) na sita (6) Shahada ya uzamili.

Chuo cha Taifa cha Usafirishaji (NIT)

250. Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2019/2020. Chuo kiliendelea kutoa mafunzo ya muda mfupi na muda mrefu ili kukabiliana na changamoto ya uhaba wa wataalamu wa uchukuzi ili kuimarishwa utoaji huduma katika Usafiri kwa njia ya Anga, Maji, Reli na Barabara. Katika mwaka 2019/2020, Chuo kilitoa kozi ndefu 24 ikilinganisha na kozi 21 zilizotolewa katika mwaka wa masomo 2018/2019. Kozi hizi zilidahili jumla ya Wanafunzi 3,561 ikilinganishwa na Wanafunzi 2,877 waliidahiliwa katika mwaka wa masomo 2018/2019 sawa na ongezeko la asilimia 24. Kutokana na ubora wa taaluma na mafunzo yanayotolewa katika Chuo hiki, hadi, Machi, 2020, Chuo kilikuwa na jumla ya Wanafunzi 7,694 ikilinganishwa na Wanafunzi 6,688 waliokuwepo katika kipindi kama hiki katika mwaka. Hili ni sawa na ongezeko la asilimia 15. Aidha, katika mwaka 2019/2020, jumla ya Wanafunzi 1,966 walihitimu mafunzo yao katika kozi ndefu ikilinganishwa na Wanafunzi 1,550 waliohitimu katika mwaka wa masomo 2018/2019. Hili ni ongezeko la asilimia 27.

251. Mheshimiwa Spika, Serikali imeanzisha Kituo cha Umahiri katika Taaluma ya Mafunzo ya Usafiri wa Anga na Operesheni za Usafirishaji (Center of Excellence in Aviation and Transport Operations

- CEATO) kilichoko chini ya Chuo cha Taifa cha Usafirishaji. Lengo la kuanzisha kituo hiki ni kukiwezesha Chuo kufundisha wataalamu wabobezi wa Sekta ndogo za usafiri wa Anga, Reli, Barabara na usafiri kwa njia ya Maji. Kazi ya kuandaa Mitaala sita (6) ya kufundisha wataalamu hawa imekamilika na sasa iko kwenye hatua za mwisho za kupata Ithibati kutoka Baraza la Taifa la Elimu la Ufundi (NACTE) na Mamlaka ya Usafiri wa Anga (TCAA).

252. Mheshimiwa Spika, Serikali inatambua uwepo ya changamoto za ajali za barabarani na usalama katika uchukuzi. Ili kukabiliana na changamoto hizi, Serikali imepata mkopo kutoka Benki ya Maendeleo ya Afrika (AfDB) ili kuanzisha Kituo cha Kikanda cha Umahiri wa Mafunzo ya Usalama Barabarani (Regional Centre of Excellence in Road Safety). Kituo hiki kitawajengea uwezo zaidi wataalamu wa masuala ya usalama barabarani. Pia, kituo kitafanya tafiti mbalimbali ili kushauri namna bora ya kusaidia kupunguza ajali za barabarani. Chuo kinaendelea na taratibu za kuanzisha Kituo hiki.

253. Mheshimiwa Spika, kwa upande wa uboreshaji wa miundombinu na mazingira ya kufundishia na kufanyia kazi, katika kipindi cha Julai, 2019 hadi Machi, 2020, Chuo kimeendelea kukamilisha upanuzi wa majengo ya utawala na uhasibu; na ujenzi wa jengo jipya la ghorofa mbili (Aviation Complex) ambalo litakuwa na madarasa, ofisi za Wahadhiri, Ukumbi wa Mikutano, Maabara pamoja na Karakana ya Ndege.

Chuo cha Usafiri wa Anga Dar es Salaam (CATC)

254. Mheshimiwa Spika, Serikali imeendelea kuhakisha kuwa Chuo cha Usafiri wa Anga Dar es Salaam kinaendelea kuboreshwa ili kukidhi matakwa ya kitaifa na kimataifa. Chuo hiki ambacho kimepata Ithibati ya Kudumu ya Shirika la Usafiri wa Anga Duniani Oktoba, 2019, kina ushirikiano wa karibu na Umoja wa Vyuo vya Tasmania ya Usafiri wa Anga vya Afrika (The Association of African Aviation Training Organisations - AATO). Aidha, Chuo kimeendelea kudahili wanafunzi kutoka nchi za Uganda, Botswana, Namibia, Eswatini, Zambia, Burundi, Rwanda, Somalia, Nigeria, Liberia, Sierra Leone na Guinea Conakry. Aidha, sehemu kubwa ya wahitimu wa Chuo hiki ni kutoka nje ya Tanzania ambapo kati ya wanafunzi 1,395 waliohitimu mafunzo katika mwaka 2018/2019, wazawa ni 55 na waliotoka nje ya nchi ni 1,340.

Chuo cha Hali ya Hewa Kigoma

255. Mheshimiwa Spika, Serikali imeendelea kuboresha miundombinu ya Chuo cha Hali ya Hewa Kigoma ili kuweka mazingira bora ya ufundishaji. Katika mwaka 2019/2020, jumla ya Wanafunzi 68 walidahiliwa ikilinganishwa na wanafuzi 58 waliodahiliwa katika mwaka 2018/2019. Kati ya hao, wanafunzi 14 walikuwa ngazi ya Cheti na 54 ngazi ya Diploma. Aidha, jumla ya wanafunzi 57 walihitimu mafunzo yao ambapo wanafunzi 30 walihitimu mafunzo ya hali ya hewa katika ngazi ya Cheti na 27 walihitimu mafunzo ya hali ya hewa katika ngazi ya Diploma.

C.3 MASUALA MTAMBUKA

Ushirikishwaji wa Wanawake Katika Kazi za Barabara

256. Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2019/20, Wizara imeendelea kutekeleza mikakati mbalimbali ya kuongeza ushiriki wa wanawake katika kazi za barabara. Kazi zilizofanyika ni pamoja na kuendelea kutoa elimu kwa wadau kuhusu kazi za ushirikishwaji wa wanawake katika kazi za barabara ikiwa ni pamoja na elimu juu ya Mwongozo wa Ushirikishwaji Wanawake katika kazi za barabara. Kazi nyingine ilikuwa ni kutoa mafunzo kwa wanawake Makandarasi **20** kutoka Mikoa ya Tabora, Kigoma, Katavi na Rukwa kuhusu usimamizi wa mikataba, teknolojia ya nguvukazi na namna bora ya ujazaji zabuni yaliyofanyika mkoani Kigoma. Lengo ni kuwajengea uwezo wa kumudu ushindani katika kazi za ukandarasi na hatimaye kuwezesha makampuni yao kupanda madaraja. Wizara vilevile iliratibu na kuendesha mafunzo mkoani Morogoro kwa wanawake **50** waliotoka katika vikundi na kampuni kutoka mikoa ya Dodoma, Kilimanjaro, Singida, Shinyanga, Songwe, Ruvuma, Manyara na Tanga ili kuwapa ujuzi wa kushiriki katika kazi za barabara kwa kutumia teknolojia ya nguvukazi.

Maboresho ya Sheria za Kisekta

257. Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2019/20, Wizara iliendelea na kazi ya kupitia sheria zinazohusu sekta kwa lengo la kuainisha maeneo yenye mapungufu na yanayohitaji kufanyiwa marekebisho. Sheria zinazofanyiwa mapitio ni pamoja na Sheria ya Barabara Sura ya 167, Sheria ya Baraza la Taifa la Ujenzi Sura ya 162,

Sheria ya Usajili wa Makandarasi Sura ya 263, Sheria ya Usajili wa Wahandisi Sura ya 63 na Sheria ya Usajili wa Wabunifu Majengo na Wakadiriaji Majenzi Sura ya 269. Baada ya mapitio na marekebisho ya Sheria kufanyika, Wizara itafanya mapitio ya Kanuni na Sheria Ndogondoggo zilizotungwa chini ya Sheria hizo ili kuleta ufanisi wenye tija wakati wa utekelezaji wake.

Ushiriki wa Wizara Katika Jumuiya Mbalimbali za Kimataifa

258. Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2019/20, Wizara imeendelea kushiriki katika mikutano inayohusu Sekta ya Ujenzi katika Jumuiya za Kimataifa na Kikanda hususan Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC), Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC) na Jumuiya za Utatu (COMESA, EAC and SADC Tripartite Free Trade Area).

259. Mheshimiwa Spika, kutokana na ushiriki wa Wizara katika mikutano hiyo, tumeweza kupata mafanikio mbalimbali ikiwemo kupata fedha kutoka NEPAD-IPPF/AfDB kwa ajili ya Upembuzi yakinifu na usanifu wa kina na ujenzi wa miradi ya barabara ya Lusahunga – Rusumo/Kayonza – Kigali inayounganisha Tanzania na Rwanda; barabara ya Nyakanazi – Kasulu – Manyovu/Rumonge – Rutunga – Bujumbura inayounganisha Tanzania na Burundi; na upembuzi yakinifu na usanifu wa kina wa barabara ya Bugene – Kasulo – Kumnazi na Kyaka – Mutukula – Masaka inayounganisha Tanzania na Uganda. Aidha, Benki ya Dunia imeonesha nia ya kutekeleza miradi mbalimbali ya barabara kupitia program zifuatazo: **Development Corridors Transport Project - DCTP**, Miradi itakayotekelezwa chini ya programu hii ni ukarabati wa barabara ya Mtwara – Mingoyo – Masasi (km 200); ukarabati wa barabara ya Lusahunga – Rusumo (km 92); ukarabati wa barabara ya Makambako – Songea (km 295); ujenzi wa barabara ya Iringa – Msembe (Ruaha National Park) - km104 na ujenzi wa Viwanja vya ndege vya Iringa, Lake Manyara na Tanga. Kuhusu **Lake Victoria Transport Programme - LVTP** miradi itakayotekelezwa ni pamoja na upembuzi yakinifu, usanifu wa kina na ujenzi kwa kiwango cha lami barabara za Musoma Port Access na Nansio - Rugezi Port access. Kazi nyingine ni kufanya mapitio ya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina pamoja na ukarabati wa barabara ya Mara /Simiyu Border – Nyanguge (km 100.4) na mapitio ya Upembuzi yakinifu na usanifu wa kina pamoja na ujenzi wa barabara ya Nyamuswa – Bunda – Bulamba - Kisorya (km 106) na Bukoba - Bukoba Port Access. Aidha,

Programu ya Lake *Tanganyika Transport Programme (LTTP)* miradi itakayotekelezwa chini ya programu ya **LTTP** ni upembuzi yakinifu, usanifu wa kina na ujenzi kwa kiwango cha lami barabara ya Kagwira – Karema (km 112) na ujenzi wa barabara ya Mpanda (Vikonge) – Uvinza (km 159).

260. Mheshimiwa Spika, kwa upande wa Jumuiya ya Maendeleo Nchi za Kusini mwa Afrika (SADC), baadhi ya masuala muhimu yanayojadiliwa ni pamoja na:

- i. Uwianishaji wa Sheria, Kanuni, Miongozo na Viwango kuhusu usafirishaji wa mizigo mizito kwa magari makubwa kwa njia ya barabara. Majadiliano hayo yamehusisha Jumuiya za Utatu (COMESA, EAC and SADC Tripartite Free Trade Area) ambapo lengo kuu ni kurahisisha ufanyaji wa biashara katika Jumuiya tatu kwa kuwianisha viwango vya usafirishaji wa mizigo pamoja na ujenzi wa Vituo vya Pamoja vya Ukaguzi wa Magari.
- ii. Kufuatilia utekelezaji wa miradi ya barabara iliyojumuishwa katika Mpango Kamambe wa Uendelezaji wa Miundombinu kwa Nchi Wanachama wa SADC. Miradi hiyo ni ukarabati wa barabara ya Makambako – Songea (km 295) na ujenzi wa barabara ya Kidatu – Ifakara – Malinyi – Londo – Lumecha (km 496) kwa kiwango cha lami.

Rasilimali watu na Maendeleo ya Watumishi

261. Mheshimiwa Spika, Wizara ina jumla ya watumishi **520**. Katika mwaka wa fedha 2019/20, watumishi **24** walistaafu; mmoja (**1**) aliacha kazi na mmoja (**1**) aliachishwa kazi. Watumishi waliostaafu kazi kwa mujibu wa Sheria waligharamiwa na Wizara kuhudhuria mafunzo ya kujiandaa na maisha baada ya kustaafu kazi wakati mafao yao yanaandaliwa na Mfuko wa Hifadhi ya Jamii kwa Watumishi wa Umma (PSSSF). Aidha, Wizara imewaendeleza watumishi wake kitaaluma kwa kuwapeleka katika mafunzo ya muda mrefu na mfupi ikiwa ni pamoja na kutumia fursa mbalimbali za wafadhili. Hadi Machi, 2020, jumla ya watumishi **179** wamehudhuria mafunzo. Kati ya hao, watumishi **21** walishiriki mafunzo ya muda mrefu ndani na nje ya nchi na watumishi **158** walishiriki mafunzo ya muda mfupi ndani ya nchi.

Masuala Mengine Yaliyotekelezwa na Wizara

262. Mheshimiwa Spika, Wizara yangu inaendelea kuchukua hatua mbalimbali ili kukabiliana na mlipuko wa maambukizi ya ugonjwa wa homa kali ya mapafu inayotokana na virusi vya corona (COVID - 19) tangu kugundulika kwa virusi hivyo nchini China Disemba, 2019. Hatua hizo ni pamoja na:

- i. Kuendelea kuhamasisha watumishi wa Wizara na Taasisi zilizo chini yake kuhusu kufuata miongozo inayotolewa na Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Watoto;
- ii. Kutoa elimu endelevu kwa wafanyakazi wanaohudumia abiria na ndege katika viwanja vyote vya ndege na vituo vya mabasi nchini;
- iii. Kutoa huduma ya vifaa kinga na vitakasa mikono kwa abiria wanaoingia na kutoka kwenye vyombo vya moto vya abiria na viwanja vya ndege;
- iv. Kutoa taarifa sahihi kwa wateja kuhusiana na kuwepo/kutokuwepo kwa safari zao za ndege;
- v. Kutoa huduma ya usafiri wa treni ya abiria ya mjini kwa siku za Jumamosi ili kupunguza msongamano wa abiria;
- vi. Kushirikiana na Jeshi la Polisi (Kitengo cha Usalama barabarani) kuhakikisha kuwa mabasi ya mijini hayazidishi abiria (level seat), Mabasi ya UDART yanabeba abiria kwa kiwango cha asilimia 60 tu, Mabasi ya masafa marefu yanabeba abiria kulingana na idadi ya viti ndani ya basi; na
- vii. Kuendelea kutunza mazingira ndani na nje ya vyombo vya usafiri wa Umma.

263. Mheshimiwa Spika, Wizara imeendelea kutoa elimu kwa Umma kuhusu Sera na Mipango inayosimamiwa na Wizara pamoja na kuzitunza na kuhifadhi barabara zetu, kuzingatia Sheria na Kanuni za Matumizi ya Barabara. Aidha, Wizara imeendelea kuboresha matumizi ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA) ili kuongeza ufanisi na kutoa huduma kwa wakati. Mfumo wa utoaji wa vibali vya kusafirisha mizigo isiyo ya kawaida (Abnormal Loads Permit System ALPS) kwa njia ya kielektroniki unaendelea kutoa huduma kwa wasafirishaji nchini na nje ya nchi. Tovuti ya Wizara imeboreshwa ili kuhakikisha kuwa wananchi wengi wanapata taarifa mbalimbali

zinazohusiana na Sekta ya Ujenzi. Wizara pia ipo katika hatua za maandalizi ya uundaji wa mifumo ya usimamizi na ufuatiliaji wa shughuli za Wizara pamoja na Taasisi zake. Mifumo hiyo ni “Intergrated Infrastructure Management System (IIMS)” na “Ferry Management System (FMS)”.

C.5 CHANGAMOTO ZINAZOIKABILI WIZARA NA MIKAKATI YA KUZITATUA

264. Mheshimiwa Spika, katika utekelezaji wa majukumu yake, Wizara ilikabiliwa na changamoto mbalimbali. Changamoto hizo ni pamoja na mahitaji makubwa ya fedha kwa ajili ya utekelezaji wa Miradi ya Miundombinu na utoaji wa huduma za uchukuzi. Ili kukabiliana na changamoto hii, Serikali inaendelea kujadiliana na wawekezaji mbalimbali ikiwa ni pamoja na Taasisi za fedha ili kupata mikopo yenye masharti nafuu kwa ajili ya kutekeleza miradi mikubwa ya maendeleo. Aidha, Serikali inaendelea kushawishi Sekta Binafsi kuwekeza katika uendelezaji na uboreshaji wa miradi ya uchukuzi.

265. Mheshimiwa Spika, vilevile, kuna changamoto ya tishio la homa inayosababishwa na virusi vya Corona (COVID 19). Hali hii imeleta hofu kubwa katika Sekta ya Uchukuzi hususan kwenye Bandari na Viwanja vya Ndege hivyo kuathiri Utendaji wa Taasisi zinazotoa huduma katika maeneo hayo. Wizara inaendelea kuchukua tahadhari katika vituo vya Mipakani, Viwanja vya Ndege na maeneo ya Bandari ili kudhibiti maambukizi ya virusi vya Corona. Aidha, vifaa vya kinga vimeendelea kutolewa kwa wafanyakazi katika maeneo hayo pamoja na utoaji wa elimu kwenye vyombo vya usafiri.

266. Mheshimiwa Spika, changamoto nyingine ni uvamizi, uharibifu na hujuma kwa Miundombinu ya Reli, hususan Reli zenyewe, Mataruma, Vifungio na Madaraja. Wizara itaendelea kushirikiana na vyombo vya Dola pamoja na jamii inayozunguka maeneo ya Reli ili kusimamia Sheria zilizopo kuhusu uharibifu huo pamoja na kutoa elimu na hamasa kwa jamii inayopakana na maeneo ya Reli ili kuelewa umuhimu wa Reli na kuwa walinzi wa miundombinu hiyo.

267. Mheshimiwa Spika, kuna changamoto ya Mabadiliko ya hali ya hewa (Climate Change) yanayosababisha Mifumo ya hali ya hewa kubadilika mara kwa mara na kusababisha uharibifu wa miundombinu

kutokana na mafuriko. Kwa kutambua hili, Wizara imeendelea kupanua Mtandao wa Rada za Hali ya Hewa, kuongeza vifaa na kupanua Mtandao wa vituo vya hali ya hewa nchini kwa lengo la kuboresha utoaji wa utabiri na tahadhari juu ya matukio ya hali mbaya ya hewa na kuelimisha jamii juu ya umuhimu wa kutumia huduma za hali ya hewa.

D. MPANGO NA MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA FEDHA KWA SEKTA ZA WIZARA KWA MWAKA WA FEDHA 2020/21

268. Mheshimiwa Spika, Mpango na Makadirio ya mapato na matumizi ya fedha kwa mwaka 2020/21 ni wa tano (5) na wa mwisho katika utekelezaji wa Mpango wa Pili wa Maendeleo wa Miaka Mitano (2016/17 –20/21). Katika mwaka wa fedha 2020/21, Mpango na Bajeti ya Wizara umelenga kuzingatia vipaumbele ambavyo ni Miradi iliyoainishwa kwenye Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ya mwaka 2015 na Ilani ya Chama cha Mapinduzi ya Awamu zilizopita; Miradi iliyoainishwa kwenye Mpango wa Pili wa Taifa wa Maendeleo wa Miaka Mitano (2016/17 – 2020/21); Miradi iliyoainishwa kwenye malengo ya Mpango Mkakati wa Wizara; Miradi iliyopo kwenye ahadi mbalimbali za Viongozi wa Serikali tangu Awamu ya Kwanza; Miradi ambayo Washirika wa Maendeleo wameonesha nia ya kutoa fedha za utekelezaji ambapo Serikali inatakiwa kutoa mchango wake (Counterpart Fund); Miradi ya Kimkakati (kama vile ya ulinzi wa mipakani, inayoelekea kwenye vivutio vya utalii, Bwawa la kufua umeme la Nyerere, ujenzi wa Reli mpya ya *Standard Gauge*, ufufuaji wa Kampuni ya Ndege Tanzania na ujenzi na ukarabati wa Meli katika Maziwa Makuu) inayohusu barabara, madaraja, bandari, viwanja vya ndege, reli na vivuko ambayo itakuwa na matokeo makubwa katika Sekta nyingine za kiuchumi; Miradi ya Makao Makuu ya Nchi kama vile miradi ya barabara za kupunguza msongamano katika Jiji la Dodoma, uwanja wa ndege wa Msalato, treni za abiria mijini (commuter trains), nyumba za Watumishi wa Umma na majengo ya Serikali.

269. Mheshimiwa Spika, Wizara itaendelea kutekeleza miradi yote kwa uwazi na kwa kuzingatia Sheria na Kanuni za Ununuzi wa Umma ili kuepusha kuwepo kwa vitendo vya rushwa. Aidha, Wizara itachukua hatua stahiki dhidi ya watakaobainika kukiuka sheria, kanuni na taratibu zilizopo.

D.1.1 SEKTA YA UJENZI

Makadirio ya Bajeti ya Matumizi ya Kawaida na Miradi ya Maendeleo

270. Mheshimiwa Spika, Bajeti ya Matumizi ya Kawaida kwa Sekta ya Ujenzi kwa mwaka wa fedha 2020/21 ni **Shilingi 38,774,425,000.00**. Kati ya fedha hizo, **Shilingi 36,420,026,000.00** ni Bajeti ya Mishahara na **Shilingi 2,354,399,000.00** ni Bajeti ya Matumizi Mengineyo. Aidha, Sekta ya Ujenzi imetengewa jumla ya **Shilingi 1,577,586,781,000.00** kwa ajili ya kutekeleza miradi ya maendeleo. Kati ya fedha hizo, Shilingi **1,252,222,598,000.00** ni fedha za ndani na Shilingi **325,364,183,000.00** ni za fedha za nje.

Mgawanyo wa fedha za maendeleo pamoja na miradi iliyotengewa fedha ni kama inavyoonyeshwa katika **Kiambatisho Na.1**. Maelezo kuhusu Miradi ya Maendeleo ni kama ifuatavyo:

MRADI WA KUJENGA UWEZO (INSTITUTIONAL CAPACITY BUILDING)

271. Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2020/21, mradi huu umetengewa jumla ya **Shilingi milioni 302.50** fedha za ndani kwa lengo la kujenga uwezo wa watumishi wa Sekta ya Ujenzi kwa kuwapatia mafunzo na vitendea kazi vya ofisi kwa ajili ya kuboresha utendaji wa Sekta ya Ujenzi.

MIRADI YA VIVUKO, UJENZI WA NYUMBA NA MAJENGO YA SERIKALI

Ujenzi na Ukarabati wa Vivuko na Maegesho ya Vivuko

272. Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2020/21, mradi Ujenzi na Ukarabati wa Vivuko na Maegesho ya Vivuko umetengewa jumla ya **Shilingi milioni 13,785.11** kama ifuatavyo:

i) Ujenzi wa Maegesho ya Vivuko

273. Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2020/21 jumla ya **Shilingi milioni 2,868.82** zimetengwa kwa ajili ya upanuzi wa jengo la abiria na maegesho ya Kigamboni; ujenzi wa maegesho ya Bukondo na Zumacheli; ujenzi wa maegesho ya Nyamisati – Mafia; ujenzi na ukarabati wa maegesho nane **(8)** ya Bugolora – Ukara, Rugezi

– Kisorya, Kilambo – Namoto, Utete – Mkongo, Iramba – Majita, Nyakarilo – Kome, Kasharu – Buganguzi na Kigongo – Busisi; ujenzi wa ofisi, jengo la abiria na uzio kwenye vituo **10** vya vivuko (Bugolora, Ukara, Kome, Nyakaliro, Misome, Kaunda, Nkome, Kisorya, Musoma, na Kinesi)pamoja na ujenzi wa maegesho ya vivuko vya Ngara – Nyakiziba na Muleba – Ikuza. Lengo ni kuwezesha abiria na magari kupanda na kushuka kwenye vivuko nyakati zote za mwaka.

ii) Ujenzi wa Vivuko Vipya

274. Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2020/21, mradi huu umetengewa **Shilingi milioni 6,748.62** kwa ajili ya kukamilisha manunuzi na ujenzi wa vivuko vipya vya Nyamisati – Mafia na Bugolora – Ukara; kuanza manunuzi ya kivuko kipya cha Kisorya – Rugezi, boti 1 ya uokozi kwa ajili ya Utete – Mkongo pamoja na ununuzi wa vifaa vya karakana za TEMESA.

iii) Ukarabati wa Vivuko

275. Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2020/21, mradi Ukarabati wa Vivuko umetengewa jumla ya **Shilingi milioni 4,167.67** kwa ajili ya kukamilisha ukarabati wa Vivuko MV Tegemeo (Mwanza), MV Musoma (Mara), MV Mara (Mara), MV Misungwi (Mwanza), MV Sengerema (Mwanza), MV Ujenzi (Mwanza), MV Kigamboni (Dar es Salaam), MV Kome II (Mwanza) na boti ya uokozi MV KIU (Mwanza). Kazi nyingine ni kuanza ukarabati wa MV Nyerere (Mwanza), MV Kilombero I (Morogoro) na MV Kilombero II (Morogoro).

Ujenzi na Ukarabati wa Nyumba na Majengo ya Serikali

276. Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha wa 2020/21, mradi wa Ujenzi na Ukarabati wa Nyumba na Majengo ya Serikali umetengewa jumla ya **Shilingi milioni 66,870.38** kwa ajili ya kutekeleza miradi ifuatavyo:

i) Ujenzi wa Nyumba za Viongozi

277. Mheshimiwa Spika, katika mwaka fedha 2020/21 jumla ya **Shilingi milioni 6,991.66** zimetengwa kwa ajili ya ujenzi wa nyumba **20** za Viongozi Dodoma pamoja na kuendelea na ujenzi wa nyumba **6** za Majaji katika Mikoa ya Dar es Salaam, Kilimanjaro, Mtwara, Shinyanga, Kagera na Tabora.

ii) Ujenzi wa nyumba 150 za Watumishi wa Umma

278. Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2020/21, jumla ya **Shilingi milioni 10,500.00** zimetengwa kwa ajili ya ujenzi wa nyumba **150** za Watumishi wa Umma Jijini Dodoma na mikoa mingine.

iii) Ujenzi wa jengo la ofisi ya Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano

279. Mheshimiwa Spika, katika mwaka fedha 2020/21 mradi wa ujenzi wa jengo la ofisi ya Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano katika Mji mpya wa Serikali Mtumba – Dodoma, umetengewa jumla ya **Shilingi milioni 5,598.04** kwa ajili ya kukamilisha usanifu na kuanza ujenzi.

iv) Ujenzi wa Nyumba za Makazi Eneo la Magomeni (Magomeni Quarters)

280. Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2020/21, jumla ya **Shilingi milioni 14,650.00** zimetengwa kwa ajili ya kukamilisha ujenzi wa nyumba za Makazi za waliokuwa wakazi wa Magomeni Quarters, Dar es Salaam.

v) Ukarabati wa Nyumba na Manunuzi ya Samani kwa Ajili ya Nyumba za Viongozi

281. Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2020/21, jumla ya **Shilingi milioni 14,290.20** zimetengwa kwa ajili ya ukarabati wa nyumba za viongozi na ununuzi wa samani. Kazi zilizopangwa ni ukarabati wa nyumba 40 za viongozi Dodoma na nyumba 30 mikoa mingine, ukarabati wa nyumba 400 zilizokuwa zinamilikiwa na iliyokuwa Mamlaka ya Ustawishaji Makao Makuu Dodoma (CDA) zilizohamishiwa Wakala wa Majengo Tanzania (TBA), ukarabati wa nyumba zilizokuwa zinamilikiwa na TAMISEMI na NHC zilizohamishiwa TBA katika mikoa 20 pamoja na ununuzi wa samani za nyumba za Ikulu na Ikulu Ndogo za Serikali.

vi) Kujenga Uwezo wa Wabunifu Majengo, Wakadiriaji Majenzi na Huduma za Ushauri

282. Mheshimiwa Spika, katika mwaka fedha 2020/21 jumla ya

Shilingi milioni 1,271.52 zimetengwa kwa ajili ya kuwajengea uwezo Wabunifu Majengo (Architects) na Wakadiriaji Majenzi (Quantity Surveyors) kupitia Bodi ya Usajili wa Wabunifu Majengo na Wakadiriaji Majenzi (AQRB), Huduma za Ushauri pamoja na maandalizi ya viwango vya msawazo (*standards and specifications*) kwa ajili ya kazi na miradi ya ujenzi na ukarabati wa nyumba na majengo ya Serikali pamoja na samani.

vii) Ujenzi na Ukarabati wa Karakana za TEMESA na TBA

283. Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2020/21, jumla ya **Shilingi milioni 8,138.96** zimetengwa kwa ajili ya ukarabati wa karakana kumi na moja (11) za TEMESA zilizopo Tabora, Mwanza, Arusha, Mtwara, Mbeya, M.T Depot Dar es Salaam, Kigoma, Mara, Ruvuma, Pwani na Vingunguti. Kazi nyingine ni kuendelea na ujenzi wa karakana za TEMESA katika Mikoa ya Songwe, Simiyu, Geita, Njombe na Katavi na ujenzi wa karakana mpya ya magari jijini Dodoma. Kazi nyingine ni ukarabati wa karakana za TBA sita (6) katika mikoa ya Tabora, Arusha, Mwanza, Dodoma, Mbeya na Dar es Salaam pamoja na ujenzi wa kiwanda kipya cha kutengeneza samani.

viii) Ufuatiliaji na Tathmini kwenye Miradi ya Ujenzi na Ukarabati wa Nyumba na Majengo ya Serikali

284. Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2020/21, jumla ya **Shilingi milioni 830.00** zimetengwa kwa ajili ya ufuatiliaji na tathmini (monitoring and evaluation) kwenye miradi ya ujenzi na ukarabati wa nyumba na majengo ya Serikali.

ix) Ununuzi wa Karakana Sita (6) Zinazohamishika (Mobile Workshops)

285. Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2020/21, jumla ya **Shilingi milioni 1,000.00** zimetengwa kwa ajili ya ununuzi wa karakana sita zinazohamishika kwa ajili ya matengenezo ya magari ya Serikali katika wilaya ambazo ziko mbali na makao makuu ya mikoa.

x) Kusanifu na Kusimika Mfumo wa Usimamizi na Ufuatiliaji wa Matengenezo ya Magari

286. Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2020/21, jumla ya **Shilingi milioni 3,000.00** zimetengwa kwa ajili ya kusanifu na

kusimika Mfumo wa Usimamizi na Ufuatiliaji wa Matengenezo ya Magari.

xi) Kuanzisha Karakana za Wilaya Pamoja na Kusimika Mfumo wa Usimamizi wa Matengenezo ya Magari

287. Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2020/21, jumla ya **Shilingi milioni 600.00** zimetengwa kwa ajili ya kuendelea na ujenzi na ukarabati wa karakana sita za wilaya (Same, Simanjiro, Masasi, Ukerewe, Chato na Kyela) pamoja na kusimika mifumo ya usimamizi wa taarifa za ukarabati wa magari.

MIRADI YA BARABARA NA MADARAJA

288. Mheshimiwa Spika, miradi ya barabara na madaraja itakayotekelezwa katika mwaka wa fedha 2020/21 ni kama ifuatavyo:

Barabara ya Soni - Bumbuli - Dindira – Korogwe (km 74)

289. Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2020/21, mradi huu umetengewa jumla ya **Shilingi milioni 840.00** kwa ajili ya maandalizi ya kuanza ujenzi kwa kiwango cha lami.

Barabara ya Mtwara – Newala - Masasi (km 221)

290. Mheshimiwa Spika, katika bajeti ya mwaka wa fedha 2020/21, jumla ya **Shilingi milioni 10,000.00** zimetengwa kwa ajili ya kuendelea na ujenzi wa barabara ya Mtwara – Newala – Masasi kwa sehemu ya Mtwara – Mnivata (km 50) na maandalizi ya kuanza ujenzi wa sehemu ya Mnivata – Tandahimba (km 50).

Barabara ya Likuyufusi – Mkenda (km 122.50)

291. Mheshimiwa Spika, katika bajeti ya mwaka wa fedha 2020/21, jumla ya **Shilingi milioni 1,590.00** zimetengwa kwa ajili ya kuanza ujenzi wa sehemu ya barabara hiyo yenye urefu wa kilometa 10.

Barabara ya Nachingwea – Liwale (km 130)

292. Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2020/21, jumla ya **Shilingi milioni 250.00** zimetengwa kwa ajili ya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina wa barabara ya Nachingwea - Liwale.

Barabara ya Ubena Zomozi - Ngerengere (km 11.6)

293. Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2020/21, jumla ya **Shilingi milioni 730.00** zimetengwa kwa ajili ya maandalizi ya ujenzi wa barabara ya Ubena – Zomozi – Ngerengere kwa kiwango cha lami.

Barabara ya TAMCO – Vikawe – Mapinga (km 24)

294. Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2020/21, mradi huu umetengewa jumla ya **Shilingi milioni 950.00** kwa ajili ya kuendelea na ujenzi wa barabara ya TAMCO – Vikawe – Mapinga.

Barabara ya Makofia – Mlandizi (km 36.7)

295. Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2020/21, barabara ya Makofia – Mlandizi imetengewa jumla ya **Shilingi milioni 10.00** kwa ajili ya maandalizi ya ujenzi kwa kiwango cha lami.

Barabara ya Musoma - Makojo - Busekela (km 92)

296. Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2020/21, barabara hii imetengewa jumla ya **Shilingi milioni 2,625.00** kwa ajili ya kuendelea na ujenzi kwa kiwango cha lami.

Barabara ya Kongwa Jct – Mpwapwa – Gulwe – Kibakwe (km 98)

297. Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2020/21, barabara hii imetengewa jumla ya **Shilingi milioni 1,650.00** kwa ajili ya kuendelea na ujenzi kwa kiwango cha lami.

Barabara ya Muhutwe – Kamachumu – Muleba (km 54)

298. Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2020/21, barabara hii imetengewa jumla ya **Shilingi milioni 1,080.00** kwa ajili ya kuendelea na ujenzi kwa kiwango cha lami.

Barabara ya Iringa – Ruaha National Park (km 104)

299. Mheshimiwa Spika, Katika mwaka wa fedha 2020/21, barabara hii imetengewa jumla ya **Shilingi milioni 1,000.00** kwa ajili ya kuanza ujenzi wa barabara ya Iringa – Msembe - Ruaha National Park kwa kiwango cha lami.

Barabara ya Muheza – Amani (km 36)

300. *Mheshimiwa Spika*, katika mwaka wa fedha 2020/21, jumla ya **Shilingi milioni 1,590.00** zimetengwa kwa ajili ya kuendelea na ujenzi kwa kiwango cha lami.

Barabara ya Mtwara – Mingoyo – Masasi (km 200)

301. *Mheshimiwa Spika*, katika mwaka wa fedha 2020/21, jumla ya **Shilingi milioni 1,000.00** zimetengwa kwa ajili ya ukarabati wa barabara hii kwa kiwango cha lami.

Barabara ya Kibaoni - Majimoto - Muze - Kilyamatundu (km 189)

302. *Mheshimiwa Spika*, katika mwaka wa fedha 2020/21, jumla ya **Shilingi milioni 5,420.00** zimetengwa kwa ajili ya kuanza ujenzi kwa kiwango cha lami wa barabara za Kibaoni – Majimoto – Inyonga (km 152) na Ntendo – Muze – Kilyamatundu sehemu ya Ntendo – Muze (km 37) kwa kiwango cha lami.

Daraja la Kigongo - Busisi na Barabara Unganishi

303. *Mheshimiwa Spika*, katika mwaka wa fedha 2020/21, jumla ya **Shilingi milioni 21,295.00** zimetengwa kwa ajili ya kuendelea na ujenzi wa Daraja la Kigongo - Busisi (km 3.2) na barabara unganishi.

Daraja la Mzinga

304. *Mheshimiwa Spika*, katika mwaka wa fedha 2020/21, jumla ya **Shilingi milioni 20.00** zimetengwa kwa ajili ya maandalizi ya ujenzi wa Daraja la Mzinga.

Daraja la Ugalla

305. *Mheshimiwa Spika*, katika mwaka wa fedha 2020/21, jumla ya **Shilingi milioni 250.00** zimetengwa kwa ajili ya maandalizi ya ujenzi wa Daraja la Ugalla.

Daraja la Kitengule na Barabara Unganishi

306. *Mheshimiwa Spika*, katika mwaka wa fedha 2020/21, jumla ya **Shilingi milioni 1,500.00** zimetengwa kwa ajili ya kuendelea na ujenzi wa Daraja la Kitengule pamoja na barabara unganishi zenye urefu wa kilometa 18.

Barabara ya Morogoro - Dodoma (km 260.0) Pamoja na Daraja la Mkundi

307. Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2020/21, jumla ya **Shilingi milioni 1,125.00** zimetengwa kwa ajili ya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina wa ukarabati wa barabara ya Morogoro – Dodoma pamoja na Daraja la Mkundi.

Daraja Jipya la Wami

308. Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2020/21, jumla ya **Shilingi milioni 3,500.00** zimetengwa kwa ajili ya kuendelea na ujenzi wa Daraja Jipya la Wami lililopo mkoani Pwani.

Barabara ya Njombe - Makete - Isyonje (km 157.4)

309. Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2020/21, jumla ya **Shilingi milioni 22,000.00** zimetengwa kwa ajili ya kuendelea na ujenzi kwa kiwango cha lami wa barabara ya Njombe – Makete – Isyonje sehemu ya Njombe – Moronga (km 53.9) na Moronga – Makete (km 53.5). Aidha, kazi nyingine ni kuanza ujenzi wa barabara ya Isyonje – Makete (km 50) kwa kiwango cha lami.

Barabara ya Omugakorongo - Kigarama - Murongo (km 105)

310. Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2020/21, jumla ya **Shilingi milioni 8,000.00** zimetengwa kwa ajili ya fidia na kuanza ujenzi wa barabara hii kwa kiwango cha lami.

Barabara ya Nanganga - Ruangwa - Nachingwea (km 145)

311. Mheshimiwa Spika, jumla ya **Shilingi milioni 7,430.00** zimetengwa katika mwaka wa fedha 2020/21 kwa ajili ya kuanza ujenzi wa barabara za Masasi – Nachingwea (km 45.0) na Nanganga – Ruangwa – Nachingwea (km 100.0) sehemu ya Nanganga – Ruangwa (km 53.2) kwa kiwango cha lami.

Barabara ya Mpemba – Isongole (km 51.2)

312. Mheshimiwa Spika, jumla ya **Shilingi milioni 5,310.00** zimetengwa katika mwaka wa fedha 2020/21 kwa ajili ya kuendelea na ujenzi kwa kiwango cha lami wa barabara ya Mpemba – Isongole (km 51.2). Aidha, kazi nyingine ni kuendelea na maandalizi ya ujenzi kwa

kiwango cha lami wa barabara za Ruanda – Iyula – Nyimbili (km 21.0) na kuanza ujenzi kwa utaratibu wa *Design and Build* barabara ya Katumbasongwe - Kasumulu - Ngana – Ileje (km 90.10) kwa kiwango cha lami.

Barabara ya Tanga - Pangani – Makurunge (km 174.5)

313. Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2020/21, jumla ya **Shilingi milioni 50,800.00** zimetengwa kwa ajili ya kuendelea na ujenzi kwa kiwango cha lami wa barabara ya Tanga - Pangani (km 50). Kati ya hizo, fedha za ndani ni **Shilingi milioni 7,000.00** na **Shilingi milioni 43,800.00** ni fedha za nje. Kazi nyingine ni kuanza ujenzi wa barabara ya Pangani – Mkange (km 124.5) kwa kiwango cha lami na Daraja la Pangani.

Barabara ya Kisarawe – Maneromango (km 54)

314. Mheshimiwa Spika, jumla ya **Shilingi milioni 1,400.00** zimetengwa katika mwaka wa fedha 2020/21 kwa ajili ya kuendelea na ujenzi wa barabara hii kwa kiwango cha lami.

Barabara ya Geita – Bulyanhulu – Kahama (km 120)

315. Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2020/21, jumla ya **Shilingi milioni 11,500.00** zimetengwa kwa ajili ya kuanza ujenzi kwa kiwango cha lami barabara za Geita – Bulyanhulu Jct (km 58.3), Bulyanhulu Jct – Kahama (km 61.7) na Uyogo – Nyamilangano – Nyandekwa – Kahama (km 54).

Barabara ya Nyamirembe Port – Katoke (km 50)

316. Mheshimiwa Spika, jumla ya **Shilingi milioni 20.00** zimetengwa katika mwaka wa fedha 2020/21 kwa ajili ya maandalizi ya ujenzi wa barabara hii kwa kiwango cha lami.

Barabara ya Geita – Nzera (km 54)

317. Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2020/21, jumla ya **Shilingi milioni 1,000.00** zimetengwa kwa ajili ya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina wa barabara hii.

Barabara ya Arusha - Moshi - Himo - Holili (km 199.51)

318. Mheshimiwa Spika, jumla ya **Shilingi milioni 4,800.00**

zimetengwa katika mwaka wa fedha 2020/21 kwa ajili ya kuendelea na ujenzi wa barabara ya Kijenge – Usa River (km 20). Aidha, fedha hizi zitahusisha maandalizi ya kuanza ujenzi wa barabara ya Mianzini – Ngaramtoni (km 18.0) kwa kiwango cha lami na upanuzi wa barabara ya Tengeru – Moshi – Himo (km 105) pamoja na ujenzi wa Mizani ya Himo.

Barabara za Kuelekea Kwenye Mradi wa Kufua Umeme Katika Maporomoko ya Mto Rufiji (Access Roads To Rufiji Hydropower Project)

319. Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2020/21, mradi huu umetengewa jumla ya **Shilingi milioni 3,179.00** kwa ajili ya ukarabati kwa kiwango cha changarawe wa barabara za Bigwa – Matombo – Mvuha (km 70), Maneromango - Vikumburu - Mloka (km 100) na Kibiti – Mloka - Mtemele – Rufiji. Aidha, mradi huu utahusisha ukarabati kwa kiwango cha changarawe sambamba na kufanya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina wa barabara ya Ubena Zomozi - Mvuha - Kisaki - Mtemele Jct (km178) ikiwa ni mandalizi ya kuijenga kwa kiwango cha lami.

Barabara ya Dar es Salaam – Chalinze – Morogoro (km 152.3)

320. Mheshimiwa Spika, mradi huu umetengewa jumla ya **Shilingi milioni 3,810.00** katika mwaka wa fedha 2020/21 kwa ajili ya kuendelea na ukarabati (*overlay*) wa barabara ya Mlandizi – Chalinze (km 44) na ujenzi kwa kiwango cha lami wa barabara ya Kwa Mathiasi (Morogoro Road) – Msangani (km 8.3).

Barabara ya Wazo Hill – Bagamoyo – Msata (km 54.1)

321. Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2020/21, mradi huu umetengewa jumla ya **Shilingi milioni 80.00** kwa ajili ya kuanza maandalizi ya ukarabati na upanuzi wa barabara ya Wazo Hill – Bagamoyo – Msata (Tegeta – Bagamoyo Section) (km 46.9) na barabara ya Mbegani – Bagamoyo (km 7.2).

Barabara ya Usagara – Geita – Buzirayombo – Kyamyorwa (km 110)

322. Mheshimiwa Spika, mradi huu umetengewa jumla ya **Shilingi milioni 10.00** katika mwaka wa fedha wa 2020/21, kwa ajili ya kulipa sehemu ya malipo ya Makandarasi kwa sehemu za Uyovu –

Bwanga (km 43) na Bwanga – Biharamulo (km 67).

Barabara ya Nyakahura - Kumubuga - Rulenge - Kabanga Nickel Road (km 141)

323. Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha wa 2020/21, mradi huu umetengewa jumla ya **Shilingi milioni 30.00** kwa ajili ya kuendelea na kazi ya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina wa barabara ya Nyakahura – Kumubuga – Murusagamba na Kumubuga – Rulenge – Kabanga Nickel (km 141) ikiwa ni maandalizi ya ujenzi kwa kiwango cha lami.

Barabara ya Kigoma – Kidahwe – Uvinza – Kaliua – Tabora (km 389.7)

324. Mheshimiwa Spika, mradi huu umetengewa jumla ya **Shilingi milioni 25,440.00** katika mwaka wa fedha wa 2020/21. Kati ya fedha hizo, **Shilingi milioni 10,440.00** ni fedha za ndani na **Shilingi milioni 15,000.00** ni fedha za nje kwa ajili ya kuendelea na ujenzi wa sehemu za Urambo – Kaliua (km 28), Kazilambwa – Chagu (km 42) na kuanza ujenzi wa kwa kiwango cha lami sehemu ya Uvinza – Malagarasi (km 51.1).

Barabara ya Ifakara - Kihansi - Mlimba - Madeke - Kibena (Njombe) (km 220)

325. Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha wa 2020/21, mradi huu umetengewa jumla ya **Shilingi milioni 6,000.00** kwa ajili ya kuanza ujenzi wa barabara ya Kibena – Lupembe (km 50) kwa kiwango cha lami na maandalizi ya ujenzi kwa kiwango cha lami barabara za Ifakara – Kihansi (km 50) na Lupembe – Madeke (km 50).

Barabara ya Karatu - Mbulu - Haydom - Sibiti River - Lalago - Maswa (km 389)

326. Mheshimiwa Spika, mradi huu umetengewa jumla ya **Shilingi milioni 5,000.00** katika mwaka wa fedha wa 2020/21, kwa ajili ya kuanza ujenzi kwa kiwango cha lami barabara ya Karatu – Mbulu – Haydom – Sibiti River – Lalago – Maswa sehemu ya Mbulu – Haydom (km 50).

Barabara ya Marangu – Tarakea – Rongai – Kamwanga /Bomang’ombe – Sanya Juu (km 84.80)

327. Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha wa 2020/21, mradi huu umetengewa jumla ya **Shilingi milioni 1,700.00** kwa ajili ya kuendelea na ujenzi wa barabara za Kwa Sadala – Masama – Machame Junction (km 16) na Kiboroloni – Kiharara – Tsuduni – Kidia (km 10.8).

Barabara ya Tukuyu – Mbambo – Katumba (km 80.3)

328. Mheshimiwa Spika, mradi huu umetengewa jumla ya **Shilingi milioni 2,850.00** katika mwaka wa fedha wa 2020/21 kwa ajili ya kuendelea na ujenzi kwa kiwango cha lami wa sehemu ya Tukuyu – Mbambo (km 34.6). Kazi nyingine ni kuanza ujenzi wa sehemu za Bujesi – Mbambo (km 26.0) na Mbambo – Ipinda (km 19.7).

Barabara ya Dodoma – Manyoni (km 127) na Barabara ya Mchepuo Kuingia Manyoni Mjini (km 4.8)

329. Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha wa 2020/21, mradi huu umetengewa jumla ya **Shilingi milioni 160.00** kwa ajili ya kuendelea na ujenzi wa Kituo cha Pamoja cha Ukaguzi (One Stop Inspection Station – OSIS) cha Muhalala (Manyoni).

Barabara ya Tabora - Mambali - Bukene - Itobo (km 114)

330. Mheshimiwa Spika, mradi huu umetengewa jumla ya **Shilingi milioni 1,000.00** katika mwaka wa fedha wa 2020/21, kwa ajili ya kuanza ujenzi kwa kiwango cha lami.

Barabara ya Namanyere - Katongoro - New Kipili Port (km 64.80)

331. Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha wa 2020/21, mradi huu umetengewa jumla ya **Shilingi milioni 310.00** kwa ajili ya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina ikiwa ni maandalizi ya ujenzi kwa kiwango cha lami.

Barabara ya Dumila – Kilosa – Mikumi (km 119)

332. Mheshimiwa Spika, mradi huu umetengewa jumla ya **Shilingi milioni 13,520.00** katika mwaka wa fedha wa 2020/21 kwa ajili ya kuendelea na ujenzi kwa kiwango cha lami wa sehemu ya

Rudewa – Kilosa (km 24) na kuanza ujenzi wa barabara ya Kilosa – Ulaya – Mikumi (km 50) kwa kiwango cha lami.

Barabara ya Sumbawanga – Matai – Kasanga Port (km 112)

333. *Mheshimiwa Spika*, katika mwaka wa fedha wa 2020/21, jumla ya **Shilingi milioni 11,000.00** zimetengwa kwa ajili ya kukamilisha ujenzi wa barabara ya Sumbawanga – Matai – Kasanga Port (km 112) na kuanza ujenzi wa barabara ya Matai – Kasesya (km 50) kwa kiwango cha lami.

Ujenzi wa Madaraja Makubwa

334. *Mheshimiwa Spika*, mradi huu umetengewa jumla ya **Shilingi milioni 14,185.00** katika mwaka wa fedha wa 2020/21 kwa ajili ya kuanza ukarabati wa daraja la Kirumi (Mara); kuendelea na ujenzi wa Daraja la Sibiti (Singida) na barabara zake unganishi, Daraja la Msingi (Singida), Daraja la Ruhuhu (Ruvuma) na Daraja la Sukuma (Mwanza). Aidha, kazi nyingine ni kufanya mapitio ya usanifu na ujenzi wa Daraja la Mirumba (Katavi); ujenzi wa Daraja la Simiyu (Mwanza), Daraja la Kiegeya (Morogoro), Daraja la Sanza (Singida) na Daraja la Mkenda (Ruvuma). Vilevile, mradi huu utahusisha kuendelea na upembuzi yakinifu na usanifu wa kina wa Daraja la Mtera (Iringa/Dodoma), Daraja la Godegode (Dodoma) na Daraja la Mitomoni (Ruvuma); kuanza upembuzi yakinifu na Usanifu wa Kina wa Daraja la Malagarasi Chini (Kigoma) na kununua Vipuri vya Daraja la vyuma la dharura (Emergency Steel Bridge Parts).

Barabara ya New Bagamoyo (Kawawa Jct – Tegeta (km 17.2)

335. *Mheshimiwa Spika*, katika mwaka wa fedha 2020/21, jumla ya **Shilingi milioni 11,363.89** zimetengwa ambapo fedha za ndani ni **Shilingi milioni 260.00** na fedha za **nje Shilingi milioni 11,103.89** kwa ajili ya kuendelea na upanuzi wa sehemu ya Morocco – Mwenge (km 4.3) na kuboresha mifereji ya maji ya mvua kwenye sehemu ya Mwenge – Tegeta (km 14).

Barabara ya Kyaka – Bugene – Kasulo (km 222.10)

336. *Mheshimiwa Spika*, jumla ya **Shilingi milioni 2,010.00** zimetengwa katika mwaka wa fedha 2020/21 kwa ajili ya kukamilisha mapitio ya usanifu wa barabara za Kumunazi - Bugene – Kasulo (km

133) na Kyaka - Mutukula (km 30) ikiwa ni maandalizi ya ujenzi kwa kiwango cha lami.

Barabara ya Isaka – Lusahunga (km 392.0)

337. Mheshimiwa Spika, jumla ya **Shilingi milioni 2,740.00** zimetengwa katika mwaka wa fedha 2020/21 kwa ajili ya kuendelea na ujenzi wa kituo cha Pamoja cha Ukaguzi – OSIS cha Nyakanazi pamoja na kuanza ukarabati wa sehemu ya Lusahunga – Rusumo na Nyakasanza - Kobero (km 150).

Barabara ya Manyoni – Itigi – Tabora (km 259.7)

338. Mheshimiwa Spika, jumla ya **Shilingi milioni 23,364.47** zimetengwa katika mwaka wa fedha 2020/21, ambapo **Shilingi milioni 650.00** ni fedha za ndani na **Shilingi milioni 22,714.47** ni fedha za nje kwa ajili ya kuendelea na ujenzi wa sehemu ya Nyahua – Chaya (km 85.4) kwa kiwango cha lami.

Barabara za Mikoa (km 630.62)

339. Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2020/21, jumla ya **Shilingi milioni 48,880.96** zimetengwa kwa ajili ya barabara za mikoa na madaraja katika mikoa yote 26 ya Tanzania Bara. Kati ya hizo, **Shilingi milioni 48,500** ni fedha za ndani na **Shilingi milioni 380.96** ni fedha za nje. Kazi zilizopangwa kutekelezwa ni ukarabati wa jumla ya **kilometa 589.31** kwa kiwango cha changarawe, kujenga kilometa **41.31** kwa kiwango cha lami na ujenzi na ukarabati wa madaraja/Makalavati **24**. Kazi nyingine ni kuwezesha mafunzo kwa vitendo kwa Wahandisi Wahitimu (Structured Engineers Apprenticeship Programme - SEAP). Orodha ya miradi ya barabara za Mikoa itakayotekelezwa kwa kutumia fedha za Bajeti ya Maendeleo kutoka Mfuko Mkuu wa Serikali imeoneshwa katika **Kiambatisho Na. 2**.

Barabara ya Mwanza/Shinyanga Border – Mwanza (km 102)

340. Mheshimiwa Spika, jumla ya **Shilingi milioni 310.00** zimetengwa katika mwaka wa fedha 2020/21, kwa ajili ya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina ili kuifanyia ukarabati barabara hii.

Mradi wa Kuondoa Msongamano Barabara za Dar es Salaam (km 152.16)

341. Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2020/21, mradi huu umetengewa jumla ya **Shilingi milioni 7,070.00** kwa ajili ya kuendelea na ujenzi wa barabara ya Banana – Kitunda – Kivule – Msongola (km 14.7) na Wazo Hill – Madale (km 6.0); kuanza ujenzi wa barabara za Kibamba – Kisopwa – Kwembe – Makondeko (km 14.66) sehemu ya Mloganzila – Mloganzila Citizen (km 4.0), Ardhi – Makongo (km 5.0), Kongowe – Mjimwema – Kivukoni Ferry Road (One Lane Widening), Mji Mwema – Kimbiji – Pembamnazi (km 27.0) na Goba – Matosa – Temboni (km 6.0) pamoja na kuanza upanuzi wa barabara ya Mwai Kibaki (km 9.1) na Kongowe – Mji Mwema – Kivukoni (km 25.1).

Barabara ya Nyamuswa – Bunda – Kisorya (km 106)

342. Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2020/21, jumla ya **Shilingi milioni 4,790.00** zimetengwa kwa ajili ya kuendelea na ujenzi wa barabara za Nansio – Kisorya – Bunda – Nyamuswa (sehemu ya Kisorya – Bulamba (km 51) na Nyamuswa – Bunda - Bulamba (km 55) kwa kiwango cha lami.

Barabara ya Kolandoto - Lalago - Ng'oboko - Mwanhuzi (km 84)

343. Mheshimiwa Spika, jumla ya **Shilingi milioni 2,500.00** zimetengwa katika mwaka wa fedha 2020/21, kwa ajili ya maandalizi ya ujenzi kwa kiwango cha lami wa barabara za Kolandoto – Mwanhuzi (km 10) na Lalago – Ng'oboko – Mwanhuzi (km 74).

Barabara ya Ndundu – Somanga (km 60)

344. Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2020/21, jumla ya **Shilingi milioni 10.00** zimetengwa kwa ajili ya kulipa sehemu ya madai ya Mkandarasi wa ujenzi wa barabara hii.

Barabara ya Kasulu – Manyovu (km 68)

345. Mheshimiwa Spika, jumla ya **Shilingi milioni 11,000.09** zimetengwa katika mwaka wa fedha 2020/21 kwa ajili ya kuendelea na ujenzi wa barabara ya Kasulu – Manyovu pamoja na barabara za kuingia Kasulu mjini (km 68). Kati ya hizo **Shilingi milioni 2,570.00** ni fedha za ndani na **Shilingi milioni 8,430.09** ni fedha za nje.

Barabara ya Dodoma City Outer Dual Carriageway Ring Road Lot1 & 2 (km 112.3)

346. Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2020/21, jumla ya **Shilingi milioni 41,097.73** zimetengwa katika mradi huu. Kati ya fedha hizo, **Shilingi milioni 22,830.00** ni fedha za ndani na **Shilingi milioni 18,267.73** ni fedha za nje kwa ajili ya kuendelea na ujenzi wa barabara ya mzunguko ya Dodoma (Dodoma City Outer Dual Carriageway Ring Road) sehemu ya Nala – Veyula – Mtumba – Ihumwa Dry Port (km 52.3), sehemu ya Ihumwa Dry Port – Matumbulu – Nala (km 60.0) na kulipa fidia kwa ajili ya ujenzi na upanuzi wa barabara ya Makulu Jct. - Ntyuka R/About - Image R/About - Bahi R/About. Kazi nyingine ni kuanza ujenzi kwa kiwango cha lami wa barabara ya Ntyuka Jct. - Mvumi Hospital - Kikombo Junction (km 76.07) na barabara ya Kikombo Jct. - Chololo - Mapinduzi (JWTZ HQ) (km 18). Aidha, mradi huu utahusisha maandalizi ya upanuzi wa barabara kuu zinazolingia katikati ya mji wa Dodoma (km 200) zinazohusisha barabara ya Dodoma - Morogoro (km 50), Dodoma - Iringa (km 50), Dodoma - Singida (km 50) na Dodoma - Arusha (km 50).

Barabara ya Kidatu – Ifakara – Lupilo – Malinyi – Londo – Lumecha/Songea (km 464)

347. Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2020/21, mradi huu umetengewa jumla ya **Shilingi milioni 105.00** kwa ajili ya kuendelea na ujenzi wa sehemu ya Kidatu – Ifakara (km 68) na kuendelea na maandalizi ya ujenzi wa barabara ya Ifakara – Lupilo – Malinyi – Londo – Lumecha (km 396.0).

Barabara ya Tabora – Ipole – Koga – Mpanda (km 383.00)

348. Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2020/21, jumla ya **Shilingi milioni 33,518.44** zimetengwa kwa ajili ya mradi huu. Kati ya fedha hizo, **Shilingi milioni 2,080.00** ni fedha za ndani na fedha za nje **Shilingi milioni 31,438.44** zimetengwa kwa ajili ya kuendelea na ujenzi kwa kiwango cha lami wa sehemu za Usesula – Komanga (km 115.5), Komanga – Kasinde (km 112.8) na Kasinde – Mpanda (km 111.7).

Barabara ya Makutano – Natta – Mugumu/Loliondo – Mto wa Mbu (km 235)

349. Mheshimiwa Spika, mradi huu umetengewa jumla ya **Shilingi milioni 12,160.00** katika mwaka wa fedha 2020/21 kwa ajili ya kuendelea na ujenzi kwa kiwango cha lami kwa sehemu za Makutano – Sanzate (km 50.0) na Waso – Sale Jct. (km 50.0). Aidha, kazi nyingine ni kuanza ujenzi kwa sehemu za Sanzate – Natta (km 40.0), Natta – Mugumu (km 45.0) na Tarime – Mugumu (km 50) kwa kiwango cha lami.

Barabara ya Ibanda – Itungi Port (km 26)

350. Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2020/21, mradi huu umetengewa jumla ya **Shilingi milioni 13,395.20**. Kati ya fedha hizo, **Shilingi milioni 7,843.26** ni fedha za ndani na fedha za nje ni **Shilingi milioni 5,551.94** kwa ajili ya ukarabati wa sehemu ya Ibanda – Itungi Port (km 26) kwa kiwango cha lami na kuendelea na ujenzi wa Kituo cha Pamoja cha Ukaguzi mpakani Songwe/Kasumulu (Songwe/Kasumulu - Tanzania/Malawi Border - OSBP). Kazi nyingine ni kuanza ujenzi wa sehemu ya Iponjola - Kiwira Port (km 6).

Barabara ya Nzega – Tabora (km 289.7)

351. Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2020/21, mradi huu umetengewa jumla ya **Shilingi milioni 2,020.00** kwa ajili ya kuanza upembuzi yakinifu na usanifu wa kina kwa ajili ya ukarabati kwa kiwango cha lami wa barabara ya Shelui – Nzega (km 110.0) na kuanza ujenzi wa barabara za Nzega – Kagongwa (km 65.0).

Barabara ya Sumbawanga – Mpanda – Nyakanazi (km 432.56)

352. Mheshimiwa Spika, mradi huu umetengewa jumla ya **Shilingi milioni 14,320.00** katika mwaka wa fedha 2020/21, kwa ajili ya kukamilisha ujenzi wa barabara ya Mpanda – Ifukutwa – Vikonge (km 30) na kuanza ujenzi sehemu za Kibaoni – Sitalike (km 71.0) na Kizi – Lyambalyamfipa – Sitalike (km 86.3) kwa kiwango cha lami.

Barabara ya Nyanguge – Musoma/ Usagara – Kisesa Bypass (km 202.25)

353. Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2020/21 jumla

ya **Shilingi milioni 903.00** zimetengwa kwa ajili ya kuendelea na ujenzi wa barabara ya Musoma – Makojo – Busekela (km 92). Kazi nyingine ni kuanza maandalizi ya ukarabati wa sehemu ya Nyanguge – Simiyu/Mara Border (km 100.4) kwa kiwango cha lami.

Barabara ya Magole – Mziha – Handeni (km 149.2)

354. Mheshimiwa Spika, mradi huu umetengewa jumla ya **Shilingi milioni 6,280.00** katika mwaka wa fedha 2020/21 kwa ajili ya kuanza ujenzi wa kilometa 50 za barabara ya Turiani – Mziha – Handeni (km 104).

Ujenzi wa Barabara za Juu (Flyovers) Jijini Dsm na Barabara Unganishi

355. Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2020/21, mradi huu umetengewa jumla ya **Shilingi milioni 5,731.94**. Kati ya fedha hizo, **Shilingi milioni 180.00** ni fedha za ndani na **Shilingi milioni 5,551.94** ni fedha za nje kwa ajili ya kuendelea na ujenzi wa barabara za juu katika makutano ya Ubungo (Ubungo Interchange) pamoja na upembuzi yakinifu na usanifu wa kina kwa ajili ya kuboresha makutano ya barabara katika maeneo ya KAMATA, Magomeni, Mwenge, Tabata/Mandela, Morocco, Buguruni, Mbezi Mwisho, *Fire* pamoja na makutano ya barabara za Kinondoni/Ali Hassan Mwinyi na Selander (Ali Hassan Mwinyi/UN Road Jct). Aidha, kazi nyingine ni kuendelea na maandalizi ya ujenzi wa *Mabey Flyovers* katika jiji la Dar es Salaam, Dodoma na Mwanza.

Barabara ya Mwigumbi – Maswa – Bariadi – Lamadi (km 181.8)

356. Mheshimiwa Spika, mradi huu umetengewa jumla ya **Shilingi milioni 3,519.99** katika mwaka wa fedha 2020/21 kwa ajili ya kuendelea na ujenzi kwa kiwango cha lami sehemu ya Maswa – Bariadi (km 49.7). Aidha, Wizara imepanga kuanza maandalizi ya ujenzi kwa kiwango cha lami wa barabara ya Isabdula (Magu) – Kwimba Station – Ngudu – Ng'hungumalwa (km 10).

Barabara ya Tabora – Ipole – Rungwa (Sehemu ya Ipole – Rungwa (km 172)

357. Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2020/21, mradi huu umetengewa jumla ya **Shilingi milioni 1,150.00** kwa ajili ya

kuanza ujenzi kwa kiwango cha lami.

Barabara ya Kidahwe – Kasulu – Kibondo – Nyakanazi (km 341.25)

358. Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2020/21, mradi huu umetengewa jumla ya **Shilingi milioni 44,966.31**. Kati ya fedha hizo, **Shilingi milioni 21,250.00** ni fedha za ndani na fedha za nje ni **Shilingi milioni 23,716.31** kwa ajili ya kukamilisha ujenzi wa barabara ya Kidahwe – Kasulu (km 63) na kuendelea na ujenzi wa barabara za Nyakanazi – Kakonko (Kabingo) (km 50), Kanyani Junction – Mvugwe (km 70.5), Mvugwe – Nduta Junction (59.35), Nduta Junction – Kabingo (km 62.5) na Nduta Junction – Kibondo (km 25.9). Aidha, kazi nyingine ni kuanza ujenzi wa barabara ya Kibondo – Mabamba (km 35) kwa kiwango cha lami.

Barabara ya Kwenda Kiwanja cha Ndege cha Mafia (Mafia Airport Access Road (km 16)

359. Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2020/21, mradi huu umetengewa jumla ya **Shilingi milioni 10.00** kwa ajili ya kulipa sehemu ya madai ya Mkandarasi na Mhandisi Mshauri aliyesimamia ujenzi wa barabara hii.

Dodoma University Road (km 16.5)

360. Mheshimiwa Spika, mradi huu umetengewa jumla ya **Shilingi milioni 20.00** katika mwaka wa fedha 2020/21, kwa ajili ya kulipa madai ya Makandarasi na Wahandisi Washauri wa barabara za kutoka Ihumwa kuelekea Chuo Kikuu cha Dodoma (km 12.0) na Barabara za Ikulu ya Chamwino (km 4.5).

Daraja la Nyerere (Kigamboni) na Barabara Unganishi

361. Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2020/21, mradi huu umetengewa jumla ya **Shilingi milioni 2,800.00** kwa ajili ya kuendelea na ujenzi wa barabara unganishi za Kigamboni (Daraja la Nyerere) – Vijibweni (km 1.5). Kazi nyingine ni kuendelea na upembuzi yakinifu na usanifu wa kina wa barabara za Tungi – Kibada (km 3.8), Kibada – Mjimwema (km 1.6) na kuanza ujenzi wa barabara ya Kibada – Mwasonga – Tundwisongani Jct/Tundwisongani – Kimbiji (km 41.0) kwa kiwango cha lami.

Barabara ya Mutukula – Bukoba – Muhutwe – Kagoma (km 215.88)

362. *Mheshimiwa Spika*, katika mwaka wa fedha 2020/21, mradi huu umetengewa jumla ya **Shilingi milioni 1,090.00** kwa ajili ya kuanza upembuzi yakinifu na usanifu wa kina wa barabara za Mutukula – Bukoba – Muhutwe – Kagoma (km 136.0), Bukoba Mjini – Busimbe – Maluku – Kanyangereko – Ngongo na Kanazi (Kyetema) – Ibwera – Katoro – Kyaka II (km 60.7).

Fedha za Matengenezo na Ukarabati wa Barabara

363. *Mheshimiwa Spika*, mradi huu umetengewa jumla ya **Shilingi milioni 641,746.37** katika mwaka wa fedha 2020/21 kwa ajili ya matengenezo na ukarabati wa barabara, upembuzi yakinifu na usanifu wa kina, udhibiti wa uzito wa magari, usalama barabarani na mazingira, matengenezo na ukarabati wa vivuko pamoja na kujenga uwezo wa Wizara na Taasisi zinazosimamia masuala ya barabara na vivuko. Fedha hizi zinasimamiwa na Bodi ya Mfuko wa Barabara.

Ujenzi wa Njia za Magari Mazito na Maegesho ya Dharura Katika Barabara Kuu ya Ukanda wa Kati (Providing Lane Enhancement Including Climbing Lanes, Passing Bays, Rest and Emergency Lay Bays on Central Corridor)

364. *Mheshimiwa Spika*, katika mwaka wa fedha 2020/21, mradi huu umetengewa jumla ya **Shilingi milioni 150.00** kwa ajili ya kuwezesha (facilitate) kazi za usanifu wa kina wa maeneo ya kujenga njia za magari mazito kwenye miinuko na kujenga maegesho ya dharura katika barabara kuu ya Ukanda wa Kati.

Upanuzi wa Barabara ya Kimara – Kibaha (km 25.7) Ikijumuisha Upanuzi wa Madaraja ya Kibamba, Kiluvya na Mpiji

365. *Mheshimiwa Spika*, katika mwaka wa fedha 2020/21, mradi huu umetengewa jumla ya **Shilingi milioni 9,000.00** kwa ajili ya kuendelea na upanuzi wa barabara ya Kimara – Kibaha (km 25.7); sehemu ya Kimara – Kibaha Mizani (km 19.2) na madaraja ya Kibamba, Kiluvya na Mpiji kwa utaratibu wa kusanifu na kujenga (*Design and Build*).

Barabara ya Kisarawe – Mlandizi (km 119.0)

366. *Mheshimiwa Spika*, mradi huu umetengewa jumla ya

Shilingi milioni 630.00 katika mwaka wa fedha wa 2020/21 kwa ajili ya maandalizi ya ujenzi wa barabara hii kwa kiwango cha lami.

Barabara ya Pugu – Kifuru – Mbezi Mwisho – Mpiji Magoe – Bunju (km 34.0)

367. Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2020/21, jumla ya **Shilingi milioni 20.00** zimetengwa kwa ajili ya maandalizi ya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina wa sehemu za Pugu – Kifuru – Mbezi Mwisho (km 12.7) na Mbezi Mwisho – Mpiji Magoe – Bunju (km 21.3).

Barabara ya Kagoma – Lusahunga (km 172.50)

368. Mheshimiwa Spika, kiasi cha **Shilingi milioni 1,180.00** zimetengwa katika mwaka wa fedha 2020/21 kwa ajili ya kuendelea na ujenzi wa sehemu za Muleba – Kanyambogo – Rubya (km 18.5) kwa kiwango cha lami.

Barabara ya Singida – Shelui (km 110)

369. Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2020/21, kiasi cha **Shilingi milioni 1,000.00** zimetengwa kwa ajili ya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina ikiwa ni maandalizi ya kuanza ukarabati wa barabara hii.

Barabara ya Dar es Salaam – Mbagala (Kilwa Road) – Gerezani (Sehemu ya Kamata – Bendera Tatu: km 1.3)

370. Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2020/21, zimetengwa jumla ya **Shilingi milioni 8,837.91** kwa ajili ya mradi huu. Kati ya fedha hizo, **Shilingi milioni 510.00** ni fedha za ndani na **Shilingi milioni 8,327.91** ni fedha za nje. Kiasi kilichotengwa ni kwa ajili ya kuendelea na ujenzi wa Daraja la Gerezani na maandalizi ya upanuzi wa barabara ya Mbagala Rangi Tatu – Kongowe (km 3.8).

Barabara ya Msimba – Ruaha Mbuyuni/Ikokoto Mafinga (km 535.25)

371. Mheshimiwa Spika, jumla ya **Shilingi milioni 8,960.00** zimetengwa katika mwaka wa fedha 2020/21 kwa ajili ya kukamilisha ujenzi wa barabara ya Mbarali – Ubaruku (km 8.9) kwa kiwango cha lami na kuanza ujenzi wa barabara za Rujewa – Madibira – Mafinga (km

152.0). Aidha, mradi huu utahusisha kuendelea na upembuzi yakinifu na usanifu wa kina wa barabara ya Mafinga – Mgololo (km 78.0) na kufanya ukarabati wa barabara ya Morogoro – Iringa sehemu ya Tumbaku Jct. - Mangae/Melela - Mikumi – Iyovi (km 156.45).

Barabara ya Same – Mkumbara – Korogwe (km 147.5)

372. Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2020/21, jumla ya **Shilingi milioni 6,060.00** zimetengwa kwa ajili ya kuanza maandalizi ya ukarabati wa sehemu za Same – Himo (km 76.0) na Mombo – Lushoto (km 32.0) kwa kiwango cha lami. Aidha, kazi nyingine ni kuendelea na maandalizi ya ujenzi wa barabara za Lushoto – Magamba – Mlola (km 34.5) na Same - Kisiwani - Mkomazi (km 97) sehemu ya Same – Kisiwani (km 5.0) kwa kiwango cha lami.

Barabara ya Mbeya – Makongolosi (km 267.90)

373. Mheshimiwa Spika, jumla ya **Shilingi milioni 11,060.00** zimetengwa katika mwaka wa fedha 2020/21 kwa ajili ya kuendelea na ujenzi wa sehemu ya Chunya – Makongolosi (km 39) na maandalizi ya ujenzi wa sehemu za Mkiwa - Itigi - Noranga (km 56.9), Mbalizi – Makongolosi (km 50) na Makongolosi – Rungwa – Noranga (sehemu ya Makongolosi – Rungwa (km 50) kwa kiwango cha lami.

Barabara ya Itoni – Ludewa – Manda (km 211)

374. Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2020/21, jumla ya **Shilingi milioni 12,000.00** zimetengwa kwa ajili ya kuendelea na ujenzi wa barabara kwa kiwango cha zege kwa sehemu ya Lusitu – Mawengi (km 50) na kuanza ujenzi kwa kiwango cha lami kwa sehemu ya Itoni – Lusitu (km 50).

Ujenzi wa Daraja Jipya la Selander

375. Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2020/21, jumla ya **Shilingi milioni 48,161.93** fedha za nje zimetengwa kwa ajili ya kuendelea na ujenzi wa Daraja Jipya la Selander (km 1.030) na barabara unganishi zenye jumla ya urefu wa kilometa 5.2.

Barabara ya Handeni – Kibirashi – Kijungu – Kibaya – Njoro – Olboloti – Mrijo Chini – Dalai – Bicha – Chambalo – Chemba – Kwa Mtoro – Singida (km 460)

376. Mheshimiwa Spika, jumla ya **Shilingi milioni 6,000.00** zimetengwa katika mwaka wa fedha 2020/21 kwa ajili ya kuanza ujenzi wa barabara hii kwa kuanzia na sehemu ya Handeni – Kibirashi (km 50.0) kwa kiwango cha lami.

Barabara ya Makambako – Songea Na Barabara Ya Mchepuo Ya Songea (Songea Bypass) (km 295)

377. Mheshimiwa Spika, katika bajeti ya mwaka wa fedha 2020/21, jumla ya **Shilingi milioni 20.00** zimetengwa kwa ajili ya kuendelea na usanifu wa kina wa barabara ya Mchepuo ya Songea na maandalizi ya ukarabati wa barabara ya Makambako – Songea.

Barabara ya Dodoma – Iringa (km 267.1)

378. Mheshimiwa Spika, jumla ya **Shilingi milioni 3,020.00** zimetengwa katika bajeti ya mwaka wa fedha 2019/20 kwa ajili ya kuendelea na ujenzi kwa kiwango cha lami barabara ya mchepuo ya Iringa (km 7.3) na kuimarisha matabaka ya barabara ya Iringa – Dodoma.

Barabara ya Dodoma – Babati (km 263.4)

379. Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2020/21, jumla ya **Shilingi milioni 60.00** zimetengwa kwa ajili ya kuendelea na upembuzi yakinifu na usanifu wa kina kwa ajili ya ujenzi wa barabara ya mchepuo wa Babati (Babati Bypass km 12).

Barabara ya Masasi – Songea – Mbamba Bay (km 343.20)

380. Mheshimiwa Spika, katika bajeti ya mwaka wa fedha 2020/21 mradi huu umetengewa jumla ya **Shilingi milioni 22,921.82**. Kati ya fedha hizo, **Shilingi 15,030.00** ni fedha za ndani na **Shilingi milioni 7,891.82** ni fedha za nje kwa ajili ya kuendelea na ujenzi wa barabara za Mbinga – Mbamba Bay (km 66), kilometa tano (5) za barabara ya Kitai – Lituhi (km 90.0) pamoja na daraja la Mnywamaji.

Ujenzi wa Barabara za Chuo cha Uongozi (Uongozi Institute)

381. Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha wa 2020/21, jumla ya **Shilingi milioni 20.00** zimetengwa kwa ajili ya kuendelea na maandalizi ya ujenzi wa barabara ndani ya eneo la Chuo cha Uongozi Bagamoyo kwa kiwango cha lami.

Barabara ya Igawa – Songwe – Tunduma na Mbeya Bypass (km 273.40)

382. Mheshimiwa Spika, jumla ya **Shilingi milioni 60.00** zimetengwa katika mwaka wa fedha 2019/20 kwa ajili ya kuendelea na upembuzi yakinifu na usanifu wa kina wa barabara za Igawa – Songwe – Tunduma (km 218), barabara ya mchepuo ya Mbeya (Uyole – Songwe km 48.9) na barabara ya Iwambi – Mbalizi (km 6.5) kwa ajili ya ujenzi na ukarabati kwa kiwango cha lami.

Miundombinu ya Mabasi Yaendayo Haraka (BRT Phase I – V: km 69.8)

383. Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2020/21, jumla ya **Shilingi milioni 51,749.43** zimetengwa kwa ajili ya mradi huu. Kati ya fedha hizo, **Shilingi milioni 7,870.00** ni fedha za ndani na **Shilingi milioni 43,879.43** ni fedha za nje kwa ajili ya kuendelea na ujenzi wa miundombinu ya Mabasi Yaendayo Haraka Awamu ya Pili. Aidha, kazi nyingine ni kuanza ujenzi wa Miundombinu ya Mabasi Yaendayo Haraka Awamu ya Tatu na Nne na kufanya maandalizi ya maboresho ya miundombinu ya mabasi yaendayo haraka iliyojengwa katika Awamu ya Kwanza katika eneo la Jangwani. Mradi huu utahusisha pia kufanya mapitio ya usanifu wa mradi wa ujenzi wa Miundombinu ya Mabasi Yaendayo Haraka Awamu ya Tano.

Ujenzi wa Jengo la Makao Makuu ya Taasisi ya Teknolojia ya Ujenzi (Institute Of Construction Technology - ICoT)

384. Mheshimiwa Spika, jumla ya **Shilingi milioni 1,000.00** zimetengwa katika mwaka wa fedha wa 2020/21 kwa ajili ya usanifu na ujenzi (Design and Build) wa jengo la Makao Makuu ya Taasisi ya Teknolojia ya Ujenzi (ICoT).

Ujenzi wa Makao Makuu ya Wakala wa Barabara Tanzania

385. Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2020/21, jumla

ya **Shilingi milioni 15,020.00** zimetengwa kwa ajili ya kuendelea na ujenzi wa jengo la Makao Makuu ya Wakala wa Barabara Tanzania (TANROADS) pamoja na Ofisi za Mikoa ya Dar es Salaam, Katavi, Geita, Simiyu, Njombe, Lindi na Songwe.

MIRADI YA USALAMA BARABARANI NA MAZINGIRA

386. Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2020/21, Wizara itaendelea kutekeleza majukumu yanayohusu kuratibu na kuimarisha shughuli za usalama barabarani, mazingira na kudhibiti uzito wa magari yanayotumia barabara zetu. Mradi wa **Usalama Barabarani** umetengewa jumla ya **Shilingi milioni 1,832.00** kwa ajili ya ujenzi wa Vituo vya Pamoja vya Ukaguzi, uwekaji wa miundombinu ya kisasa ya upimaji magari (Load Cell), kufanya maboresho katika mfumo wa ukusanyaji wa taarifa za ajali barabarani, ukaguzi wa alama na usalama wa barabara pamoja na mapitio ya Sera ya Usalama Barabarani. Kazi nyingine ni kutoa elimu ya usalama barabarani kwa umma, pamoja na uendeshaji wa Mfumo wa Upatikanaji na Utoaji Taarifa za Ajali Barabarani.

387. Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2020/21, mradi wa **Menejimenti ya Utunzaji wa Mazingira** umetengewa **Shilingi milioni 148.00** kwa ajili ya kutoa mafunzo kuhusu Tathmini ya Athari kwa Mazingira (TAM) na hifadhi ya mazingira katika Sekta ya Ujenzi. Kazi nyingine ni kuandaa mfumo wa kusimamia mazingira (Environmental Management System) na kutoa elimu ya weledi wa usimamizi wa mazingira hususan utekelezaji wa Sheria ya Mazingira Na. 20 ya mwaka 2004 kwa menejimenti ya Wizara. Aidha, fedha hizi zitatumika kuandaa programu za udhibiti wa uchafuzi wa mazingira katika sekta (Sectoral Pollution Control Programme).

MIRADI YA UJENZI WA MIUNDOMBINU YA VIWANJA VYA NDEGE

388. Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2020/21 miradi ya ujenzi wa miundombinu ya viwanja vya ndege imetengewa kiasi cha **Shilingi milioni 91,885.299**. Kati ya fedha hizo, **Shilingi milioni 60,737.98** ni za ndani na **Shilingi milioni 31,147.32** ni fedha za nje. Miradi ifuatayo itatekelezwa:

Ujenzi wa Kiwanja cha Ndege cha Kigoma

389. Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2020/21, mradi

huu umetengewa jumla ya **Shilingi milioni 7,757.18**. Kati ya fedha hizo, **Shilingi milioni 5,000.00** ni fedha za ndani na **Shilingi milioni 2,757.18** ni fedha za nje. Fedha hizi zimetengwa kwa ajili ya ujenzi wa Jengo la Abiria, maegesho ya ndege, maegesho ya magari na barabara ya kuingia na kutoka kiwanjani, usimikaji wa taa na mitambo ya kuongozea ndege, ujenzi wa uzio, jengo la kuongozea ndege na jengo la uchunguzi wa hali ya hewa.

Ujenzi wa Kiwanja cha Ndege cha Mpanda

390. Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2020/21, mradi huu umetengewa jumla ya **Shilingi milioni 10.00** fedha za ndani kwa ajili ya ukarabati wa uzio wa usalama, ujenzi wa barabara ya kuzunguka uzio na upanuzi wa jengo la abiria.

Ujenzi wa Kiwanja cha Ndege cha Tabora

391. Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2020/21 mradi huu umetengewa jumla ya **Shilingi milioni 2,891.18**. Kati ya fedha hizo, **Shilingi milioni 134.00** ni fedha za ndani na **Shilingi milioni 2,757.18** ni fedha za nje kwa ajili ya ujenzi wa Jengo la Abiria, jengo la kuongozea ndege, barabara ya kuingia na kutoka kiwanjani, maegesho ya magari, uzio wa usalama pamoja na jengo la uchunguzi wa hali ya hewa.

Ujenzi wa Kiwanja cha Ndege cha Songwe

392. Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2020/21 mradi huu umetengewa jumla ya **Shilingi milioni 8,900.00** kwa ajili ya kumaliza ujenzi wa Jengo la Abiria, usimikaji wa taa za kuongozea ndege na ukarabati wa tabaka la juu la barabara ya kutua na kuruka ndege na barabara ya kiungio (taxiway), ujenzi wa uzio wa usalama pamoja na ukarabati wa eneo la usalama kwenye barabara ya kutua na kuruka ndege (Runway End Safety Area-RESA).

Ukarabati wa Kiwanja cha Ndege cha Mwanza

393. Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2020/21, mradi huu umetengewa jumla ya **Shilingi milioni 3,023.40** fedha za ndani kwa ajili ya ujenzi wa Jengo jipya la Abiria, ujenzi wa uzio wa usalama pamoja na malipo ya Mkandarasi na Mshauri Elekezi wakati wa kipindi cha uangalizi wa mradi (Defect Notification Period).

Ukarabati wa Kiwanja cha Ndege cha Arusha

394. Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2020/21, mradi huu umetengewa jumla ya **Shilingi milioni 200.00** kwa ajili ya kurefusha barabara ya kuruka na kutua ndege; ujenzi wa maeneo ya kugeuzia ndege (Turning Pad), uzio wa usalama, barabara mpya ya kuingilia kiwanjani pamoja na kukarabati maegesho ya magari.

Ukarabati wa Kiwanja cha Ndege cha Mtwara

395. Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2020/21, mradi huu umetengewa kiasi cha **Shilingi milioni 5,355.00** kwa ajili ya ukarabati wa barabara ya kuruka na kutua ndege, viungio vyake pamoja na maegesho ya ndege. Kazi zingine ni kusimika taa na mitambo ya kuongozea ndege, ujenzi wa barabara ya kuingia kiwanjani, maegesho ya magari na uzio wa usalama.

Ujenzi wa Kiwanja cha Ndege cha Sumbawanga

396. Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2020/21, mradi huu umetengewa jumla ya **Shilingi milioni 2,867.18**. Kati ya fedha hizo, **Shilingi milioni 110.00** ni fedha za ndani na **Shilingi milioni 2,757.18** ni fedha za nje kwa ajili ya ujenzi wa barabara ya kutua na kuruka ndege na viungio vyake, maegesho ya ndege, jengo la abiria, jengo la kuongozea ndege, jengo la uchunguzi wa hali ya hewa, uzio wa usalama, barabara ya kuingia kiwanjani na maegesho ya magari. Kazi nyingine ni usimikaji wa taa na mitambo ya kuongozea ndege.

Ujenzi wa Kiwanja cha Ndege cha Shinyanga

397. Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2020/21, mradi huu umetengewa jumla ya **Shilingi milioni 2,867.18**. Kati ya fedha hizo, **Shilingi milioni 110** ni fedha za ndani na **Shilingi milioni 2,757.18** ni fedha za nje. Fedha hizo zitatumika kwa ajili ya ujenzi wa barabara ya kutua na kuruka ndege na viungio vyake, maegesho ya ndege, jengo la abiria, jengo la kuongozea ndege, jengo la uchunguzi wa hali ya hewa, barabara ya kuingia kiwanjani, maegesho ya magari na usimikaji wa taa na mitambo ya kuongozea ndege pamoja na ujenzi wa uzio wa usalama.

Uendelezaji wa Viwanja vya Ndege vya Mikoa

398. *Mheshimiwa Spika*, katika mwaka wa fedha 2020/21, mradi huu umetengewa jumla ya **Shilingi milioni 18,237.98**. Kati ya fedha hizo, **Shilingi milioni 17,787.98** ni fedha za ndani na **Shilingi milioni 450.00** ni fedha za nje kwa ajili ya ujenzi wa viwanja vya ndege vya Geita, Songea, Iringa, Musoma, Tanga, Lake Manyara, Moshi, Lindi na kiwanja kipya cha Simiyu. Aidha, kazi nyingine ni ujenzi wa uzio wa usalama pamoja na barabara ya kufanyia ukaguzi kwenye kiwanja cha ndege cha Dodoma.

Ujenzi wa Kiwanja cha Ndege cha Msalato

399. *Mheshimiwa Spika*, katika mwaka wa fedha 2020/21, mradi huu umetengewa jumla ya **Shilingi milioni 39,714.20**. Kati ya fedha hizo, **Shilingi milioni 20,045.60** ni fedha za ndani na **Shilingi milioni 19,668.60** ni fedha za nje kwa ajili ya kuanza ujenzi wa kiwanja kipya cha Msalato mkoani Dodoma. Aidha, kazi nyingine ni kulipa fidia kwa wakazi watakaoathiriwa na utekelezaji wa mradi huu.

Ujenzi wa Kiwanja cha Ndege cha Bukoba

400. *Mheshimiwa Spika*, katika mwaka wa fedha 2020/21, mradi huu umetengewa kiasi cha **Shilingi milioni 10.00** fedha za ndani kwa ajili ya maandalizi ya ujenzi wa jengo la watu mashuhuri (VIP Lounge), ukarabati wa meta 200 barabara ya kuruka na kutua ndege pamoja na usimikaji wa taa za kuongozea ndege.

Ujenzi wa Jengo la Tatu la Abiria Katika Kiwanja cha Ndege cha Kimataifa cha Julius Nyerere (JNIA)

401. *Mheshimiwa Spika*, katika mwaka wa fedha 2020/21, mradi huu umetengewa jumla ya **Shilingi milioni 52.00** kwa ajili ya kulipa madai ya Mkandarasi na Mshauri Elekezi wa Jengo la Tatu la Abiria (Terminal III) pamoja na miundombinu yake. Aidha, kazi nyingine ni maandalizi ya Usanifu wa Kina kwa ajili ya ukarabati wa Jengo la Pili la Abiria (Terminal II).

FEDHA ZA MFUKO WA BARABARA

402. *Mheshimiwa Spika*, katika mwaka wa fedha 2020/21 jumla ya **Shilingi 641,746,370,000.00** zimetengwa kwa ajili ya kufanya kazi za matengenezo na ukarabati wa barabara kuu na za mikoa. Kati ya fedha hizo, TANROADS imetengewa **Shilingi 572,604,616,096.20** kwa ajili ya matengenezo ya barabara na Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano (Ujenzi) imetengewa **Shilingi 63,622,735,121.80** kwa ajili ya kazi za ukarabati wa barabara za mikoa, upembuzi yakinifu na usanifu wa kina wa barabara, ukarabati na ununuzi wa vivuko, usalama barabarani pamoja na usimamizi na ufuatiliaji wa miradi hiyo. Aidha, **Shilingi 5,519,081,782.00** zitatumika kugharamia uendeshaji wa Bodi ya Mfuko wa Barabara.

403. *Mheshimiwa Spika*, kiasi cha **Shilingi 63,622,735,121.80** ni fedha za maendeleo kutoka Mfuko wa Barabara zilizotengwa kwa ajili ya Wizara (Ujenzi). Kati ya hizo, **Shilingi 14,672,483,000.00** ni kwa ajili ya kufanya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina wa barabara zenye urefu wa kilometa **7,032.9**. Kiasi cha **Shilingi 4,740,226,000.00** ni kwa ajili ya manunuzi na ukarabati wa vivuko pamoja na ujenzi wa maegesho ya vivuko; **Shilingi 6,291,577,575.80** ni kwa ajili ya miradi ya Usalama Barabarani na Mazingira na **Shilingi 6,908,984,546.00** ni kwa ajili ya kazi za usimamizi na ufuatiliaji wa miradi inayotekelezwa na Wizara (Ujenzi) pamoja na kujenga uwezo wa watumishi. Aidha, miradi ya barabara za mikoa imetengewa **Shilingi 31,009,464,000.00** kwa ajili ya kufanya ukarabati wa jumla ya kilometa **416.02** kwa kiwango cha changarawe na kujenga kilometa **23.41** kwa kiwango cha lami pamoja na ujenzi na ukarabati wa madaraja/makalavati **27** katika mikoa mbalimbali nchini.

Mchanganuo wa miradi itakayotekelezwa kwa fedha za Mfuko wa Barabara zilizotengwa kwa ajili ya Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano (Sekta ya Ujenzi) umeonyeshwa katika **Viambatisho Na. 3 na 4**.

404. *Mheshimiwa Spika*, jumla ya **Shilingi 572,604,616,096.20** ni fedha za Mfuko wa Barabara ambazo zimetengwa kwa ajili ya Wakala wa Barabara Tanzania (TANROADS). Fedha hizo zitatumika kufanya matengenezo ya barabara kuu, barabara za mikoa, madaraja na uendeshaji wa mizani.

Mchanganuo wa matumizi ya fedha hizo umeoneshwa katika **Viambatisho Na. 5, 5A - 5D.**

MPANGO WA KAZI WA TAASISI ZILIZO CHINI YA SEKTA YA UJENZI KWA MWAKA WA FEDHA 2020/21

Wakala wa Barabara Tanzania

405. Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2020/21, Wakala wa Barabara Tanzania umepanga kujenga barabara zenye urefu wa **kilometa 455.75** kwa kiwango cha lami, ujenzi wa madaraja **11** pamoja na ukarabati wa **kilometa 25** kwa kiwango cha lami katika barabara kuu. Aidha, Wakala umepanga kufanya matengenezo ya barabara kuu na barabara za mikoa ambayo yatahusisha matengenezo ya kawaida (routine and recurrent maintenance) kwa **kilometa 34,268.29**, matengenezo ya muda maalum **kilometa 4,886.67** na sehemu korofi **kilometa 743.49** pamoja na matengenezo ya madaraja **3,390**. Mpango huu pia unajumuisha shughuli za udhibiti wa uzito wa magari na hifadhi za barabara, kazi za dharura pamoja na mradi wa matengenezo ya barabara kwa mikataba ya muda mrefu.

Kwa upande wa barabara za mikoa, Wakala utajenga kwa kiwango cha lami barabara zenye urefu wa **kilometa 64.72** ambapo **kilometa 41.31** zitajengwa kwa kutumia fedha za Mfuko Mkuu wa Serikali na **kilometa 23.41** zitajengwa kwa fedha za Mfuko wa Barabara. Aidha, **kilometa 1,005.33** zitakarabatiwa kwa kiwango cha changarawe. Kati ya hizo, **kilometa 589.31** na madaraja/makalavati **24** yatakarabatiwa kwa kutumia fedha za Mfuko Mkuu wa Serikali na **kilometa 416.2** pamoja na madaraja **27** yatajengwa/yatakarabatiwa kwa kutumia fedha za Mfuko wa Barabara.

406. Mheshimiwa Spika, Wakala vilevile utaendelea na jukumu la kusimamia miradi ya ujenzi na ukarabati wa Viwanja vya Ndege. Kazi zitakazotekelezwa ni pamoja na kuendelea na ujenzi wa kiwanja kipya cha Ndege cha Geita pamoja na ukarabati na upanuzi wa viwanja vya Ndege vya Songea, Mtwara na Songwe. Kazi nyingine ni kuanza ujenzi wa Kiwanja kipya cha Ndege cha Kimataifa cha Msalato, ukarabati na upanuzi wa Viwanja vya Ndege vya Kigoma, Shinyanga, Tabora, Sumbawanga, Iringa, Musoma, Tanga na Lake Manyara ambavyo vipo katika hatua mbalimbali za manunuzi. Aidha, Wakala utaendelea na maandalizi ya ukarabati wa Jengo la Pili la Abiria (Terminal Building II) katika kiwanja cha Ndege cha Kimataifa cha Julius Nyerere (JNIA) pamoja na ukarabati wa viwanja vya Ndege vya Lindi, Arusha, Bukoba,

Moshi, Nachingwea, Dodoma na viwanja vingine mikoani.

Wakala wa Majengo Tanzania

407. Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2020/21 Wakala wa Majengo Tanzania umepanga kuendelea kusimamia miradi ya nyumba za viongozi ambazo utekelezaji wake upo katika hatua mbalimbali ikiwemo ujenzi wa nyumba za Waheshimiwa Majaji katika mikoa mbalimbali na Ujenzi wa nyumba ya makazi Ikulu Dodoma. Aidha, Wakala utaendelea kufanya matengenezo ya nyumba na ununuzi wa samani kwa nyumba za Viongozi. Aidha, Wakala utaendelea na ujenzi, ukarabati na ununuzi wa samani katika nyumba za viongozi. Vilevile, Wakala utatekeza miradi ya Ukarabati wa nyumba DSM na Mikoani; Umaliziaji wa Jengo la kibiashara simioni Arusha; Ujenzi wa nyumba 172 za watumishi wa umma Jijini Dodoma na mikoa mingine; Ukamilishaji wa Ukumbi wa matumizi Mbalimbal-Area II Dar es Salaam; Ujenzi wa jengo la kibiashara Kyela Mbeya - EX TACOSHILI; Upatikanaji wa hati miliki za viwanja vya TBA; Ujenzi wa Ofisi ya Mkoa -Geita; na Ununuzi wa Samani katika jengo la Chimala.

Wakala wa Ufundi na Umeme

408. Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2020/21, Wakala wa Ufundi na Umeme umepanga kuendelea na usimamizi na uendeshaji wa Vivuko vya Serikali vipatavyo **32** na boti **11** ambavyo vinatarajiwa kuvusha abiria **40,174,764**, magari **1,684,524** na tani za mizigo **428,172**.

409. Mheshimiwa Spika, katika miradi ya **maegesho ya vivuko**, Wakala umepanga kuendelea na upanuzi wa jengo la abiria na maegesho upande wa Kigamboni kwa ajili ya kivuko cha Magogoni – Kigamboni; ujenzi wa maegesho ya Bukondo na Zumacheli kwa ajili ya kivuko cha Chato – Nkome; ujenzi wa maegesho ya Nyamisati – Mafia kwa ajili ya kivuko cha Nyamisati – Mafia; ujenzi na ukarabati wa maegesho katika vituo 8 vya Bugolora – Ukara, Rugezi – Kisorya, Kilambo – Namoto, Utete – Mkongo, Iramba – Majita, Nyakarilo – Kome, Kasharu – Buganguzi na Kigongo – Busisi. Kazi nyingine ni ujenzi wa miundombinu (majengo ya abiria, ofisi na uzio) kwa vituo kumi (Bugolora, Ukara, Kome, Nyakaliro, Maisome, Kaunda, Nkome, Kisorya, Musoma na Kinesi) pamoja na ujenzi wa maegesho ya vivuko vya Ngara – Nyakiziba na Muleba – Ikuza. Aidha, Wakala utaendelea na

ujenzi wa miundombinu (jengo la kukatia tiketi, jengo la abiria na ofisi) kwa ajili ya kivuko kipyaa cha Kayenze - Bezi mkoani Mwanza na kivuko cha Itungi Port (Mwaya - Kajunjumele) mkoani Mbeya.

410. Mheshimiwa Spika, kwa upande wa **ununuzi wa vivuko,** miradi itakayotekelezwa na Wakala ni pamoja na kukamilisha ujenzi wa vivuko vipya vitakavyotoa huduma ya usafiri kati ya Nyamisati – Mafia, Bugolora – Ukara na Chato – Nkome; ujenzi wa boti ‘*fibber boat*’ itakayotoa huduma ya usafiri kati ya Utete - Mkongo; ununuzi wa vitendea kazi kwa ajili ya karakana pamoja na vivuko. Kazi nyingine ni ununuzi wa kivuko kipyaa kitakachotoa huduma ya usafiri kati ya Kisorya – Rugezi, kufanya usanifu na kusimika Mfumo wa Usimamizi na Uendeshaji wa Vivuko vya Serikali.

411. Mheshimiwa Spika, kwa upande wa **ukarabati,** Wakala umepanga kukamilisha ukarabati wa vivuko MV Tegemeo, MV Musoma, MV Mara, MV Sengerema, MV Ujenzi, MV Kigamboni, MV Misungwi na boti ya uokozi MV KIU. Aidha, Wakala unatarajia kuanza ukarabati wa vivuko MV Nyerere, MV Kilombero I, MV Kilombero II, MV Ruhuhu na MV Tanga pamoja na ukarabati wa mitambo ya karakana ya TEMESA Morogoro na mitambo ya Chuo cha Ujenzi Morogoro.

412. Mheshimiwa Spika, Wakala pia umepanga kujenga karakana 5 kwa ajili ya matengenezo ya magari na mitambo ya Serikali katika mikoa ya Songwe, Simiyu, Geita, Njombe na Katavi; kujenga karakana ya kisasa Jijini Dodoma na ununuzi wa karakana sita zinazohamishika (mobile workshops) pamoja na vitendea kazi vyake. Kazi nyingine ni kukarabati karakana 11 ambazo ni karakana ya MT Depot Dar es Salaam, Mtwara, Mbeya, Tabora, Mwanza, Arusha, Kigoma, Mara, Ruvuma, Pwani na Vingunguti (Dar es Salaam); kuanzisha karakana 6 za ngazi ya wilaya (Simanjiro, Same, Chato, Masasi, Kyela na Ukerewe) pamoja na kusanifu na kusimika Mfumo wa Usimamizi wa Matengenezo ya Magari.

413. Mheshimiwa Spika, Wakala vilevile umepanga kufanya matengenezo ya magari **45,681**, matengenezo na usimikaji wa mifumo **394** ya umeme, mifumo **1,395** ya majokofu na viyoyozi pamoja na mifumo **166** ya elektroniki. Vilevile, Wakala umepanga kutoa ushauri wa kihandisi kwa miradi ya usimikaji wa mifumo ya umeme, mitambo, elektroniki, viyoyozi na majokofu inayofikia **118** na kusimamia mifumo hiyo ipatayo **62**. Aidha, Wakala utaendelea kutoa huduma ya

ukodishaji wa Mitambo ya Ujenzi wa Barabara.

Bodi ya Mfuko wa Barabara

414. Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2020/21, Mfuko wa Barabara unatarajia kukusanya jumla ya **Shilingi 916,780,529,000** kutoka katika vyanzo mbalimbali ikiwemo tozo ya mafuta, tozo kwa magari ya kigeni yanayosafirisha mizigo nje ya nchi pamoja na faini za uzidishaji mizigo barabarani na mizigo yenye vipimo visivyo vya kawaida. Kati ya fedha hizo, **Shilingi 641,746,370,000** zitagawanywa kwa ajili ya matengenezo ya barabara kuu na za mikoa, ukarabati wa barabara za mikoa, upembuzi yakinifu na usanifu wa kina, udhibiti wa uzito wa magari, usalama barabarani na mazingira, matengenezo na ukarabati wa vivuko pamoja na kujenga uwezo wa Wizara na Taasisi zinazosimamia masuala ya Barabara na Vivuko chini ya Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano (Fungu 98 -Ujenzi). Aidha, **Shilingi 275,034,159,000** zimetengwa kwa ajili ya matengenezo ya barabara za Wilaya zilizo chini ya Ofisi ya Rais –TAMISEMI (Fungu 56).

415. Mheshimiwa Spika, mchanganuo wa bajeti ya Mfuko wa Barabara kwa mwaka wa fedha 2020/21 ni kama ifuatavyo: Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano (Ujenzi) **Shilingi 63,622,735,121.80**, Wakala wa Barabara Tanzania **Shilingi 572,604,616,096.20**, Ofisi ya Rais, TAMISEMI **Shilingi 27,266,886,523.26** TARURA **Shilingi 245,401,978,709.34** na Bodi ya Mfuko wa Barabara **Shilingi 7,884,312,549.40**.

416. Mheshimiwa Spika, ili kuandaa mkakati endelevu wa matengenezo ya barabara nchini, Bodi kwa ufadhili wa Benki ya Dunia inatarajia kukamilisha tathmini ya mtandao wa barabara (*Road inventory and condition survey*) ili kubaini thamani, urefu na hali ya barabara nchini. Takwimu hizi zitasaidia kuandaa mkakati endelevu wa matengenezo ya barabara nchini. Vilevile, Bodi itagharimia utafiti wa teknolojia mbadala na rahisi katika matengenezo ya barabara ili kupata teknolojia nafuu ya matengenezo ya barabara itakayopunguza gharama na kuongeza ufanisi katika matumizi ya fedha za Mfuko. Aidha, Bodi itaendelea na ufuatiliaji wa ubora wa kazi za matengenezo ya barabara katika mikoa yote nchini pamoja na kuendelea kuishauri Serikali juu ya namna ya kuongeza mapato ya Mfuko kulingana na wakati muafaka.

Bodi ya Usajili wa Wahandisi

417. Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2020/21 Bodi imepanga kusajili wahandisi **2,300**, mafundi sanifu **210** na kampuni za ushauri wa kihandisi **20**. Bodi pia imepanga kusimamia utekelezaji wa mpango wa mafunzo kwa vitendo kwa wahandisi wahitimu **3,500**. Kati ya hao **2,796** ni wanaoendelea na mafunzo na **704** ni wapya wanaofadhiliwa na Serikali, Wafadhili na sekta binafsi. Aidha, Bodi itaendelea kufanya kaguzi za shughuli za kihandisi nchini ili shughuli zote za kihandisi zifanywe na wahandisi waliosajiliwa na kwa kufuata maadili ya utendaji kazi za kihandisi. Vilevile, Bodi itaendelea kutembelea na kukagua miradi ya ujenzi wa barabara Tanzania Bara, ikiwa ni pamoja na barabara za Halmashauri.

Bodi vilevile itaendelea kusimamia mafunzo ya kujiendeleza kitaaluma kwa wahandisi wataalam na washauri, kwa ajili ya kuwaendeleza wahandisi kwa ujumla pamoja na kuwashawishi wahandisi wataalam waanzishe kampuni za ushauri wa kihandisi mikoani na hivyo kusogeza huduma hii muhimu karibu na watumiaji.

Bodi ya Usajili wa Wabunifu Majengo na Wakadiriaji Majenzi

418. Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2020/21, Bodi imepanga kusajili Wataalam **120**, katika fani za Ubunifu Majengo na Ukadiriaji Majenzi na fani zinazoshabihiana nazo. Aidha, Bodi imepanga kusajili kampuni **18** za Ubunifu Majengo na Ukadiriaji Majenzi. Vilevile, Bodi imepanga kuendelea na mafunzo kwa vitendo kwa wahitimu **120** katika fani za Ubunifu Majengo na Ukadiriaji Majenzi.

Bodi pia imepanga kufanya ukaguzi wa miradi ya ujenzi **2,000** katika mikoa yote, Tanzania Bara na kusajili miradi ya majengo **1000**. Aidha, Bodi imepanga kuendesha mitihani ya kitaalam kwa wahitimu **120** katika fani za Ubunifu Majengo na Ukadiriaji Majenzi na fani zinazoshabihiana nazo.

Bodi vilevile itaendesha mashindano ya insha kwa wanafunzi wa sekondari, ikiwa ni njia ya kuwahamasisha kusoma masomo ya sayansi na hatimaye kusomea taaluma za ubunifu majengo, ukadiriaji majenzi na taaluma zinazoshabihiana nazo.

Bodi ya Usajili wa Makandarasi

419. Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2020/21, Bodi imepanga kusajili jumla ya makandarasi wapya **950** na kukagua jumla ya miradi ya ujenzi **3,100**. Aidha, Bodi inatarajia kuendesha kozi **5** za mafunzo katika mikoa ya Mwanza, Dodoma, Arusha, Dar es Salaam na Njombe. Bodi vilevile imepanga kuendesha warsha **2** za mafunzo ya ushirikiano wa ubia (Joint Venture) katika mikoa ya Dar es Salaam na Mwanza. Bodi pia itaendeleza Mfuko maalum wa Kutoa Dhamana ya Kusaidia Makandarasi Wadogo na wa Kati (CAF). Jitihada za kuhamasisha makandarasi wazalendo kujiunga ili kuomba zabuni kwa utaratibu wa ubia pia zitaendelea.

Baraza la Taifa la Ujenzi

420. Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2020/21, Baraza limepanga kukamilisha mapitio ya Sheria iliyoanzisha Baraza na kuandaa Kanuni za Utekelezaji wake; kuratibu na kutoa mafunzo katika Sekta ya Ujenzi, kutoa ushauri wa kiufundi na kitaalam kwa wadau wa Sekta ya Ujenzi na kuratibu utatuzi wa migogoro inayojitokeza wakati wa utekelezaji wa miradi ya ujenzi.

Baraza pia litaendelea kufanya tafiti zinazohusu: kuboresha kanuni ya ukokotoaji wa mabadiliko ya gharama katika miradi ya ujenzi wa majengo nchini; kutathmini changamoto na matatizo ya ushindani wa makandarasi na Washauri wa Kitaalam wazalendo katika kutekeleza miradi ya ujenzi ukilinganisha na Makandarasi na Washauri wa Kitaalam wa kigeni; kutathmini mafanikio na changamoto katika usimamizi wa miradi ya ujenzi wa miundombinu kwa njia ya “Design and Build”; kutathmini mwenendo wa ukuaji wa Sekta ya Ujenzi nchini na mwenendo wa mahitaji ya ujuzi na weledi unaohitajika ili kutekeleza miradi ya ujenzi ipasavyo.

421. Mheshimiwa Spika, Baraza pia litaendelea na wajibu wake wa kutoa huduma za ukaguzi wa kiufundi wa miradi ya ujenzi kwa wadau wa sekta ya ujenzi; ukusanyaji na utoaji wa takwimu na taarifa za Sekta ya Ujenzi pamoja na kuendelea na mchakato wa kuanzisha Kituo Maalum cha Taarifa za Sekta ya Ujenzi. Kazi nyingine ni kuratibu mpango wa kukuza uwazi na uwajibikaji (Construction Sector Transparency Initiative - CoST) katika utekelezaji wa miradi ya ujenzi ya umma na kuhamasisha ushiriki wa sekta isiyo rasmi katika

utekelezaji wa miradi ya ujenzi kwa lengo la kukuza vipato vya wananchi katika maeneo husika.

Kituo cha Usambazaji wa Teknolojia Katika Sekta ya Ujenzi na Usafirishaji Tanzania (Tanzania Transportation Technology Transfer Centre)

422. *Mheshimiwa Spika*, katika mwaka wa fedha 2020/21, Kituo kimepanga kuendelea na jukumu lake la kusambaza teknolojia katika sekta ya ujenzi na usafirishaji hapa nchini. Pamoja na kusambaza majarida kutoka kwa wadau, Kituo kitaandaa, kuchapisha na kusambaza majarida yake yanayohusu teknolojia mbalimbali katika sekta ya ujenzi na usafirishaji ambayo yataandaliwa mara nne kwa mwaka. Vilevile, kituo kitaendelea kutoa huduma ya maktaba ikiwa imeboreshwa zaidi.

Aidha, kituo kimepanga kuendesha makongamano kwa kushirikiana na Mamlaka mbalimbali za barabara hapa nchini, taasisi za ufundishaji, wataalamu binafsi wa ndani na nje ya nchi na taasisi zisizo za kiserikali kwa lengo la kujadili na kutafuta majawabu ya changamoto mbalimbali zinazoikabili sekta ya barabara na uchukuzi. Majawabu yatakayopatikana yatafikishwa kwa wahandisi wetu kupitia mafunzo ya muda mfupi ambayo kituo kimepanga kuyaandaa.

D.1.2 SEKTA YA UCHUKUZI

Makadirio ya Ukusanyaji wa Mapato, Matumizi ya Kawaida na Bajeti ya Miradi ya Maendeleo

423. *Mheshimiwa Spika*, katika mwaka wa fedha 2020/2021, Sekta ya Uchukuzi (Fungu 62) imetengewa jumla ya **Shilingi 3,152,858,745,000** kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na Utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo. Kati ya fedha hizo, **Shilingi 90,710,109,000** zimetengwa kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na **Shilingi 3,062,148,636,000** kwa ajili ya utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo. Mgawanyo wa fedha za maendeleo pamoja na miradi iliyotengewa fedha ni kama inavyooneshwa katika **Kiambatisho Na.6**. Fedha za Matumizi ya Kawaida zinajumuisha **Shilingi 63,639,165,000** kwa ajili ya Mishahara ya Watumishi na **Shilingi 27,070,944,000** kwa ajili ya Matumizi Mengineyo. Katika Fedha za Miradi ya Maendeleo zilizotengwa, **Shilingi 2,937,678,923,000** ni fedha za Ndani na **Shilingi 124,469,713,000** ni fedha za Nje.

424. Mheshimiwa Spika, ili kuendelea kuboresha huduma za usafiri na usalama wa watu na vyombo vya usafiri katika Ziwa Victoria, Ziwa Tanganyika na Ziwa Nyasa, Kampuni ya Huduma za Usafiri wa Meli katika Maziwa (MSCL) imetengewa jumla ya **Shilingi bilioni 135** fedha za ndani. Fedha hizo zimetengwa ili kugharamia mipango ifuatayo:

- i. Kuendelea na ujenzi wa Meli mpya ya abiria na mizigo katika Ziwa Victoria;
- ii. Kuanza ujenzi wa Meli mpya ya mizigo katika Ziwa Victoria (Wagon ferry);
- iii. Kuanza ukarabati mkubwa wa Meli ya MV.Umoja katika Ziwa Victoria;
- iv. Kuanza ukarabati mkubwa wa Meli ya MT. Nyangumi katika Ziwa Victoria;
- v. Kuanza ukarabati mkubwa wa Meli ya MT. Ukerewe katika Ziwa Victoria;
- vi. Kuanza ujenzi wa Meli mpya ya abiria na mizigo katika Ziwa Tanganyika;
- vii. Kuanza Ukarabati mkubwa wa MV. Liemba iliyo katika Ziwa Tanganyika;
- viii. Kuanza Ukarabati mkubwa wa MT. Sangara iliyo katika Ziwa Tanganyika;
- ix. Kuanza Ujenzi wa meli ya mizigo katika Ziwa Tanganyika;
- x. Kuanza Ujenzi wa Meli mpya ya mizigo katika Bahari ya Hindi; na
- xi. Kuendelea na ufungaji wa Mifumo ya TEHAMA.

425. Mheshimiwa Spika, jumla ya **shilingi bilioni 13** zimetengwa ili kuwezesha uendeshaji na uwekaji wa miundombinu katika Jengo la Tatu la Abiria (TB III) lililo katika Kiwanja cha Ndege cha kimataifa cha Julius Nyerere (JNIA). Fedha hizi zitatumika kwa ajili ya kugharamia umeme, maji, vifaa vya zimamoto, viyoyoyi, madaraja ya Ndege, daraja la abiria, vyoo, maegesho, huduma za mtandao, kuboresha mazingira ya nje ya jengo la abiria, kamera na kituo cha wasindikizaji.

Aidha, jumla ya **Shilingi bilioni 3.4** fedha zinazotokana na mapato ya ndani ya TAA zimetengwa ili kutekeleza kazi zifuatazo:

- i. Ujenzi wa uzio wa ulinzi na usalama katika viwanja vya

- Ndege vya Mwanza na Dodoma;
- ii. Kukamilisha utayarishaji wa Mpango Bora wa Matumizi ya Ardhi katika viwanja vya Ndege vya Dodoma, Iringa, Geita, Tanga na Lake Manyara;
- iii. Kufanya Usanifu wa Kina kwa ajili ya ujenzi wa *Runway End Safety Area* (RESA) katika Kiwanja cha Ndege cha Kimataifa cha Julius Nyerere;
- iv. Kukamilisha urefushaji wa barabara ya kutua na kuruka ndege kwa mita 200 pamoja na maeneo ya kugeuzia ndege (Turning bay) katika Kiwanja cha Ndege cha Arusha.

426. Mheshimiwa Spika, Mfuko wa Reli (Railway Fund) umetengewa jumla ya **Shilingi bilioni 289.679** fedha za ndani ili kugharamia ukarabati wa miundombinu ya Reli iliyopo, kujenga Reli mpya ya *Standard Gauge*, ukarabati wa vitendea kazi na kugharamia stadi mbalimbali kwa ajili ya Miradi ya ujenzi wa Reli. Kazi zitakazotekelezwa ni pamoja na:

- i. Kuunda upya vichwa vya Treni 9 kwa ajili ya sogeza na njia kuu;
- ii. Kurejesha na kuimarisha huduma za usafiri wa Treni kwa Reli ya Kaskazini (Tanga – Arusha);
- iii. Kugharamia kazi za Upembuzi na Usanifu wa awali wa ujenzi wa Reli;
- iv. Ukarabati wa Karakana, Stesheni na Majengo ya Reli; na
- v. Kuchangia katika gharama za ujenzi wa Reli ya *Standard Gauge* na matengenezo ya reli ya Kati.

427. Mheshimiwa Spika, kuhusu ugharamiaji wa ujenzi wa reli mpya ya standard gauge, ununuzi wa injini na mabehewa ya mizigo na abiria, Upembuzi Yakinifu kwa ajili ya miradi ya reli, na ukarabati wa reli iliyopo jumla ya **Shilingi bilioni 2.020** fedha za ndani na **Shilingi bilioni 95.0** fedha za nje kupitia Mradi wa TIRP zimetengwa ili kutekeleza miradi ifuatayo:

- i. Kukamilisha ujenzi wa Reli ya kati ya *Standard Gauge* kwa kipande cha Dar es Salaam hadi Morogoro (Km 300);
- ii. Kuanza majaribio na uendeshaji wa treni ya *Standard gauge* kutoka Dar es Salaam hadi Morogoro;
- iii. Kuendelea na ujenzi wa Reli ya Kati kwa kipande cha Morogoro hadi Makutupora (Km 422) kwa *Standard Gauge*;

- iv. Kuanza ujenzi wa Reli ya kati kwa *Standard Gauge* kutoka Makutupora hadi Mwanza (Km 673);
- v. Kuendelea na taratibu za upatikanaji wa Mkandarasi kwa ajili ya ujenzi wa Reli mpya ya *Standard Gauge* kwa sehemu za Makutupora - Tabora (Km 294), Tabora – Isaka (Km 133) na Isaka-Mwanza (Km 246);
- vi. Kuendelea na taratibu za upatikanaji wa Mkandarasi, Mshauri Mwelekezi na utwaaji wa maeneo kwa ajili ya ujenzi wa Reli mpya ya *Standard Gauge* kwa sehemu za Tabora - Kigoma (km 411), Kaliua – Mpanda - Karema (km 320), Isaka – Rusumo (km 371) na Uvinza - Musongati (km 240);
- vii. Kukamilisha kazi ya kuandaa maandiko na kutafuta wawekezaji kwa ajili ya miradi ya Mtwara – Songea – Mbamba Bay pamoja na matawi ya kwenda Mchuchuma na Liganga na Tanga – Arusha - Musoma kwa mfumo wa ubia baina ya Sekta ya Umma na Binafsi (PPP);
- viii. Kukamilisha ukarabati wa njia ya reli ya Kati iliyopo (meter gauge) kwa kutandika reli nzito za ratili 80 kwa yadi katika umbali wa Kilomita 970 kati ya Dar es Salaam na Isaka;
- ix. Kuendelea na ujenzi wa madaraja na makalvati katika njia ya reli ya Tanga - Arusha;
- x. Ujenzi wa sehemu ya kuunganisha treni (Marshalling yard) katika eneo la Gerezani; na
- xi. Ununuzi wa vifaa ikiwemo injini 3 na mabehewa 44 ya njia ya reli ya Kati iliyopo sasa;
- xii. Kukamilisha kazi ya upembuzi na usanifu wa awali na kuanza ujenzi wa reli ya Jijini Dodoma (Dodoma Commuter train);
- xiii. Ununuzi wa vichwa vya treni 5, mabehewa ya abiria 60, mabehewa ya mizigo 1,430 kwa ajili ya uendeshaji wa SGR;
- xiv. Ukarabati wa karakana, stesheni na majengo ya reli iliyopo; na
- xv. kusafirisha tani za mizigo 672,000 na abiria 667,328 kuanzia Dar es Salaam hadi Kigoma, Mwanza na Mpanda; abiria 320,141 kwa treni ya kisasa toka Dar es Salaam hadi Morogoro na abiria 5,000,000 kwa usafiri wa treni ya mjini Dar es Salaam.

428. Mheshimiwa Spika, Serikali itaendelea kutekeleza mradi wa

kuboresha utabiri wa hali ya hewa nchini kuhakikisha uwepo wa mtandao wa rada saba (7), ununuzi wa vifaa pamoja na kuimarisha miundombinu mbalimbali ya utabiri wa hali ya hewa. Katika mwaka 2020/21, **Shilingi bilioni 30** fedha za ndani zimetengwa ili kutekeleza kazi zifuatazo:

- i. Ununuzi wa Rada mbili (2) za hali ya hewa;
- ii. Kununua vifaa vya hali ya hewa ikiwemo kubadilisha vifaa vinavyotumia zebaki na vitambuzi vya matukio ya radi (lightening detectors);
- iii. Kukamilisha malipo ya mwisho ya Rada mbili (2) na ujenzi wa miundombinu yake kwa ajili ya Rada hizo katika maeneo ya Mbeya na Kigoma; na
- iv. Ukarabati wa mabweni na majengo ya Utawala katika Chuo cha Hali ya Hewa Kigoma.

429. Mheshimiwa Spika, Mradi wa kuboresha huduma za Kampuni ya Ndege Tanzania (ATCL) ili iweze kutoa huduma za usafiri wa anga ndani ya nchi, kikanda na kimataifa kwa ufanisi umetengewa **Shilingi milioni 450,000.00** fedha za ndani. Fedha hizi zitatumika kutekeleza kazi zifuatazo:

- i. Kulipa malipo ya awali ya ununuzi wa Ndege mbili (2) mpya aina ya Boeing 787-8 Dreamliner;
- ii. Kulipa malipo ya awali ya ununuzi wa Ndege moja ya mizigo (freighter) aina ya Boeing 767-300. Ndege hii itasaidia kuongeza mnyororo wa thamani katika bidhaa zetu ikiwemo maua, samaki na bidhaa zitokanazo na samaki, nyama, korosho, matunda na mboga mboga;
- iii. Ununuzi wa vifaa vya kuhudumia ndege (Ground Handling Service Equipment), kulipa malipo ya mwisho na gharama za kuanzia kwa Ndege mpya mbili za aina ya A220-300 na Ndege moja aina ya Q400 zitakazopokelewa (Entry into service costs), kulipa madeni yaliyohakikiwa, ukarabati wa karakana za matengenezo ya Ndege (Hangar) zilizopo JNIA na KIMAFa, ukarabati wa nyumba 38 za Watumishi wa ATCL zilizopo KIA, ukarabati wa Jengo la ATCL makao makuu na ukarabati wa Ghala la kuhifadhi vifaa vya Ndege iliyoko JNIA; na
- iv. Kupanua mtandao wa safari za anga. Kwa safari za ndani ni kuanzisha safari za Arusha, na kurejesha safari za Songea na

Mtwara. Kikanda ni kuongeza safari za Lubumbashi, DR Congo na Gatwick, London; na kurejesha safari za Afrika ya Kusini.

430. Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2020/2021, Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari imelenga kuongeza kiwango cha shehena, idadi ya Meli, mapato na ziada kama ifuatavyo:

- i. Kuhudumia Shehena ya tani milioni 15.295 ikijumuisha tani za shehena ya makasha (TEUs) 175,300 zitakazohudumiwa na vitengo vya TPA. Aidha, Kitengo cha TICTS kinatarajia kuhudumia makasha (TEUs) 656,100;
- ii. Kuhudumia jumla ya Meli 3,980 zenye ukubwa wa (GRT) milioni 33.524. Kati ya hizo, Meli 1,283 ni za Kimataifa (Deep Sea), Meli 923 ni za Mwambao (coasters) na Meli 1,769 zitahudumiwa katika bandari za Maziwa; na
- iii. Kukusanya mapato ya jumla ya shilingi bilioni 1,164.406.

Aidha, ili kufikia malengo hayo, katika mwaka 2020/21 Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari Tanzania (TPA) imetenga jumla ya **Shilingi milioni 700,000**. Kati ya fedha hizo, **Shilingi milioni 500,000** ni fedha zinazotokana na vyanzo vya Ndani ya Mamlaka na **Shilingi milioni 200,000** ni fedha za Nje za mkopo kutoka Benki ya Dunia (International Development Agency - IDA). Kazi zitakazotekelezwa ni pamoja na:

- i. Kukamilisha Mradi wa uboreshaji wa Gati Na. 5 - 7 katika Bandari ya Dar es Salaam;
- ii. Kukamilisha ujenzi wa Gati moja (multipurpose terminal) lenye urefu wa mita 300 katika Bandari ya Mtwara;
- iii. Kuendelea na Mradi wa kupanua na kuchimba Lango la kuingilia na eneo la kugeuzia Meli (entrance channel and turning basin) katika Bandari ya Tanga;
- iv. Kuanza utekelezaji wa Mradi wa Ujenzi wa Matanki ya kuhifadhia Mafuta katika Bandari ya Dar es Salaam;
- v. Kuanza kutekeleza Mradi wa kupanua na kuchimba Lango la kuingilia na eneo la kugeuzia Meli (entrance channel and turning basin) katika Bandari ya Dar es Salaam;
- vi. Kuendelea na ununuzi wa Mitambo na vifaa mbalimbali kwa Bandari zote;

- vii. Kuendelea kuimarisha matumizi ya TEHAMA na mfumo wa usalama bandarini (Port Integrated Security System - ISS);
- viii. Kuendelea na ujenzi wa Bandari Kavu ya Kwala, Ruvu; na
- ix. Kuendelea na miradi ya uboreshaji wa Bandari zote.

431. Mheshimiwa Spika, Mamlaka ya Usafiri wa Anga (TCAA) imetenga **Shilingi bilioni 13.5** kutoka katika vyanzo vyake ili kudhibiti ubora wa huduma na miundombinu ya Usafiri wa Anga nchini. Kazi zitakazofanyika ni:

- i. Kukamilisha ufungaji wa Rada za kuongozea Ndege katika Kituo kilicho Kiwanja cha Ndege cha Songwe;
- ii. Kununua Mfumo wa Usambazaji Taarifa za Ndege kimtandao (AXIM - Aeronautical Information Exchange Modal);
- iii. Kuandaa Kanzi Data kwa ajili ya sehemu za uwanda wa Nchi unaoonesha miinuko, milima, mabonde na vizuizi (e-TOD – Electronic terrain and obstacle data) katika viwanja vya kimataifa vya Julius Nyerere, Kilimanjaro na Abeid Amani Karume;
- iv. Kununua vipuri mbalimbali kwa ajili ya Mitambo mbalimbali;
- v. Kujenga uzio katika Mtambo wa kuongozea Ndege unaotumia mawasiliano ya redio (Non-Directional Beacon-NDB katika kituo cha Songwe;
- vi. Kuandaa Mfumo wa urekebishaji wa njia za Ndege kwa ajili ya kuingia na kutoka viwanjani (DAR-FIR AIRSPACE RESTRUCTURING); na
- vii. Kuandaa michoro na uhakiki katika Viwanja vya Ndege vya Songwe, Tabora, Iringa, Chato, Dodoma, Zanzibar, Kigoma, Bukoba na Mpanda.

432. Mheshimiwa Spika, Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini (LATRA) imetenga **Shilingi bilioni 36.528** kutoka katika vyanzo vyake ili kusimamia huduma za Usafiri Ardhini. Fedha hizo zitatumika kutekeleza miradi ifuatayo:

- i. Kuimarisha ushindani na kuhakikisha kuwa huduma za usafiri wa ardhini zinakuwa endelevu;
- ii. Kuimarisha Usalama, Ulinzi na Ubora wa huduma za

usafiri wa ardhini;

- iii. Kuhakikisha mazingira endelevu sambamba na maendeleo ya huduma ya usafiri kwa jamii; na
- iv. Kuongeza uwezo wa kutekeleza majukumu kiufanisi zaidi.

433. Mheshimiwa Spika, Shirika la Uwakala wa Meli Tanzania (TASAC) limetenga jumla ya **Shilingi bilioni 66.8** fedha zinazotokana na makusanyo yake ya ndani ili kutekeleza kazi mbalimbali zenye lengo la kudhibiti huduma za usafiri kwa njia ya maji. Kazi zitakazotekelezwa ni pamoja na:

- i. Kuimarisha ushindani na kuhakikisha huduma za Usafiri kwa njia ya Maji zinakuwa endelevu;
- ii. Kuimarisha Usalama, Ulinzi na Ubora wa huduma za usafiri kwa njia ya Maji;
- iii. Kuhimiza na kutunza mazingira dhidi ya uchafuzi wa mazingira baharini utokanao na Meli na kuhakikisha mazingira endelevu;
- iv. Kuboresha Sheria, Kanuni, Sera na mahusiano ya kitaasisi katika Sekta za usafiri kwa njia ya Maji; na
- v. Kuongeza uwezo wa Shirika kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi.

434. Mheshimiwa Spika, Mamlaka ya Reli ya Tanzania na Zambia (TAZARA) imetenga jumla ya **Shilingi bilioni 108.4** fedha kutoka katika vyanzo vyake vya ndani kwa ajili ya kutoa huduma za usafiri wa abiria na mizigo kati ya Tanzania, nchi za SADC na DRC; kusimamia na kuimarisha usalama wa abiria, mizigo na vyombo vya usafiri, pamoja na kuzishauri Serikali za Tanzania na Zambia kuhusu masuala yanayohusu usafiri wa Reli ya TAZARA. Fedha hizo zitatumika kutekeleza kazi zifuatazo:

- i. Kuboresha ukusanyaji wa mapato ya Mamlaka kutoka Shilingi bilioni 92.8 mwaka 2019/2020 hadi Shilingi bilioni 95.5 mwaka 2020/2021;
- ii. Kuongeza huduma za usafirishaji wa shehena ya mizigo hadi kufikia tani 450,000 na abiria 800,000 kwa njia kuu;
- iii. Kukarabati Injini saba (7) za njia kuu;
- iv. Kukarabati na kuimarisha miundombinu ya njia kuu ya Reli iliyopo;
- v. Kununua mataruma ya mbao 13,000;

- vi. Kufanya matengenezo na kukarabati Injini, Mitambo, na Mabehewa ya Mizigo na Abiria; na
- vii. Kukarabati Majengo, Karakana ya Mbeya, na Kiwanda cha Kokoto na uzalishaji wa Mataruma ya Zege cha Kongolo.

435. Mheshimiwa Spika, Kampuni ya Ubia kati ya Tanzania na China (SINOTASHIP) imetenga **Shilingi bilioni 3.0** kutoka katika vyanzo vyake ili kuboresha utoaji huduma ya usafiri wa mizigo ya masafa marefu kwa njia ya bahari pamoja na kusimamia usalama wa Mabaharia, Mizigo na Meli. Fedha hizo zitatumika kwa ajili ya kazi zifuatazo:

- i. Kuboresha ukusanyaji wa mapato kutoka Shilingi bilioni 16.9 mwaka 2019/20 hadi Shilingi bilioni 17.50 mwaka 2020/2021;
- ii. Kutoa huduma ya usafirishaji wa mizigo kutoka tani 600,000 mwaka 2019/2020 na kufikia tani 610,000 ifikapo Juni, 2021;
- iii. Kuongeza mapato nje ya biashara ya msingi (core business) kwa njia ya kushawishi kuongeza idadi ya Meli na mizigo itakayoingia katika Bandari nchini kutoka makasha 47,000 mwaka 2019 na kufikia makasha 50,000 mwaka 2020; na
- iv. Kupunguza gharama za uendeshaji wa Kampuni kutoka Shilingi bilioni 14.6 mwaka 2019/20 na kufikia Shilingi bilioni 12.5 mwaka 2020/21.

436. Mheshimiwa Spika, Kampuni ya Kuendeleza Kiwanja cha Ndege cha Kimataifa cha Kilimanjaro (KADCO) imetenga **Shilingi bilioni 11.33** kutoka katika vyanzo vyake ili kuendesha na kuendeleza miundombinu ya Kiwanja cha Ndege cha Kimataifa cha Kilimanjaro (KIA). Kazi zilizopangwa kutekelezwa ni pamoja na:

- i. Kuanza ukarabati wa njia ya kuruka na kutua Ndege (runway resurfacing);
- ii. Uwekaji wa Mfumo mpya wa Taa za kuongozea Ndege (Aeronautical Ground Lighting – AGL);
- iii. Kupima msugvano wa njia ya kurukia Ndege na magurudumu ya Ndege na kuweka alama muhimu za kuongozea Ndege;
- iv. Maboresho ya maegesho ya magari (Car Parking);

- v. Kuanza ujenzi wa uzio wa eneo la kurukia na kutua Ndege;
- vi. Kununua kifaa cha kutibu maji ya kisima cha KIA yaliyo na madini mengi ya chumvi na fluoride;
- vii. Kununua Mashine ya kukusanya na kudhibiti mapato yanayotokana na maegesho ya magari kiwanjani; na
- viii. Kununua vifaa mbalimbali vya Ulinzi na Usalama kiwanjani.

D.1.3 SEKTA YA MAWASILIANO

437. Mheshimiwa Spika, Kwa mwaka wa fedha 2020/21 Sekta ya Mawasiliano inakadiria kutumia kiasi cha **Shilingi 15,654,466,000**. Kati ya fedha hizo **Shilingi 4,654,466,000** ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na **Shilingi 11,000,000,000** ni kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo.

438. Mheshimiwa Spika, Katika mwaka 2020/21, Sekta ya Mawasiliano itaendelea kutekeleza Mpango wa Muda wa Kati na Muda Mrefu ambao umetilia mkazo katika maeneo yafuatayo:

TEHAMA

- i. Kusimamia uimarishaji na uendelezaji wa mradi wa Ujenzi wa Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano ili kufikisha huduma za Mkongo kwenye nchi zote zinazopakana na Tanzania na kufikisha mkongo hadi Makao Makuu ya Wilaya zote nchini;
- ii. Kufikisha miundombinu ya Mkongo kwa watumiaji wa mwisho ikiwemo taasisi za Serikali mijini na vijijini (Last Mile connectivity) ili kuwezesha mifumo mbalimbali iliyopo kufanya kazi kwa ufanisi ikiwemo mfumo wa ukusanyaji wa mapato ya serikali (GePG);
- iii. Kuweka utaratibu wa kuwezesha upatikanaji wa huduma za Intaneti kwa gharama nafuu katika maeneo ya umma;
- iv. Kuratibu ukamilishaji wa Sheria ya kulinda taarifa binafsi (Personal Data Protection Act);
- v. Kusimamia utekelezaji wa mkakati wa mtandao wa TEHAMA wenye kasi zaidi (National Broadband Strategy); na
- vi. Kusimamia utekelezaji wa mkakati wa kitaifa wa usalama wa mitandao (National Cyber security strategy).

MAWASILIANO

- i. Kukamilisha uhuishaji wa Sera ya Taifa ya Posta ya Mwaka 2003 na kuhuisha Sheria ya Posta ya mwaka 1993 ili iendane na ukuaji wa Teknolojia na kiuchumi;

- ii. Kufanya tathmini ya utekelezaji wa Sera ya Taifa ya TEHAMA ya mwaka 2016;
- iii. Kuendelea kuratibu utekelezaji wa Mpango wa Anwani za Makazi nchini;
- iv. Kuratibu uanzishaji wa vituo vya HUDUMA PAMOJA (One Stop Service Centres); na
- v. Kuimarisha mashirikiano na mashirika ya kimataifa na kikanda.

Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA)

439. Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2020/21, Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania itatekeleza masuala yafuatayo:

- i. Kwa kushirikiana na Baraza la Ushauri la Watumiaji wa Huduma za Mawasiliano (TCRA CCC) kuendelea kuelimisha watumiaji wa huduma za mawasiliano kuhusu Sheria, haki na wajibu wa watumiaji, kuhusu matumizi ya Mfumo mpya wa anwani za makazi na misimbo ya Posta, uhakiki wa usajili wa laini za simu za kiganjani, wajibu wa watumiaji katika masuala ya tahadhari dhidi ya uhalifu kupitia mtandao na kufanikisha ufumbuzi wa malalamiko kati ya watumiaji na watoa huduma za Mawasiliano;
- ii. Kuendelea kutekeleza usimamizi wa usalama wa mitandao ya mawasiliano kupitia TZ- CERT;
- iii. Kuendelea kusimamia na kuboresha mfumo wa usimamizi wa huduma za mawasiliano, TTMS, ili uendane na mahitaji pamoja na mabadiliko ya Teknolojia;
- iv. Kuandaa Muongozo juu ya matumizi ya utangazaji wa kidigiti kwa redio na mwingiliano wa Smart Card za Vingamuzi;
- v. Kujenga Jengo la Ofisi za Shirika la Posta Afrika (Pan African Postal Union-PAPU) - Arusha, Jengo la TCRA - Dodoma na Ofisi za Zanzibar;
- vi. Kuendelea kutekeleza mifumo ya utendaji kazi (Quality Management System) ili kuongeza ufanisi wa udhibiti wa Mawasiliano ya simu, Posta na Utangazaji;
- vii. Kuendelea kusimamia Sekta ya mawasilino na kuhakikisha kuwa watoa huduma wote wanatoa huduma kwa mujibu wa Sheria, Kanuni na Miongozo;
- viii. Kuendelea kuhakiki gharama na tozo mbalimbali katika matumizi ya huduma za mawasiliano;
- ix. Kuendelea kujenga uwezo wa kukabiliana na uhalifu wa matumizi mabaya ya mtandao kwa Taasisi za Ulinzi na Usalama; na
- x. Kuendelea kuboresha mfumo wa utoaji wa leseni za huduma za mawasiliano.

Shirika la Posta Tanzania (TPC)

440. Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2020/21, Shirika la Posta linatarajia kutekeleza majukumu yafuatayo:

- i) Ujenzi wa Jengo la Ofisi ya Posta eneo la Mtumba (Awamu ya Kwanza), vituo vya kutolea huduma za Posta (Namanyere, Bariadi, Kilosa na Kondoa) na ukarabati wa majengo 30 ya Posta za wilaya na majengo 7 ya posta kuu za mikoa;
- ii) Mradi wa ununuzi wa magari kwa ajili ya kuboresha usafirishaji na ufikishaji wa mizigo, barua, nyaraka na vipeto pamoja na kuimarisha miundombinu na mifumo ya TEHAMA;
- iii) Kuandaa 'Post Office Directory' ya Shirika la Posta Tanzania;
- iv) Kufikisha huduma ya Posta Mlangoni (Last mile delivery) katika maeneo yote ambayo utoaji wa anuani za makazi na postikodi umekamilika;
- v) Kufanya ukaguzi wa ofisi na kukamilisha taratibu na maandalizi ya msingi ya miundombinu kwa ajili ya kutoa huduma ya Jamii centre, na kuanza utekelezaji wake;
- vi) Kufanya maandalizi ya msingi na kukamilisha taratibu muhimu za utekelezaji wa mradi wa Ecom-Africa katika utoaji wa huduma za biashara ya kielektroniki kupitia mtandao wa Shirika la Posta Tanzania; na
- vii) Kupanua wigo wa utoaji wa huduma ya usafirishaji wa sampuli za maabara kwa wakati.

Shirika la Mawasiliano Tanzania (TTCL)

441. Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka 2020/21 Shirika la Mawasiliano Tanzania litatekeleza majukumu yafuatayo:

- i) Kupanua na kuboresha huduma kwa wateja, biashara, usambazaji na masoko kwa kuongeza matumizi ya TEHAMA katika kutoa huduma na uendeshaji.
- ii) Kuongeza idadi ya wateja hai (Active Customers) wa huduma mbalimbali za mawasiliano (simu na data) kutoka 1,008,455 mwezi Februari, 2020 hadi 1,800,000 kwa mwaka wa fedha 2020/21.
- iii) Kuendelea kusimamia na kuendesha Miundombinu mkakati ikiwemo Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano na Kituo cha Data cha Taifa (National Data Centre);
- iv) Uboreshaji wa Mifumo ya Usalama wa Mtandao kwa wateja wa Shirika. (Modernization of Broadband Traffic Management & Security);
- v) Upanuzi na uboreshaji wa Mifumo ya Mtandao Mhimili (Expansion of Core Network Systems), Usafirishaji wa Data

- (Expansion of Transmission/Transport Networks) na Simu za Mkononi (Expansion of Radio Access Network); na
- vi) Kuisaidia serikali katika kukusanya mapato na kuchangia katika mfumo wa fedha kwa kielektroniki kupitia kampuni tanzu ya TPesa.

Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote (UCSAF)

442. Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2020/21, Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote (UCSAF) utatekeleza kazi zifuatazo:

- i) Kukamilisha utekelezaji wa miradi ya kufikisha huduma ya mawasiliano vijijini katika kata 252 awamu ya 4 zenye vijiji 555 ili kuhakikisha kuwa huduma za wananchi zinawafikia wananchi wengi zaidi;
- ii) Kukamilisha utekelezaji wa miradi ya kufikisha huduma ya mawasiliano vijijini katika maeneo ya kata 38 kwenye maeneo ya mipakani na yenye uhitaji maalum awamu ya 5;
- iii) Kuboresha usikivu wa matangazo ya TBC maeneo ya mikoani na pembezoni mwa nchi;
- iv) Kutoa vifaa vya TEHAMA na kuunganisha mtandao wa intaneti katika shule za sekondari 150;
- v) Kutoa mafunzo ya TEHAMA kwa walimu 1,000;
- vi) Kutoa mafunzo ya TEHAMA kwa Wanafunzi wasichana 248;
- vii) Kuendeleza ushirikiano na Taasisi ya Teknolojia Dar es Salaam (DIT) na Hospitali ya Taifa ya Muhimbili katika uunganishwaji wa mtandao wa mawasiliano katika hospitali za Serikali ili kuleta ushirikiano wa kitabibu kwa njia ya mtandao na kuondoa tatizo sugu la uhaba wa madaktari bingwa; na
- viii) Ujenzi wa Ofisi za Mfuko jijini Dodoma.

Tume ya TEHAMA (ICTC)

443. Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2020/21, Tume ya TEHAMA itatekeleza mambo yafuatayo:

- i) Kusajili na kujenga uwezo wa wataalam wa TEHAMA wasiopungua 800;
- ii) Kuwezesha matukio ya kuvutia uwekezaji na kuendeleza miradi 10 ya TEHAMA katika kituo cha SoftCenter;
- iii) Kufanya utafiti wa kupima viashiria vya Jamii Habari (measuring Information Society and impact of digital transformation indicators) kwa kushirikina na wadau wa utafiti kutoka ndani na nje ya nchi; na

- iv) Kutekeleza Mradi wa ujenzi wa kituo cha kuendeleza ubunifu na bidhaa za TEHAMA nchini.

Baraza la Ushauri la Watumiaji wa Huduma za Mawasiliano (TCRA CCC)

444. Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka 2020/21 Baraza litaendelea kufanya yafuatayo:

- i. Kuelimisha umma kuhusu matumizi sahihi ya huduma na bidhaa za mawasiliano. Baraza litaingia makubaliano na Tanzania Bus Owners Association (**TABOA**) ili kurusha documentary yenye kuelimisha watumiaji wa huduma za mawasiliano katika Mabasi yaendayo mikoani. Kupitia Makubaliano hayo Baraza linategemea kufikia watu kati ya 15,000 hadi 20,000 kwa siku na watu 500,000 kwa mwezi;
- ii. Kupokea taarifa na maoni kutoka kwa watumiaji wa huduma na bidhaa za mawasiliano na kuziwasilisha kwa taasisi husika ili kuboresha ufanisi na kupunguza changamoto kwa watumiaji;
- iii. Kuanzisha Kamati za Watumiaji wa Huduma za Mawasiliano, kuendesha mikutano ya elimu na mashauriano katika mikoa ya Rukwa, Manyara, Geita na Kigoma;
- iv. Kuanzisha na kujengea uwezo vilabu vya Mawasiliano katika shule 56 za Sekondari katika mikoa 13 ya Morogoro, Mbeya, Dodoma, Iringa, Lindi, Mtwara, Mjini Magharibi, Kusini Pemba, Tanga, Arusha, Mwanza, Kagera na Dar es Salaam; na
- v. Baraza litaendelea kumwakilisha mtumiaji wa huduma za mawasiliano kwa kuwasilisha maoni, taarifa na kushauriana na Waziri na Mamlaka ya Mawasiliano. Aidha Baraza litaendelea kushauriana na Watoa huduma kuhusu masuala yanayomhusu mtumiaji.

D. 2 TAASISI ZA MAFUNZO

Chuo cha Ujenzi Morogoro

445. Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2020/21, Chuo kimepanga kufundisha jumla ya wanafunzi **1,440** katika fani za ufundi sanifu (technicians) na ufundi stadi (Basic Artisans) wa fani za barabara na ukaguzi wa madaraja, majengo, magari, utengenezaji wa mitambo (plant mechanics), uendeshaji wa mitambo (plant operations), madereva wa magari ya Umma (Public Professional Drivers), madereva wa awali (Basic driving) na madereva wa magari ya abiria (PSV), mafunzo ya kompyuta na Teknolojia ya Nguvukazi stahiki. Kazi

nyingine ni pamoja na kukarabati magari, samani, majengo na miundo mbinu ya Chuo; kufanya tathmini ya mafunzo na kununua vifaa kwa ajili ya kuboresha mradi wa kuosha magari.

Chuo cha Matumizi ya Teknolojia Stahiki ya Nguvukazi (Appropriate Technology Training Institute – ATTI) - Mbeya

446. Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha wa 2020/21, Chuo kitaendelea na utoaji wa mafunzo yenye lengo la kuimarisha matumizi endelevu ya teknolojia stahiki ya nguvukazi kwa kada za watendaji ili kujenga weledi na ujuzi wa kutosha katika utekelezaji wa miradi inayotumia nguvukazi. Mafunzo yatahusisha Wahandisi **10**, Mafundi Sanifu **30** na wasimamizi wa barabara **30**. Aidha, Chuo kitaendelea na utoaji wa mafunzo kwa vikundi vya vijana na wanawake ili kuimarisha matumizi endelevu ya teknolojia stahiki ya nguvukazi na kujenga weledi na ujuzi wa kutosha katika utekelezaji wa miradi inayotumia nguvukazi, lengo ni kutoa mafunzo haya kwa wanawake **50** na vijana **50**.

447. Mheshimiwa Spika, kazi zingine zilizopangwa ni kuendelea kuhamasisha matumizi ya Teknolojia Stahiki ya Nguvukazi katika Ujenzi na ukarabati wa barabara kwa kutembelea na kutoa ushauri wa matumizi ya Teknolojia Stahiki ya Nguvukazi kwa wadau mbalimbali katika Halmashauri; kuimarisha na kuboresha utendaji wa Chuo kwa kuongeza idadi ya watumishi wa kada mbalimbali na kuwajengea uwezo kwa kushiriki kwenye mikutano na makongamano ya kitaifa, kimataifa na kikanda.

448. Mheshimiwa Spika, Chuo pia kimepanga kufanya matengenezo ya magari na mitambo ya mafunzo na kuongeza vifaa na huduma mbali mbali kwa ajili ya matumizi ya mafunzo; kuendelea kusimamia ukarabati na matengenezo ya barabara kwa kupitia barabara za mafunzo katika utoaji wa mafunzo kwa jamii ili kuendelea kuhamasisha matumizi ya Teknolojia Stahiki ya Nguvu Kazi kwa umma pamoja na kuendelea kushiriki katika uanzishaji wa Taasisi ya Teknolojia ya Ujenzi nchini inayoratibiwa na Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano.

Chuo cha Taifa cha Usafirishaji (NIT)

449. Mheshimiwa Spika, Chuo cha Taifa cha Usafirishaji (NIT)

kimetengewa jumla ya **Shilingi bilioni 25.379** fedha za mkopo kutoka Benki ya Dunia ili kuboresha miundombinu ya Chuo, utoaji wa mafunzo na maeneo ya kufundishia. Fedha hizo zitatumika kutekeleza mipango ifuatayo:

- i. Kuanza ujenzi wa Kituo cha Mafunzo ya Usafiri wa Anga kitakachokuwa Katika Kiwanja cha Ndege cha Kilimanjaro (KIA);
- ii. Kuendelea na Ujenzi wa Kituo cha Rasilimali Mafunzo kilichopo Mabibo, Dar es Salaam;
- iii. Kuanza ujenzi wa Majengo mapya sita (6) katika Kampasi ya Mabibo Dar-es- Salaam;
- iv. Ununuzi wa Ndege mbili (2) za kufundishia kozi ya urubani na vifaa mbalimbali vya mafunzo; na
- v. Kukamilisha upatikanaji wa Ithibati ya kufundisha kozi za Marubani kutoka Mamlaka ya Usafiri wa Anga Tanzania (TCAA).

Chuo cha Bahari Dar es Salaam (DMI)

450. Mheshimiwa Spika, Chuo cha Bahari Dar es Salaam (DMI) kimetenga jumla ya **Shilingi billioni 4.842** fedha zinazotokana na vyanzo vyake vya mapato ili kutekeleza malengo yafuatayo:

- i. Kuongeza udahili wa wanafunzi kwenye fani mbalimbali za ujuzi (competency) na taaluma (academic) kwenye Sekta ya Bahari kutoka 1,126 hadi kufikia 1,500 kwa kozi ndefu;
- ii. Kufanya tafiti na kutoa ushauri elekezi kwenye Sekta ya Bahari;
- iii. Kuendeleza walimu kitaaluma katika Shahada za Uzamili, Uzamivu na kuwapatia mafunzo kwa vitendo melini (Sea time training) ili kuwaongezea sifa na uwezo wa kutoa mafunzo;
- iv. Kuanza kutoa kozi za Uhandisi katika fani za Fundi Mchundo (welding and fabrication Engineering) na *offshore Oil and Gas Engineering* ili kutoa Wataalamu wenye sifa kwenye Miradi ya Utafiti, Uchimbaji na Usafirishaji wa Mafuta na Gesi Baharini;
- v. Kuandaa mitaala ya Uzamili katika fani za *Marine Engineering* na *Nautical Science*; na

- vi. Kukamilisha taratibu za ununuzi wa Mkandarasi wa ujenzi wa Jengo la madarasa na ofisi katika eneo la Sokoine Drive.

D.3 MASUALA MTAMBUKA

Ushirikishwaji wa Wanawake katika Kazi za Sekta ya Ujenzi

451. Mheshimiwa Spika, ili kuongeza ushiriki wa wanawake katika kazi za ujenzi, Wizara kwa mwaka wa fedha 2020/21 imepanga kutoa mafunzo kwa makandarasi wanawake ya namna ya kuomba zabuni na kujaza zabuni kwa usahihi; kutoa mafunzo kwa wanawake na vikundi vya wanawake juu ya kufanya matengenezo na ukarabati wa barabara kwa kutumia teknolojia ya nguvu kazi na kuwasaidia kusajili kampuni zao za ujenzi. Aidha, Wizara itaendelea kufuatilia kwa karibu kazi za sekta ya ujenzi zinazofanywa na makandarasi wanawake, ili kubaini changamoto zinazowakabili kwa lengo la kutafuta ufumbuzi pamoja na kuendelea kuelimisha umma juu ya ushirikishwaji wa wanawake katika kazi hizo.

Wizara pia imepanga kutembelea shule za Sekondari ili kuwahamasisha wasichana wanaosoma masomo ya sayansi na hisabati pamoja na kuendelea kusambaza nakala za Miongozo ya Ushirikishwaji wa Wanawake katika Kazi za Sekta ya Ujenzi.

E. SHUKRANI

452. Mheshimiwa Spika, napenda kuchukua fursa hii kuwashukuru kwa dhati viongozi wenzangu katika Wizara ninayoiongoza nikiianza na **Mheshimiwa Elias John Kwandikwa (Mb.)**, **Naibu Waziri (Ujenzi)**; **Mheshimiwa Mhandisi Atashasta Justus Nditaye (Mb.)**, **Naibu Waziri (Uchukuzi na Mawasiliano)**; **Makatibu Wakuu: Mbunifu Majengo Elius Asangalwisye Mwakalinga (Ujenzi)**; **Mhandisi Dkt. Leonard Madaraka Chamuriho (Uchukuzi)**; **Dkt. Maria Leticia Sasabo** (Aliyekuwa Katibu Mkuu wa Sekta ya Mawasiliano) na **Dkt. Jim James Yonaz**, Naibu Katibu Mkuu (Mawasiliano). Aidha, nawashukuru Wakuu wa Idara/Vitengo; Wenyeviti wa Bodi zilizo chini ya Wizara; Viongozi wa Taasisi na Watendaji wote wa Wizara kwa ushirikiano mzuri ambao wamekuwa wakinipa na juhudi walizofanya kuhakikisha kwamba tunatimiza majukumu tuliyokabidhiwa na Taifa ipasavyo. Ushirikiano wao ndio ulioweza kutekeleza majukumu ya Wizara yetu katika mwaka uliopita. Naomba waendeele na juhudi hizo

katika kipindi kijacho ili tuweze kutimiza malengo tuliyojiwekea.

453. Mheshimiwa Spika, Washirika mbalimbali wa Maendeleo wamechangia katika utekelezaji wa Programu na Mipango mbalimbali ya Wizara. Napenda kuchukua fursa hii kuwashukuru na kuwatambua Washirika hao wa Maendeleo ambao ni pamoja na Shirika la Kimataifa la Usafiri wa Majini (IMO), Shirika la Kimataifa la Usafiri wa Anga (ICAO), Shirika la Hali ya Hewa Duniani (WMO), Benki ya Kiarabu ya Maendeleo ya Afrika (BADEA), OPEC Fund, Umoja wa Nchi za Ulaya, “Third World Organization for Women in Science (TWOWS)”, UNESCO, Benki ya Maendeleo ya Afrika (AfDB), Benki ya Dunia (WB), Japan (JICA), Korea Kusini (KOICA), Abu Dhabi Fund, Ujerumani (KfW), Uingereza (DFID), Uholanzi (ORIO), Jumuiya ya Nchi za Ulaya (EU), Benki ya Uwekezaji ya Ulaya (EIB), Shirika la Maendeleo la Marekani (USAID), Kuwait (KFAED), Uturuki, HSBC, TMEA, Sekretarieti ya Jumuiya ya Afrika Mashariki, Sekretarieti ya Jumuiya ya Nchi za SADC, Nchi za Urusi, Afrika Kusini, Uingereza, Marekani, Uholanzi, Japan, India, China, Denmark, Norway, Ubelgiji, Ujerumani, Taasisi za fedha za CRDB, NSSF, PSSF na TIB, Asasi zisizokuwa za Kiserikali; Sekta Binafsi pamoja na wengine wengi.

454. Mheshimiwa Spika, mwisho, nakushukuru tena wewe binafsi na Mhe. Naibu Spika. Hotuba hii pia inapatikana katika tovuti ya Wizara (www.mwtc.go.tz).

F.MUHTASARI WA MAOMBI YA FEDHA YA WIZARA YA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO KATIKA MWAKA WA FEDHA 2020/21

455. Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2020/21, Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano inaomba kuidhinishiwa jumla ya **Shilingi 4,784,874,417,000.00**. Kati ya fedha hizo, **Shilingi 1,616,361,206,000.00** ni kwa ajili ya Sekta ya Ujenzi, **Shilingi 3,152,858,745,000.00** ni kwa ajili ya Sekta ya Uchukuzi na **Shilingi 15,654,466,000.00** ni kwa ajili ya Sekta ya Mawasiliano. Mchanganuo wa fedha zinazoombwa kwa kila Fungu ni kama ifuatavyo:

SEKTA YA UJENZI (FUNGU 98)

456. Mheshimiwa Spika, jumla ya **Shilingi 1,616,361,206,000.00** za Fungu 98 (Ujenzi) zinajumuisha **Shilingi 38,774,425,000.00** kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida ya Wizara

(Ujenzi) na Taasisi ambapo **Shilingi 36,420,026,000.00** ni za Mishahara ya Watumishi na **Shilingi 2,354,399,000.00** ni za Matumizi Mengineyo. Bajeti ya Maendeleo ni Shilingi **1,577,586,781,000.00** ambazo zinajumuisha **Shilingi 1,252,222,598,000.00** fedha za ndani na **Shilingi 325,364,183,000.00** fedha za nje. Fedha za ndani zinajumuisha **Shilingi 641,746,370,000.00** za Mfuko wa Barabara na **Shilingi 610,476,228,000.00** za Mfuko Mkuu wa Serikali.

SEKTA YA UCHUKUZI (FUNGU 62)

457. Mheshimiwa Spika, Sekta ya Uchukuzi imetengewa jumla ya **Shilingi 3,152,858,745,000.00** kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na Utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo. Kati ya hizo, **Shilingi 90,710,109,000.00** ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida ambapo **Shilingi 63,639,165,000.00** ni za Mishahara ya Watumishi na **Shilingi 27,070,944,000.00** ni za Matumizi Mengineyo. Aidha, miradi ya maendeleo imetengewa **Shilingi 3,062,148,636,000.00** Kati ya fedha hizo, **Shilingi 2,937,678,923,000.00** ni fedha za Ndani na **Shilingi 124,469,713,000.00** ni fedha za Nje.

SEKTA YA MAWASILIANO (FUNGU 68)

458. Mheshimiwa Spika, Sekta ya Mawasiliano imepangiwa jumla ya **Shilingi 15,654,466,000.00**. Kati ya fedha hizo, **Shilingi 4,654,466,000.00** ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na **Shilingi 11,000,000,000.00** ni kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo.

459. Mheshimiwa Spika, pamoja na Hotuba hii, nimeambatanisha Miradi ya Wizara itakayotekelezwa katika mwaka wa fedha 2020/21 **(Kiambatisho Na. 1-7)** ikiwa ni pamoja na kiasi cha fedha kilichotengwa kutekeleza Miradi hiyo. Naomba viambatisho hivyo vichukuliwe kama sehemu ya vielelezo vya hoja hii.

460. Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja.

MGAWANYO WA FEDHA ZA BAJETI YA MAENDELEO KWA MWAKA WA FEDHA 2020/21

Kasma	Jina la Mradi	Urefu (km)	Makadirio ya Bajeti kwa Mwaka 2020/21 (Shilingi Milioni)			Chanzo cha Fedha
			Fedha za Ndani	Fedha za Nje	Jumla	
SUBVOTE 1003: POLICY AND PLANNING DIVISION						
6267	Institutional Support		302.50	0.00	302.50	GOT
	TOTAL SUB VOTE: 1003		302.50	0.00	302.50	
SUBVOTE 2002: TECHNICAL SERVICES DIVISION						
4125	Construction of Ferry Ramps					
	(i) To carry out expansion of Kigamboni ferry terminal.		455.00	0.00	455.00	GOT
	(ii) To construct Bukondo and Zumacheli ramps for Chato - Nkome crossing.		470.20	0.00	470.20	GOT
	(iii) To construct Nyamisati - Mafia ferry ramps.		610.25	0.00	610.25	GOT
	(iv) To construct and rehabilitate ferry ramps at eight (8) crossings (Bugolora - Ukara, Rugezi - Kisorya, Kilambo - Namoto, Utete - Mkongo, Iramba - Majita, Nyakarilo - Kome, Kasharu - Buganguzi and Kigongo - Busisi).		510.62	0.00	510.62	GOT
	(v) To construct ferry infrastructure (waiting longue, office and fences) for ten (10) ferry stations (Bugolora, Ukara, Kome, Nyakalilo, Maisome, Kaunda, Nkome, Kisorya, Musoma na Kinesi).		442.55	0.00	442.55	GOT
	(vi) To construct (Ngara - Nyakiziba, Muleba - Ikuza) ferry ramps.		300.00	0.00	300.00	GOT
	(vii) To conduct monitoring and evaluation of ferry ramps activities.		80.20	0.00	80.20	GOT
	Sub Total		2,868.82	0.00	2,868.82	

Kasma	Jina la Mradi	Urefu (km)	Makadirio ya Bajeti kwa Mwaka 2020/21 (Shilingi Milioni)			Chanzo cha Fedha
			Fedha za Ndani	Fedha za Nje	Jumla	
4139	Procurement of Ferries					
	To procure one ferry to ply between Nyamisati – Mafia.		2,500.00	0.00	2,500.00	GOT
	To procure on new ferry to ply between Bugolora - Ukara crossing.		2,200.00	0.00	2,200.00	GOT
	To procure tool for TEMESA workshops.		605.51	0.00	605.51	GOT
	To procure one ferry to ply between Kisorya – Rugezi.		1,020.91	0.00	1,020.91	GOT
	To procure one fibber boats for Utete - Mkongo crossing.		150.00	0.00	150.00	GOT
	To conduct monitoring and evaluation of ferries.		272.20	0.00	272.20	GOT
	Sub Total		6,748.62	0.00	6,748.62	
4144	Rehabilitation of Ferries					
	To complete rehabilitate of MV Tegemeo, MV Musoma and MV Mara.		510.62	0.00	510.62	GOT
	To complete rehabilitation of MV KIU.		340.41	0.00	340.41	GOT
	To complete rehabilitation of MV Sengerema and MV Ujenzi.		780.31	0.00	780.31	GOT
	To complete rehabilitation of MV Kigamboni and MV Kome II.		1,035.62	0.00	1,035.62	GOT
	To complete rehabilitation of MV Misungwi.		425.51	0.00	425.51	GOT
	To rehabilitate MV Nyerere.		600.00	0.00	600.00	GOT
	To rehabilitate MV Kilombero II and Kilombero I		400.00	0.00	400.00	GOT
	To conduct monitoring and evaluation of ferries.		75.20	0.00	75.20	GOT

Kasma	Jina la Mradi	Urefu (km)	Makadirio ya Bajeti kwa Mwaka 2020/21 (Shilingi Milioni)			Chanzo cha Fedha
			Fedha za Ndani	Fedha za Nje	Jumla	
	Sub Total		4,167.67	0.00	4,167.67	
6327	Construction of Government Houses					
	To complete construction of 6 tied quarters for Judges residence in mainland Tanzania.		1,441.60	0.00	1,441.60	GOT
	To construct 20 houses for Government Leaders and Residential Houses at State Houses in Dodoma.		5,550.06	0.00	5,550.06	GOT
	To conduct monitoring and evaluation of construction & maintenance projects for Government houses and buildings.		830.00	0.00	830.00	GOT
	To construct houses for former Magomeni Quarters Residents at Kinondoni Municipality, Dar es Salaam.		14,650.00	0.00	14,650.00	GOT
	To facilitate consultancy services for Government buildings construction, maintenance projects & preparation of standards and specifications for Government building construction.		721.52	0.00	721.52	GOT
	To construct 150 houses for public Servants at Dodoma City and other regions.		10,500.00	0.00	10,500.00	GOT
	To rehabilitate 400 houses for public servants transferred to TBA from former CDA		1,200.00	0.00	1,200.00	GOT
	To rehabilitate public servant houses to 20 regions transferred to TBA from TAMISEMI/NHC.		5,200.00	0.00	5,200.00	GOT
	To rehabilitate 40 Government Leaders houses – Dodoma.		4,000.00	0.00	4,000.00	GOT

Kasma	Jina la Mradi	Urefu (km)	Makadirio ya Bajeti kwa Mwaka 2020/21 (Shilingi Milioni)			Chanzo cha Fedha
			Fedha za Ndani	Fedha za Nje	Jumla	
	To rehabilitate 30 Government Leaders houses in other regions.		2,890.20	0.00	2,890.20	GOT
	To procure furniture State Lodges		1,000.00	0.00	1,000.00	GOT
	Construction of five (5) new TEMESA workshops (Songwe, Simiyu, Geita, Njombe and Katavi) in newly established five (5) Regions.		605.89	0.00	605.89	GOT
	To procure six mobile workshop complete with all tools.		1,000.00	0.00	1,000.00	GOT
	To construct new modern Dodoma workshop in Dodoma.		1,051.03	0.00	1,051.03	GOT
	To establish district workshop in (Same, Simajiro, Masasi, Ukerewe, Chato and Kyela) and Motor vehicle Maintenance Management Information System.		600.00	0.00	600.00	GOT
	To design, supply, install and commissioning the system which monitor all activities within the workshops.		3,000.00	0.00	3,000.00	GOT
	To construct new MoWTC office block in Dodoma at Mtumba Government City.		5,598.04	0.00	5,598.04	GOT
	To Rehabilitate eleven (11) workshops in Mwanza, Arusha, Mtwara, Mbeya, Mt Depot, Tabora, Kigoma, Mara, Ruvuma, Pwani and Vigunguti.		1,976.54	0.00	1,976.54	GOT
	To rehabilitate Six (6) TBA furniture workshops in Arusha, Mwanza, Dodoma, Tabora, DSM and Mbeya and establish furniture factory.		4,505.50	0.00	4,505.50	GOT
	To facilitate capacity building to 50 Architects		550.00	0.00	550.00	GOT

Kasma	Jina la Mradi	Urefu (km)	Makadirio ya Bajeti kwa Mwaka 2020/21 (Shilingi Milioni)			Chanzo cha Fedha
			Fedha za Ndani	Fedha za Nje	Jumla	
	and 50 Quantity Surveyors.					
	Sub Total		66,870.38	0.00	66,870.38	
	GRAND TOTAL SUB VOTE 2002		80,655.49	0.00	80,655.49	
SUBVOTE 2005: ROADS DEVELOPMENT DIVISION						
4001	Soni - Bumbuli - Dindira - Korogwe	74.00	840.00	0.00	840.00	GOT
	Mtwara - Newala - Masasi (221km)					
4002	i) Mtwara - Mnivata Section	50.00	7,000.00	0.00	7,000.00	GOT
	ii) Mnivata - Tandahimba Section	50.00	3,000.00	0.00	3,000.00	GOT
	Sub-total	100.00	10,000.00	0.00	10,000.00	
4003	Likuyufusi - Mkenda (km 122.50)	10.00	1,590.00	0.00	1,590.00	GOT
4004	Nachingwea - Liwale (FS & DD)	130.00	250.00	0.00	250.00	GOT
4005	Ubena Zomozi - Ngerengere (Upgrading to bitumen standard)	11.60	730.00	0.00	730.00	GOT
4006	TAMCO - Vikawe - Mapinga	24.00	950.00	0.00	950.00	GOT
4007	Makofia - Mlandizi	36.70	10.00	0.00	10.00	GOT
4008	Musoma - Makojo - Busekela	92.00	2,625.00	0.00	2,625.00	GOT
4009	Kongwa Jct - Mpwapa- Gulwe- Kibakwe	98.00	1,650.00	0.00	1,650.00	GOT
4010	Muhutwe - Kamachumu - Muleba	54.00	1,080.00	0.00	1,080.00	GOT
4011	Iringa - Ruaha National Park	104.00	1,000.00	0.00	1,000.00	GOT
4012	Muheza - Amani	36.00	1,590.00	0.00	1,590.00	GOT
4013	Mtwara - Mingoyo - Masasi (DD Review and Rehabilitation)	200.00	1,000.00	0.00	1,000.00	GOT
4014	Kibaoni - Majimoto - Muze - Kilyamatundu					
	(i) Kibaoni - Majimoto - Inyonga Section	152	420.00	0.00	420.00	GOT

Kasma	Jina la Mradi	Urefu (km)	Makadirio ya Bajeti kwa Mwaka 2020/21 (Shilingi Milioni)			Chanzo cha Fedha
			Fedha za Ndani	Fedha za Nje	Jumla	
	(ii) Ntendo - Muze - Kilyamatundu (200km) (Ntendo - Muze Section)	37	5,000.00	0.00	5,000.00	GOT
	Sub-total	189	5,420.00	0.00	5,420.00	GOT
4015	Kigongo - Busisi Bridge and its approaches	1No	21,295.00	0.00	21,295.00	GOT
4016	Mzinga Bridge	1 No	20.00	0.00	20.00	GOT
4017	Ugalla Bridge	1 No	250.00	0.00	250.00	GOT
4018	Kitengule Bridge and Approach Roads (18km)	1 No	1,500.00	0.00	1,500.00	GOT
4019	Morogoro Dodoma Road including Mkundi Bridge (FS & DD)	260	1,125.00	0.00	1,125.00	GOT
4020	New Wami Bridge (Construction)	1 No	3,500.00	0.00	3,500.00	GOT
	Njombe - Makete - Isyonje Road					
4022	i) Njombe – Moronga	53.9	8,000.00	0.00	8,000.00	GOT
	ii) Moronga – Makete	53.5	8,000.00	0.00	8,000.00	GOT
	iii) Isyonje - Makete	50.00	6,000.00	0.00	6,000.00	GOT
	Sub-total	57.40	22,000.00	0.00	22,000.00	
4023	Omugakorongo - Kigarama - Murongo Road	105.00	8,000.00	0.00	8,000.00	GOT
	Nanganga - Ruangwa - Nachingwea Road					
4024	i) Masasi – Nachingwea	45.00	1,430.00	0.00	1,430.00	GOT
	ii) Nanganga – Ruangwa – Nachingwea	100.00	6,000.00	0.00	6,000.00	GOT
	Sub-total	145.00	7,430.00	0.00	7,430.00	GOT
	Mpemba - Isongole Road					
4025	i) Mpemba - Isongole Road	51.20	4,000.00	0.00	4,000.00	GOT
	ii) Ruanda – Iyula – Nyimbili	21.00	310.00	0.00	310.00	GOT
	iii) Katumbasongwe - Kasumulu - Ngana - Ileje	90.10	1,000.00	0.00	1,000.00	GOT
	Sub-total	162.30	5,310.00	0.00	5,310.00	
	Tanga - Pangani - Makurunge					
4101	i)Tanga - Pangani Section	50.00	5,000.00	0.00	5,000.00	GOT

Kasma	Jina la Mradi	Urefu (km)	Makadirio ya Bajeti kwa Mwaka 2020/21 (Shilingi Milioni)			Chanzo cha Fedha
			Fedha za Ndani	Fedha za Nje	Jumla	
	ii) Pangani Bridge	1No	1,000.00	22,600.00	23,600.00	GOT/AfD B
	iii) Pangani – Mkange section	124.50	1,000.00	21,200.00	22,200.00	GOT/AfD B
	Sub-total	174.50	7,000.00	43,800.00	50,800.00	
4102	Kisarawe - Maneromango	54.00	1,400.00	0.00	1,400.00	GOT
4103	Geita - Bulyanhulu - Kahama (120km)					
	i) Geita – Bulyanhulu Jct Road	58.30	5,000.00	0.00	5,000.00	GOT
	ii) Bulyanhulu Jct – Kahama Road	61.70	2,000.00	0.00	2,000.00	GOT
	iii) Uyogo - Nyamilagano - Nyandekwa - Kahama	54.00	4,500.00	0.00	4,500.00	GOT
	Sub-total	174.00	11,500.00	0.00	11,500.00	
4104	Nyamirembe Port – Katoke Road	50.00	20.00	0.00	20.00	GOT
4105	Geita – Nzera Road	54.00	1,000.00	0.00	1,000.00	GOT
4106	Arusha - Moshi - Himo - Holili					
	i) Sakina - Tengeru Section and Arusha bypass	56.51	10.00	0.00	10.00	GOT
	ii) Tengeru – Moshi – Himo Section including Himo Weighbridge	105.00	10.00	0.00	10.00	GOT
	iii) Kijenge - Usa River (Nelson Mandela AIST)	20.00	1,150.00	0.00	1,150.00	GOT
	iv) Mianzini - Ngaramtoni	18.00	3,630.00	0.00	3,630.00	GOT
	Sub-total	199.51	4,800.00	0.00	4,800.00	
4107	Access Roads to Rufiji Hydropower Project					
	i) Bigwa – Matombo - Mvuha (Rehab. To gravel standard)	70.00	859.00	0.00	859.00	GOT
	ii) Ubena Zomozi - Mvuha - Kisasi - Mtemele Jct (FS & DD)	178.00	1,800.00	0.00	1,800.00	GOT

Kasma	Jina la Mradi	Urefu (km)	Makadirio ya Bajeti kwa Mwaka 2020/21 (Shilingi Milioni)			Chanzo cha Fedha
			Fedha za Ndani	Fedha za Nje	Jumla	
	iii) Maneromango - Vikumburu - Mloka (Rehabilitation to gravel standard)	100.00	500.00	0.00	500.00	GOT
	iv) Kibiti - Mloka - Mtemele - Rufiji		20.00	0.00	20.00	GOT
	Sub-total	348.00	3,179.00	0.00	3,179.00	
	Dar es Salaam – Chalinze – Morogoro Express Way					
4108	i) Dar es Salaam – Chalinze Expressway	100	10.00	0.00	10.00	GOT
	ii) Backlog Rehabilitation of Mlandizi – Chalinze	44.00	2,000.00	0.00	2,000.00	GOT
	iii) Kwa Mathias (Morogoro Road) - Msangani	8.30	1,800.00	0.00	1,800.00	GOT
	Sub-total	152.30	3,810.00	0.00	3,810.00	
	Wazo Hill – Bagamoyo – Msata					
4109	i) Wazo Hill – Bagamoyo – Msata (Tegeta - Bagamoyo Section)	46.90	10.00	0.00	10.00	GOT
	ii) Mbegani - Bagamoyo	7.20	70.00	0.00	70.00	GOT
	Sub-total	118.10	80.00	0.00	80.00	
	Usagara – Geita –Buzirayombo – Kyamyorwa					
4110	i)Uyovu - Bwanga - Biharamulo (Lot 1 & Lot 2)	110.00	10.00	0.00	10.00	GOT
	Sub-total	110.00	10.00	0.00	10.00	
	Nyakahura - Kumubuga - Rulenge - Kabanga Nickel road 32km) (FS & DD)					
4111	i) Nyakahura - Kumubuga - Murusagamba road	34.00	10.00	0.00	10.00	GOT
	ii)Kumubuga - Rulenge - Murugarama	75.00	10.00	0.00	10.00	GOT
	iii)Rulenge - Kabanga Nickel road	32.00	10.00	0.00	10.00	GOT
	Sub - total	141.00	30.00	0.00	30.00	
	Kigoma – Kidahwe – Uvinza – Kaliua – Tabora					
4112	i) Malagarasi Bridge and Associated Approach Roads	48.00	10.00	0.00	10.00	GOT

Kasma	Jina la Mradi	Urefu (km)	Makadirio ya Bajeti kwa Mwaka 2020/21 (Shilingi Milioni)			Chanzo cha Fedha
			Fedha za Ndani	Fedha za Nje	Jumla	
	ii) Kidahwe – Uvinza	76.60	10.00	0.00	10.00	GOT
	iii) Uvinza – Malagarasi Road	51.10	390.00	15,000.000	15,390.00	GOT/OPE C
	iv) Tabora – Ndono Road	42.00	10.00	0.00	10.00	GOT
	v) Ndono – Urambo Road	52.00	10.00	0.00	10.00	GOT
	vi) Urambo – Kaliua – Ilunde – Uvinza Road (Kaliua - Kazilambwa Section)	56.00	10.00	0.00	10.00	GOT
	vii) Urambo – Kaliua – Ilunde – Uvinza Road (Urambo - Kaliua section)	28.00	5,000.00	0.00	5,000.00	GOT
	viii) Urambo – Kaliua – Ilunde – Uvinza Road (Kazilambwa - Chagu section)	36.00	5,000.00	0.00	5,000.00	GOT
	Sub-total	389.70	10,440.00	15,000.000	25,440.00	
	Ifakara - Kihansi - Mlimba - Madeke - Kibena (Njombe)					
4113	i) Ifakara - Kihansi Section	50.00	20.00	0.00	20.00	GOT
	ii) Kibena – Lupembe Section	50.00	5,960.00	0.00	5,960.00	GOT
	iii) Lupembe – Madeke Section	50.00	20.00	0.00	20.00	GOT
	Sub-total	150.00	6,000.00	0.00	6,000.00	
4114	Karatu - Mbulu - Haydom - Sibiti River - Lalago - Maswa (389 km)	50.00	5,000.00	0.00	5,000.00	GOT
	Marangu -Tarakea - Rongai - Kamwanga/ Bomang'ombe - Sanya Juu					
4115	i) Sanya Juu - Kamwanga (Sanyajuu - Alerai section)	32.00	10.00	0.00	10.00	GOT
	ii) KIA – Mererani	26.00	10.00	0.00	10.00	GOT
	iii) Kwa Sadala – Masama – Machame Junction	16.00	840.00	0.00	840.00	GOT
	iv) Kiboroloni – Kiharara – Tsuduni – Kidia	10.80	840.00	0.00	840.00	GOT
	Sub-total	84.80	1,700.00	0.00	1,700.00	

Kasma	Jina la Mradi	Urefu (km)	Makadirio ya Bajeti kwa Mwaka 2020/21 (Shilingi Milioni)			Chanzo cha Fedha
			Fedha za Ndani	Fedha za Nje	Jumla	
4116	Tukuyu – Mbambo – Katumba (60.6km)					
	i) Bujesi – Mbambo section	26.00	1,260.00	0.00	1,260.00	GOT
	ii) Tukuyu – Mbambo section	34.60	1,290.00	0.00	1,290.00	GOT
	iii) Mbambo - Ipinda (FS & DD)	19.70	300.00	0.00	300.00	GOT
	Sub - total	80.30	2,850.00	0.00	2,850.00	
4118	Dodoma – Manyoni Road (Incl. Manyoni Access Road)					
	i) Manyoni One Stop Inspection Station – OSIS	1 NO	150.00	0.00	150.00	GOT
	ii) Nala Weigh in Motion	1 NO	10.00	0.00	10.00	GOT
	Sub total		160.00	0.00	160.00	
4119	Tabora - Mambali - Bukene - Itobo	114.00	1,000.00	0.00	1,000.00	GOT
4121	Namanyere - Katongoro - New Kipili Port (FS & DD)	64.80	310.00	0.00	310.00	GOT
4123	Dumila – Kilosa – Mikumi					
	i) Dumila – Rudewa Section	45.00	10.00	0.00	10.00	GOT
	ii) Rudewa – Kilosa Section	24.00	4,500.00	0.00	4,500.00	GOT
	iii) Dakawa Weigh Bridge including WIM	1 NO	10.00	0.00	10.00	GOT
	iv) Kilosa - Ulaya - Mikumi	50.00	9,000.00	0.00	9,000.00	GOT
	Sub-total	119.00	13,520.00	0.00	13,520.00	
4124	Sumbawanga – Matai – Kasanga Port					
	i) Sumbawanga – Matai – Kasanga Port Road	112.00	6,000.00	0.00	6,000.00	GOT
	ii) Matai – Kasesya Road	50.00	5,000.00	0.00	5,000.00	GOT
	Sub-total	162.00	11,000.00	0.00	11,000.00	
4126	Construction of Bridges					
	i) Kirumi Bridge (Rehabilitation)	1 No	500.00	0.00	500.00	GOT
	ii) Sibiti Bridge (Construction)	1 No	3,000.00	0.00	3,000.00	GOT

Kasma	Jina la Mradi	Urefu (km)	Makadirio ya Bajeti kwa Mwaka 2020/21 (Shilingi Milioni)			Chanzo cha Fedha
			Fedha za Ndani	Fedha za Nje	Jumla	
	iii) Magufuli Bridge (Construction)	1 No	10.00	0.00	10.00	GOT
	iv) Ruhuhu Bridge (Construction)	1 No	1,100.00	0.00	1,100.00	GOT
	v) Momba Bridge (Construction)	1 No	10.00	0.00	10.00	GOT
	vi) Sukuma Bridge (Construction)	1 No	310.00	0.00	310.00	GOT
	vii) Simiyu Bridge (Design & Construction)	1 No	340.00	0.00	340.00	GOT
	ix) Mlalakuwa Bridge (Construction)	1 No	10.00	0.00	10.00	GOT
	x) Mara Bridge (Construction)	1 No	10.00	0.00	10.00	GOT
	xii) Mtera Dam Bridge (FS & DD)	1 No	10.00	0.00	10.00	GOT
	xiii) Magara Bridge (Construction)	1 No	860.00	0.00	860.00	GOT
	xiv) Lukuledi Bridge (Construction)	1 No	10.00	0.00	10.00	GOT
	xvi) Lower Malagarasi Bridge (FS & DD)	1 No	345.00	0.00	345.00	GOT
	xvii) Msingi Bridge (Construction)	1 No	630.00	0.00	630.00	GOT
	xviii) Steel Bridge Emergency Parts	1 No	630.00	0.00	630.00	GOT
	xx) Godegode Bridge (Design & Construction)	1 No	160.00	0.00	160.00	GOT
	xxiii) Mitomoni Bridge	1 No	140.00	0.00	140.00	GOT
	xxiv)Mkenda Bridge	1 No	110.00	0.00	110.00	GOT
	xxv)Mirumba Bridge (Design Review & Construction)	1 No	500.00	0.00	500.00	GOT
	xxvi) Sanza Bridge (Construction)	1No	500.00	0.00	500.00	GOT
	xxvii) Kiegeya Bridge	1No	5,000.00	0.00	5,000.00	GOT
	Sub-total		14,185.00	0.00	14,185.00	
4127	New Bagamoyo (Kawawa Jct - Tegeta)					
	i) Widening of Morocco - Mwenge	4.30	10.00	11,103.887	11,113.89	GOT/JICA
	ii) Improvement of Drainage System along Mwenge - Tegeta Road	14.00	250.00	0.00	250.00	GOT
	Sub-total	18.30	260.00	11,103.887	11,363.89	

Kasma	Jina la Mradi	Urefu (km)	Makadirio ya Bajeti kwa Mwaka 2020/21 (Shilingi Milioni)			Chanzo cha Fedha
			Fedha za Ndani	Fedha za Nje	Jumla	
4128	Kyaka – Bugene – Kasulo					
	i) Kyaka – Bugene Section	59.10	10.00	0.00	10.00	GOT
	ii) Kumunazi - Bugene – Kasulo and Kyaka - Mutukula (FS & DD)	163.00	2,000.00	0.00	2,000.00	GOT
	Sub-total	222.10	2,010.00	0.00	2,010.00	
4129	Isaka – Lusahunga					
	i) Isaka – Ushirombo (Rehabilitation)	132.00	10.00	0.00	10.00	GOT
	ii) Ushirombo – Lusahunga (Rehabilitation)	110.00	2,290.00	0.00	2,290.00	GOT
	iii) Lusahunga – Rusumo & Nyakasanza – Kobero	150.00	290.00	0.00	290.00	GOT
	iv) Nyakanazi One Stop Inspection Station (OSIS)	1 NO	150.00	0.00	150.00	GOT
	Sub-total	392.00	2,740.00	0.00	2,740.00	
4130	Manyoni – Itigi – Tabora					
	(i) Tabora – Nyahua Section	85.00	10.00	0.00	10.00	GOT
	(ii) Nyahua – Chaya Section	85.40	630.00	22,714.472	23,344.47	GOT/ KUWAIT
	(iii) Manyoni– Itigi – Chaya Section	89.35	10.00	0.00	10.00	GOT
	Sub-total	259.75	650.00	22,714.472	23,364.47	
4132	Regional Roads Rehabilitation (26 Regions)	630.62	48,500.00	380.966	48,880.96	GOT/NO RWAY
4133	Mwanza – Shinyanga/Mwanza Border road Rehabilitation (FS&DD)	102.00	310.00	0.00	310.00	GOT
4138	De-congestion of DSM Roads					
	i) Mbezi – Malambamawili – Kinyerezi – Banana	14.00	10.00	0.00	10.00	GOT
	ii) Tegeta - Kibaoni - Wazo Hill - Goba - Mbezi (Moro Rd); Mbezi Mwisho - Goba Section	20.00	10.00	0.00	10.00	GOT

Kasma	Jina la Mradi	Urefu (km)	Makadirio ya Bajeti kwa Mwaka 2020/21 (Shilingi Milioni)			Chanzo cha Fedha
			Fedha za Ndani	Fedha za Nje	Jumla	
	iii) Tangi Bovu – Goba	9.00	10.00	0.00	10.00	GOT
	iv) Kimara Baruti – Msewe – Changanyikeni	2.60	10.00	0.00	10.00	GOT
	v) Kibamba – Kisopwa – Kwembe – Makondeko	14.66	620.00	0.00	620.00	GOT
	vi) Banana – Kitunda – Kivule – Msongola	14.70	530.00	0.00	530.00	GOT
	vii) Ardhi – Makongo – Goba (Goba – Makongo Section: 4km)	4.00	340.00	0.00	340.00	GOT
	viii) Ardhi – Makongo – Goba (Ardhi – Makongo Section: 5km)	5.00	1,000.00	0.00	1,000.00	GOT
	ix) Widening of Mwai – Kibaki Road	9.10	10.00	0.00	10.00	GOT
	x) Kongowe – Mjimwema – Kivukoni Ferry Road (One Lane Widening)	25.10	520.00	0.00	520.00	GOT
	xi) Mjimwema – Kimbiji – Pembamnazi	27.00	1,500.00	0.00	1,500.00	GOT
	xii)Tegeta Kibaoni – Wazo Hill – Goba – Mbezi/Morogoro Road (Mbezi Mwisho); Wazo Hill (Madale) – Goba Section	6.00	10.00	0.00	10.00	GOT
	xiii) Tegeta Kibaoni – Wazo Hill – Goba – Mbezi/Morogoro Road (Mbezi Mwisho); Wazo Hill – Madale Section	9.00	1,500.00	0.00	1,500.00	GOT
	xiv) Goba - Matosa - Temboni	6.00	1,000.00	0.00	1,000.00	GOT
	Sub-total	166.16	7,070.00	0.00	7,070.00	GOT
4141	Nyamuswa - Bunda - Kisorya (106km)					
	i) Kisorya – Bulamba section	51.00	2,000.00	0.00	2,000.00	GOT
	ii) Nyamuswa – Bunda - Bulamba section	55.00	2,790.00	0.00	2,790.00	GOT
	Sub - total	106.00	4,790.00	0.00	4,790.00	

Kasma	Jina la Mradi	Urefu (km)	Makadirio ya Bajeti kwa Mwaka 2020/21 (Shilingi Milioni)			Chanzo cha Fedha
			Fedha za Ndani	Fedha za Nje	Jumla	
4142	Kolandoto - Lalago - Ng'oboko - Mwanhuzi (84km)					
	i) Kolandoto – Mwanhuzi	10.00	2,000.00	0.00	2,000.00	GOT
	ii) Lalago – Ng'oboko – Mwanhuzi	74.00	500.00	0.00	500.00	GOT
	Sub - total	84.00	2,500.00	0.00	2,500.00	
4143	Ndundu – Somanga	60.00	10.00	0.00	10.00	GOT
4145	Kasulu – Manyovu including Kasulu Town Links	68.00	2,570.00	8,430.088	11,000.09	GOT/AfD B
4146	Dodoma City Outer Dual Carriageway Ring Road Lot 1 & 2 (112.3 km)					
	(i) Lot 1: Nala – Veyula – Mtumba – Ihumwa Dry Port Section	52.30	4,370.00	8,327.915	12,697.91	GOT/CHI NA
	(ii) Lot 2: Ihumwa Dry Port – Matumbulu - Nala Section	60.00	4,460.00	9,939.814	14,399.81	GOT/AfD B
	(iii) Improvement of Dodoma City Roads (Dodoma Inner Ring Roads: Bahi R/About - Image R/About - Ntyuka R/About - Makulu R/About))		1,000.00	0.00	1,000.00	GOT/JIC A
	(iv) Widening up of Dodoma Outer Roads Sections (Dodoma - Morogoro Road 50km; Dodoma - Iringa Road 50km; Dodoma - Singida - 50km and Dodoma - Arusha Road 50km)	200.00	1,000.00	0.00	1000.00	GOT
	(v) Rehabilitation of Kikombo Jctn - Chololo - Mapinduzi (JWTZ HQ) Road	18.00	6,000.00	0.00	6,000.00	GOT
	vi) Ntyuka Jct - Mvumi Hospital - Kikombo Junction	76.07	6,000.00	0.00	6,000.00	GOT
	Sub - total	406.37	22,830.00	18,267.729	41,097.73	

Kasma	Jina la Mradi	Urefu (km)	Makadirio ya Bajeti kwa Mwaka 2020/21 (Shilingi Milioni)			Chanzo cha Fedha
			Fedha za Ndani	Fedha za Nje	Jumla	
4147	Kidatu - Ifakara - Lupiro - Malinyi - Londo - Lumecha/Songea					
	i) Ifakara – Lupilo – Malinyi – Londo – Lumecha/Songea	396.00	85.00	0.00	85.00	GOT
	ii) Mikumi - Kidatu - Ifakara (Kidatu - Ifakara Section- 68km)	103.00	20.00	0.00	20.00	GOT
	Sub-total	499.00	105.00	0.00	105.00	
